

# **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 23 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2011/2012 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. NAOMI AMY MWAKYOMA KAIHULA - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 235

**Kupandisha Hadhi kwa Kituo cha Afya Igawilo**

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE** aliuliza:-

Je, ni lini Kituo cha Afya cha Igawilo Jijini Mbeya kitaanza kufanya kazi kama Hospitali ya Wilaya baada ya kupata kibali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba upo mpango wa Serikali wa kikipandisha Kituo cha Afya cha Igawilo kuwa Hospitali ya Jiji la Mbeya. Kwa kuzingatia hilo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mnamo tarehe 29 Oktoba, 2011 ilifanya ukaguzi ili kujiridhisha kama kituo hicho kinakidhi kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Jiji. Taarifa ya ukaguzi huo ilipendekeza kwamba Kituo hicho kipandishwe hadhi na kuwa Hospitali ya Jiji.

Aidha, Kamati ilielekeza kwamba Halmashauri ifanye marekebisho ya mapungufu yaliyobainika yakiwemo ukosefu wa chumba cha upasuaji, wodi ya watoto na mama wajawazito, mfamasia, vitanda vya wagonjwa katika wodi mpya na majokofu katika chumba cha kuhifadhi maiti.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri katika mwaka 2012/2013 imetenga shilingi milioni 210 ambazo zitatumika kukamilisha wodi ya watoto na mama wajawazito, ununuzi wa majokofu vikiwemo vifaa kwa ajili ya upasuaji.

Aidha, Halmashauri imeomba kibali cha kuajiri watumishi 14 wa kada za afya kwa ajili ya kituo hicho. Kimsingi Wizara kuitia Kamati iliyokagua kituo hicho iliridhia baadhi ya huduma zikiwemo huduma za mama na mtoto na upasuaji wa dharura kwa akina mama ziendelee kutolewa katika kutuo hicho zikiwa na hadhi ya Hospitali ya Wilaya.

Hivyo kituo hicho kitapatiwa kibali cha kutoa huduma zote zenye hadhi ya Hospitali ya Jiji baada ya kukamilika kwa kazi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa ili kukidhi matakwa ya mwongozo wa utoaji huduma za afya hapa nchini. (*Makofî*)

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ya swali langu. Lakini naomba kuchukua nafasi fupi kwa niaba ya wananchi wa Jiji la Mbeya kuishukuru sana Serikali kwa kutekeleza ahadi yake ya kukiinua Kituo cha Igawilo kuwa Hospitali ya Jiji. (*Makofî*)

Kwa kuwa hatua imefikia ni kubwa sana ya kukamilisha mpango huu wa kikipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Igawilo kuwa Hospitali ya Jiji na kwa kuwa Serikali iliahidi kutokana na maombi ya Jiji kuwapatia watumishi 14 ili waweze kufanya kazi katika kituo hiki. Je, ni lini sasa Serikali itawatuma watumishi hao ili waanze kazi mara moja? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum Mbeya, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba huduma katika hospitali ile imeshaanza kuwa ya hadhi ya Jiji na baadhi ya vifaa vilishafikishwa lakini pia kama ambavyo nimeshaeleza kwenye jibu la msingi kwamba Halmashauri yenye wewe imeshajitengea fedha zaidi ya milioni 110 kwa ajili ya kukamilisha utoaji wa huduma hizo. (*Makofî*)

Suala la watumishi Ofisi ya Waziri Mkuu ikishirikiana pamoja na Wizara ya Afya wakati wa ajira mwaka jana mwaka 2011/2012 Wizara ya Afya ilitoa kibali cha kuajiri watumishi 9,000 kufikia Mei, 30 mwaka huu 2012 Wizara ya Afya ilikuwa ilishatoa kibali na watumishi 5600 walishaajiriwa. Kwa hiyo, tuna nafasi ya watumishi zaidi 3400 ambao pia wanaweza kuajiriwa wakiwemo wale 12 wanaokwenda kwenye Hospitali ile ya Jiji kule Mbeya.

**MHE. SUZAN A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali ni matatizo ya vituo vya afya, lakini mimi nataka kuuliza Serikali katika Jimbo la Morogoro Kusini, Kata ya Serembala Kijiji cha Kiburomo kuna Zahanati ya Mradi wa TASAF na nguvu za wananchi na nimekwenda kule nimeshuhudia mwenyewe viongozi wa Serikali wameweka mahabusu ya ng'ombe wanaokamatwa wanaokula kwenye mashamba ya wakulima na matokeo yake akina mama na wananchi wanakosa huduma. Je, Serikali imeliona hilo na wanachukua hatua gani kwa watendaji kama hao? (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ungeulizwa jumla yake tu lingekuwa sawa sawa ukiuliza kijiji wala hakujandaa habari ya kijiji. Lakini basi atajibu hivyo hivyo jibu lisiloridhisha.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Kiwanga, kama ifuatavyo:-

Kwanza nishukuru kupata taarifa kwamba kule kwenye kijiji kile ulichokitaja ambacho kwa sasa nimesahau jina ulilolitamka kwamba ile zahanati iliyojengwa kwa ushirikiano wa Serikali na wananchi sasa haitumiki kama ilivyokusudiwa na badala yake mtendaji wa kijiji au Serikali eneo lile wameamua kufanya ghala la mifugo. Kwa taarifa hii kwa kweli ni ya kusikitisha, kama Mkurugenzi wa Halmashauri anaisikia kauli hii sasa hivi aende aondoe mifugo hiyo na eneo hilo likarabatiwe na huduma za afya zirejeshwe ahamishe watumishi kutoka *dispensary* nyingine wapelekwe pale waendelee kutoa huduma na vifaa vipelekwe ili eneo lile wananchi wawzeze kunufaika. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. VITA RASHIDA MFAUME KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imetujengea Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo na phase ya kwanza imekamilika lakini tuna upungufu wa watumishi wa ngazi ya Hospitali ya Wilaya. Je, Serikali iko tayari kutuletea watumishi wa Hospitali ya Wilaya?

**SPIKA:** Hapo swali ni upungufu wa watumishi lakini habari ya Namtumbo yeye hakujandaa hivyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Kama ambavyo nimesema kupitia jibu la nyongeza la Mheshimiwa Cynthia Ngoye, Mbunge Viti Maalum Mbeya, kwamba Wizara ya Afya ndio inashughulikia na ajira na hasa kuomba kibali cha ajira na kwa bahati nzuri mwaka wa fedha wa 2011/2012 iliweza kupata kibali cha ajira cha watumishi 9,000 lakini kwa bahati nzuri sana pia kufikia mwezi Mei mwaka huu, watumishi walipata nafasi ya kuajiriwa na wale 5600 bado Wizara ya Afya ina nafasi ya watumishi 34000 ili kuweza kuajiri na kuweza kuapeleka maeneo mengine. (*Makofî*)

Labda Mheshimiwa Mbunge, ulikuwa unapenda kujuu kama je, watumishi hawa watakwenda pia Namtumbo? Nataka nikuhakikishie kwamba kati ya hawa 3400.

Kwa mujibu wa sekretarieti ya Mkoa iliyotoa taarifa ya upungufu wa watumishi kwenye sekti ile watakapoajiriwa mgao utakapokuwepo itakuwemo pamoja na Namtumbo. (*Makofî*)

Na. 236

#### Fidia kwa Wananchi wa Mbagala na Kongowe

**MHE. DKT. HAMIS KIGWANGALLA (K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE)** aliuliza:-

Baadhi ya wakazi wa Mbagala na Kongowe walibomolewa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara wa Kilwa na wamekuwa wakitaabika kutafuta haki yao:-

- (a) Je, Serikali inatambua uwepo wa kikundi hiki?
- (b) Je, watu hawa watalipwa lini fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa wananchi wanaodai kulipwa fidia kutokana na nyumba zao zilizokuwa zimejengwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara ya Kilwa kubomolewa kwa mujibu wa sheria ya namba 167 ya mwaka 1967.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nyumba hizi zilijengwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara na hivyo kukiuka sheria ya barabara namba 167 ya mwaka 1967 watu hawa hawastahili kulipwa fidia. (*Makof*)

**MHE. DKT. HAMISI KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa niaba ya Mheshimiwa Ndugulile...

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kigwangala ulilouliza kwa niaba ni lile swalii la msingi haya mengine ni ya kwako.

**MHE. DKT. HAMISI KIGWANGALLA:** Sawa ya kwangu sasa.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa madai ya wananchi hawa ni ya kweli na Serikali haijatoa msimamo wake . Je, Serikali sasa iko tayari kutoa msimamo huo leo hii?

(b) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Dkt. Shukuru Kawambwa aliyepita katika Wizara hii alikuwa ameyakubali. Je, Serikali inatekeleza lini madai hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi ni kwamba watu hawa waliokuwa wanadai fidia wakati wako ndani ya hifadhi ya barabara. Kwa hiyo, kwa mujibu wa sheria hii ambayo Bunge hili limepitisha hawastahili kulipwa.

Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na kauli mbili kwamba tutatoa kauli hapa leo kwamba watalipwa wakati wamevunja sheria. Nirudie tena kusema kwamba mtu ye yote ambaye amejenga ndani ya hifadhi ya barabara tunasema mita 45 yaani mita 22.5 kila upande kwa sheria ya zamani na imerekebishwa mwaka 2007 ni mita 60 kwa hiyo, mita 30 upande mmoja na mita 30 upande wa pili na tumeweka alama nyekundu kuonyesha kabisa kuwa wewe uko ndani ya hifadhi na hustahili kulipwa.

Yule aliywewkewa alama ya kijani tunamjulisha kwamba hii sheria imerikeshishwa imeongezwa upana kwa hiyo, ni kumpa taarifa kwamba uko ndani ya hifadhi ili usifanye maendelezo na sheria itaangalia utaratibu wa kuweza kuwalipa.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ninalo swalii la nyongeza, Mheshimiwa Waziri je, kama unasema Serikali haiyatambui madai hayo kwa nini Serikali ya Mkoa wa Dar es Salaam inaweka kamati maalum ya kuhakiki madeni haya na hii kamati inatumia ghamama kubwa kwa nini sasa hili suala hawalitupili mbali kama wewe unaongea kwamba hili suala haliko katika utaratibu wa kulipwa? Lakini pia Mheshimiwa Waziri kama kweli Serikali....

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisanga swalii moja. (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisanga, kama ifuatavyo:-

Kama kuna mtu anadai na sisi wanasiwa ni lazima tuwaelimisha wananchi, kama wananchi wanadai lazima twende tuhakiki, kweli wanachokisema ni sawa sawa ili kila mmoja

pande zote mbili ziridhike, kama mtu yumo ndani ya hifadhi mridhike kwamba hawezi kulipwa, lakini kama yupo ndani ya hifadhi ili hiyo kamati pia iseme hawa watu ndani ya hifadhi waweze kulipwa.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa kuna mradi wa ujenzi wa barabara ya Dodoma, Mtera mpaka Iringa unaoendelea na kwa kuwa kuna baadhi ya wananchi walibomolewa nyumba zao kufidia ujenzi huo je, mpaka sasa hivi wananchi hao wameshalipwa?

**SPIKA:** Atajuaje hilo swali halikuwepo kwenye *original*. Mheshimiwa Waziri kwa sababu anajua masuala yote basi anataka kujibu lakini halikuwa swali la msingi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kabati kama ifuatavyo, barabara ya Dodoma hadi Iringa yenyenye jumla ya kilomita 261 ina makandarasi watatu wanaoshughulika kujenga kwa kiwango cha lami.

Kwa mujibu wa sheria ambayo siku zote tumekuwa tukisisitiza imeanza tangu mwaka 1932 ikafanyiwa mabadiliko katika miaka iliyofuata. Lakini kupitia pia *Cap. 167* ya mwaka 1968 na ikafanyiwa mabadiliko pia kupitia sheria namba 13 ya mwaka 2007 lakini pia kwa mujibu wa sheria za ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na sheria ya vijiji ya ardhi namba 5 ya mwaka 1999 kifungu namba 3 (g) wale wote walio ndani ya hifadhi ya barabara hakuna fidia.

Hii ni kwa sababu sheria imepitishwa na barabara haijengwi juu ya nyumba, barabara inajengwa katika eneo lilitambulika kwa mujibu wa sheria. Lakini wale ambao wako nje ya *road reserve* kwa barabara ya kutoka Iringa kuja Dodoma kwa maana nyingine wako nje ya mita 30 wale watalipwa fidia. Walio ndani ya mita 30 hawatalipwa fidia. Narudia hawatalipwa fidia. (*Makofii*)

**SPIKA:** Amewajibu wote wanaohusika na fidia.

Na. 237

#### Barabara ya Lami Kidatu – TAVETA

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE RWAKATARE** aliuliza:-

Je, Serikali itatekeleza lini ujenzi wa barabara ya lami kutoka Kidatu – Taveta?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kidatu – Taveta yenyenye urefu wa kilometra 278 ni barabara kuu na inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Mkoa wa Morogoro. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kidatu – Ifakara – Taveta umekuwa ukitekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha kama ifuatavyo:-

- (i) Ujenzi wa kilomita 10 za lami kutoka Kiberege (Magereza) hadi Ziginali ulikamilika mwaka 2006;

- (ii) Ujenzi wa kilometra 6.17 za lami kutoka Kibaoni (Ifakara) hadi Ifakara Mjini ulikamilika mwaka 2008;
- (iii) Ujenzi wa kilometra 24 za lami kati ya Kihansi na Mlimba ulikamilika mwaka 1999;
- (iv) Usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Ifakara (Kibaoni) hadi Ziginali (Km 16.8) ulikamilika mwaka 2010/2011. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi;
- (v) Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa sehemu ya barabara ya Ifakara hadi Kihansi yenye urefu wa kilometra 126 umepangwa kuanza mwaka 2013/2014; na
- (vi) Sehemu Mlimba – Taveta yenye urefu wa kilometra 54.5 itaendelea kufanyiwa matengenezo kwa kiwango cha changarawe kulingana na upatikanaji wa fedha ili iweze kuitika kwa urahisi majira yote ya mwaka.

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, nilikuwa na maswali mawili madogo kwa ajili ya swali hili:-

(a) Tumechoka na majibu ya mkato, upembuzi yakinifu umekamilika wakati bado. Mimi nilikuwa naomba kwa sababu Waziri wa Ujenzi Dkt. Magufuli ni msikiu, mahiri, mkakamavu. Tukimaliza Bunge, twende naye niwaonyeshe madaraja ya barabara hii yote ni ya *temporary*. Barabara nzima ni ya *temporary* kama vile Wilaya ya Kilombero ni ya *temporary*, sisi ni Wilaya ya kudumu kama Wilaya zingine, tunaomba barabara za kudumu za lami.

(b) Mimi tangu nimekuwa nasoma *primary* darasa la tano, barabara hii imekuwa barabara ya vumbi mpaka sasa hivi. Kila Waziri anatuahidi. Sasa hivi imesogezwa mpaka 2014. Je, atawaambia nini wananchi wa Kilombero? Mimi nashindwa niwaambie nini. Anisaidie Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Getrude P. Rwakatare, kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza naomba Mheshimiwa Rwakatare usichoke tunapotaja upembuzi yakinifu. Ukishaona barabara inafanyiwa upembuzi yakinifu maana yake Serikali imekubali kujenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, ni hatua. Kwa hiyo, ningekupongeza kwanza usichoke na ujipongeze kwamba umefuatilia kwa bidii.

(b) Ni kweli barabara ile ni ya vumbi na kama tunavyosema, tunazo barabara nyingi, lakini tumeshaanza kuzitekeleza na barabara hii tayari tunaposema tunaanza upembuzi yakinifu maana yake tumeikubali na tutaanza kutekeleza katika mwaka wa fedha 2013/2014.

**MHE. LOLENSIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipokuja Nyarugusu mwaka 2010, aliahidi barabara ya lami kutoka Geita mpaka Kahama na kutoka Katoro mpaka Bukombe. Ningependa kuuliza sasa ni lini ahadi hizi zitaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Lollesia, hilo swali jipya kabisa. Naomba sana mwelewe mnapouliza swali jipya kabisa hapa tunafanya udanganyifu tu hapa wa majibu. Sababu Waziri wenyewe wanajua barabara zote jibu lakini nisingependa hivyo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swalii la nyongeza ya Mheshimiwa Lolensiwa Bukwimba kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa sisi tumeshasema ahadi za Rais ni katika kipindi cha miaka mitano na sisi tutazifanyia kazi hizo barabara. Utaratibu lini barabara hizo ambazo Rais alizagiza kulingana na upatikanaji wa fedha tuweze kuanza kutekeleza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mangungu, sio barabara ya Kilwa tena. (*Makofî/Kicheko*)

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ningependa nimwulize swalii la nyongeza kwamba wakati tunawasilisha Bajeti ya Wizara ya Ujenzi hapa tuliiomba Serikali ituainishie ni lini itatekeleza mpango wa ujenzi wa barabara za lami katika maeneo husika ikiwemo barabara ya kutoka njia nne Kipatimo na Dundu Samanga?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti yetu ya mwaka 2012/2013, tulainisha miradi yote ambayo itatekelezwa katika kipindi cha mwaka huu lakini pia katika llani ya Uchaguzi kuanzia ukurasa wa 72 hadi wa 83 umeainisha barabara zote zitakazotekelawa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2010 hadi 2015.

Na. 238

#### **Wachimbaji Wadogo Wadogo- Mavota na Lusahunga**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA (K.n.y. MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imewasaidiaje wachimbaji wadogo wadogo Kata ya Mavota na Lusahunga ili kupata zana za kuchimbia ikiwa ni pamoja na kutengewa maeneo maalum?

(b) Je, ni athari zippi kimazingira zimesababishwa na wachimbaji hao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Anthony Gervas Mbassa, Mbunge wa Bihamarulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, eneo la Lusahunga linajumuisha Kata za Nyakahura, Nyakatanga na Kinyiha. Katika Kata hizo uchimbaji usio rasmi unafanyika katika maeneo ya Busili na Ngazi Saba katika Kata ya Nyakahula; na maeneo ya Mavota na Matwiga yaliyoko katika Kata ya Kinyiha. Zaidi ya wananchi 1000 wanakadiriwa kuendesha shughuli za uchimbaji katika maeneo hayo ambapo kuna leseni za utafutaji mkubwa wa madini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imebainisha eneo la Busili lenye hekta 250 na eneo la Ngazi Saba lenye hekta 420 na tayari utaratibu umeshaanza wa kuyatenga maeneo hayo ili yawe maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Eneo la Busili lina ombi la leseni kubwa; eneo la Ngazi Saba linamiliikiwa na kampuni ya *Meru Minerals Resources* yenye leseni ya utafiti madini Na. 5853/2009; eneo la Matwiga linamiliikiwa na kampuni ya *Pangea Minerals* yenye leseni ya utafutaji madini Na. 6141/2009.

Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010, leseni zote hizo muda wa awali unaisha mwaka huu na kutakiwa kurejeshwa nusu endapo zitahitaji kuhuishwa. Utaratibu huu utawezesha kupatikana kwa maeneo mengi zaidi kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya taratibu za kuyatenga kukamilika na kuwamilikisha wachimbaji wadogo na kuanza kuchimba kwa mujibu wa Sheria, wachimbaji kwa vikundi/ushirika watasaidiwa vifaa vya kisasa, huduma za ugani, mafunzo mbalimbali ya ujuzi na maarifa ya uchimbaji madini ili uchimbaji wao uwe wenye manufaa zaidi.

Huduma hizo zitatolewa na Wizara katika utaratibu wa kutekeleza mikakati ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo ambayo itatekelezwa kwa kushirikiana na *STAMICO*, Taasisi za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Madini-Dodoma na Wakala wa Jiolojia Tanzania (*GST*).

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli zipo athari za mazingira zilizojitekeza kutokana na uchimbaji usio rasmi katika maeneo ya Busili na Ngazi Saba katika Kata ya uchimbaji usio rasmi katika meneo ya Busili na Ngazi Saba katika Kata ya Nyakahula na maeneo ya Mavota na Matwiga katika Kata ya Kinyiha.

Athari hizo ni pamoja na kuwepo kwa mashimo mengi yaliyoachwa wazi bila kufunikwa; kuwepo kwa ukataji wa miti hovyo na kusambaa kwa kemikali aina ya zebaki (*mercury*) katika mazingira kutokana na shughuli za uchenjuaji dhahabu zinazofanyika bila kuzingatia taratibu sahihi na salama za matumizi ya zebaki katika uchenjuaji.

Serikali inaendelea kudhibiti athari hizi kwa kupitia wakala wa ukaguzi wa madini (*TMAA*), Kitengo cha Mazingira na sehemu ya Ukaguzi wa Migodi zilizopo chini ya Wizara kwa kutoa elimu juu ya athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa wachimbaji wadogo katika nchi yetu ni watu masikini na kwa kuwa sasa kupitia majibu ya Waziri Serikali imeona kwamba ni muhimu kuwatengea wachimbaji wadogo maeneo yao na kwa kuwa wananchi wale wanayahitaji maeneo haya:-

(a) Naomba Waziri aniambie kwamba haya anayoahidi sio maneno atupe muda maalum wachimbaji wadogo wadogo wajue ni lini watapewa maeneo?

(b) Kwa kuwa wachimbaji wadogo wadogo katika nchi yetu wananyanyaswa na wakati mwingine kuporwa mali zao. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka sasa wachimbaji hawa kulipwa fidia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Conchesta, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ahadi hii ya kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo sio ahadi hewa na tayari Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine wasubiri kwenye Bajeti yetu tumeainisha maeneo ambayo tumeyatenga na tumetenga fedha kwa ajili ya kukamilisha zoezi hilo. Maeneo yote haya tutawawekea katika *pigeon hole* Wabunge wote waweze kuona pamoja ikiwemo na ramani za nchi yetu yote, maeneo yote yenye leseni na maeneo ambayo hayana leseni.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la kulipa fidia kwa wachimbaji wadogo, kumekuwa na tatizo la kufahamu namna Sheria ya Madini inavyofanya kazi na wananchi wengi wanaomiliki maeneo kwa Sheria za Vijiji, wanadhani kwamba ndiyo tayari uhalali wa kuwa na leseni ama kuendesha shughuli za uchimbaji. Kwa Wizara tumejipanga kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi waweze kuelewa kwamba kumiliki eneo la Kijiji ama shamba haitoshi kukupa uhalali wa kuchimba na bado unahitaji kuomba leseni ya uchimbaji ambazo Wizara inatoa kupitia ofisi zetu za Kanda hapo ndiyo utapata uhalali wa kuchimba kwa kutumia leseni. (*Makofii*)

Sasa migogoro mingi imejitoneza kwamba wananchi kwenye mashamba yao wanapoambiwa kuna mtu ana leseni, inakuwa ni ugomvi kwamba huyu mtu amepataje leseni na

hili eneo ni la kwetu la muda mrefu. Kwa hiyo, pia haimzui mtu mwingine kuomba leseni katika eneo lolote lile ambalo linamilikiwa na wanakijji. Kwa hiyo, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuelewa nini maana ya leseni na nini maana ya kumiliki mashamba.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Maeneo mengi ya Tanzania ambapo wachimbaji wadogo wadogo wanachimba bado hayakufanyiwa *environmental impact assessment* ukiacha ile migodi mikubwa na kwa kuwa wananchi wengi sasa wanachimba na kwa kuwa hawana uwezo wa kufanya hiyo kazi ya kutunza mazingira.

Je, Serikali kwa nini katika mpango wake wa kuwamilikisha maeneo haya isifanye vile vile *environmental impact assessment* kabla ya kuwakabidhi hayo maeneo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye jibu langu la msingi, nimeeleza kwamba katika maeneo ambayo Serikali wale wenye leseni za utafiti watakapotaka kuzihuisa watapaswa kuachia eneo nusu. Sasa nimeeleza katika swalii la msingi kwamba Serikali kuptitia Wizara Kisheria inairuhusu kukaa na eneo hilo kwa kipindi cha miezi mitatu mpaka minne ili kuangalia uwezekano wa kuwapa *either wachimbaji wadogo wadogo au kama hilo eneo linafaa kwa uchimbaji mkubwa*.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, Kamishna wa madini ndipo anapofanya kazi ya kutathmini taratibu zote za kimazingira kuptitia wakala wetu wa jeolojia na kabla ya kuwapa wachimbaji wadogo. Kwa hiyo, nimuhakikishie tu Mheshimwa Mbunge kwamba kazi hiyo tunaifanya kuptitia wakala wetu wa jeolojia. (*Makofi*)

Na. 239

#### **Mradi wa Umeme Kupitia MCC Vijiji vya Kondoaa Kaskazini**

**MHE. ZABEIN M. MUHITA** aliuliza:-

Taarifa ya miradi inayofadhiliwa na MCC Jimbo la Kondoaa Kaskazini imejumuisha Vijiji vitatu vya Pahi, Kolo, Mnenia na kuacha Kijiji cha Kingale na gereza la King'anga'a:-

- (a) Je, miradi hiyo itaanza lini na imetengewa fedha kiasi gani?
- (b) Je, kwa nini Kijiji cha Kingale na Gereza la King'ang'a havikuorodheshwa wakati vilikuwapo katika mpango wa awali?

#### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zabein Muhaji Muhita, Mbunge wa Kondoaa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, miradi inayofadhiliwa na MCC katika Mkoa wa Dodoma tayari imeshaanza tangu mwezi Juni, 2011 katika Wilaya za Dodoma Mjini, Kongwa, Mpwapwa, Bahi, Chamwino na Kondoaa. Miradi hiyo inajumuisha mradi wa kupeleka Umeme katika Vijiji vya Pahi, Kolo na Mnenia.

Miradi hii inahusisha ujenzi wa njia ya Umeme yenye msongo wa kilovolti 33 yenye urefu wa kilometra 35; ujenzi wa laini za usambazaji umeme zenye msongo wa KV 0.4 zenye jumla ya kilometra 14. Katika utekelezaji wa mradi huu asilimia 8.74 ya nguzo za msongo wa KV 33 na asilimia 86.56 ya msongo wa KV 0.4 zimesimamishwa.

Utandazaji wa waya utaanza baada ya kukamilisha kazi ya usimamishaji wa nguzo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2012.

(b) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Kingale na Gereza la King'ang'a tayari vipo katika orodha ya miradi inayofadhiliwa na Serikali kuitia mfuko wa Wakala wa Nishati Vijiji ni itakavyoanza kutekelezwa mwaka wa fedha 2012/2013. (*Makof*)

**MHE. ZABEIN M. MUHITA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa majibu mazuri ambayo yameleta matumaini kwa Vijiji nilivovizungumzia. Lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu huu wa *MCC* unapita Tandala ambako ni kilomita 5 tu mpaka Kijiji cha Busi. Je, Serikali in ampango gani wa kufikisha Umeme katika Kijiji hiki cha Busi?

(b) Vile vile kwa kuwa mradi huu wa *MCC* tayari utafika katika Kijiji cha Kolo na Kijiji cha Kolo kiko karibu sana na Vijiji vya Wisi kwa Ntisi, Kwadinu, Bukulu, Masawi na Bereko viko karibu sana na viko kando kando ya barabara. Mheshimiwa Naibu Waziri anapafahamu.

Je, Serikali nayo haiyoni umuhimu wa kupeleka Umeme katika Vijiji hivi? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zabein Muhaji Muhiita, kama ifauatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Zabein Muhiita kwa namna ambavyo anafuatilia sana masuala ya Umeme katika Jimbo lake.

Nadhani ameshakuja kwangu karibu mara tatu. Lakini swalilake la kwanza anataka kujua kwamba je, katika mradi huu wa *MCC* ambao utaishia umbali wa kilomita 5 na Busi.

Mimi niseme tu kwamba kwa hali ilivyo na dhamira hii njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba tunapeleka Umeme Vijiji sio rahisi sana tukaweza kupeleka katika maeneo yote kwa mara moja.

Kwa hivyo, nitakachowenza kufanya tu hapa ni kwamba nitajitahidi tuweze kuona, tuwasiliane na Meneja wetu wa Kondo, tuweze kuona unapoishia mradi wa Jimbo la Mheshimiwa Nkamia wa *MCC* *ni distance* kiasi gani na hadi Busi kwa sababu kwa hali ilivyo kwa hapa siwezi nikajibu chochote kile mpaka njiridhishe na hali ilivyo kwenye *site* kutokana na mradi ule unaoendelea wa *MCC*. (*Makof*)

(b) Lakini na pili ni Vijiji vya Wisi kwa Ntisi na Bereko. Nikiri kwamba naifahamu Bereko ilipo na nikiri kwamba ni mahali ambapo panastahili kuwa na Umeme. Lakini kama nilivoyosema napo panahitaji pia njiridhishe tuweze kuona ni *distance* kiasi gani, kwa sababu ukisema Bereko sasa ni karibu na Babati. Sasa tujaribu kuona tunaweza tukafanya nini.

Mimi nimwahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tujaribu kuwasiliana tuone tunaweza tukafanya nini kwa sababu *option* zile tukijadiliana na wewe zinaweza zikawa bora zaidi na wananchi wakaweza kunufaika na matunda ya umerme Vijiji. (*Makof*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri amejibu na eneo langu naomba nisilize swalilake la nyongeza, lakini nawapongeza sana kwa kujali Wilaya ya Kondo na Chemba. (*Makof*)

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Naomba kuiuliza Serikali kwa sababu muda mwengi watu wengi wamekuwa wakiongelea kuhusu habari ya Vijiji.

Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba Makao Makuu ya Wilaya zote mpya Tanzania pamoja na zile za zamani ambazo hazijapatiwa umeme zinapata Umeme kabla hatujaenda kwenye Viji? (Makof)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kandege anataka kujua kama sisi tuna mpango gani, sisi Serikali ya kupekela umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya zote. Katika Bajeti yetu ya mwaka 2012/2013 ambayo tutaiwakilisha wiki ijayo.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie kwamba tumejaribu kuzingatia sana na hilo jambo lina kipaumbele sana kwetu kuhakikisha kwamba Wilaya zote, Makao Makuu ya Wilaya zote zinapata Umeme.

Kwa hivyo, niombe tu ushirikiano wa Waheshimiwa Wabunge katika kuhakikisha kwamba Bajeti ya Wizara yetu inapita ili haya ninayoyasema ya kupeleka Umeme katika Makao Makuu zote za Tanzania yawewe kutekelezwa. Ahsante sana.

Na. 240

#### **Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Kufungwa**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE)** aliuliza:-

Kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools*, ambacho zamani kilikuwa kinazalisha vipuri na kutoa ajira, kimefungwa kwa muda mrefu:-

(a) Je, Serikali, imetumia kiasi gani cha fedha na watumishi kutunza kiwanda hicho tangu kimefungwa?

(b) Je, ni nini tathmini ya thamani ya kiwanda kwa sasa?

(c) Je, Serikali, ina mpango gani kuzuia uchakavu na upoteaji wa kiwanda hiki na mazingira yake?

#### **NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Bisahara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mbunge wa Hai, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali, imetumia jumla ya 361,105,009/= hadi sasa kwa ajili, ya kutunza Kiwanda cha *Machine Tools Co. Ltd. (KMT)* na kina Watumishi sita (6) waliobaki. Aidha, mwaka 2008, *NDC* ilipokabidhiwa kiwanda, walikuwepo watumishi wanane (8).

(b) Mheshimiwa Spika, tathmini ya kiwanda kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

Mashine na Mitambo ni	-	3,279,133,000/=
Majengo ni	-	5,162,000,000/=
Ardhi ni	-	3,050,000,000/=
<b>Jumla</b>	<b>-</b>	<b>11,491,133,000/=</b>

(c) Mheshimiwa Spika, kiwanda kwa sasa ni muhimu kwa maendeleo ya Sekta ya Viwanda na Sekta nyingine za Kiuchumi nchini. Hivyo, Serikali, inaendelea kuyaweka majengo na mazingira yake katika hali nzuri na ya kuvutia wawekezaji.

Hii ni pamoja na kufanya ukarabati wa majengo ya kiwanda. Kwa sasa, ukarabati unafanyika kwa awamu ambapo, awamu ya kwanza ya kukarabati majengo ya utawala imekamilika. Awamu ya pili itakayohusisha majengo ya karakana yenye mashine na mitambo mingine, itafanyika mara fedha zitakapopatikana. Mashine na mitambo ya kiwanda hiki, ziko katika hali nzuri kwani, wafanyakazi wachache waliopo, wameendelea kuhakikisha kuwa, mashine zinafanyiwa uangalizi wa kiufundi (*maintenance*) wa mara kwa mara (*regular maintenance*) na mitambo kuzungushwa pale inapobidi. (*Makof*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali inakiri kwamba, kiwanda hiki ni muhimu kwa uchumi wa nchi. Na kwa kuwa, mashine pamoja na mitambo vyote vinafanya kazi. Ni kwa sababu, gani Serikali, isione umuhimu wa wa kuendesha hiki kiwanda yenewe badala ya kupoteza muda kusubiri mwekezaji ambaye haijulikani atapatikana lini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, eneo, kwa maana ya ardhi linalozunguka kiwanda ni kubwa sana. Kwa nini Serikali, isione umuhimu wa kuligawa hilo eneo, ili sehemu yake iweze kutolewa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, ili Halmashauri, iweze kutafuta Wawekezaji kwa maana ya wajasiriamali, watakaoanzisha viwanda vidogovidogo, eneo hilo liweze kupata matumizi badala ya kukaa jinsi liliyo, kwa faida ya uchumi wa Wilaya ya Hai na wa Taifa kwa ujumla?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Bisahara, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa lile swali la kwanza kwamba, ni kwa nini Serikali, isione umuhimu wa kuendesha yenewe kiwanda hiki?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, mashine za kiwanda hiki ambacho kilianza mwaka 1984, kwa kweli, zilishapitwa na wakati. Sasa hivi, Serikali, ina mkakati, kupitia *NDC*, baada ya *NDC* kukabidhiwa kwamba, mashine zile sasa angalao lile eneo muhimu la kuyeyusha chuma ambazo zingetumiwa kama malighafi ya kiwanda, liweze kupatiwa msaada wa pesa. Kupitia *NDC* sasa hivi, mkakati unafanyika, ili kuweza kukopa sehemu ya pesa, ili tuweze kufufua sehemu ile ambayo ni ya *laundry*, ambayo tunaweza kuyeyusha chuma, kwa ajili ya kupata malighafi ya kiwanda chenyewe. Kwa hiyo, mkakati huo upo na Serikali, inatambua hilo.

Mheshimiwa Spika, na kuhusu swali la pili la eneo, kwamba, eneo ligawiwe sasa. Ni kweli, kwamba, eneo la *Machine Tools* lina upana au ukubwa wa hekta 250 hivi. Kwa hiyo, sasa hivi mkakati unafanyika wa kuweza kulipima hilo eneo liwe *industrial Estate*, kama ilivyo sehemu nyingine. Kule Kibaha, kuna sehemu ya *TAMCO* pale, nalo lina mkakati huu huu wa kuweza kupimwa na kuweza kugawia wananchi sehemu za kufanya viwanda vidogovidogo. Sehemu hii ya *Machine Tools* kwa sababu, ya hekta 250 hizo tunao utaratibu wa kuzipima, ili baadaye ziwe *Industrial Estate*, ziweze kutumika kama viwanda vidogo vidogo. (*Makof*)

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza swali moja dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, viwanda vingi nchi hii vilikufa. Na vilipokufa vikafungwa. Wakati vinafungwa vilikuwa vinadaiwa pesa nyingi na wafanyakazi ambaa walikuwa wakifanya kazi, kwa mfano kiwanda cha *General Tyre* kule Arusha. Na kwa sababu, sasa Serikali, ina mkakati wa kufufua hivi viwanda, ningependa pia kujua, Je, wana mkakati gani kuhakikisha kwamba, wale wafanyakazi waliokuwa wanadai fedha zao wanalipwa kwanza madai yao ya awali, kabla hata ya kuvifufua? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Serikali, sasa hivi ina mkakati wa kuweza kufufua viwanda vyote ambavyo vilikuwa vinazalisha huko nyuma, lakini azma ya Serikali, ni kwamba, hatuwezi kufufua kiwanda bila kwanza, sisi wenyewe kukaa na kujiridhisha kwamba, kwa nini kiwanda kile kilikufa hapo awali. Kwa sababu, unaweza kuchukua mzigo ambaa haubebeki.

Mheshimiwa Spika, na suala la kusema kwamba, wale watumishi waliokuwa wanafanya pale kazi, fidia yao inakuwaje?

Mheshimiwa Spika, Serikali iko makini na inategemea kwamba, kiwanda kilichokuwa kimebinafsishwa na sasa hivi kinafufuliwa, mafao ya wale watumishi waliokuwa wanafanya kazi pale, kama stahiki zao kama ni sahihi, wanalipwa kama kawaida. Kutegemea na hali ya kiwanda ilivyoachwa.

Na. 241

#### **Uuzaji wa Mahindi – Mkoa wa Rukwa**

**MHE. ABIA M. NYABAKARI** aliuliza:-

Wakulima wa Mahindi wa Mkoa wa Rukwa, huuza mahindi yao kwenye maghala ya vijji, lakini kwenye baadhi ya maghala, watumishi wakishayapima mahindi, kama hakuna pesa za kuwalipa wakati huo, huwaambia wakulima wayaache Mahindi mpaka pale pesa itakapopatikana watalipwa bila kuwapa *document* yoyote:-

- (a) Je, huu ni utaratibu wa Serikali, kubaki na mali ya mtu bila maandishi yoyote?
- (b) Je, endapo kwa bahati mbaya ghala likaungua, moto na mali za wakulima kuteketetea, ni nani atawajibika kuwalipa wakulima hao fidia?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshiniwa Abia Muhamma Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kununua mahindi kutoka kwa wakulima, hufanyika baada ya tathmini ya kina kubaini maeneo yenye ziada ya mahindi yenye ubora unaohitajika. Wakala, kuititia Kanda zake za Manunuzi, hufanya uchunguzi, tathmini na ufuutilaji wa mara kwa mara, kubaini hali ya uzalishaji, kiwango cha unyevunyevu, kwa maana ya *moisture* kwenye mahindi na bei za soko zikilinganishwa na gharama za uzalishaji kwa mkulima. Ununuzi wa mahindi, hufanyika kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha, vitendea kazi kama magunia na dawa za kuhifadhia mahindi, pamoja na uwezo wa kuhamisha mzigo. Wataalam wa Wakala, hukagua ubora wa mahindi na kupima uzito, na baada ya upimaji kukamilika, Muuzaji/Mkulima, anapaswa kupewa stakabadhi.

Mheshimiwa Spika, inatokea wakati mwininge wakulima wanapofikisha mahindi Kituo cha Mauzo, inawachukua muda mrefu kabla mahindi yao hayajakaguliwa na kupokelewa ghalani. Hali hii inatokana na uwezo wa ununuzi na uhifadhi wa mahindi katika Kituo husika. Mahindi yote ambayo hayajapokelewa na Wakala na kuhifadhiwa, bado yanakuwa mikononi mwa Mkulima husika. Kufuatia hali hiyo, iwapo kutatokea msukosuko wa aina yoyote ile kama wizi, moto au mvua, Wakala hauwajibiki kulipa fidia kwa kuwa, mzigo huo unakuwa bado haujawa mali ya wakala.

Mheshimiwa Spika, nawashauri Wakulima, kuhakikisha wanapewa Stakabadhi, ambayo inaitwa *GRN* (*Good Received Note*), wanapoacha mahindi yao katika maghala ya *NFRA*, ili iwe rahisi kudai, mara uharibifu au upotevu unapotokea. Kwa maana hiyo, ninawaagiza Mawakala, Maafisa wa *NFRA* wahusika, waache utaratibu pale ambapo unatumika, wa kupokea mahindi bila kutoa *GRN*.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Mkulima huyu wa Rukwa, aliyechoka, anapopeleka mahindi yake, ili auze anaambiwa kwanza, alipe 1,500/= mpaka 2,000/= kwa ajili, ya upimaji na kwa ajili ya kupanga *steak* ile. Akiangalia kwamba, ametoka mbali, pengine amelipa 2,000/=, sasa je, swalii langu linakuja; Serikali, iko tayari kuwaruhusu hawa Wakulima, wenyewe nguvu kazi, ili wapime mahindi yao wao wenywewe?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa, Mkao wa Rukwa, kuna baadhi ya maghala ambayo, sasa hivi hayafanyi kazi na mengine pia, hayajamalizika.

Je, Serikali, iko tayari kukarabati maghala hayo? Na kumalizia maghala haya mengine, ili kuepusha usumbufu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Abia Nyabakari, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nilikuwa nataka kusema yafuatayo; pale kwenye kila Kituo, panakuwa na Watumishi watatu. Panakuwa na Afisa Ugani, panakuwa na Mtaalam wa Kupima na kuangalia ule ubora wa nafaka na panakuwa na Mhasibu. Kwa kawaida, anatakiwa Mkulima, anapofika pale na mahindi yake apime aondoke. Sasa kama panatokea pana tatizo, labda kwamba, pana uwingi wa watu au pana matatizo kidogo, labda fedha haijafika, na kadhalika, ndio tunaona kuna matatizo kama haya.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu, hivi ninavyozungumza, tayari Waziri wa Kilimo, ameagiza kwamba, utaratibu ufanyike, ili wale wakulima wanapopeleka mahindi hivi sasa, waachane na huu usumbufu; nimecha sijui 1,500/=, 2,000/= huu utaratibu tunaufanyia kazi, hautakiwi kuwepo. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Wakulima wa Tanzania, kwamba, tunataka wakifika pale wapewe pesa waondoke. Labda iwe ni matatizo kama labda wakiwa wengi, na kadhalika. Uwezo tulioweka ni kwamba, japo wafikie tani 200 kwa siku, ambayo ni mzigo mkubwa kusema kweli wa pesa na kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, sikulisikia vizuri. Amesema?

**SPIKA:** Kasema, kuna maghala kule, ambayo hayajaisha ukarabati wake?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Sumbawanga kwa maana ya Kanda ile, ina maghala matatu (3), kuna maghala Mpanda, Laela na Sumbawanga yenywewe. Kule kwingine, kuna Vituo Vldogo ambavyo mwaka jana vilikuwa 14, tumeongeza nadhani kama Vituo vitatu (3) kwa sasa hivi, viko Vituo 17 au 17.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kusema kweli na Vituo vile, vinawekwa kulingana na uwezo wa uzalishaji kwenye yale maeneo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Abia, kwamba, mpaka sasa hivi, hatujaona tatizo la *efficiency* kwenye kukusanya mazao. Tatizo lililokuwepo, labda ni upatikanaji wa fedha kwa sababu, ya uwingi wa mahindi yanayopatikana. Na hilo, tunalifanyia kazi. (*Makofii*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, ni kwa nini Serikali, haitaki kuingiza pato linalotokana na uuzwaji wa mahindi katika Mkao wa Singida? Ahsante sana.

**SPIKA:** Naomba urudie tena swali.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naiuliza Serikali, ni kwa nini, haitaki kuingiza pato linalotokana na uuzwaji wa mahindi katika Mkao wa Singida, kwenye pato la Mkao? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu Swalii la Nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hili, hata juzi wakati tunaanza taratibu za kuhitimisha Makadirio ya Wizara, tulikuwa tumejibu swalii hilo.

Mheshimiwa Spika, takwimu za uzalishaji wa mahindi kwa kila Mkao, hazianzii kwenye Serikali Kuu, zinaanzia Mikoani kwenyewe. Kwa hiyo, wao wenyewe ndio wanaanza kwenye Halmashauri, wanaleta Wilayani na sisi tunapokea Taarifa za kila Wilaya, zinazosema kwamba, labda Mkao wa Singida, una uzalishaji wa mahindi wa tani kadhaa, ambao unatokana na Wilaya zake kadhaa, kadhaa, kadhaa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nimwahidi tu Mheshimiwa Martha Mlata, kama nilivyojibu Jumamosi, kwamba, mahindi yakiwa yanazalishwa Singida, kwetu ni vizuri. Kwa sababu, tukiwa na takwimu hiyo, tunajua kwamba, kwa Kanda ile, tunakabiliana na mahitaji ya mahindi na mtama na tunaweza ku-*balance* mahitaji hayo kwa ajili ya kukabiliana na shida ya njaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimjibu kama nilivyomwahidi juzi, kwamba, tunalifanya kazi pamoja na utawala wa Mkao, ili tupate takwimu sahihi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa, gharama za uzalishaji katika kilimo zimepanda. Je, Serikali, inatoa bei elekezi kwa *NRFA* kununua mahindi kwa kilo kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika, naomba kujibu Swalii la Nyongeza la Mheshimiwa Ignas Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huu utaratibu wa kutoa bei elekezi kwa mazao, nadhani tumekubaliana kwamba, kwa upande wa Serikali, ni muhimu sana kuangalia soko liliyvo na utaratibu na gharama za uzalishaji. Kuna vigezo vingi vingi sana ambavyo kusema kweli, inabidi tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, na kwa sasa hivi, labda niseme tu, kwa sababu, msimu unaanza kwa upande wa uzalishaji wa mahindi, kwa maana najua ndio Mheshimiwa Malocha, anachoulizia; nadhani *NFRA* wanalifanya kazi, ili waangalie.

Lakini tunaliangalia soko kwa maana ya wazalishaji wakuu kwa maana ya Songea, Iringa, maeneo ya Mbozi na Sumbawanga. Lakini nadhani, nitakutana na Wabunge wahusika wa maeneo haya, ili kuwapatia mwelekeo huo wa bei elekezi kama *NFRA* watakuwa wameitoa.

Na. 242

**Kuvitoza Kodi Vyama Vya Ushirika wa Mazao na SACCOS**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikivitoza Vyama vya Ushirika na *SACCOS* Kodi ya 30% wakati vyama hivyo, havifanyi biashara zaidi ya kutoa huduma:-

- (a) Je, kwa nini Serikali, isibadili mfumo huo wa kuvitoza kodi vyama vya ushirika?
- (b) Je, Serikali, haionti umuhimu wa kuacha kutoza kodi hiyo, ili kuwasaidia wananchi wa hali ya chini, ambao wengi wao ndio wanachama wa vyama hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Chakula Kilimo na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Suleimani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) hutoza Kodi ya Mapato (*Corporate Tax*) kwa Taasisi mbalimbali, vikiwemo Vyama vya ushirika na *SACCOS*, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004, Sura 332. Kodi hiyo, hutozwa kwa kiwango cha 30% kwenye faida, baada ya kuondoa gharama za uendeshaji.

Hivyo, kwa Chama cha Ushirika na *SACCOS*, ambavyo havitengenezi faida au hakitapata faida, hakiwezi kutozwa kodi hiyo kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa rai kwa Vyama vya Ushirika na *SACCOS*, kufanya juhudzi za kuimarisha huduma hizo wanazotoa kwa wanachama wao, ili zilenge pia kupata faida itayoviwezesha kuboresha utoaji wa huduma na hivyo, kuviwezesha pia kulipa kodi ya mapato kama ilivyo kwa mabenki na taasisi zingine za fedha.

- (b) Mheshimiwa Spika, *SACCOS* zinafanya biashara ya fedha ya kuweka na kukopa. Katika kufanya hivyo, kama zinaendeshwa vizuri, zinapata faida kiasi fulani.

Kwa kuwa, *SACCOS* kwa jumla zinatoa huduma kwa wanachama wake, basi ninatoa ahadi kwamba, tutafanya mazungumzo na Wizara ya Fedha, kujenga hoja ya kuona ni namna gani *SACCOS*, zinaweza kusamehewa kodi na kwa kiwango gani, kama Waziri wa Fedha, atakavyoona inafaa. (*Makofii*)

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wizara inakiri kuwa Vyama vya Ushirika havifanyi biashara, bali hutoa huduma.

Je, ni lini Wizara, italeta Sheria ya mabadiliko, ili iweze kuvisaidia Vyama hivyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, *SACCOS* nyingi zimekuwa zikitozwa riba kubwa na mabenki. Je, Wizara, inavisaidia vipi vyama hivyo, ili kuweza kuepuka riba kubwa inayotozwa na mabenki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu Maswali ya Nyongeza, ya Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hili la kwanza, inabidi nirejee nyuma kidogo. *SACCOS* ziliikuwa hazitozwi kodi kabla ya Sheria hii ya Mapato na Matumizi ya Mwaka 2004. Kusema kweli, katika kipindi hicho tuliona mabadiliko makubwa, *SACCOS* zilitoka kwenye *SACCOS* kama mia moja hivi, zikafika mpaka *SACCOS* 5,000. Wanachama kutoka 65,000 mpaka wanachama karibu 1,600,000 kwa hiyo, tuliona ukuaji mkubwa wa *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye biashara yoyote ya fedha ya kukopa, kwa maana ya hii akiba ya kuweka na kutoa, kunakuwa na dhamana ya wanachama na kunakuwa na dhamana ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaona kwenye mapendekezo aliyotoa *SCART* moja walilolitoa ni kwamba *SACCOS* ambazo zinatengeneza faida ya kutoka shilingi milioni 50 sasa kile kiwango cha faida kiende 150 ili kuanzia 150 ndiyo hapo kodi ya *Corporate Tax* itolewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kumhakikishia tu kwamba linafanyiwa kazi tayari lakini pia na sisi kama tulivyosema tunahamasisha ubora wa utoaji huduma na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ambalo ni riba lipo kwenye utaratibu wa kufanyiwa tathmini kwenye *financial sector reform* na tunaangalia kwa sababu kwa kuwa *SACCOS* inakusudia kutoa *financial services* kwenye maeneo ya vijiji ni vema tukaangalia namna ya kuwapunguzia kodi ili wakulima walio wengi na Watanzania walio wengi wanaoishi kwenye mazingira ya vijiji wapate huduma hii. (*Makofî*)

Na. 243

#### **Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo – Kawe**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Mwaka 2011/2012 Serikali iliahidi kujenga jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo Kawe na kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo ambao hadi sasa haujaanza.

- (a) Je, ucheleweshaji wa ujenzi huo umesababishwa na nini?
- (b) Je, ujenzi huo sasa unatarajiwa kuanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mbunge wa Kawe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mwaka wa fedha uliopita wa 2011/2012 Serikali iliahidi kujenga jengo la Mahakama ya Mwanzo Kawe kwa kutumia fedha ya Wafadhili wa Benki ya Dunia ila kwa bahati mbaya mradi huo ulimalizika muda wake Desemba, 2011 kabla ya ujenzi wa Mahakama hiyo kuanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali bado inayo nia ya kuendeleza ujenzi wa Mahakama za Mwanzo hapa nchini ikiwa ni pamoja na Mahakama ya Mwanzo Kawe. Pia kuboresha mahakama zilizopo ili kusogezza huduma hii muhimu karibu na wananchi. Hivyo, kwa misingi hiyo, Serikali inatafuta vyanzo vingine vya fedha ikiwa ni pamoja na ruzuku ya Serikali kuititia mfuko wa Mahakama ili kutekeleza azma hii na kwa mpango huo napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Mahakama ya Mwanzo Kawe imewekwa kwenye mpango wa ujenzi katika mwaka wa fedha 2012/2013. (*Makofî*)

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa majibu ya Naibu Waziri yanaonyesha kwamba Mahakama hiyo itajengwa kwa mwaka huu wa fedha lakini kwa kuwa eneo husika lilikuwa ni gofu kwa muda mrefu sana na hivyo kuna baadhi ya watu ambao wameingia katika eneo la Mahakama kufanya shughuli zao.

Sasa ninataka kujuu kama Serikali tayari imeshafanya uhakiki ili kuweza kujuu maeneo ama eneo la Mahakama husika ili sasa ujenzi ukianza tuepushe migogoro na wananchi isiyokuwa na sababu?

Lakini la pili, ni kwamba Serikali imekuwa ikijenga Mahakama lakini kuna maeneo mengine ambayo Mahakama zipo na *facilities* zipo lakini majengo yamekuwa hayatumiki. Kwa mfano,

eneo la pori Barazani Kata ya Pori Jimbo la Arumeru Mashariki, kwa Mheshimiwa Joshua Nassari, kuna Mahakama imejengwa haitumiki, hadi kuwalazimisha wananchi waende Jimbo linguine la Arumeru Magharibi kwa Mheshimiwa Ole Medeye kupata huduma. Sasa ninataka kauli ya Serikali kuhusiana na jengo hili ambalo lipo lakini kwa nini halitumiki?

**SPIKA:** Yaani majengo yaliyochakaa, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhal!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMJII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima J. Mdee, kama ifuatavyo:-

Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshafanya uhakiki wa eneo ambalo Mahakama hiyo itajengwa na nikueleze zaidi kwamba hatutajenga tu jengo la Mahakama lakini mpango ni kujenga na nyumba pia ya Hakimu.

Swali lako la pili kuhusu Mahakama zipo katika baadhi ya maeneo mbalimbali hapa nchini lakini hayana Mahakimu. Nikuthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote mliokuwa hapa kwamba tayari kwa mwaka huu wa fedha Serikali imeajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 300 wenye shahada ya kwanza ya Sheria na tayari wameshasambazwa katika maeneo mbalimbali katika Wilaya ya 102 nchini.

Pia kuhusu suala la vitendea kazi kwa kuititia Mfuko wa Mahakama tumeweza kuboresha na mpango ni kuendelea kuboresha *facilities* zote ambazo zipo katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya na kama Mheshimiwa Mbunge anakumbuka wakati Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria anatoa Bajeti yake ya mwaka huu 2012/2013 alieleza kwamba Mahakama za Mwanzo kutopteka na kuwezeshwa sasa hivi zimeweza kupunguza mrundikano wa mashauri kwa 99.7% (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, kwa sababu ya muda naomba niendelee na Wizara iliyobakia ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, atauliza swali hilo.

Na. 244

#### Hali ya Nyumba za Askari Mkoani

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS (K.n.y. MHE. ALI KHAMIS SEIF)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga nyumba za Askari Polisi Mkoani ambazo zina hali mbaya?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango wa kujenga na kukarabati vituo vya Polisi na nyumba za kuishi Askari nchi nzima. Mpango huu unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Jeshi la Polisi halijatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi au ukarabati wa nyumba. Ukarabati wa nyumba alizotitaja Mheshimiwa Mbunge utagemea upatikanaji wa fedha katika Bajeti ijayo ya 2012/2013/2014.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini hayana matumaini kwa sababu anasema hata katika Bajeti ya mwakani hakuna mategemo ya kupatikana fedha na nyumba hizi zilijengwa toka wakati wa ukoloni na kwa kweli zina hali mbaya sana sasa na kwa sababu katika ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna fungu la dharura au fungu la maafa.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kupunguza fungu hili ili kukarabati nyumba hizi ili Askari hawa wasije wakafikwa na maafa ambao wao ndiyo huwa wanatusaidia katika maafa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Haroub, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jibu langu kwa kweli linatia matumaini, lakini kama hajayapata nafiajiri hakuna haja ya kwenda kwenye fungu la maafa kuhusu suala hili. Nyumba za Mkoani mimi nimezitembelea na ninazifahamu lakini tatizo hasa la msingi siyo uchakavu wa nyumba zenyewe kama nyumba isipokuwa kuna tishio la mmomonyoko wa udongo. Mmomonyoko wa udongo tumeshauangalia na tumeufanyia tathmini na tunataka tuushughulikie na ndiyo maana hili swali la nyumba tukalichelewesha vinginevyo nyumba zenyewe bado hazitosh na Bajeti ambayo tunategemea basi tunaweza tukazifanya ukarabati na zikawa ni salama kwa wale wanaoishi ndani.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na muda wenyewe pia tumezidisha. Kwa hiyo, kwanza niwatambue baadhi ya wageni waliopo humu ndani.

Tuna wageni kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto hawa ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Ndugu Bi. Kijakazi Mtengwa na Naibu Katibu Mkuu Bi. Anne Maembe. (*Makof!*)

Pia tuna wawakilishi kutoka Ubalozi wa Canada, Balozi wa Sweeden, Balozi wa Ireland na pia kuna mwakilishi wa *UN Women*, karibuni sana na ahsanteni sana. (*Makof!*)

Pia tunaye Meneja wa Benki ya Wanawake Tanzania Bi. Margrath Chacha, tunaye Mkuu wa Chuo cha Tengeru Ndugu Anthony Bunduki, tunaye Katibu wa Baraza la Taifa la *NGOs* Ndugu Ismail Suleiman, tunao Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakurugenzi Wasaidizi naomba popote walipo wasimame. Karibuni sana! Na tunawatachia kazi njema. (*Makof!*)

Tuna wageni pia kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula ambao wanaendelea lakini walikuwepo kutoka juzi, yaani tuliwatambua juzi.

Pia tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni wa Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, ambaye ni Naibu Waziri wa TAMISEMI kutoka Ruangwa ambao ni Shekhe Said Namkulya, Shekhe Hashim Lyambamba, Ndugu Said Majaliwa, yupo Ndugu Nicholous Michael na yupo Ndugu Jonas Mdoe. Kwa ujumla ni familia ya Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makof!*)

Kuna wageni wa Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari ambao ni marafiki na waliokuwa *Co-workers* wake kutoka Marekani ambao ni Ben Campbell, Rashim Jasraria, *I hope iam pronouncing your names correctly. And I have Cantilin Andrew , there is Anne Spector, that is my name so it is easy to pronounce.* Lakini wanaongozwa na Ndugu Johnson Kiwango kutoka Shirika la *Support for International Change la Arusha*. Karibuni sana kwa ajili ya kuendelea na shughuli hii. (*Makof!*)

Tuna wageni sita (6) wa Mheshimiwa Pindi Chana, ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Wanawake(UWT) Mkoa wa Njombe wakiongozwa na Ndugu S. Kevela, ambaye ni Mwenyekiti wa Mkoa huo. Karibuni sana na pia ni wageni wangu nadhani, karibuni sana. (*Makof!*)

Pia kuna wageni 12 wa Mheshimiwa Ritta E. Kabati, ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Wanawake Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ezadi Mwamwindi, ambaye ni Mwenyekiti wa Mkoa, naomba Mheshimiwa Mwamwindi asimame kwanza kisha na wengine wasimame. Karibuni sana na ahsanteni sana. (*Makof!*)

Pia tuna wageni 12 wa Mheshimiwa John Chiligati wakiongozwa na Diwani kutoka Jimbo lake Mheshimiwa Emmanuel Majeni. Karibuni sana na tunawashukuru sana. (*Makof!*)

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo hawa ni wanakwaya 40 kutoka Usharika Ihanja Singida pamoja na wenyeji wao amba ni wana kwaya kuu kutoka Usharika wa KKT Arusha Road, naomba wote wasimame. Ahsanteni sana na tunawashukuru sana. (*Makofii*)

Tuna wanachuo 68 na Walimu wao kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba, Mafinga, karibuni sana. Leo majukwaa yamejaa akina wanyalukolo tu! Karibuni sana.

Tuna wananchuo wengine 50 na Walimu wao kutoka Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Ruaha Iringa, karibuni sana. Kwa hiyo, jukwaa hili lote la akina wanyalukolo, karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo tuna shughuli za kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha kamati hiyo kitakachofanyika katika ukumbi namba 133. (*Makofii*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Andrew Chenge, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana, kutakuwa na Mkutano wa Kamati hiyo katika ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika ukumbi namba 219.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mindombini Mheshimiwa Peter Serukamba anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana kutakuwa na kikao cha kamati kitakachofanyika katika ukumbi namba 231.

Kwa hiyo, Kamati ya Miundombini itafanya kikao chao chumba namba 231, watu wawili wameandika lakini hawaku-coordinate lakini ni Kamati hiyo hiyo.

Wenyeviti wa UWT kwa Wilaya ya Njombe ndiyo Mheshimiwa Mama Kevele, huyu mume wake alikuwa Mbunge wetu hapa na Mwenyekiti wa Wilaya ya Iringa naye asimame, ahsante sana. Kama nilivyosema wanyalukolo wote mpo hapo tunaendelea. (*Makofii*)

Katibu endelea na *Order Paper!*

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2012/2013  
Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, juzi tulipoahirisha kikao kutokana na kupungua kwa quorum, tulikuwa tumefikia hatua ya Kamati ya Matumizi na kwa hiyo, tutaendelea tulipoachia.

Katibu endelea!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunaahirisha siku ile tulikuwa kwenye mshahara wa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Walitajwa wengine na waliobaki wengine tunawamalizia hao yaani tunaendelea na wale waliobaki, yaani tunaendelea nao.

Maana yake taarifa niliyokuwa nayo mimi ni kwamba tulikuwa kwenye kifungu cha Mshahara wa Waziri, walitajwa watu wakabakia ambao ninao kwenye orodha yangu. Kwa hiyo, naendelea nao. Naomba tusitumie muda vibaya, hatutumii muda vibaya.

Kanuni gani unauliza! Kama hakuna kanuni tunaendelea na kifungu kinachoendelea! Nimemwita tayari Mheshimiwa Moses Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 112 (1).

**MWENYEKITI:** Soma!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema, masharti ya Kanuni ya 77 yatatumika kuhusu Kamati ya Bunge Zima, ila tu kama idadi ya Wabunge waliohuduria itakuwa bado haifiki nusu ya Wabunge wote baada ya kipindi kilichowekwa na Kanuni ya 77(3). Mwenyekiti ataondoka kwenye kiti, Bunge litarudia na Katibu atahesabu idadi ya Wabunge waliohuduria na kama idadi yao itakuwa bado haifiki nusu ya Wabunge wote basi Spika ataaahirisha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wote ulioendeshwa siku ya Jumamosi hatukuwa na idadi ya Wabunge ambayo iliyofikia nusu ya Wabunge wote.

Kwa mantiki hiyo *process* yote iliyofanyika toka mwanzo, Bunge lilikitaarifu kiti halikuweza kufanya kwa mujibu wa Kanuni zetu kama ambavyo Kanuni ya 112 inaeleza na ile ya 77.

Kwa hiyo, ule mchakato wote unapaswa uachwe na leo tuanze upya Kifungu kwa Kifungu. Hapo ndipo tutakuwa tumezingatia matakwa ya Kanuni ya 77 hali kadhalika Kanuni ya 112. Kwa hiyo, ushauri wangu niombe tuanze *process* upya ili tuweze kuhoji kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, nashukuru. Hatuanzi upya kwa sababu hatukufikia maamuzi. Kama Naibu Spika angewahoji pale ingekuwa siyo sahihi. Pale hatukufikia maamuzi, siyo suala la kugoma, hili ni suala la Kanuni. Sasa tunaendelea, na wanaoendelea ninamwita Mheshimiwa Marombwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa tumeishamaliza hatuwezi kurudia suala lile lile mara mbili.

(*Hapa Wabunge walionekana kunung'unika*)

**MWENYEKITI:** Hatuwezi kuhojiana juu ya suala lile lile mara mbili. Mheshimiwa Abdul Marombwa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Nilipokuwa nachangia kwa kuongea nilizungumzia namna ambavyo wakulima wanaathirika kutokana na mazao yao kuwekwa ghalani kwa kutumia mpango wa stakabadhi ghalani na hasa kutokana na *interest rate* kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia pia kwa mkoa wa Pwani kwamba vyama vyote vya msingi kwa sasa ambavyo vilikopa fedha za kununulia korosho *interest rate* zao ni kubwa na zinaendelea kuwa kubwa kwa sababu mpaka sasa Serikali kwa kushirikiana na hivyo vyama vya msingi haijaweza kuuza korosho hizo. (*Makof*)

Nilieleza wazi kwamba, itakapofika mwezi wa kumi mwaka huu, *interest rate* itafikia asilimia 21 kutoka 15 na gharama hizi zote zitakwenda kumpata yule mwenye mazao yake kwa maana ya mkulima.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa kuweza kuhakikisha kuwa hii *interest rate* iliyowekwa haimgusi mkulima na badala yake Serikali iingilie katili kuhakikisha kuwa mkulima anapata fedha zake kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunachangia hoja juzi tulisema hivi, hili ni tatizo kubwa kweli kwa ukanda wa Pwani na tumejaribu kulifanyia kazi. Tumeita benki zote kwa maana ya CRDB na NMB na uongozi wa vyama vya ushirika wamekuwa Dodoma kujadiliana kuhusu suala hili.

Kilichopatikana ni kwamba, kuna vyama vya msingi ambavyo vimepokea fedha yao yote lakini havikuwapa wakulima, vime- *engage* kwenye matumizi ambayo siyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hatua inayoendelea ni kwamba, mrajisi amerejea na timu yake yote na anakagua vyama vya msingi kwa maana ya wilaya za Mkuranga, Rufiji na wapi ili kubaini pale ambapo kumetokea uhalifu. Pale ambapo ni kweli fedha hazijatolewa Serikali itaingilia katili, benki zitatoa zile fedha.

Pia kwenye masuala haya ya riba na kadhalika tumeishaongea na benki na tutayafanya kazi. Lakini ukweli ni kwamba viko vyama vya msingi vingi ambavyo vimeishapokea fedha lakini hesabu zile hazionekani kuwa sawa, kwa hiyo tunapitia mahesabu yao upya.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi hii. Katika taarifa ya Kamati ya Kilimo tulizungumzia juu ya baadhi ya wakulima katika maeneo mbalimbali ya Tanzania likiwemo Mbarali kutozwa ushuru wanapotoa mazao yao mashambani kupeleka majumbani kwao.

Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko rasmi kwamba, si vyema kuwatoza ushuru wakulima wanapotoa mazao mashambani mwao hasa ndani ya Wilaya wakati hawajafanya biashara yoyote.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya leo hali yangu siyo nzuri lakini naomba niendelee tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuru wakulima wanatozwa wanapokuwa wamekwenda sokoni, lakini anapotoa mazao shambani kwenda nyumbani kwake hatozwi ushuru. Kama kuna mtu anayemtoza ushuru mkulima anapotoa mazao shambani kupeleka nyumbani kwake kwa kweli hilo ni kosa.

Tutawasiliana na Halmashauri zinazohusika kama zinaendelea kufanya hivyo na tutawasiliana na TAMISEMI kuangalia namna ya kudhibiti hali hiyo. Lakini wakifika sokoni kwa taratibu walizojiwekea wenyewe na Halmashauri husika basi ushuru amba unahusika utaendelea kutozwa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia tatizo la mashambulizi ya ugonjwa amba umetoka Afrika ya Kati ukaingia Uganda na kuingia mkoa wa Kagera, amba unashambulia migomba wanaita

mnyauko au mnyanjano. Katika mchango wangu nikaelezea njia ambazo zinaweza kutumika kukabili ugonjwa huo. Sasa kwa kuwa Serikali imesema kuna fungu limekuwa *ring fenced* la kukabili magonjwa ya maambukizi.

Je, Serikali iko tayari kutumia *model* niliyoeleza kwenye mchango wangu ili kutumia Tarafa ya Nsamba, Kamachumu na Izigo kuweza ku-control na kuondoa huu ugonjwa wa mnyauko kwa kutumia *ring fenced amount* na ile *model* niliyoiwasilisha?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mwijage kwa sababu suala hili amelleta mara nyingi kwangu kwa njia ya maswali. Tuko tayari kabisa tutaangalia uwezekano wa kuitumia ile *model* iweze kutusaidia.

Lakini pia nimemwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa vile Uganda wameweza kufanikia kwa kiasi kikubwa, Wizara yangu imetenga fedha na tutawapeleka wakulima kutoka mkoa wa Kagera waende kule wakaone wenzetu wa Uganda wamefanyaje ili wakirudi pia tutumie *models* hizi ambazo ame- *suggest* tuangalie namna ya kudhibiti ugonjwa huu. (*Makofii*)

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vituo vya utafiti hapa nchini kama nilivyochangia viko hoi sana. Mimi ni mjumbe katika Kamati ya Kilimo, ombi langu na ningependa kupata ufanuzi, kilimo hapa nchini tunakiendesa kwa mazoea.

Sasa niombe katika Wizara hii kwa umahiri wa Mawaziri tulio nao wavitembelee vituo hivi maana vingine kuna sehemu zimefungwa kabisa haziwezi kufanya kazi kwa sababu ya bajeti finyu. Kwa maana ya maandalizi ya bajeti ijayo sasa nataka kujua vituo hivi tunapaswa kuiyendesa namna gani, tuvifikirie ili tutoke katika kilimo cha mazoea na sisi tukapata mbegu ndani ya nchi yetu ambazo tunazalisha wenyewe kwa kutumia vituo hivi.

Je, Waziri anatueleza nini ili tuweze kukidhi mahitaji ndani ya nchi yetu kwa kutumia vituo vyetu? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge. Mimi mwenyewe nimeishaanza kutembelea vituo vyetu, hata viongozi wetu wakubwa wametembelea. Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na hata Naibu Waziri wangu akitoka hapa amepanga kutembelea vituo hivyo. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba, vituo hivi kwanza tunavikarabati halafu tunavipatia vitendea kazi ili viweze kwenda kwenye kiwango hiki anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge. Nakubaliana naye kabisa katika hili.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilihoji sera au sheria ya hiki kitu kinaitwa mafilisi. Mko wa Mara kulikuwa na chama kikuu cha *ushirika Mara Cooperative Union (MARA COPU)* ambacho kilikuwa kinamiliki mali pamoa na viwanda vya kuchambua pamba na magodauni ya kahama. Kulikuwa na *Kibara ginnery, Ushashi ginnery*, Mgango na kule Tarime magodauni ya kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ni zaidi ya miaka 17 mali hizo zimekaliwa na huyo mtu anaitwa Mfilisi. Sasa mimi nataka kujua hii sera au sheria ya Mfilisi anatakiwa akalie mali za wananchi kwa miaka mingapi?

Naamini kuna mchezo mchafu unachezwa, kuna kitu wamejenga na sasa hivi imebaki ni kuhamisha vipuri wanapeleka kwenye viwanda vingine wakati mwengine wanauza mali chakavu.

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri na katika jambo hili sina utani. Sitakubali Bajeti yako ipitishwe kama hutaniambia hii sera ya sheria ya Mfilisi anatakiwa akalie mali za watu kwa muda gani, ikiwa sasa ni zaidi ya miaka 17?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimwombe Mheshimiwa Kange Lugola aunge mkono hoja hii. Ninachowea kumwahidi ni kwamba, huyu Mfilisi ana taratibu zake anazozifuata za kisheria.

Sasa naomba nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawasiliana na Mwanasheria Mkuu tumwangilie huyu Mfilisi hiki kitu ambacho kinalalamikiwa ni nini. Kwa kweli sasa hivi sina jibu la haraka, lakini nitalifuatilia kupitia kwa Mwanasheria Mkuu halafu tuone majibu yatakuwa namna gani ili kumsaidia.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Katika mchango wangu niliulizia na kutaka kujua mpango wa Wizara kuhusiana na kuanzisha mpango maalum wa kilimo cha umwagiliaji kanda ya Ziwa na Kati kutokana na fedha ambayo Serikali imeahidiwa dola za Marekani milioni 897 kuanzia mwaka ujao wa fedha kwa sababu mwaka huu wa fedha, fedha nydingi ya Wizara imeelekezwa kwenye mpango wa kilimo wa kusini *SAGCOT*.

Sasa tungependa kilimo cha umwagiliaji kiwe mpango wa kitaifa kwa kanda ya Ziwa badala ya kuomba miradi midogo midogo kupitia Halmashauri za Wilaya. Ahsante sana. (*Makof*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kamani alitaka kujua hizi dola milioni 897 ambazo tumezitaja humu.

Ningependa nimfahamishe tu kwamba, hizi ni fedha ambazo zimeahidiwa na zile nchi tajiri sana duniani (*G 8*) ambazo Mheshimiwa Rais alizitolea maeleo tukiwa kule Marekani na fedha hizi ni mahususi kwa ajili ya kuendeleza mpango wa *SAGCOT*.

Sasa mpango wa *SAGCOT* siyo kwamba ndiyo mwanzo na mwisho, iko mipango mingine, hii ni Kongani ya kwanza tu inaanza, baadaye zitafuata kongani nydingine za Magharibi, Kaskazini, lakini hii ni ya kwanza kabisa ambayo ni *model* ambayo itakuwa imeanza. Nina hakika baadaye pia tutapitia upande wa kanda hizo nydingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mikoa hii ya Magharibi, ukanda wa ziwa bado tunayo mipango mingine ambayo inaendelea. Tuna *DASP*, na hii tumeiweka mahususi kabisa kwa ajili ya mikoa ile, ndiyo maana ukitazama huwezi kukuta *DASP* kwenye mikoa ya Kaskazini. Tuliiweka huko makusudi ili mikoa ambayo hai- *enjoy* misaada mingi nayo iweze kufaidika, ndiyo maana *DASP* iko pale.

Lakini pia tunayo *ASDP*. Kwa hiyo, nataka tu nimhakikishie kwamba, miradi mingine itaendelea kwa utaratibu uliokuwepo na tutaendelea kutenga fedha kwa utaratibu uliokuwepo, siyo kwamba hii *SAGCOT* sasa ndiyo imekuwa mbadala wa mipango mingine ya maendeleo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza kabisa nilikuwa nitumie kifungu cha mia na tatu (103) lakini kutokana na majibu ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri aliyatoa ninaomba nisitumie kifungu hicho bali niende kwa kuunga mkono hoja. (*Makof*)

Lakini pamoja na hayo nilikuwa napenda kupata sasa ufanuzi kwamba, kama nilivosema Mkoa wa Singida una zones tatu kwenye upande wa Kilimo; kuna maeneo ambayo yanastawi mahindi, mtama, maeneo mengine alizeti na maeneo mengine mazao yote, lakini Serikali kupitia mkoa wa Singida wamekuwa wakilazimisha wananchi wasilime mahindi bali walime mtama peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mtama huu umekuwa na matatizo ambapo watoto wamekuwa wakishindwa kwenda shule kwa sababu ndiyo wamekuwa walinzi wakubwa wa mashamba hayo kwa kuhamia ndege kwa sababu Serikali inashindwa kuleta ndege ya kunyonyuzia dawa kwa wakati mwafaka. Pia zao la mahindi limekuwa likizuiwa kupata ruzuku ama pembejeo. Sasa Serikali iko tayari kutoa tamko hapa kwamba, wakulima wa mahindi watapata pembejeo na kuachwa walime zao hili kama zao la biashara na chakula? Ahsante sana.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua tu Mheshimiwa Martha Mlata aliposimamia pamoja na kuzunguka zunguka kote huko. Sisi tunazo *agro ecological zones* katika nchi hii zinazosema hapa zao hili linastawi, hapa halistawi vizuri.

Lakini hoja nzuri ambayo nafikiri ningependa kwa kiasi fulani nikubaliane nayo ni kwamba, katika mkoa wa Singida yako maeneo ambayo hasa yale yanayopakana na mkoa wa Arusha, si kweli kwamba mkoa wote kabisa ni ziro, yako maeneo ambayo wakipanda mahindi kwa kiasi fulani wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakachofanya ni kwamba nitatuma wataalam wetu wakaangalie tena maeneo ambayo tutaona hapa wakilima mahindi eneo hili yatatoka, hatuna haja ya kusema basi hakuna kulima tena. Lakini yale maeneo ambayo tunaona kwamba, hapa kwa kweli wakilima tunapata sifuri, kwani yako maeneo ambayo hata wakilima vipi wanapata sifuri, tutaendelea kuwahimiza walime mazao ambayo yanahimili ukame. Lakini nitatuma wataalam wakaangalie kama kuna kaeneo (eneo dogo) ambako kana uwezekano wakalima mahindi basi tutawasiliana na Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nakuandikia kwamba, mbona sitajwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimeulizia wakati wa mjadala wa hotuba, sera na utaratibu wa Wizara wa kuweza kutoa maamuzi juu ya vihatarishi vya soko kama vile la pamba na hivi ambavyo sasa vimesababisha kukosekana kwa amani. Watu wanachomewa nyumba na moja wapo ya vihatarishi hivyo nilisema ni uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28, tarehe 2 Aprili, 2012, tarehe 22 Aprili, 2012 uongozi wa Wizara kupitia Waziri aliyeuwepo wakati huo, alisema kwamba na yeye amekubaliana na wakulima ambao walimletea hoja kwamba, kuna shilingi bilioni 12 za viua wadudu vilivyonunuliwa lakini ni vichache tu ambavyo vimefika kwa wakulima. Mkurugenzi alikuwa analazimisha watu walipe shilingi milioni 50 ili wapate leseni na ni lazima waingie kwenye kilimo cha mkataba.

Tatu alikuwa analazimisha mbegu za *dilinte* ambazo zina- *cost* Serikali shilingi bilioni 13, na pia uongozi ulikuwa umeandika barua ya kuwaondoa baadhi ya *ginneries* ili kupunguza wigo wa watu ambao wanaweza kununua na ubabe ambao ni kibao.

Sasa nauliza wewe Mheshimiwa Waziri baada ya kutuambia sisi, na- *declare interest* mimi ni Mwenyekiti wa Wabunge ambao tunatoka kwenye Pamba, tarehe 22 Waziri alituambia amemsimamisha kazi Mkurugenzi wa Bodii, lakini na pia ilionesha kwamba tarehe 5 Mei, 2012, huyu Mkurugenzi alikuwa na kujitambulisha kama ni Mkurugenzi, sasa mpaka leo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele imegonga na *issue* inatakiwa iwe moja, sasa mnajibu *issue* moja tu.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Sasa mpaka leo anaendelea kwanini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijui, suala hili Mheshimiwa Cheyo anazidi kulileta, tumelizungumza mara nyingi, hoja kubwa hapa ni kwamba Mheshimiwa Cheyo anataka Ndugu Mtunga ambaye ni Mkurugenzi awe pembeni.

Nilichosema ni hivi wakati ule mlipomtuhamu katika kikao kile cha wadau na Mheshimiwa Cheyo akiwepo na Wabunge wengine wote wanaolima pamba walisema huyu ndugu ndiye anayeleta matatizo, lakini tena wakageuka wao wenye humo humo na Mheshimiwa Shibuda akasimama akasema jamani huyu mtu matatizo yanatokea hayakutokea wakati wa muda wake, yalitokea wakati wa *previous* muda, akaja tena kiongozi wa Mheshimiwa Zitto Kabwe akaniambia tena kwa maneno mengine kama hayo hayo kwamba anaomba tuliangalie upya wazo hili kwa sababu haya yaliyotokea hayakutokea katika kipindi cha Ndugu Ntunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilichosema ni hivi *just to give them benefit of doubt*. Ndugu Ntunga tutamwambia akae pemberi tuendeshe ukaguzi tuone kama kuna matatizo ambayo yamejitokeza na wenyewe wamesema kabisa mpaka Mheshimiwa Shibuda alizungumza hapa kwamba mbona mnataka kumchinjia baharini huyu mwenzetu. Sasa nyie wenyewe ndio mnatoa kauli zinazopingana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninachosema ni kwamba sisi kwa sababu kuna tuhuma hizi tutamwambia Ntunga kaa pemberi kidogo hatumfukuzi kazi kwa sababu hajapati kana na makosa, atakaa pemberi ukaguzi utafanyika halafu tutaona kama kweli ana makosa tutachukua hatua zinazostahili.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu nilizungumzia tatizo la wananchi wangu wa Jimbo la Kondo Kusini ambalo wamenyang'anywa mashamba takriban miaka mitano iliopita kwenye eneo la Sekii. Na tatizo hili limekuwa la muda mrefu.

Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Jimbo lile alisema lazima wananchi hawa warudishiwe mashamba yao mpaka leo bado tatizo ni kubwa. Kipindi cha kilimo kinapofika watani zangu wale wa Wilaya ya Kiteto wanaingiza ng'ombe kwenye mashamba ya mahindi wanachuga bado mahindi hayajunwa.

Sasa ningeomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kama yeye labda yupo *busy* kidogo anisaidie hata kumtuma Naibu Waziri tena wengine ni shemeji zake na Naibu Waziri wanaochunga katika mashamba haya wa Wizara hiyo hiyo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba basi anisaidie twende na Naibu Waziri tukazungumze wale watu wa Kiteto na watu wa Chemba tumalize tatizo hili. Nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikwishakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba mimi na Mheshimiwa Nkamia tutaongozana twende tukajaribu kumaliza tatizo hili.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 44 inaonyesha kwamba muda wa mkopo wa matreka umeongezwa kutoka miaka miwili hadi miaka minne.

Lakini sasa hivi inaonyesha kwamba kwenye fomu zile za mikopo bado inaonyesha miaka miwili na wananchi sasa hivi wamechanganyikiwa huko hawajui cha kufanya. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri aweze kuwaelewesha wananchi kwamba siyo miaka miwili ni miaka minne ili wananchi waendelee kukopa yale matreka.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imechukua muda tu kubadilisha fomu hizi, lakini kimsingi tumekwishakubaliana na SUMA JKT kwamba muda wa kurejesha mkopo huo uongezwe.

Kwa hiyo, wananchi wajue hilo kwa sababu tumekwishalitamka hata Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka hapa Bungeni. Kwa hiyo, ni suala tu kwamba zile fomu bado zinasomeka kama zilivyoukuwa, tutawasiliana nao waweze kuzirekebisha.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi katika mchango wangu kwa kauli. Nilimshukuru sana Waziri kwa kutambua umuhimu wa kilimo cha bustani na kukubaliana na kauli yake katika ukurasa 28 na 29 kwamba kuongezeka kwa kilimo cha bustani ni njia mojawapo ya kusaidia kuinua uchumi na kumsaidia mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia kwangu nilimtambulisha Waziri kwamba kilimo hiki ni ghali, wananchi wa Lushoto kwa sasa hawana mazao mengine wanaishi kwa ajili ya kilimo cha bustani na nikaomba Serikali itamke itawasaidiaje wananchi hawa. Kwa sababu kilimo cha bustani unahitaji kutumia pembejeo kama madawa na kadhalika.

Sasa Waziri anatamka nini angalau hata kutoa ruzuku ya pembejeo ya viatilifu pamoja na mbolea?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Shekifu alizungumzia hili jambo. Tumejipanga na watu wa *Hot-culture* kwamba waende wakaangalie hili suala kwa kina kwa utaratibu ule ule tulivyozungumzia vile upande wa biashara ya vitunguu kwa upande wa Mkarama na upande *spices* hapa katikati Dakawa na maeneo ya Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba suala hili la *Hot-culture* na matunda linafanyiwa kazi kwa pamoja ili tuangalie namna ya kukuza kilimo hiki na kiwe na manufaa zaidi kwa ajili ya wananchi wake.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1002 - *Finance Accounts* ... .... Shs.1,413, 375,990/=  
Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... .... Shs. 1,917,403,640/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute* Shs. 7,692,523,140/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo *sub-vote* hii aliyoitaja lakini kifungu kidogo 220800 *Training Domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba fungu hili linahusiana sana na *Extension Officers* na Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakihoji upungufu mkubwa sana wa Maafisa Ugani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiangalia kifungu hiki naona kwamba fungu hili pamoja na kwamba tuna huo upungufu lakini limepungua kwa karibu shilingi bilioni moja. Je, tutaendelea kupata kweli hao Maafisa Ugani kwa mtindo huu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kifungu hili ni kwa ajili ya kugharamia mafunzo kwa wanafunzi waliope kwenye Vyuo vya Kilimo pamoja na mafunzo ya muda mfupi na watumishi wa Idara. Lakini gharama hizi zinazingatia masuala ya chakula, malazi, maji na umeme. Lakini kwa mwaka huu kwa kasma hii hapa punguzo limetokana na kutojumuisha kwa gharama za maji na umeme kwa mwaka huu 2012/2013 ndiyo maana kuna upungufu huo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 1005 - *Internal Audit Unit* ... .... Shs.274,879,050/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Internal Audit Unit* kasma ya 221000 *Travel in Country* ambayo inahusu Wakaguzi kusafiri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema Mfuko ule wa *CDTF Cotton Development Trust Fund* unaondeshwa ovyo ovyo na watu wanajigawia hela tu.

Nilimwomba Mheshimiwa Waziri apeleke *Auditors*, lakini nimeona hapa hela ni kidogo sana. Sasa nauliza je, hizi ndiyo hela zitazotosha kupeleka *Auditors* kule ili angalu tuanze *Internal Audit*, halafu baadaye iwekwe njia kwa ajili ya *Control and Auditor General* kwa sababu hizi ni

*Public Fund* zinachukuliwa kwa wakulima kwa sababu ya Sheria ya *CDTF* watu wanakatwa kwa lazima hawatoi kwa hiari.

Kwa hiyo, ni lazima kama ni *public funds* ziwe subject to audit na kabla wewe hujapeleka hela nyingine ya ruzuku hii kwanza iangaliwe zile fedha zilizopelekwa zimetumika vizuri, viatilifu vimetumika vizuri vimewafikia wakulima na vitu kama hivyo siyo kuachia *public funds* zinaliwa na watu.

**MWENYEKITI:** Je, hizi fedha ni kusudio hilo.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha hizi zinaonekana ni kidogo na ni kutokana tu na ufinyu wa Bajeti. Lakini jambo la msingi ambalo nililitaja pia wakati nikijibu hoja hapa ni kwamba Mifuko hii wakfu ya *CDTF* ni Mifuko ambayo tunaweka fedha za Serikali hata kwenye pamba tulisema tutaweka bilioni 8 na nikaahidi kwamba tunapoweka fedha za Serikali ni lazima kwa kweli tuzifuatilie tujue zimetumikaje.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa John Cheyo kwamba hata mimi mwenyewe binafsi nimekwishaamua kwamba lazima mifuko yote siyo ya pamba tu, hata kwenye korosho popote pale ambapo kuna mifuko wakfu tunapoingiza fedha hizi tutakwenda kukagua.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 -*Procurement Management Unit* ... Shs. 673,244,200/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 220800 *Training Domestic wametenjea* milioni moja tu na ukilinganisha na miaka ya nyuma. Ningependa Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi kwa nini imetengwa milioni moja tu ukizingatia kwamba *Procurement Management* ni muhimu sana. Naomba kupata ufanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutambua kwamba hii ni gharama kwa ajili ya mafunzo ya watumishi katika Kitengo hiki kwa maana ya mafunzo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ni kweli zimepungua lakini zimetokana na ufinyu wa Bajeti.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 *Government Communication Unit* ... Shs. 211,874,600/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma ya 229900 *other operating expenses* wameweka milioni tano mwaka huu wa fedha, lakini miaka miwili iliyopita ya fedha hapakuwa na amount yoyote iliyokuwa imetengwa. Naomba kupata ufanuzi kwa nini mwaka huu wameweka milioni tano?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala lipo wazi tu kwamba vifaa vikishanunuliwa mwaka uliopita na miaka mingine si vinachakaa lazima tuweke fedha kwa ajili ya uchakavu. Kwa hiyo, tumetenga fedha kwa ajili ya uchakavu wa vifaa.

*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 -*Legal Unit* ... ... ... ... ... ... Shs. 272,313,950/=

Kif. 1009 - *Management Information Systems Unit* ... Shs. 295,044,390/=

Kif. 1010 - *Environment Management Unit* ... ... ... Shs. 304,565,100/=

*(Vifungu kilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 *Crop Development* ... ... ...Shs. 97,833,093,670/=

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuhoji kasma 210300 inayohusu *personnel allowances* na vilevile 210500.

**MWENYEKITI:** *Ask one at a time.*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** *Related to the same matter.*

**MWENYEKITI:** *No, just ask that one and then you will continue.* Hatuuilizi vifungu viwili kwa wakati mmoja. Uliza hicho kwanza.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hili suala la posho katika Bodi za Uendelezaji wa Mazao especially. Hiyo Kasma nilioitaja ni shilingi milioni 466,770,040.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hawa watu wanaofanya kazi katika Bodi za Uendelezaji wa Mazao, wajumbe wa Bodi hasa hasa wanatakiwa walipwe posho kiasi gani kwa sababu katika Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani imejitokeza ushahidi kwamba watu wanalipwa posho tu kwa utaratibu usiojulikana. Kwa mfano, posho ya kujikimu *per-diem* kuna mtu amelipwa 750,000/= kwa siku anaitwa Bwanausi, kwenye kikao hicho hicho mwngine amelipwa 900,000/= anaitwa Anna Abdallah, mwngine amelipwa 375,000/= anaitwa Mrs. Mudhihiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kikao hicho hicho mtu amelipwa posho ya kikao *sitting allowance* 800,000/= anaitwa Bwanausi, kikao hicho hicho amelipwa *sitting allowance* 500,000/= huyo huyo Bwanausi, kikao hicho hicho Anna Abdallah amelipwa 400,000/= *sitting allowance*, Mrs. Mudhihiri amelipwa 200,000/. Tunataka tujue hii posho inatakiwa iwe shilingi ngapi ya kikao na posho ya kujikimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge mimi sijaona majina hayo katika kifungu hiki. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Jitu Soni ulisimama nilikuona.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama kabla.

**MWENYEKITI:** Ndiyo nilikuona.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba niulize kwenye sub-vote hiyo ya 2001 kasma 221500 *Agriculture and Livestock Supplies and Service*. Nilikuwa naomba kujua kwamba katika fungu hili ndilo linaloshughulikia masuala ya pembejeo zote na kama juzi tulivyoiezwa kuhusu masuala ya mbolea na wengi tulichangia kwamba mbolea ambayo inazalishwa nchini ndiyo itapewe kipaumbele.

Je, Serikali sasa hapa inatuambia kwamba ipo katika mpango huo kuhakikisha kwamba mbolea hiyo ambayo inazalishwa ndiyo itatumika katika pembejeo ya kupandia katika msimu huu?

**MWENYEKITI:** Kwamba hizi fedha ndiyo za kufanya hiyo kazi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoesema juzi fedha hizi ni pamoja na ruzuku na mambo mengine kwa mbolea na mbegu.

Lakini kwa maana ya mbolea ya Minjingu ambayo tumekwishakubaliana ndani ya Serikali tumelisema Bungeni na tumewaambia Wakuu wa Mikoa kwamba tuna *link fence* na ni fedha hii ndiyo itatumika kwa ajili ya hayo maeneo maalum ambayo yamekwishakadiriwa na

yamekwishatengwa na wataalam kwa ajili ya kupokea mbolea ya Mijingu kwa ajili ya msimu huu, mbolea hiyo ya *NPS*.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye hiyo *sub-vote* 2001 nimekuambia kuna grants ambazo zinatumika kwenye Bodi. Kwenye mchango nilisema kwamba ipo hatari kubwa kwa kujiingiza kwenye *GMOs* na Serikali lazima ichukue hatua kuli-study hili jambo kwa makini tusije tukajiingiza kwenye mtego ambao nchi za wenzetu kama Marekani, Brazil na hata South Africa wamejikuta wapo katika matatizo haya na tunataka ku-adopt wakati vyakula *organic* ndiyo ambavyo vinakuwa *more productive* na vina *more value*.

Kwa nini tunajitahidi kujiingiza katika mitego ya vitu ambavyo havina fidia na maslahi na ustawi wa nchi yetu? (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge unatakiwa uulize zimewekwa kwa kazi gani hiyo sera hatuizungumzii hapa. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tulilijibu sijui Mheshimiwa Mangungu hakuwepo hapa ndani. Hatujasemi kwamba tumejiingiza kwenye *GMO* wala mimi sijasimama hapa nikasema sasa Tanzania imeamua ku-adopt *GMOs* sijasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema ni hivi, *we are not living in the isolation*, Tanzania haiishi katika Kisiwa cha pekee, nchi zingine zimeanza kutumia *GMO* kwenye mazao ambayo siyo ya chakula wana taratibu zao. Sasa nilichosema ni hivi tunachofanya ni kuendeleza utafiti kuangalia na nilianza kueleza athari za *GMOs* na faida za *GMOs*.

Nikasema tutakachokifanya tunashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kuendeleza utafiti wa kina ili hatimaye tufike mahali ambapo tutafanya maamuzi ambayo hayaingizi Taifa katika matatizo. Lakini vilevile hayailetei hasara kwa kufanya maamuzi ambayo hayatusaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utafiti unaendelea na bado hatujaamua kwamba tunaingia kwenye *GMOs* moja kwa moja.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unatumia fedha hizo kwa utafiti?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za utafiti zipo katika eneo la utafiti.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana inatakiwa anayeuliza kifungu lazima kiwe kifungu kile kile na kiwe ni *specific* kwa ajili ya shughuli ile ile.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2002 - *Agriculture Mechanization* ... ... ... ... Shs. 681,065,690/=.

Kif. 2003 -*Agriculture Land Use Planning and MGT*. ... Shs. 754,991,950/=.

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2004 – *Plant Breeders' Unit* ... ... ... ... Shs. 221,454,620/=

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nilikuwa naomba kuuliza kwenye *sub vote* 2004, 411000 - *Rehabilitation and Other Civil Works*. Mwaka huu naona hajapangiwa kitu chochote na tulitegemea kwamba kwenye hii *Plant Breeder's Unit* mambo ya uzalishaji wa mbegu, sasa hapa hatujaona kiasi chochote kilichopangiwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kazi ambayo ameizungumzia Mheshimiwa Jitu, eneo lake halipo hapa. Hii hapa, *Rehabilitation and Other Civil Works*, zinahusiana na fedha ambazo ni kwa ajili ya matengenezo ya Ofisi za hicho Kitengo. Sasa kwa mwaka huu wa fedha hakuna matengenezo yatakayohusiana na hiyo Ofisi ndiyo maana hakuna bajeti iliyo tengwa.

(*Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake*)

Kif. 2005 – *Irrigation and Technical Services....* Shs. 4,115,921,900/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma ya 410700 - *Feasibility Studies, Project Preparation and Design*, wameweka Sh. 3,000,000/= tu. Nafahamu Mheshimiwa Waziri atasema kwamba ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, lakini kwa nini msiwe mna-prioritize ukizingatia kwamba *irrigation*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia, jibu unalijua kwamba hizi fedha ni za kazi gani, ndiyo suala lenyewe. Siyo habari ya sera hapa tena. Haya uliza hizi Sh. 3,000,000/= *it's against* hizi Sh. 16,000,000/= ni kwa sababu gani zimepungua? Ndiyo swali lenyewe.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa nini mwaka huu hizo fedha zimepungua?

**MWENYEKITI:** Sawasawa hilo ndiyo swali?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wala sitajibu kama anavyotaka yeye. Fedha hizi zimewekwa kidogo kwa sababu *feasibilities studies* zinataka fedha nyingi na kwa maana hiyo, tumekasimia fedha nyingi katika mipango ya maendeleo. Huu utafiti wa namna hii utagharamiwa na Mipango ya Maendeleo.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kupata ufanuzi katika kijfungu cha 229900 - *Other Operating Expenses*. Hizo fedha zimeongezeka kutoka Sh. 32,500,000/= za mwaka 2011 na mwaka huu zimefika Sh. 689,244,060/>. Fedha hizi ni kwa ajili ya kazi gani?

**MWENYEKITI:** Ongezeko hili limekuwa kwa ajili ya nini? Umekiona kifungu? Hujakiona!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Other Operating Expenses*, labda kama hajazingatia *addendum*, lakini kwa maana ya hapa, Idara ya Umwagiliaji fungu 2005 - *Other Operating Expenses*, 229900 ni Sh. 12,500,000/= ambapo gharama imepungua kutokana na sehemu ya fedha kwa ajili ya wataalamu waelekezi kukasimia katika fedha za maendeleo, ndiyo gharama yake.

**MWENYEKITI:** Mfanye masahihisho kwa sababu hapa ni Sh. 689,244,060/=.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Basi hii ilifanyiwa *addendum*.

**MWENYEKITI:** Kuna *addendum*!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko *addendum* ambayo imeambatanishwa na randama tuliyoiwasilisha Mezani.

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye *sub vote* 220300 nilitaka kujua tu kwamba katika fedha hizi liko fungu la utafiti wa magonjwa yanayokabili mikorosho ambayo kila mwaka inatulazimu kuulizia *sulphur*?

**MWENYEKITI:** Mbona wewe unauliza visivyo? Siyo hivyo hapa. Hapa ni *irrigation and technical services*. Sasa wewe tena mikorosho imeandikwa wapi?

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu cha 3001.

**MWENYEKITI:** Naona hatujafika huko.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza kwenye kasma ya 411000 -*Rehabilitation and Other Civil Works*, kwamba mwaka 2011 fedha zilizotengwa Sh. 12,000,000/= na mwaka huu ni Sh. 7,000,000/= na hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri tulivyoona kuna mabwawa, kwa mfano yale ya Kidababe, huku sasa Sh. 7,000,000=, tukiona je, hizi fedha zitatosha Kwa mfano uanzishaji....

**MWENYEKITI:** Ni za kazi gani? Wewe unajuaje kama ndizo zenywewe?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi siyo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ni kwa ajili tu ya matengenezo ya zile ofisi zetu zilizoko kule kwenye Kanda na siyo kwa ajili ya mipango ya maendeleo anayoitaja.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 3001 – *Research Development... ... ... ...* Shs. 17,146,932,070/=

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwenye kifungu hicho ambacho nilikitala awali 270300, nataka kujua tu kwamba katika hii *reserch and development* wametenga fedha kwa ajili ya kufanya utafiti wa mikorosho ambayo inasumbuliwa, kila mwaka lazima tupulizie madawa na wananchi hawana uwezo wa kupulizia. Je, fedha hizi zimo?

**MWENYEKITI:** Kwamba shughuli hii itafanyika na fedha hizi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zipo na ndiyo fedha zilizokasimiwa kwa ajili ya Kituo cha Naliendele, Mtwara ambacho ndiyo Kituo Kikuu kinachofanya utafiti wa korosho nchini.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa naomba ufanuzi kuhusu kifungu kidogo 221300 - *Education Material Supplies and Services*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo hiki cha Utafiti mara nyingi sana wakulima hawapati *materials au fliers* ambazo zinahusu tafti mbalimbali zilizofanywa kutokana na mazao yao. Kwanza, naomba kujua, kama kifungu hiki ndiyo kwa ajili ya kutoa vipeperushi kwa wakulima ambavyo vimeonyesha tafti mbalimbali au kama siyo hicho, ni kipi?

**MWENYEKITI:** Amesema! Hebu rudia kifungu mama!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu 2213000 - *Education Materials, Supplies and Services*, lakini ukiangalia pia havijatengewa hata fedha kidogo kwa mwaka huu.

**MWENYEKITI:** Umekiona 2221300? Anauliza: Je, *fliers* za elimu ziko huko?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya masuala ya mawasiliano; kazi hiyo pia tumekusudia itafanywa na *Communication information* ambacho ni kifungu 2212000.

Ni kweli hapa kwenye 221300 - *Education Material, Supplies and Services*, mwaka 2011 zilitengwa Sh. 19,000,000/= na mwaka huu fedha hizo hazikutengwa kabisa, lakini zimekusudiwa zitatengwa kwenye fungu la juu na ni kwa sababu hiyo, masuala ya ufinyu wa bajeti.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki hiki cha utafiti nilikuwa nataka kujua...

**MWENYEKITI:** Kipi hicho? Soma kifungu!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kifungu 3001.

**MWENYEKITI:** Kifungu kidogo kipi? Hatuzungumzii jumla jumla.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Nilikuwa nataka kujua hizi fedha ambazo zime...

**MWENYEKITI:** Sub item gani?

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Kwenye hizi fedha ambazo...

**MWENYEKITI:** Sub item bwana!

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwenye hizi ambazo...

**MWENYEKITI:** Ahaal! Mheshimiwa kama hujajiandaa, kafungu kadogo kadogo, kapi? Tunaendelea.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Nimeshakiona Mheshimiwa Mwenyekiti. Nilikuwa nazungumzia hii sub vote 2300700.

**MWENYEKITI:** Hako ni ka sub item. Haya tunaendelea.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua kwamba tumeanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ambayo na yenye inahusika na mambo ya utafiti pamoja na kwamba walitengewa fedha ili waanze kununua mahindi na kusaga. Sasa nilitaka kujua kama hiyo Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na yenye imetengewa fedha kwenye hicho kifungu.

**MWENYEKITI:** Hamna. Hapo unasema *Routine Maintenance and Repair of Office Equipment and Appliances*.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika 410400 - *Acquisition of Specialized Equipment*, mwaka 2011 ilikuwa ni Sh. 205,000,000/= na mwaka huu ni Sh. 20,000,000/= na huko tulikuwa tunataka kujua: Je, katika fedha hizi katika vituo vyetu vya utafiti vya Mikocheni na Makutupora kwa ajili ya *tissue culture*, hii fedha ndiyo itatumika au kuna fungu lingine?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya utafiti. Katika bajeti ya mwaka huu, vifaa vya Kisayansi kwa ajili ya utafiti vitanunuliwa kupitia kifungu ambacho kinaitwa *Agricultural Equipment* ambazo fedha tayari zimeshatengwa kwa ajili ya utafiti.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu kidogo 221500 - *Agricultural and Livestock Supplies and Services*). Ningependa kujua kwenye hii fedha iliyo tengwa hapa Sh. 99,000,000/= Chuo cha Kibaha cha Utafiti kimoja cha Tanzania ambacho nilikizungumzia sana wakati nachangia kwa kuongea hapa Bungeni, kipo kwenye kuendelezwa mwaka huu kwenye hizi fedha au kiko wapi? Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimo lakini siwezi kumwambia ni kwa kiasi gani katika hizi Sh. 99,000,000/=.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *Program 50, sub vote 5001, sub item 270600 - Current Grant to Non-Financial Public Units (Agencies)* Sh. 30,000,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa hizi Sh. 30,000,000,000/= ndizo ambazo zinakwenda kununulia mahindi kwa wakulima. Fedha hizi wakulima wanapouza mahindi yao huwa wanakatwa ushuru. Yaani...

**MWENYEKITI:** Aah! Mheshimiwa, tusiende mbali. Hizi fedha ni za kazi gani? Ndiyo swali lenyewe? Maana unaendelea kutoa hotuba wakati pengine kazi yake siyo hiyo. Hebu uliza swali lako vizuri.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, nilikuwa nafahamu hizi fedha ni za ununuza wa mahindi. Sasa huwa wanakata wakulima kodi na wanapokatwa kodi yao...

**MWENYEKITI:** Naomba uulize swali, wakikata kodi kule inaingia humu tena?

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inaingia kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, *Food Security*...

**MWENYEKITI:** Hapana!

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hawawalipi Halmashauri. Mwaka 2011 Halmashauri hatujalipwa fedha hizo Sh. 83,000,000/. Nilikuwa nataka kufahamu kama Serikali inaweza ikasaidia wakalipwa na mwaka huu usiendelee kutolipwa ushuru wao.

**MWENYEKITI:** Kwamba hizi fedha ni za kulipa hiyo kodi? Ndiyo swali lenyewe. Tunazungumzia hizi Sh. 30,000,000/, no other money.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Fedha hizi za kulipa wakulima na kulipa kodi ya ushuru, ni za Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya *operations* zile za kawaida za watumishi pale. Lakini pia fungu kubwa ni kwa ajili ya kununulia mazao hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijibu maswali ya awali hapa, katika kipindi chako tumekusudia kwamba Halmashauri zinazodaiwa na *NFRA* zitalipwa fedha yake na *NFRA* imetengewa fedha kwa ajili ya kulipa madeni hayo mwaka huu.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *Sub vote 5001 Item 270600, ziko Shilingi bilioni 30. Ningependa kujua, kuna tatizo kubwa la mizani,...*

**MWENYEKITI:** Kanuni inasema akishauliza mwenzio kifungu kilekile, wewe tena huulizi maana yake maelezo ni hayo hayawezi kuwa tofauti. Ni tofauti, lakini...

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Ni tofauti Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Hapana, ndio hicho kifungu chenyewe? Fedha ni Shilingi bilioni 30, haiwezi kuwa na maelezo tofauti. Yaani unanielewa ninachokisema? Mheshimiwa naomba uketi chini. Tunachozungumzia hapa ni Sh. 30,904,956,850/. Amekwambia kazi yake ni nini, sasa wewe huwezi kuuliza habari nyingine, maana yake kazi yake umeshaambiwa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua tu kwa nini kwenye hiyo *sub vote 221200, safari hii hakijapangisha fedha na upo umuhimu wa kuwasilisha mawasiliano kati ya Wizara na wananchi?*

**MWENYEKITI:** Hebu rudia tena *sub item*, hatujakusikia vizuri.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Sorry! Ukienda kwenye kasma ya 221300, haina fedha kabisa.

**MWENYEKITI:** Tulikuwa tunataka *sub item* yenyewe, tulikuwa hatujasikia. Mheshimiwa Waziri umeiona *sub item*? Kwa nini haijapangiwa fedha?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hapa amezungumza kasma 2213000 kwenye *Education Materials and Supplies and Services*, hazikutengewa fedha kwa sababu ya ufinyu wa bajeti tu. Lakini hata mwaka 2011 fedha zilitengwa kidogo, Sh. 7,000,000/= mwaka huu ikaonekana zitengwe zitafanywa na Idara nyingine na mikakati mingine.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

#### **MATUMIZI YA MAENDELEO**

##### **Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1003 – *Policy and Planning* ..... Shs. 19,840,181,700/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake*)

Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute* .... Shs. 1,596,700,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 2221 - *Agriculture and Training Institute*. Wakati wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri alisema kwamba Chuo cha Moshi na cha Tumbi Tabora cha Kilimo vimetengewa fedha za kufanya ukarabati mwaka huu. Naomba kujua hapa kwenye *Agriculture and Training Institute*, hii fedha iliyotengewa hapa Sh. 438,000,000/=, hivi Vyuo pia viko hapa hapa? Maana yake naona fedha ni kidogo sana. Ahsante.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetenga Sh. 100,000,000/=, ni kweli fedha haziwezi kutosha kumaliza kazi zote. Lakini tutaendelea kutumia fedha hizi kidogo kidogo kwa wakati mpaka hapo tutakopomaliza kazi hii. Inawezekana kabisa zisimalize kazi hii yote ambayo imepangiwa kwa vituo vyote.

**MWENYEKITI:** Lakini vyuo hivyo vimo hapo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo hivyo vimo hapo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 1009 – *Mgt. Information Systems Unit* ... Shs. 92,623,700/=  
(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 1010 – *Environment Management Unit*... Shs. 184,828,900/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2001 - *Crop Development*... Shs. 13,333,942,000/=

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa kifungu 2001- *Crop Development sub vote* 4486, Sh. 12,000,000,000/=.  
*Crop Development* ni pamoja na kusaldia kutengeneza au kulima mbegu kama vile mbegu za pamba. Nilipokuwa natoa mchango wangu, nilisema kwamba mbegu hizi zinazuwa kwa Sh. 1,000/=.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali linalohusika. Sh. 12,933,942,000/=, je, ndio za mbegu ya pamba? Maana yake usitoe hotuba hapa, muda wenyewe mdogo. Haya uliza vizuri.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Naomba nimalizie swali langu.

**MWENYEKITI:** Naomba usitoe *narration* ya nini kinachofanyika, tulishaongea. Hapa unatakiwa uulize hizi Sh. 12,000,000,000/= kazi yake ni kitu gani, ndio maswali yenyewe. Hatuongezi wala hatupunguzi.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Nilikuwa natumia dakika tatu zangu. Kwa kuwa umeonyesha wazi kwamba mbegu hizi ambazo ni *linked* ni kama vile zinasukumwa na Serikali kwa lazima na bei yake ni ya juu, Sh. 1,500/= kwa kilo badala ya Sh. 300/= kwa kilo. Je, hizi fedha za Serikali, Shilingi bilioni 12 ndio zitakwenda kwa mradi wa namna hiyo ambaao kwa maoni yangu hauleti tija?

**MWENYEKITI:** Hilo ndio swali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki 4886 - ASB extension, hizi Shilingi bilioni 12 ni fedha za nje ambazo zimeongezeka sana kutohana na mchango mkubwa wa Serikali ya Japan kwa ajili ya *policy and human resource development*. Kwa hiyo lina mambo mengi, na katika hilo analolizungumza Mzee Cheyo la tofauti ya mbegu baina ya Sh. 300/= na Sh. 1500/= haliko hapa. Hilo ni suala ambalo liko kwenye utafiti baina ya mbegu ambayo ni mbegu za kienyeji na mbegu za kisasa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. 4409 *PADEP*. Tuliona huko nyuma inasaidia sana. Kwanini haikutengewa fedha?

**MWENYEKITI:** Ya mwanzo kabisa. Lakini siyo mwaka huu tu hajapangwa hela, hata mwaka mwingine ilikuwa haina hela.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi ni mradi ambao unakwenda mwisho. Kwa hiyo, siyo mwaka huu tu, hata mwaka uliopita tulianza kusimama kwa kuitengea fedha.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 2002 – *Agricultural Mechanization* . . . . . Shs. 4,670,536,400/=

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nauliza, ile 4486 - *Agriculture Sector Development Program* naona imetoka Shilingi milioni 248 mpaka Shilingi milioni 500. Sasa nilitaka kujua, imeongezeka kwa sababu gani? Lakini nataka pia kufahamu kwamba, kuna mawakala ambaao wali-supply mbolea mwaka 2011. Je, hizo fedha ni kifungu hiki au ziko kwenye kifungu gani? Kwa sababu hawajalipwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, *Agricultural Mechanization* haiwezekani kuwa *supply* ya mbolea. Mheshimiwa Jitu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika hizi Shilingi bilioni 4.97: Je, hapa kumewekwa fedha kwa ajili ya kupeleka vifaa vya *mechanization* katika Vyuo vyetu vya ufundishaji?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya kazi za *mechanization*. Siyo zote, lakini ni pamoja na mchango wetu wa Serikali kwa ajili ya vifaa hivi ambavyo ni vya *mechanization* huko kwa wananchi. Wala siyo kwamba Serikali ndiyo

itafanya kazi zote za kupeleka vifaa. Wapo hata watu binafsi na mashirika wanafanya shughuli hizo. Lakini sisi pia tuna *stake* katika hiyo. Kwa hiyo, huu ni mchango wa Serikali katika kazi hii.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, majibu ya Waziri yametosheleza na yamekidhi.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 2003 – *Agricultural land use planning & Mgt* ... Shs 361,897,800/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kif. 2005 – *Irrigation and tech Tech Servc* ... Sh 16,414,154,200/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 4486 - *Agricultural Sector Development* na hii inahusiana na masuala ya umwagiliaji. Ni ukweli ulio wazi kwamba sasa hivi kuna mabadiliko makubwa ya tabia nchi na nchi yetu imeendelea kuwa kame, na kwa maana hiyo, kilimo cha umwagiliaji tu ndiyo itakuwa tija kwa Taifa letu. Lakini ukiangalia fungu hili katika *local funds* ni Shilingi bilioni saba wakati mwaka 2011 tulikuwa na Shilingi bilioni 10, na hali ya ukame inaendelea kuzidi. Nilikuwa naomba sababu ya fedha zetu za ndani kupungua huku tukijua kabisa fedha za nje tunazitegemea, lakini mara nyingi zinapika kwa kucheleva au kutokupata kabisa.

**MWENYEKITI:** *Actually*, siyo Shilingi bilioni saba ni Shilingi bilioni tano kwa sababu wamefanya *amendment*. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda hajapata kusoma kwenye *addendum*, lakini majibu halisi ni kwamba, kama tulivyosema baada ya wenzetu kuahidi kutupatia fedha zile dola millioni 897, haiwezekani sisi kama nchi tukakaa tu tuisitenge kiasi fulani. Kwa hiyo, tulichokifanya kulingana na bajeti ili yopo hapa, tumejaribu *allocate* fedha kutoka kwenye maeneo mengine ili eneo lile la *SAGCOT* nalo liweze kupata fedha za ndani. Kwa hiyo, huu ni mchango wetu ili angalau tuwa-*encouraged* wale wenzetu ambao wanatuchangia wasione kama wao wanaleta fedha zao tu, sisi hatuna kitu tunachokiweka. Ndiyo maana unaona fungu limepungua kidogo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 3001- *Research Development* ... Shs. 8,955,214,300/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 4486 - *Agricultural Sector Development Programme* wameonyesha kwamba Shilingi milioni 8.5 zitatokea nje. Naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo endapo hao wafadhili hawatataoa hizo fedha, mradi huu utatekelezwa kwa kutumia fungu gani?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwambia Mheshimiwa Nyerere, kwanini kila wakati tukae tunawawazia hawa watu jambo bay? Sisi tumejipanga kwamba tumeweka fedha za ndani na tunatarajia pesa za kutoka nje. Ni dhahiri kabisa pesa za nje zitakapokuwa hazijafika, tutatekeleza kwa kiwango kulingana na fedha zile za ndani tulizonazo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

Kif. 5001 - *National Food Security* ... Shs. 1,810,075,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake*)

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilitaka kujua katika kifungu hiki kama pesa kwa ajili ya kununua mizani iko hapa, kwa sababu kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi kipindi cha kununua mazao na msongamano mkubwa sana wakati wa kusafirisha mazao.

**MWENYEKITI:** National Food Security, mizani ni wapi? Hebu tuambie Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli havihusiani. Lakini nadhani ana hoja nzuri kutokana na soko la pamba. Niseme tu mizani hii inanunuliwa siyo katika fungu hili. Mizani hii wanunuwa wenye kwenye mafungu hayo. Kwa hiyo, fedha hizi hazihusiki na fungu hili. Ni kwamba, mizani ile ya rula ambayo tulikuwa tumeizua mwaka huu, tumekubali itumike sambamba na ile ya *digital*.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku. Katika fungu hili kama unavyokumbuka, ulituagiza kwenda Iringa kuangalia kinu cha usagishaji unga. Tunataka kujua kwamba kweli Serikali hivi sasa katika fungu hili wametenga kuwezesha Bodi ya Mazao Mchanganyiko kuanza kusagisha unga na kuingiza katika soko ili kushusha bei ya vyakula na mfumko wa bei kwa wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa hizi ni kwa ajili ya mikakati ya kuongeza thamani kwenye mazao. Lakini hilo analoliulizia Mheshimiwa Mangungu ni kweli limefanyiwa kazi ili Bodi ya Mazao Mchanganyiko iweze kuijingiza moja kwenye kusagisha na hasa kwenye kile kinu cha Iringa Mjini, ndicho tunachokusudia kuanza nacho kwa maana ya kukusanya mahindi *around*, kusaga pale na kusambaza.

**MWENYEKITI:** Fedha ndiyo hizi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana, siyo hizi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati  
ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirejea)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawashukuru wote waliochangia hoja yangu hii. Sasa naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuitia makadirio ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2012/2013, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe rasmi na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka 2012/2013  
yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Waziri na Watendaji wako Wakuu wajue kwamba tunategemea kilimo. Kwa hiyo, wazidi kufanya kazi vizuri zaidi na matumizi mazuri ya fedha zinazohusika. Tunaendelea.

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 –  
Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto**

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, na kwa kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ikiongozwa na Mwenyekiti wake mahiri, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama na Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia kwa kuchambua na kujadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri na maelekezo ya Kamati hiyo yameiwezesha Wizara kuandaa na kuboresha bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, nami kwa majozini makubwa nitoe salamu zangu za pole kwa Watananzia wote kwa ajali kubwa ya meli ya *MV Skagit* iliyotoka katika bahari ya Hindi. Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira wenzetu waliondokewa na ndugu na jamaa. Pia tunawaomba Marehemu wote wapumzike mahali pema Peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, aidha, nakupa pole wewe na Waheshimiwa Wabunge wote ambaa waliondokewa na ndugu na wapenzi wao. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Merehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kwangu na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ninaahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuendelea kutekeleza majukumu niliyopewa kwa kushirikiana na watumishi wenzangu na wadau wengine wote ndani na nje ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa umahiri wake katika kuongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. Chini ya uongozi wake, Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wakati wa uchaguzi Mkuu, na kama zilivyoainishwa katika llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yameweza kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini na washirika wa maendeleo kuona umuhimu wa kuendelea kuiunga mkono Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Makamu wa Rais - Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal kwa uongozi wake bora. Nampongeza pia Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Aidha, hotuba alioitoa kwenye Bunge lako Tukufu wakati akiwasilisha Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2012/2013 ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi na imeonyesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2012/2013. Nampongeza pia Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Dkt. Willam Augustao Mgimwa kwa hotuba yake ambayo imainisha misingi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Pia nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu - Mheshimiwa Stephen Masato Wasira kwa hotuba yake kuhusu hali ya Uchumi ya mwaka 2011/2012 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2012/2013. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza wafuatao kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, kuwa Waziri wa Fedha; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali H. Mwinyi, kuwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Balozi Khamis Sued Kagasheki, kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Prof. Sospeter M. Muhongo, kuwa Waziri wa Nishati na Madini; Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe, kuwa Waziri wa Uchukuzi; Mheshimiwa Dkt. Fenella E. Mukangara, kuwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara; Mheshimiwa Eng. Christopher K. Chiza, kuwa Waziri wa Kilimo, Chakula na

Ushirika na Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, kuwa Waziri asiyé na Wizara maalumu. Halikadhalika nampongeza Mheshimiwa James Mbatia kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Alhaj Adam Omar Kimbisa, Mheshimiwa Shy-Rose Saddrudin Banji, Mheshimiwa Anjela Charless Kizigha, Mheshimiwa Maryam Ussi Yahaya, Mheshimiwa Ndirakindo Perpetua Kessy, Mheshimiwa Dkt. Twaha Issa Taslima, Mheshimiwa Abdullah Ali Hassan Mwinyi, Mheshimiwa Bernard Musomi Murunyana na Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Nawataki kila la kheri katika kutekeleza majukumu yao ya kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa umahiri wako katika kusimamia na kuratibu shughuli za Bunge kwa ufanisi na umakini mkubwa. Nawapongeza pia Naibu Spika - Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge wa Kongwa na Waheshimiwa Wenyevitii wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, natoa salamu za rambirambi kwa familia za Marehemu Mheshimiwa Musa K. Silima, aliyekuwa Mbunge mteule kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Marehemu heshimiwa Jeremiah Solomon Sumari, aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki na Marehemu Mheshimiwa Regia Estelatus Mtima, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu Morogoro. Michango yao katika Bunge lako Tukufu itakumbukwa daima. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia maeneo manne ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010; Hali halisi ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii na changamoto zilizopo; Utekelezaji wa mpango wa Mwaka 2011/2012; Malengo ya mwaka 2012/2013 na maombi ya fedha za utekelezaji wa mpango wa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mafanikio ya Wizara yangu katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa kipindi cha Januari 2011 hadi Machi 2012.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM, Ibara ya 78 imeelekeza kuimarisha na kupanua mafunzo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili vipokee vijana wengi zaidi na kuwapatia mafunzo ya maarifa ya kisasa katika fani za kilimo, biashara, ufundi stadi na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi, imetoa mafunzo ya maarifa na stadi mbalimbali kwa wananchi 62,702 wakiwemo wanawake 29,764 na wanaume 32,938 ili kuinua viwango vya uzalishaji kwenye kazi zao. Hii ni sawa na asilimia 96.8 ya lengo. Aidha, Wizara ilifanya ukarabati mdogo katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Muhukuru.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 85 ya Ilani ya CCM imeelekeza kuongeza udahili wa wanafunzi katika Vyuo vya Elimu ya Juu. Katika kutekeleza azma hii, Wizara kuitia Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru iliendelea kudahili wanafunzi katika shahada ya kwanza ya fani za upangaji na usimamizi shirkishi wa miradi, maendeleo ya jamii, maendeleo ya jinsia na stashahada ya uzamili ya maendeleo ya jamii. Jumla ya wanafunzi 173 wakiwemo wanawake 103 na wanaume 70 walidahiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika ibara za 204 na 205 ya Ilani ya CCM ya mwaka 2010, imeelekezwa kuwa mikataba ya haki za wanawake na watoto iliyordhiwa itekelezwe kikamilifu. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeandardi rasimu ya tafsiri ya Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 katika lugha ya Kiswahili, na kukamilisha taarifa ya tatu, nne na tano ya nchi kuhusu Utekelezaji Wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto na kuiwasilisha katika Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Mtoto.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na Wizara kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuwapatia mikopo yenyé masharti nafuu kuitia Benki ya Wanawake Tanzania na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012, Benki ya Wanawake

Tanzania ilitoa mikopo yenye thamani ya Sh. 1,285,550,000/= kwa wanawake 5,270 na wanaume 1,157. Aidha, Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 120 katika Halmashauri 15 zilizofanya marejesho ya mikopo ya awali.

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti ukatili dhidi ya wanawake, Wizara imeunda na kuzindua Kamati ya Kitaifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto. Aidha, imeandaa Mwongozo wa Kudhibiti Ukatili wa Kijinsia na Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Nchini kwa lengo la kutumiwa na Kamati za Ukatili wa Kijinsia, Ulinzi na Usalama katika ngazi za Mikoa, Halmashauri za Wilaya pamoja na wadau wengine nchini.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 188 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, imeelekeza kuhakikisha kwamba Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) yanajishughulisha na majukumu ambayo yameandikishwa kufanya na kwamba hayapati nafasi ya kuijendesha kinyume na makusudio hayo.

Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara iliendelea kuelimisha wananchi kuhusu matakwa ya Sera ya Taifa ya *NGOs* (2001), Sheria ya *NGOs* Na. 24 (2002) na Kanuni za Maadili ya *NGOs* kwa wadau 4,047. Wadau hao walitoka katika Taasisi za Elimu, Taasisi za Fedha, Taasisi za Kiserikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na watu binafsi. Fursa zilizotumika kutoa elimu hii ni kupitia Ofisi ya Msajili wa *NGOs*, Mikutano ya Bodi ya Taifa ya Uratibu wa *NGOs*, Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma na Maonesho ya Saba Saba kwa lengo la kuwawezesha kukidhi matakwa ya sheria, taratibu za usajili na kutoa taarifa kwa Msajili wa *NGOs* pindi mashirika hayo yanapojidesha kinyume na taratibu zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii kwa ujumla imeendelea kuimarika. Kuimarika kwa sekta kumetokana na ushirikiano mzuri tuliuopata kutoka kwa wadau wetu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Majukumu yalilenga kufanikisha uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, usawa wa kijinsia, upatikanaji wa haki za mtoto na uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, hali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi inaridhisha. Vyuo vimeendelea kutoa mafunzo ya stadi na maarifa yanayowezesha wananchi kujajiri na kuajiriwa, hivyo, kuwapunguzia umaskini. Udhili wa wananchi katika Vyuo hivi umeongezeka kutoka 31,877 mwaka 2010/2011 na kufikia 32,133 mwaka 2011/2012. Vyuo hivi kwa sasa vina umuhimu mkubwa kutokana na ukweli kwamba vinadahili idadi kubwa ya vijana walliomala Elimu ya Msingi na Sekondari ambao hawakufanikiwa kuendelea na mafunzo ya juu. Pamoja na umuhimu wa Vyuo hivi, hali ya majengo na miundombinu yake bado ni chakavu kutokana na ukosefu wa matengenezo ya mara kwa mara. Changamoto nytingine ni uhaba wa vyombo vya usafiri, upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali, nyumba za watumishi, madarasa, karakana, mabweni, vifaa na mitambo ya kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wataalamu wa maendeleo ya jamii katika ngazi za Taifa, Mkoa na Halmashauri ni ya kuridhisha. Hali hii imesababisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo kuendelea kuimarika. Ushiriki huu umetokana na matumizi ya mbinu shirkishi katika uandaaji na utekelezaji wa programu mbalimbali za maendeleo zinazowezeshwa na wataalamu hawa katika ngazi ya Kata na Vijiji. Changamoto inayokabili eneo hili ni upungufu wa wataalamu wa maendeleo ya jamii katika ngazi ya Kata. Hivi sasa ni Kata 1,329 tu katil ya Kata 3,321 zenye wataalamu hawa, sawa na upungufu wa asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, jitihada za kufikia usawa wa kijinsia na kuwapatia uwezo wanawake kupitia programu mbalimbali za maendeleo zimeendelea kuimarika. Hii inatokana na Serikali kutambua kuwa usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wa wanawake ni masuala muhimu kufikia maendeleo. Maeneo ambayo yamezingatia usawa wa kijinsia ni pamoja na nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali. Mfano, uwakilishi wa wanawake katika Bunge, Halmashauri za Wilaya na Taasisi mbalimbali za Serikali. Aidha, udhili wa wanafunzi katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo umezingatia usawa wa kijinsia. Pamoja na mafanikio hayo, bado zipo changamoto ambazo zinakwamisha juhudi za kuleta usawa wa kijinsia. Mpaka sasa bado zipo mila, desturi na imani potofu ambazo zinaendelea kuathiri haki ya wanawake katika masuala ya kutoa maamuzi na

kushika nafasi mbalimbali za uongozi. Aidha, suala la mimba na ndoa za utotoni zinachangia katika kudhoofisha maendeleo ya elimu ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, jitihada nyine ambazo Wizara imefanya katika kuleta usawa wa kijinsia ni kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, mila zenyne madhara kwa wanawake na watoto wa kike, ukatili kwa watoto na albino. Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo na Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Nchini kwa lengo la kutumiwa na Kamati za Ukatili wa Kijinsia, Ulinzi na Usalama katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri pamoja na wadau wengine nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008 na Sheria ya Mtoto Na. 9 ya mwaka 2009 ili kuleta maendeleo na upatikanaji wa haki za mtoto kote nchini. Baadhi ya jitihada ambazo zimefanyika ni pamoja na kuratibu maandalizi ya seti saba za kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 (2009). Seti hizo za kanuni ni pamoja na Makao ya Watoto, kuasili, Shule za Maadilisho, Mahabusu ya Watoto, *Apprenticeship, Creches*, na Kulelea Watoto Mchana.

Aidha, seti nne za kanuni zinafanyiwa kazi. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa dhidi ya vitendo mbalimbali vya kikatili na hatimaye kuishi katika mazingira salama. Changamoto iliyopo katika utoaji wa haki za msingi za mtoto ni pamoja na ongezeko la watoto wanaoishi/kufanya kazi Mitaani, tatizo la VVU na UKIMWI na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyofanywa na wazazi/walezi. Mmomonyoko wa maadili pamoja na umaskini uliokithiri mionganii mwa jamii ya Watanzania, ni katii ya sababu kuu zinazochangia ongezeko la watoto wanaoishi/kufanya kazi Mitaani.

Mheshimiwa Spika, Mashirika yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakiongezeka na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii. Hivi sasa kuna jumla ya mashirika 6,669 yaliyoandikishwa chini ya Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002. Kati ya hayo mashirika 5,837 yamepatiwa Cheti cha Usajili na mengine 832 yalipatiwa Cheti cha Ukubalifu. Mashirika haya yanafanya kazi katika ngazi ya Wilaya, Mkoa, Taifa na Kimataifa. Aidha, shughuli za mashirika haya zimejikita katika nyanja mbalimbali za maendeleo ikiwemo haki za binadamu, maendeleo ya jinsia, afya, elimu, maendeleo shirkishi, kilimo, mazingira, haki za watoto, ustawi wa jamii na utetezi kuhusu sera mbalimbali. Changamoto zinazokabili NGOs kwa sasa ni utegemezi mkubwa kwa wafadhili na kutokuwepo mfumo madhubuti wa kubainisha michango yao katika maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi. Aidha, katika mwaka 2012/2013 maeneo matatu yafuatayo yamepewa kipaumbele:-

(i) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na mafunzo ya maarifa, ujuzi na stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, hususan kuongeza mafunzo ya ufundi stadi katika Vyuo 25 vya Maendeleo ya wananchi;

(ii) Kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili washiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo kwa kuendelea kutambua fursa mpya na muafaka hasa za kiuchumi zinazojitokeza katika maendeleo yao; na

(iii) Kusimamia sera na sheria na kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, kikanda na kimataifa inayohusu ustawi, haki na maendeleo ya wanawake na watoto kwa kutoa miongozo ya kukusanya takwimu za watoto wanaonyanyaswa na wanaoishi Mitaani.

Mheshimiwa Spika, hali ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2011/2012 na malengo ya mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, taaluma ya maendeleo ya jamii ni muhimu katika kuwajengea uwezo na fikra sahihi wananchi na kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za maendeleo. Taaluma hii

hapa nchini hutolewa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo viko tisa nchini. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Vyuo hivyo, ilidahili jumla ya wanachuo 3,074 wakiwemo wanaume 830 na wanawake 2,244. Jumla ya wanachuo 173 walidahiliwa katika ngazi ya shahada, wanachuo 385 ngazi ya stashahada na wanachuo 2,516 ngazi ya astashahada. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kudahili wanachuo katika taaluma ya maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Wizara yangu katika mwaka 2011/2012 iliyafanya ukarabati majengo na miundombinu katika Vyuo. Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Mabughai – Lushoto, Tanga Kilifanyiwa ukarabati. Aidha, vyanzo vya maji vya Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Mlale – Songea vijiji, Mkoani Ruvuma vilijengewa uzio ili kuhifadhi na kulinda mazingira yake. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu inatarajia kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo vingine, kwa kutegemea rasilimali fedha zitakazopatikana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu ililendesha Mkutano Mkuu wa mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya jamii. Mkutano huo uliwapa fursa wataalamu wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii na wadau wake kutathmini mwenendo wake na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo katika sekta hiyo hapa nchini. Jumla ya washiriki 280 kutoka Wizarani, Vyoni, Halmashauri, Sekretariati za Mikoa na sekta nydingine walihudhuria.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya ujuzi na stadi mbalimbali kwa wananchi yana umuhimu wa pekee kwa sasa kwa sababu yanawawezesha wananchi kujajiri na kuajiriwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi iliwapatia mafunzo ya ujuzi na stadi wananchi 32,133 wakiwemo wanawake 15,632 na wanaume 16,501. Wizara inaendelea kuwashauri wahitimu kujungu katika vikundi vya uzalishaji mali ili waweze kukopesheka kirahisi. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itadahili na kutoa mafunzo kwa wananchi 35,820 ndani na nje ya Vyuo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi, itaanzisha rasmi mafunzo ya ufundi stadi yatakayofuata mfumo wa VETA. Jumla ya vijana 1,250 watadahiliwa katika Vyuo hivyo kuanzia mwezi Januari, 2013. Mfumo huo utawezesha wahitimu kujajiri, kuajiriwa na pia kuijendeleza kupitia mfumo rasmi wa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, Wizara yangu ililendelea na ukarabati katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Muhukuru kwa mwaka 2012/2013. Wizara imeandaa utaratibu wa ukarabati kwenye Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi vinavyotarajiwa kuendesha mafunzo ya ufundi stadi kwa mfumo wa VETA. Vilevile, Wizara itajenga karakana zisizopungua tano na kuziwekea vifaa vipyaa vya mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ililandaa programu ya kutoa mafunzo na kusambaza teknolojia sahihi kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wa kazi wananchi na kuwaongezea kipato. Hivyo, kukuza uchumi wao. Hadi mwezi Machi, 2012 wakufunzi 52 walipatiwa mafunzo hayo. Sambamba na mafunzo hayo, aina sita za teknolojia rahisi zilinunuliwa na kusambazwa vyoni. Teknolojia hizo ni mashine za kufyatulia tofali, wanyama kazi, mikokoteni, mashine za kuangulia vifaranga, mashine za kukaushia matunda na mboga za majani na meko sanifu. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusambaza teknolojia hizo ili ziweze kuwafikia wananchi wengi vijiji.

Mheshimiwa Spika, uwezesajhi wanawake kiuchumi ni suala linalopewa kipaumbele katika kutekeleza mikataba na maazimio mbalimbali yanayohusu maendeleo ya wanawake. Ili kuwakwamua wanawake kiuchumi, Wizara yangu ililendelea kuratibu na kusimamia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa kushirikiana na Halmashauri. Katika kipindi cha 2011/2012, Wizara yangu kupitia mfuko huo ilitoa jumla ya Shilingi milioni 120 kwa Halmashauri 15 zilizokamilisha marejesho ya mikopo kwa ajili ya kuwakopesha wanawake wajasiriamali. Wanawake hao hupewa mikopo yenye masharti nafuu ambayo wanapaswa kuirejesha ndani ya mwaka mmoja, ili wanawake wengine waweze kukopeshewa. Mikopo hii itaendelea kutolewa kwa kipindi cha mwaka 2012/2013 ili wanawake waendelee kunufaika na kujkwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa masoko ni tatizo linalowakabili wanawake wengi wafanyabiashara. Ili kupunguza tatizo hili, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*) na wadau wengine imekuwa ikiwezesha wafanyabiashara wanawake kupata masoko ndani na nje ya nchi. Mkakati unaotumika ni kuwapatia mafunzo ya biashara na ujasiriamali na kuwawezesha kushiriki maonesho ya kimataifa ya biashara hapa kwetu na nje ya nchi. Kwa mwaka wa fedha uliopita, jumla ya wanawake 350 walipatiwa mafunzo ya biashara na ujasiriamali na kuwezeshwa kushiriki katika maonesho ya biashara ya kimataifa ya Dar es Salaam.

Aidha, wanawake 20 (15 kutoka bara na 5 kutoka visiwani) waliwezesha kushiriki maonesho ya biashara ya kimataifa nchini Rwanda ambako pia mimi mwenyewe nilihudhuria na baadhi ya wataalamu wa Wizara. Kwa mwaka 2012/2013 Wizara yangu itaendelea kuratibu na kusimamia ushiriki wa wanawake wajasiriamali katika maonesho mbalimbali ya biashara ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, taarifa za ukatili wa kijinsia zimekuwa zikitolewa kwa wingi sana na vyombo vya habari (*TV, radio* na magazeti). Hali hii imetokana na elimu na hamasa kubwa iliyotolewa na Wizara yangu na wadau wengine. Katika kukabiliana na tatizo hili, Wizara yangu katika kipindi cha mwaka 2011/2012, iliratibu Mkutano wa Mawaziri wa Maendeleo ya Wanawake na Jinsia kutoka Nchi Wanachama wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Arusha tarehe 04 Novemba, 2011.

Lengo la Mkutano huo ilikuwa ni kuandaa mapendekezo kuhusu kutokomeza ukatili wa kijinsia katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Mapendekezo hayo yaliwasilishwa na kuitishwa na Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano Maalumu uliohusu upigaji vita ukatili wa kijinsia uliofanyika tarehe 16 Desemba, 2011 Kampala Uganda. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuratibu na kutekeleza mipango na mikakati ya kutokomeza ukatili wa kijinsia. Aidha, Wizara itatoa elimu zaidi na mbinu thabitii za kuzuia na kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, juhudii nyingine zilizofanyika ili kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini, ziliikuwa ni uzinduzi wa Kamati ya Kitifa ya Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake, Watoto na Albino tarehe 19 Desemba, 2011. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Umoja wa Afrika, iliandaa tukio la kupanda Mlima Kilimanjaro ambalo kaulimbiu yake ilikuwa "*Speak Out-Climb Up*". Jumla ya washiriki 74 kutoka nchi 36 za Afrika, Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika walishiriki katika zoezi hilo ambalo lilitinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete -Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 05 Machi, 2012.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kampeni hii yalikuwa ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu madhara ya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika Afrika na kuziomba Serikali husika ziujibike katika kupiga vita ukatili kwa wanawake na wasichana. Katika Kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii ili kupiga vita ukatili wa kijinsia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imesaini na kuridhia mikataba mbalimbali inayohusu maendeleo ya jinsia na wanawake. Ili kuweza kutekeleza mikataba na maazimio hayo, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Hali ya Wanawake, Kikao Maalumu cha Baraza kuu la Umoja wa Mataifa (*United Nations General Assembly Special Session - UNGASS*) na Mkutano wa Maziwa Makuu Kuhusu Masuala ya Wanawake. Maazimio ya Mikutano hiyo pamoja na mambo mengine yalikuwa ni kuinua kiwango cha usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kushiriki katika Mikutano hiyo na kuratibu utekelezaji wa makubaliano yatakayoafikiwa.

Mheshimiwa Spika, sanjari na kuanzisha madirisha ya taarifa kwa wanawake, Wizara imeanzisha Kituo cha Utafiti na Utunzaji Kumbukumbu za Wanawake katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru. Kituo hicho ni tawi la Kituo cha Kanda cha Utafiti na Utunzaji Kumbukumbu za Wanawake kilichopo Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo. Kituo hiki kina umuhimu wa pekee wa kuwawezesha Watanzania kupata matokeo ya tafiti mbalimbali zinazohusu jinsia

zinazofanywa katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu kupitia Maktaba ya Digitali. Aidha, matokeo ya tafiti zitakazofanywa na Kituo cha Tengeru yataweza pia kusambazwa kwa nchi wanachama wa Maziwa Makuu kupitia Maktaba ya Digitali. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau (*UNESCO*) itaendelea kukiimarisha Kituo hicho kwa kukiongezea vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutafakari mafanikio na changamoto zinazokabili jamii, hususan wanawake, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali huratibu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani tarehe 08 Machi, kila mwaka.

Lengo la maadhimisho haya ni kuwakutanisha wanawake ili waweze kubadilishana uzoefu katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili. Kila mwaka maadhimisho haya huambatana na kaulimbiu kulingana na mazingira na uhitaji wa wakati husika. Kaulimbiu ya mwaka 2012 ilikuwa ni "Ushiriki wa Wasichana, Unachochea Maendeleo." Kaulimbiu hii illenga kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwashirikisha wasichana katika mipango mbalimbali ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa fursa sawa kati ya wasichana na wavulana katika elimu, mafunzo, uchumi, siasa na utamaduni. Wizara yangu itaendelea kuratibu maadhimisho haya mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, suala la ulinzi na ustawi wa watoto ni mojawapo ya kipaumbele cha Wizara. Ili kutimiza ule msemo kuwa "watoto ni taifa na viongozi wa kesho", tunapaswa kuwalinda na kuwakinga dhidi ya maambukizi ya magonjwa yakiwemo UKIMWI pamoja na ukatili wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya watoto hapa nchini, iliunda Kikosi Kazi cha Kitaifa ambacho kimeandaa rasimu ya awali ya mpango wa miaka mitano wa utekelezaji wa kutatua tatizo la watoto wanaishi/kufanya kazi Mitaani. Mwezi Agosti, 2011, Wizara yangu ilizindua Ripoti ya Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Nchini Tanzania. Ripoti hiyo imetoa makadirio ya awali ya ukubwa na sura ya ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili yanayowasibu wavulana na wasichana hapa nchini. Ripoti hiyo imeonesha kwamba, takribani wanawake watatu kati ya 10 na mwanaume mmoja kati ya saba walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na watu wazima walipokuwa watoto chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kukabiliana na tatizo hili. Aidha, yatasaidia kuanzisha taratibu za kuboresha huduma kwa wahanga wa ukatili na kuandaa miongozo na kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itasambaza kanuni na miongozo hiyo katika Halmashauri zote nchini, ili wananchi waweze kuzielewa na kuzizingatia. Pia, Wizara itatayarisha mwongozo wa kukusanya takwimu za watoto wanaonyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, moja ya haki za msingi za mtoto, kama zilivyoainishwa katika mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda, ni haki ya kushiriki na kushirikishwa katika masuala yanayomhusu. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa masuala ya watoto hapa nchini, iliandaa Zana za Ushiriki wa Watoto (*Child Participation Toolkit*) pamoja na Rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Ushiriki wa Watoto. Zana zote hizi zinalenga kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kumshirikisha mtoto katika masuala yanayomhusu kama ilivyobainishwa katika mikataba ya kimataifa na kikanda kuhusu haki na ustawi wa mtoto. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuimarisha Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mabaraza ya Watoto ya Mikoa na Wilaya ili yaweze kutoa fursa nzuri za ushiriki wa watoto katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Wizara itasambaza zana za ushiriki wa watoto kwa wadau wote wa maendeleo ya watoto hapa nchini ili waweze kuzielewa na kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto ni muhimu katika kujenga msingi wa Taifa lenye watu makini na wanaoweza kukabiliana na changamoto za maendeleo. Mwezi Februari, 2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau iliandaa Mkutano wa Kimataifa uliohusisha wadau wa ndani na nje ya nchi wa masuala ya watoto. Mkutano huu

ulizingatia masuala makuu matatu ambayo ni kuandaa kiunzi (*framework*) kitakachoonesha namna nzuri ya kutekeleza malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, kuanzisha namna bora ya ushirikiano wa kiutendaji, na kutoa fursa kwa wadau kubadilishana uzoefu na maarifa katika masuala yanayohusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu pamoja na masuala mengine uliazimia kwa kukubaliana kuwa wadau wote hasa familia na kaya kuwekeza zaidi katika malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ili kuwa na Taifa bora la baadaye kutokana na ukweli kuwa maendeleo na ukuaji wa mtoto (katika maisha yake yote) hutegemea jinsi aliviyotunzwa na kulelewa kuanzia umri wa siku 0 hadi 1,000. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itakamilisha uandaaji wa Sera Jumui ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kwa kuzingatia maelekezo tuliyopewa na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliratibu maadhisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo yaliadhishwa katika ngazi ya Mkoa. Kila Mkoa ulipata fursa ya kuadhishwa siku hii kulingana na rasilimali zilizopo ikiwa ni pamoja na kushirikiana na Asasi zisizokuwa za Kiserikali katika Mkoa husika.

Kaulimbiu ya mwaka 2012 ilikuwa ni "Haki za Watoto Wenye Ulemavu." Ni jukumu letu kuzilinda, kuziheshimu, kuzitimiza na kuzitekeleza. Kaulimbiu hii ilikuwa inatukumbusha kuwa tuna jukumu la kuangalia upya utoaji wa haki za msingi kwa watoto wenye ulemavu na hasa katika miundombinu na utoaji wa huduma za msingi kama vile elimu na matibabu. Vilevile, Wizara yangu iliratibu maadhisho ya Siku ya Familia Duniani yaliyofanyika kimkoa. Kaulimbiu ilikuwa ni "Uwajibikaji Sawa katika Majukumu: Msingi wa Familia Bora." Kaulimbiu hii illengwa kuhamasisha na kushawishi wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kuwajibika kwa pamoja katika malezi ya familia. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuratibu maadhisho ya siku hizo kwa lengo la kuhamasisha jamii kuhusu haki na ustawi wa mtoto na maendeleo ya familia.

Mheshimiwa Spika, suala la kutokomeza mila zenyenye kuleta madhara kwa jamii ni miongoni mwa masuala yaliyopewa kipaumbele na Wizara yangu. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ilifanya Mkutano na Maafisa Maendeleo ya Jamii kutoka katika Halmashauri zote nchini ili kujadili masuala ya ukeketaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto wa kike. Mkutano huu uliazimia kuendelea kuhamasisha jamii zetu kuhusu madhara yanayowapata watoto wa kike wanapokeketwa. Aidha, kila Halmashauri iliandaa mpango kazi wa kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu imepanga kuendelea kuratibu utekelezaji wa mpango kazi wa kutokomeza ukeketaji na mila nyiningine zenyenye kuleta madhara kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Mashirika rasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) yana umuhimu wa pekee katika kutatua changamoto zinazokabili jamii yetu hasa makundi maalumu. Kwa kutambua umuhimu huo, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kurasimisha ushiriki wa *NGOs* katika shughuli za maendeleo nchini. Jumla ya mashirika 675 yalisajiliwa ambapo kati ya hayo mashirika 646 yalipatiwa Cheti cha Usajili na mashirika 29 yalipatiwa Cheti cha Ukubalifu.

Aidha, katika kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa *NGOs* nchini, Wizara yangu iliteua rasmi Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Wilaya kuwa Wasajili Wasaidizi wa *NGOs* katika ngazi husika. Uteuzi huu utaisaidia sana Serikali kuhakikisha kuwa mipango ya kazi ya *NGOs* inajumuishwa kwenye mipango ya maendeleo ya Halmashauri husika ili kuwepo na utumiaji endelevu wa rasilimali fedha na watu.

Aidha, Bodii ya Taifa ya Utatibu wa *NGOs* ilizinduliwa rasmi. Bodii hiyo ilipewa changamoto ya kubuni utaratibu wa kubaini mchango wa Sekta ya *NGOs* nchini ili uingizwe kwenye pato la Taifa. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kusajili na kuratibu mashirika haya ili kuyawezesha kutambulika na kuendesha shughuli zao kisheria.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya *NGOs* nchini inakabiliwa sana na changamoto ya kujengewa uwezo wa kiuendeshaji na mbinu za kuibua fursa mbalimbali za kutunisha rasilimali fedha ili iweze kuendesha shughuli zake kwa uendelevu. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa

kushirikiana na Mitandao ya Mikoa ya NGOs na Taasisi ya 'The Foundation for Civil Society' iliwezesha kufanyika uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Taifa la NGOs katika awamu ya pili.

Baraza hili jipya, limeazimia kuhakikisha kuwa wadau wote wa Sekta ya NGOs nchini wanatumia Kanuni za Maadili ya NGOs na pia, utaratibu wa sekta yenye ujifanyia tathmini ya utendaji wao ili kuongeza uwajibikaji na uwazi mionganii mwao. Aidha, katika kipindi hiki, NGOs 433 zilipatiwa rasilimali fedha kiasi cha Sh. 11,227,948,101/= . Ikiwa ni ruzuku kutoka Taasisi ya 'The Foundation for Civil Society' ili kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika uchambuzi wa sera mbalimbali, utetezi, uhamasishaji wa jamii kushiriki katika michakato mbalimbali ya kitaifa kama vile Katiba mpya, utawala bora na maendeleo ya kiuchumi kwa ujumla.

Aidha, katika kuhakikisha kuwa taarifa mbalimbali kuhusu Sekta ya NGOs nchini zinapatikana kwa wananchi, Wizara yangu iliendelea kuhuisha Tovuti ya Taifa ya Uaratibu wa NGOs na Benki ya Takwimu na taarifa za NGOs ambapo wadau 26,000 kutoka sekta binafsi, Serikali, wabia wa maendeleo, Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu na Asasi za Kiraia (CSOs) walihudumiwa. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuhimiza taasisi mbalimbali na wabia wa maendeleo kuzijengea uwezo NGOs ili kuimarishe utendaji wao na pia kuongeza uwajibikaji katika Sekta ya NGOs nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la ufuatilaji na tathmini ni muhimu katika kuhakikisha kuwa yanakuwepo matumizi mazuri ya rasilimali za umma katika Wizara. Wizara yangu katika mwaka 2011/2012 iliendelea kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi na shughuli nyiningine katika Wizara ikiwa ni pamoja na kuvitembelea Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vya Maendeleo ya Wananchi. Katika ufuatilaji na tathmini hiyo, Wizara ilibaini kwamba miradi mingi haitakamilika kutokana na upatikanaji mdogo wa rasilimali fedha. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shughuli nyiningine katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, mipango ya maendeleo ni muhimu katika kuleta ufanisi na utaratibu mzuri wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu ilikamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2011 – 2016), unaotoa dira na mwongozo wa utumiaji wa rasilimali ili kuiwezesha Wizara kufanikisha malengo yake. Katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati huo.

Mheshimiwa Spika, watumishi waadilifu na wanaowajibika ni muhimu katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kusimamia utendaji kazi kwa misingi ya haki, usawa, uadilifu, utawala bora na uwazi na kuweka mkazo katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uzembe kazini. Masuala haya ni ya msingi katika kuiwezesha Wizara kufanikisha dira na dhima yake na ya Taifa kwa ujumla. Jitihada hizi zitaendelea kutekelezwa katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa watumishi wenye uwezo ni nyenzo muhimu katika kuleta tija na ufanisi katika taasisi husika. Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia elimu na maarifa kuitia Vyuo vya Elimu ya Juu vya ndani na nje ya nchi. Jumla ya watumishi 60 walipata mafunzo ya muda mfupi, kati na ya muda mrefu katika nyanja mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itawezesha watumishi 30 kupata mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kuwapatia motisha wafanyakazi, Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012 iliwapandisha vyeo watumishi 94, iliwabadilisha kazi watumishi saba na kuwathibitisha kazini watumishi 127. Aidha, iliwaingiza kwenye masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni watumishi 139 na kuwaingiza katika masharti ya kawaida watumishi 66. Kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kupandisha vyeo watumishi kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma ili kuongeza tija katika utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Wizara yangu imekamilisha ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya Wizara. Katika mwaka 2012/2013, Wizara

itaendelea kuboresha mazingira ya nje ya Ofisi kwa kuweka maegesho ya magari, bustani na njia za kupita kwa miguu.

Mheshimiwa Spika, katika kutambua umuhimu wa afya kwa wafanyakazi, Wizara ilienendelea na juhudzi za kuwakinga dhidi ya athari za maradhi hasa UKIMWI. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliwezesha watumishi kumi kupata viini lishe, madawa na chakula. Watumishi hao ni wale walijitokeza kuwa wameathirika na Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa elimu na huduma hizo kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, suala la kujitangaza ni muhimu, kwani linawezesha wadau na umma kwa ujumla kufahamu majukumu yanayotekeliza na Wizara. Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu ilielimisha na kuhamasisha Jamii kuhusu wajibu na majukumu yake kwa kutumia machapisho na matangazo mbalimbali yanayohusu elimu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, aidha, ilitumia maonyesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba), Kilimo (Nanenane) na Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara kuelimisha umma. Katika Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru, Wizara ilijitangaza kuititia uzinduzi wa Kitabu cha Mchango wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii katika Maendeleo ya Tanzania (1961–2011); Kitabu cha Mafanikio ya Miaka 50 ya Uhuru Katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii; na maonesho ya huduma na bidhaa mbalimbali za wadau wa Wizara. Aidha, mwaka 2011/2012 Wizara ilikutana na wanahabari wa vyombo mbalimbali kama vile runinga, radio, magazeti ili kutoa taarifa za masuala yanayohusu Wizara. Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa habari muhimu kwa wananchi kuititia vyombo vya habari, majarida na maonesho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mapitio ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 na malengo ya mwaka 2012/2013 yanaonesha Wizara yangu ilivyo mtambuka na hivyo kuhitaji ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kuimarisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa Wizara. Wizara kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuiwezesha Jamii kushiriki kikamilifu katika maendeleo yao binafsi na Taifa letu kwa ujumla. Lengo letu sote, ikiwa pamoja na Wizara yangu, ni kupunguza umaskini kwa kuboresha maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kumshukuru sana Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, kwa ushirikiano, ushauri na msaada mkubwa anaonipa katika kuongoza Wizara hii. Vilevile, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Katibu Mkuu - Bibi Kijakazi Rajabu Mtengwa, Naibu Katibu Mkuu - Bibi Anna Tayari Maembe, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania, Wakuu wa Vyuo pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara yangu wa ngazi zote, waliopo kwenye taasisi zetu zote, kwa jitihada zao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, ambayo ni pamoja na kuniwezesha mimi kuwasilisha hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Juhudi zao na maarifa katika utekelezaji wa majukumu tuliyonayo umewezesha kuendeleza sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza hotuba yangu, sina budi kuwashukuru wale wote tunaofanya nao kazi na wengine ambao kwa namna moja au nyingine tunashirikiana. Peke yetu kama Wizara tusingefikia mafanikio niliyoyataja.

Naomba kuititia Bunge lako Tukufu, kutoa shukurani zangu za dhati kwa wafuatao: Asasi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA); Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF); Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP); Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA); Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA); Shirikisho la Vyama vya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (FAWETA); Medical Women Association of Tanzania (MEWATA); White Ribbon; Friedrich Ebert Stiftung (FES); Plan International; Save the Children Tanzania; Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu; mashirika mbalimbali yasiyo ya Kiserikali; pamoja na wanaofanya kazi kwa maslahi ya jamii kwa namna moja au nyingine.

Napenda pia kuzishukuru Serikali za nchi rafiki ambazo kwa kuititia mashirika yake zinaendelea kutusaidia. Nchi hizo ni pamoja na Marekani (USAID); Jamhuri ya Korea (KOICA);

Denmaki (DANIDA) na Kanada (*CIDA*). Aidha, Mashirika ya Umoja wa Mataifa ambayo ni: *UNICEF*; *UNDP*; *UNFPA*; *UNESCO*; *ILO*; Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendeleo ya Wanawake (*UN-WOMEN*). Nayashukuru vilevile mashirika mengine ya ndani na nje kwa misaada yao. Aidha, napenda kuwashukuru Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), Ubalozi wa Ayalandi, Ubalozi wa Uingereza na Benki ya Dunia kuwa tayari kushirikiana nasi.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Bajeti ya Wizara Mwaka 2012/2013, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2012/2013, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Sh. 15,616,991,000/=. Kati ya hizo, Sh. 12,155,650,000/= ni kwa matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni Sh. 8,770,125,000/= na matumizi mengineyo (*other charges*) ni Sh. 3,385,525,000/=. Aidha, Sh. 3,461,341,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo Sh. 3,000,000,000/= ni fedha za ndani na Sh. 461,341,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyeiki wangu wa Kamati, naomba taarifa hii yote iingie katika kumbukumbu zetu za *Hansard*.

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (7) na Kanuni ya 114 (11) za Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niwasilishe Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii, juu ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, naomba nitumie fursa hii kutoa salaam za pole kwa Watanzania wenzetu waliopoteza ndugu zao katika ajali ya Meli ya MV. *Skagit* iliyotokea wiki iliopita kwa kuzama baharini wakati ikitokea Dar es Salaam kwenda Zanzibar. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira, nguvu na ujasiri. Pia tunawapa pole Wabunge wengine na Watanzania wote waliowapoteza ndugu, jamaa na marafiki katika vyanzo mbalimbali vya ajali.

Mheshimiwa Spika, kati ya tarehe 01 na 04 Juni, 2012 Kamati ilifanya vikao na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam kwa lengo la kupokea na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/2012 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, mionganoni mwa mambo mengine, Wizara ilitoa taarifa kuhusiana na utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwa Wizara katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuyafanyia kazi maoni na maagizo ambayo yalitolewa na Kamati katika mwaka wa fedha uliopita. Utekelezaji huo umeiwezesha Wizara kufanikiwa kwa kiwango kikubwa katika malengo iliyokuwa imeyaweka katika mwaka wa fedha uliopita. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

(1) Kukamilika kwa mpango utakaowezesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vipatavyo 25 kutoa mafunzo ya ufundi stadi (*VETA*) kuanzia Januari, 2013 ambapo vijana 1,250 wanatarajiwa kudahiliwa. Aidha, fedha zaidi zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya Vyuo vya maeneo ya pembezoni mwa nchi;

(2) Wizara imetoa mafunzo kuhusu masuala ya jinsia kwa Watendaji katika ngazi mbalimbali za utendaji Serikalini, na pia kushirikiana na asasi za kijamii kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia masuala ya jinsia katika mipango ya maendeleo;

(3) Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*) wamewezesha kuanzishwa kwa Klabu za Watoto mashulen ambazo zitawapa fursa ya kuelimishwa na wataalam wa afya juu ya afya ya uzazi, namna ya kukabili changamoto zitokanazo na mabadiliko ya mili pamoja na athari za kujiingiza katika uhusiano wa mapenzi katika umri mdogo;

(4) Wizara imeandaa zana za ushiriki wa watoto (*Child Participation Toolkit*) na Rasimu ya Mkakati wa Taifa wa ushiriki wa watoto, vitakavyowawezesha watoto kushiriki katika ngazi mbalimbali za maamuzi kwa mujibu wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Watoto;

(5) Wizara imeendesha mafunzo ya wasimamizi wa sheria katika kanda tano kuhusiana na Sheria ya Mtoto ili kuwajengea uwezo wa kuisimamia na kuwa watetezi wa watoto kwa mujibu wa sheria hiyo;

(6) Wizara imeandaa mkakati wa jamii wa kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi au kufanya kazi Mitaani ambaa umeainisha majukumu ya kila mdaa katika jamii na namna ya kudhibiti tatizo la watoto wa Mitaani. Mkakati huo uko katika hatua ya ngazi ya maamuzi;

(7) Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi viliongeza udahili wa wananchi katika mafunzo ya ujuzi na stadi za maisha kwa asilimia 0.8 kutoka 31,877 mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 32,133 katika mwaka wa fedha 2011/2012;

(8) Kiwango cha udahili katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii killongezeka kwa asilimia 15 kutoka Wanafunzi 2,672 katika mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 3,074 katika mwaka wa fedha 2011/2012. Udhili huo ni katika ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada;

(9) Wizara imefanya ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo viwili vya Maendeleo ya Jamii (Mabughai na Mlale) na vyuo vitano vya Maendeleo ya Wananchi (Muhukuru, Mputa, Sofi, Mto wa Mbu na Gera);

(10) Kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Sekta ya Maendeleo ya Jamii, ambapo washiriki 280 kutoka Wizara, Halmashauri zote nchini, Sekretarieti za Mikoa na sekta nyingine walishiriki kujadili na kuweka mikakati ya kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta hiyo;

(11) Wizara imeendelea kutuma fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (*WDF*) kwenye Halmashauri mbalimbali kwa lengo la kuwakopesha wanawake wajasiriamali. Jumla ya Shilingi milioni 120 zilitolewa kwa Halmashauri 15 katika mwaka wa fedha 2011/2012;

(12) Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote iliratibu mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa wanawake 350 na kisha kuwawezesha kushiriki katika Maonyesho ya Saba Saba ya mwaka 2011; na

(13) Wizara iliratibu Mkutano wa Mawaziri wa Maendeleo ya Wanawake na Jinsia kutoka nchi Wanachama wa nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu uliofanyika Arusha tarehe 04 Novemba, 2011. Mkutano huo uliandaa mapendekezo ya kutokomeza ukatili wa kijinsia katika Ukanda wa Maziwa Makuu ambayo yalipitishwa na Wakuu wa Nchi za Ukanda huo kwenye Mkutano Maalum uliofanyika Kampala Uganda Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iweze kutekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2012/2013, imeomba kuidhinishiwa Shilingi bilioni 15.6. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia 3.9 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 16.2 zilizoidhinishwa kwenye Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa upungufu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara hii umeendelea kujitokeza kwa mwaka wa tatu mfululizo tangu mwaka wa fedha 2010/2011 hadi mwaka huu wa fedha.

Katika kipindi hicho cha miaka mitatu mwenendo wa kupungua kwa bajeti ya Wizara ni kama ufuatao: Mwaka 2010/2011, Bajeti ya Wizara ilikuwa Shilingi billioni 19.9, kiwango ambacho kilipungua kwa Shilingi billioni 1.8 ikilinganishwa na Shilingi billioni 21.7 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2009/2010. Upungufu huo ni sawa na asilimia 8.3. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya Wizara ilipungua kwa asilimia 18.2 kutoka Shilingi billioni 19.9 zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 hadi kufikia Shilingi billioni 16.3.

Mwenendo huo wa kupungua kwa bajeti ya Wizara umejirudia tena katika bajeti ya mwaka huu wa fedha ambapo Wizara imetengewa Shilingi bilioni 15.6 zikiwa zimepungua kwa Shilingi milioni 639 (sawa na asilimia 3.9) ikilinganishwa na bajeti ya Shilingi bilioni 16.3 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati haifurahishwi na mwenendo huu wa upungufu wa bajeti inayotengwa kwa Wizara hii hasa ikizingatiwa kwamba, miaka mitatu kabla ya kuanza kwa mwenendo huu, bajeti ya Wizara ilikuwa imeongezeka kwa miaka mitatu mfululizo kutoka mwaka wa fedha 2007/2008 hadi mwaka wa fedha 2009/2010 kwa wastani wa takribani Shilingi bilioni 3.8 kwa mwaka.

Kwa upande mwingine, ni jambo liliilo wazi kwamba, upungufu huu wa bajeti kwa kiasi kikubwa utaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele vichache ilivyojiwekea katika mwaka huu wa fedha ambavyo ni pamoja na:-

(1) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na mafunzo ya maarifa, ujuzi na stadi katika Vyuo Maendeleo ya Wananchi;

(2) Kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili washiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo; na

(3) Kusimamia sera na sheria na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa inayohusu ustawi, haki na maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, licha ya kuelezea kutoridhishwa na bajeti finyu ambayo imetengwa kwa ajili ya Wizara hii, Kamati inatambua kuwa kupata kidogo ni bora kuliko kukosa kabisa na hivyo inaunga mkono maombi ya Wizara ya Maendeleo ya jamii, Jinsia na Watoto. Hata hivyo, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, licha ya kuwa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ni finyu bado kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha hizo kutoka Hazina. Hali hii imekuwa ikiathiri Wizara katika kutekeleza majukumu yake na hasa miradi ya maendeleo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha uliomalizika Juni 30, mwaka huu hadi kufikia Aprili 30, 2012 Wizara ilikuwa imepokea Shilingi bilioni 9.7 kati ya Shilingi bilioni 16.3 ilizoidhinishiwa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 59.5 ya bajeti yote iliyoidhinishiwa. Hata hivyo, upande wa matumizi ya maendeleo uliathirika zaldi, kwani katika kipindi kama hicho Wizara ilikuwa imepokea Shilingi milioni 775.8 tu kati ya Shilingi bilioni 4.9 zilizoidhinishiwa na Bunge, kiwango ambacho ni sawa na asilimia 13.9 ya fedha yote iliyotengwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kwa mazingira kama haya, ni wazi kwamba, miradi ya maendeleo iliyokusudiwa ama haitaweza kutekelezwa kabisa au itatekelezwa kwa kususua na hivyo haitamalizika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na hali hii, Kamati inashauri yafuatayo:-

- Serikali kupitia Hazina, itoe fedha zilizoidhinishiwa kwa ajili ya Wizara kwa wakati na kwa kiwango cha kutosha hasa fedha za miradi ya maendeleo ili kuwezesha miradi hiyo kutekelezwa;

- Serikali iachane na utegemezi wa fedha za wahisani kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kwani uzoefu unaonesha wamekuwa hawatekelezi ahadi zao na kama wanatekeleza ni kwa sehemu ndogo sana, tena siyo kwa wakati. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2011/2012 wahisani wa maendeleo waliahidi kuchangia Shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo

kwa Wizara hii, lakini hadi kufikia Aprili 30, 2012 walikuwa wametoa Shilingi milioni 160.9 tu ambazo ni sawa na asilimia 8.6 ya fedha walizoahidi kuchangia.

- Serikali iimarishe utaratibu wa kutenga fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani, kwani zina uhakika wa kupatikana hata kama ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inabainisha wazi kuwa, umri unaoruhusiwa kuingia katika ndoa ni kuanzia miaka 18 kwa kijana wa kiume na kuanzia miaka 15 kwa kijana wa kike (binti). Hata hivyo, Sheria hii inakinzana na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 ambayo inamtambua mtu aliye chini ya umri wa miaka 18 kama mtoto. Kwa mantiki hii, Sheria ya Ndoa ambayo imekuwepo na kutumika kwa takribani miaka 41 sasa, inaruhusu watoto kuingia katika ndoa. Kamati inaona kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuandaa mchakato wa kuifanyia marekebisho sheria hii ili kuwanusuru watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa sehemu fulani umaskini na jamii, kutotambua umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike, vimekuwa vikichangia baadhi ya jamii kuwa ozesha watoto wa kike katika umri mdogo ili kupata mali, lakini pia kama njia ya kuwaondoa katika familia hasa kwa kuwa hawana mpango wa kuwasomesha.

Katika jamii zenye utamaduni huu, mabinti wamekuwa wakifungishwa ndoa kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. Kamati inashauri Serikali iandae mpango wa kuelimisha jamii husika juu ya umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike, na pia athari za ndoa za utotoni ambazo mionganoni mwa mambo mengine ni chanzo cha vifo vya akina mama na watoto kwa kiwango kikubwa. Wakati tafiti zikonesha kuwa asilimia 45 ya Watanzania ni watoto walio chini ya umri wa miaka 15, nusu ya idadi hiyo ni wasichana. Hivyo ni wazi kuwa iwapo wataruhusiwa kuolewa katika umri mdogo, madhara ambayo yamekuwa yakipigwa kelele hayawezi kuepukika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba, elimu ya kutosha ikitolewa kwa jamii husika kutakuwa na mwamko mkubwa wa kupinga ndoa za utotoni. Watoto wa kike wataelimishwa na hatimaye Taifa litakuwa na jamii iliyoelimika. Sambamba na hilo, mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 unapaswa kuharakishwa ili kuondoa kukinzana kwa Sheria hii na ile ya Mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, dhana ya teknolojia na jinsia ni dhana mpya lakini ya msingi kabisa kwa kuleta maendeleo katika jamii, ingawa uhusiano na uwiano wa dhana hiyo unatakiwa kulinganishwa baina ya wanaume na wanawake. Tumeshuhudia kwa kipindi kirefu sasa watoto wa kike wakipoteza hamu ya kusoma masomo ya Sayansi na hivyo kulifanya kundi kubwa la wanawake likose upevu wa kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

Mfano, utafiti uliofanywa na Bwana Sakamoto wa Japani, mwaka 1994 ulibaini kuwa uwiano wa matumizi ya kompyuta kwa watoto wa kike na wa kiume ni 1:4. (Mtoto wa kike mmoja kwa watoto wa kiume wanen. Hii ni dhahiri kuwa, uwiano katika matumizi ya teknolojia baina ya wanawake na wanaume hauridhishi. Kutokana na changamoto hii, Kamati inafikiri ni umuhimu sasa kuviboresha Vyuo vyetu katika nyanja mbalimbali ili kuhakikisha vinatoa mafunzo bora yanayoendana na teknolojia ya kisasa kwa vijana wetu na hasa wa kike, kwa kuzingatia kuwa nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa kuitia Vyuo hivi ambapo vimeendelea kuongeza udahili wa wanachuo na kutoa mafunzo bora katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada. Kutokana na kazi hiyo nzuri, idadi ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Halmashauri, Mkoa na Taifa ni ya kuridhisha. Hata hivyo, bado Taifa linakabiliwa na changamoto ya upungufu wa wataalam hao katika ngazi za Kata na Vijiji. Kwa sasa ni Kata 1328 (sawa na asilimia 40) tu ya Kata zote nchini ambazo ni 3,321 ndizo zina Wataalam wa Maendeleo ya Jamii. Hii inaashirikia kwamba, upungufu uliopo wa asilimia 60 unakwamisha kufikiwa kwa lengo la Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1996 ambayo inaelekeza kuwepo kwa angalau Mtaalam wa Maendeleo ya Jamii mmoja katika Kata.

Mheshimiwa Spika, changamoto hiyo ya kukosekana kwa Watalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata, haitokani na ukosefu wa wataalam, bali kutokuwepo kwa nafasi za ajira. Kamati inaona suala la idadi ya Watalam siyo tatizo kwa sababu kwa wastani, wanachuo waliohitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, wanazidi idadi ya Kata zote zilizopo nchini.

Kutokana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali kuongeza nafasi za ajira kwa Watalam wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata, kwani wana mchango mkubwa sana katika kuwashawishi wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo na hivyo kujikwamua na halinjumu ya kiuchumi. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba bajeti inayotengwa kwa ajili ya Vyuo hivi inaongezeka badala ya kupungua kama ambavyo imeonekana katika miaka miwili ya bajeti iliyopita, ili kuhakikisha vinakuwa na mazingira mazuri ya kujifunzia pamoja na kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilianzishwa mwaka 1975 vikilenga kutoa elimu ya maarifa na stadi za maisha kwa wahitimu wa ngazi ya tatu na nne, katika elimu ya watu wazima kwa lengo la kuwawezesha kujajiri au kujiedeleza zaidi kielimu. Katika kipindi chote tangu kuanzishwa kwake, Vyuo hivi vilikuwa vikipata ruzuku ya Serikali na ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*) hadi mwaka 1990 ufadhili wa Shirika hilo ulipositishwa. Tangu wakati huo, fedha ya ruzuku ambayo imekuwa ikitengwa na Serikali kwa ajili ya Vyuo hivi, imekuwa ikipungua jambo ambalo limeathiri utendaji na ufanisi wake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inatambua na kuthamini juhudhi ambazo zimekuwa zikifanywa na Wizara katika kukarabati na kuboresha Vyuo hivi pale ambapo uwezo wa fedha umekuwa ukiruhusu. Pia, inaunga mkono kukamilika kwa Mpango utakaowezesha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vipatavyo 25 kutoa Mafunzo ya Ufundu Stadi (*VETA*) kuanzia Januari, 2013 ambapo kwa kuanzia vijana 1,250 wanatarajiwa kupata udahili. Hii ni hatua muhimu ambayo itasaidia kutoa nafasi kwa vijana wanaohitimu Shule ya Msingi na Kidato cha Nne kupata nafasi ya kujifunza Elimu ya Ufundu Stadi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa elimu ya ufundu stadi kuwa ndiyo msaada mkubwa kwa vijana hasa waliohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari na ambao wako katika kipindi cha mpito (*transition period*), Kamati inaunga mkono mpango wa Vyuo hivi kuanza kutoa Mafunzo ya Ufundu Stadi, kwani yatawasaidia vijana kupata ujuzi ambao utawawezesha kujajiri na hivyo kukabiliana na ugumu wa maisha. Hata hivyo, kwa kuwa Wizara hii imepangiwa bajeti ndogo ambayo athari zake zinagusa pia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, ili kuvisaidia vyuo hivi visiathirike, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia asilimia moja kati ya asilimia nne zinazotokana na kodi ya kuimarisha utoaji wa stadi nchini (*Skills Development Levy*) ambazo zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu ya Juu, kwa ajili ya kusaidia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mashirika yasiyo ya kiserikali yamekuwa yakiongezeka hapa nchini mwaka hadi mwaka. Hadi sasa Mashirika yanayoratibiwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pekee ni 675, ukiacha yale ambayo yanaratibiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, chini ya Sheria ya Vyama, Sura 337 na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, chini ya Sheria ya Udhamini, Sura 375. Licha ya idadi hii kubwa, ni baadhi tu ya mashirika ambayo mchango wake unatambuliwa na kuthaminiwa na jamii hasa katika Sekta za Afya, Elimu, Mifugo, Kilimo, Mazingira na kadhalika. Kwa upande mwagine, kumekuwa na malalamiko kwamba baadhi ya mashirika yamekuwa yakiwanufaisha walioyaanzisha badala ya makundi ya walengwa katika jamii.

Aidha, kwa kutambua kuwa Wizara imeanza kuteua Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Wilaya na Mikoa kuwa Wasajili wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali, ni wazi kuwa hatua hiyo itasaidia uratibu na ufuatilaji wa kazi za mashirika hayo katika ngazi husika na hivyo kubaini mchango wake katika kusaidia makundi ambayo mashirika hayo yanadai kushughulika nayo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara kwa kutumia Mpango Mkakati wa miaka mitano (2011-2016) ambao unatoa dira na mwongozo wa utumiaji wa rasilimali ili iweze kutimiza

malengo ya kubaini hasa ni kwa kiasi gani mashirika haya yamesaidia katika kupunguza matatizo yanayokabili makundi ya kijamii na hasa yaliyo chini ya Wizara hii, yaani watoto na wanawake.

Mheshimiwa Spika, Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kuwasaidia Wanawake ili waweze kujikwamua na hali ngumu ya uchumi. Ingawa dhamira ya Mfuko huu ni nzuri, kwani inawalenga wanawake wote walio katika Halmashauri kwamba waweze kuunda vikundi na kupatiwa mikopo. Utekelezaji wake umekuwa mgumu kutokana na kwanza; fedha inayotengwa na Serikali kwa ajili ya Mfuko huu kuwa ndogo sana, baadhi ya Halmashauri zimekuwa hazichangii kikamilifu asilimia tano ya mapato yake kama ilivyoagizwa na Waziri Mkuu mwaka 1995, na katika maeneo ambayo fedha ipo na vikundi vya wanawake vimekopeshwa, urejeshaji umekuwa ni tatizo. Hali hii inaathiri mwenendo na azma ya kuanzishwa kwa Mfuko huu, kwani iwapo hakuna fedha za kutosha na zile chache zinazokopeshwa hazirejeshwi, ni wazi kwamba wanawake wachache tu ndiyo watanufaika na Mfuko huu na hasa wale wa maeneo ya mijini kwani imekuwa ni vigumu kufika maeneo ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha malengo mazuri ya Mfuko huu yanafikiwa, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

- Serikali iongeze fedha inayotengwa kwa ajili ya Mfuko huu ili uweze kuwasaidia wanawake wengi kujikwamua na hali mbaya ya kiuchumi; na
- Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao ndiyo wenye jukumu la kutembelea wananchi na kuwahimiza kujihusisha na shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na ujasiriamali, wawezeshwe kwa kupewa vyombo vya usafiri na bajeti ya kutosha ili waweze kutoka ofisini na kuzungukia wananchi katika maeneo yao na kuwahamasisha kujihusisha na shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kukopa katika Mfuko huu na kurejesha.

Mheshimiwa Spika, Benki hii illanzishwa kwa lengo zuri ambalo ni kuwakomboa wanawake kiuchumi kwa kuwawezesha kupata mikopo kwa ajili ya mitaji ya biashara. Hata hivyo, lengo hilo linaonekana kuwa mashakani iwapo litafikiwa kikamilifu katika siku za karibuni hasa kutokana na ukweli kwamba, kiwango cha fedha ambazo zinatolewa kwa ajili ya benki kama sehemu ya kukuza mtaji wake ni kidogo sana ikilinganishwa na matarajio ya awali.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, akielezea madhumuni ya kuanzishwa kwa Benki hii alisema Serikali itatoa jumla ya shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo ili kuiwezesha Benki hii kuimarka kimtaji. Hata hivyo, utaratibu huo unaendelea kukiukwa kwa mwaka wa pili mfululizo, kwani kiwango cha Shilingi bilioni 1.1 kilichotengwa kwa ajili ya kukuza mtaji wa Benki ya Wanawake kwa mwaka 2011/2012 ndicho kimetengwa tena kwa ajili ya mwaka huu wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa benki hii na changamoto ambazo zinaikabili, Kamati inapendekeza yafuatayo kwa lengo la kuifanya iweze kupiga hatua:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kiasi hicho cha fedha (Shilingi bilioni 1.1) ni sehemu ya fedha za ndani Shilingi bilioni tatu zilizotengwa katika miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013 ni wazi kuwa Wizara itabakiwa na Shilingi bilioni 1.9 tu kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuipatia Benki Shilingi bilioni 1.1 kutoka Hazina, na kuachia Wizara bajeti yote ya maendeleo inayotokana na fedha za ndani (Shilingi bilioni tatu) ili iweze kutekeleza miradi yake ya maendeleo, la sivyo miradi mingi itakwama.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Benki na Taasisi nydingi za fedha zimejikita maeneo ya mijini, huku sehemu kubwa ya Watanzania (zaidi ya asilimia 70) ikiishi maeneo ya vijiji. Kamati inashauri kuwa, sasa ni wakati muafaka kwa Benki hii kuangalia namna ya kusogea huduma zake maeneo ya vijiji. Inaweza kufanya hivyo kwa kushirikiana na SACCOS za wanawake pamoja na Benki za Kijamii - *Village Community Bank (VICOBA)* na hivyo kuwafikia wanawake wengi ambao ni wanyonge kiuchumi.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara kupitia Benki ya Wanawake Tanzania kwamba, ni wakati muafaka sasa kutumia rasimu ya mpango wa biashara kuanzia Mwaka 2010 hadi 2013, ambao unalenga kufungua matawi mikoani, kutekeleza jukumu hilo, kwani wananchi wamekuwa wakisubiri kwa hamu kuiona Benki hii ikitoka Dar es Salaam na na kwenda Mikoani.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) umebainisha watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira hatarishi (*Orphans and vulnerable children*) kuwa mionganoni mwa makundi yaliyo katika hali tata. Aidha, ripoti iliyoinduliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mwezi Agosti, 2011 kuhusiana na utafiti wa ukatili dhidi ya watoto nchini, imetoa taswira ya awali kuhusiana na ukubwa wa tatizo la ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili ambalo linawasibu watoto wa kike na kiume.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kutumia matokeo hayo ya awali ya ripoti hiyo kuandaa miongozo na kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009, na pia kwa kuandaa zana za ushiriki wa watoto (*Child participation Toolkit*) pamoja na rasimu ya Mkakati wa Taifa wa ushiriki wa watoto ambavyo vyote vinalenga kuielimisha jamii juu ya umuhimu wa kumshirikisha mtoto katika mambo yanayomhusu.

Aidha, kwa kuwa lengo kuu la Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 2008 ni kuhakikisha watoto wote wanastawi na kuwa na maisha bora kwa kupatiwa haki zao za msingi ambazo ni kuishi, kuendelezwa, kulindwa na kushiriki katika mambo yanayowahusu bila ubaguzi wa hali yoyote. Kamati inapenda kutoa ushauri ufuataao:-

(1) Halmashauri zote zifuate na kuzingatia sheria ndogo zinazohusu watoto ili kuwapatia haki zao za msingi kama ilivyotajwa hapo juu ili kupunguza wimbi kubwa la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi;

(2) Wizara iendelee kuhimiza utaratibu wa watoto kupata huduma ya chakula cha mchana shulenii ili kuwafanya wasome vizuri na kuepuwa kulaghaiwa kwa kupewa chakula na vitu vingine vidogo. Maeneo ambayo utaratibu huu umeanza, yameonesha mafanikio makubwa;

(3) Serikali iimarishe mifumo ya kijamii ya kutunza watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi, ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuanzisha vituo vya mfano ambapo watoto watakusanywa na kupatiwa huduma za msingi;

(4) Serikali iangalie namna nzuri ya kuhakikisha Mabaraza ya Watoto yanatambulika na kupata nguvu ya kisheria ili yaweze kutimiza wajibu wake kikamilifu. Mabaraza haya yameonesha mafanikio makubwa katika sehemu ambazo yamekwishaanza; na

(5) Kwa kuwa bajeti ndiyo kikwazo kikubwa katika ufuatilaji wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kubaini yale ambayo yanajinuifaisha kwa migongo ya watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha ili kuwawezesha Maafisa Maendeleo ya Jamii kutimiza jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kukubaliana na kuzingatia kaulimbiu ya maadhisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka huu iliyokuwa inasema "Haki za Watoto wenye Ulemavu", ni jukumu letu kuzilinda, kuziheshimu na kuzitekeleza. Inashauri kwamba, sote kama jamii tuna wajibu wa kutekeleza katika kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanaandaliwa mazingira rafiki ambayo yatawawezesha kupata haki za msingi sawa na watoto wengine kama vile elimu, matibabu, michezo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ubaguzi ni kitendo au hali ya kumtenga binadamu mwingine awe mwanaume au mwanamke kwa kumnyima haki zake za kimsingi. Kwa mantiki hiyo, ubaguzi dhidi ya mwanamke ni ile hali inayojitokeza pale ambapo mtu mmoja, kundi la watu au taasisi, sera za nchi au mipango na mikakati mbalimbali ya maendeleo inamkataza au kumnyima mwanamke haki zake za kimsingi. Itakumbukwa kwamba, mwaka 1985 Tanzania iliridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa 1981 ambao unaondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake, na kukubali kutekeleza baadhi ya vipengele vya mkataba huo ambavyo iliona vina maslahi kwa nchi yetu.

Aidha, Kamati inaipongeza Wizara kwa kutafsiri mkataba huo kwa lugha nyepesi ili Watanzania na hususan wanawake waweze kuuelewa. Mkataba huo unafafanua bayana maana ya usawa wa jinsia na namna ambavyo jamii inaweza kufikia usawa huo wa kijinsia. Ajenda ya usawa wa kijinsia imeelezwa katika vifungu takribani 14 ndani ya Mkataba huo. Vilevile viro vifungu vinavyohusu masuala ya uzazi, malezi, na athari za baadhi ya mambo ya utamadunui, mila na desturi katika masuala ya mahusiano ya jinsia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuridhiwa kwa Mkataba huu, ni ukweli usiopingika kuwa yako matukio mengi sana katika nchi yetu ambayo yanadhihirisha kuwa ukatili na unyanyasaji kwa wanawake umekuwa ukiendelea. Tumeshuhudia wanawake wakipigwa, kunyofolewa baadhi ya viungo vyao na hata wengine kuuawa kikatili kwa sababu tu za kijinsia au imani potofu za kishirikina. Wakati mwagine wanawake wamenyanyaswa kutokana na vivu wa kimpenzi, mila potofu kama vile ukeketaji, kurithiwa pale wanapofiya na waume zao, na kadhalika. Hii inadhihirisha kwamba kama Taifa, bado tuna safari ndefu ya kuwasaidia wanawake wa Tanzania ili waweze kuondokana na unyanyasaji wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni mionganoni mwa maeneo ambayo wanawake wamekuwa wakibaguliwa na kunyanyasika:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika nchini mwaka 2002, idadi ya wanawake ilikuwa kubwa kuliko ya wanaume. Takwimu ya sensa hiyo inaonesha kuwa wanawake walikuwa milioni 17.6 wakati wanaumwe walikuwa milioni 16.8. Kwa kuzingatia wingi huo wa idadi ya wanawake, Kamati inashauri kuwa ipo haja ya dhati kabisa ya kuongeza uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uongozi na vyombo nya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashukuru Serikali kwa kuhakikisha kuwa idadi ya watoto wa kiume na wa kike katika Elimu ya Msingi na Sekondari iko sawa. Hata hivyo, lipo tatizo kubwa la kukosekana usawa wa idadi ya wanafunzi wa kike na wale kiume katika elimu ya juu.

Kwa mujibu wa Profesa Abeli, kupitia mada aliyoiwasilisha katika Warsha iliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Agosti 5, 2010, iliyojulikana kama *Higher Education and Development: A Critical Nexus*, kwa tafsiri isiyo rasmi Elimu ya Juu na Maendeleo: Kiunganishi Muhimu, ni asilimia 35 tu ya Wanafunzi wa kike ndiyo wanapata fursa ya kujunga na elimu ya juu. Hali hii inasababisha kupungua pia kwa kiwango kikubwa kwa wasichana wanaopata ajira rasmi na zisizo rasmi baada ya kumaliza elimu hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba Serikali kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kujua chanzo cha kupungua kwa watoto wa kike wanaojunga na elimu ya juu, na kutafuta namna ya kuondoa tatizo hilo ili kuleta usawa wa kupata elimu na ajira baina ya watoto wa kike na wa kiume.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupongeza sana watu ambao wamekuwa wakisaidia kutoa msaada wa kisheria (*Paralegals*) pamoja na mtandao wa Polisi Wanawake kwa kushughulikia masuala ya haki za wanawake mbele ya sheria kwa wanawake wengi hususan wale wa vijijini. Hata hivyo, bado inahitajika nguvu ya ziada katika kuhakikisha wanawake wanapata haki zao za kisheria kikamilifu, kwani bado wanawake wanadhulumiwa na kunyimwa haki katika masuala kama vile mirathi, umiliki wa ardhi na mali nydingine, matunzo ya watoto hasa wanapoachika na pia kunyanyaswa kijinsia wakati wa ajira, na maeneo mengine kama hayo. Vilevile, baadhi ya sheria kama vile za Ndoa, Mirathi na Matunzo kwa Watoto, zimeendelea kumkandamiza na kumnyima mwanamke haki na usawa mbele ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kwanza, kufanya mapitio na mabadiliko ya sheria hizo zilizopitwa na wakati haraka iwezekanavyo. Vilevile iendelee kuandaa mazingira mazuri na shirikishi yatakayowawezesha wanawake wote kupata haki zao za kimsingi na kisheria kwa haraka, kwa wakati na bila usumbufo wowote.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi yetu imekumbwa na wimbi kubwa la hatihati za watu kujilingiza katika na mahusiano ya jinsia moja. Vitendo hivi siyo kawaada ya desturi, mila wala utamaduni wa Taifa letu. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa hali hiyo ya hatihati, Serikali imekuwa

kimya na hajawahi kutoa tamko lolote kuhusiana na hali hii. Kamati inashauri kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuititia vyombo husika iweze kuzungumzia suala hili na kutoa msimamo wa dhati ili wananchi waweze kuelewa kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ibara ya 39 (1) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, mtu ye yeyote hatastahili kuchaguliwa kushika Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa miongoni mwa sifa nyingine, awe ni mwanachama na mgombea aliyependekezwa na Chama cha Siasa. Pia katika ibara ya 39 (2) ya Katiba inatamkwa wazi kuwa, mtu ye yeyote hatakuwa na sifa za kuchaguliwa kushika Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano kama siyo mwanachama na mgombea aliyependekezwa na Chama cha Siasa.

Uzoefu unaonesha kuwa wagombea wengi wanaopendekezwa na Vyama vyao kuwania nafasi ya Urais wamekuwa wale ambaa ni Viongozi wa juu kwa wakati huo au wamewahi kushika nyadhifa za juu katika uongozi wa Vyama vyao. Ni ukweli usiopingika kuwa viongozi wengi wa Vyama vya Siasa ni wanaume. Mfano, Vyama vyote vya Siasa nchini vinaongozwa na wanaume katika nafasi za Uenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu, na kwa asilimia kubwa viongozi wa ngazi hizo ndiyo wamekuwa wakteuliwa na Vyama vyao kuwania Urais. Hii ni ishara kuwa wanawake hawana chao pale linapokuja suala la kuteuliwa kuwania Kiti cha Urais kwa sababu hawajaweza kupenya katika safu hiyo ya juu ya uongozi wa Vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, Kamati inaona kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuandaa mazingira ya makusudi ambayo yatawawezesha wanawake kupata nafasi katika uongozi wa juu wa Vyama vyao. Kamati inashauri kuwa, Sheria ya Vyama vya Siasa Sura 258 ya mwaka 1992 ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 10 (1)(c). Kifungu hiki kinatamka wazi kuwa miongoni mwa masharti ya Chama kupatiwa usajili wa kudumu ni kuwasilisha majina ya viongozi wa Chama ambaa wamepatikana kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Kamati inashauri kuwa, wakati umefika kwa sheria hii kuzingatia usawa wa kijinsia katika uongozi wa vyama vya siasa na hivyo ni vyema kifungu hicho kisiishie kutaka pande mbili za Muungano zizingatiwe katika uongozi, bali kiseme wazi kuwa ni lazima kuwe na uwakilishi ulio sawa katika uongozi wa Vyama vya Siasa baina ya wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa bila ya kuwa na juhudi za makusudi kabisa katika kuhakikisha wanawake wanashika nyadhifa za juu katika uongozi wa Vyama vya Siasa ni wazi kuwa itakuwa ndoto kwao kufikiria kuwania Kiti cha Urais katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto imekuwa ikijitahidi kutekeleza majukumu yake vizuri licha ya bajeti finyu inayotengewa na Serikali. Kwa kuwa Wizara hii inahusika na makundi muhimu sana katika jamii (wanawake na watoto), Kamati inasisitiza kwamba, makundi haya yanahitaji uangalizi wa karibu sana na hivyo inashauri yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa bajeti inayotengewa Wizara ni ndogo sana, Wizara iangalie uwezekano wa kuandaa maandiko (*proposals*) kwa lengo la kutafuta fedha zaidi nje ya Serikali. Hata hivyo, bado Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha inaitengea Wizara bajeti ya kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake;

(ii) Serikali itimize ahadi yake ya kuitengea Benki ya Wanawake fedha za kutosha ili kuiweshesha kuimariika kimtaji na hivyo iweze kujiedhesa kiushindani kama ilivyo kwa benki nyingine;

(iii) Serikali iangalie namna ya kuwatumia wanahisa katika kukuza mtaji wa Benki ya Wanawake, kwani utegemezi wa fedha za Serikali pekee unaifanya benki hiyo kuendelea kususua. Iwapo mazingira yataandalisha kwa wanahisa kushirikishwa kuchangia ni wazi kuwa mtaji wa benki utakua kwa haraka na itaweza kujiedhesa kibashara na kwa faida;

(iv) Serikali iongeze bajeti inazotenga kwa ajili ya Vyuo vya Maendeleo ya jamii na wananchi ili kuweshesha ukarabati wa majengo na miundombinu ya Vyuo hivyo ambayo yako katika hali mbaya, kuongeza watumishi na kuboresha mazingira ya kazi na ya kujifunzia;

(v) Kwa kuwa tatizo la watoto wa Mitaani linaendelea kushamiri katika miji mbalimbali hapa nchini, ni vyema Wizara ikalitambua kuwa mionganoni mwa vipaumbele vyake. Wizara inaweza kukabiliana na tatizo hili kwa kushirikiana na Halmashauri husika kuanzisha vituo vya mfano ambayo vitawakusanya na kuwatunza watoto hawa kwa kuwapatia mahitaji muhimu na kulinda haki zao za msingi;

(vi) Serikali iongeze ruzuku inayopelekwa katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na pia iboreshe mazingira na miundombinu katika Vyuo vilivypo pembezoni ili kuwavutia walimu na watumishi wanaopangiwa kufanya kazi huko;

(vii) Kwa kuwa ni asilimia 40 ya Kata nchini ndizo zina Wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Serikali iangalie namna ya kuzalisha Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa kutosha kujaza nafasi hizo, la sivo mambo mengi yataendelea kukwama katika maeneo ambayo hayana wataalam hao;

(viii) Serikali iendelee kuwajengea wanawake uwezo wa kushiriki katika shughuli za ujasiriamali, kwa kuwapatia elimu ya biashara na teknolojia, pamoja na mitaji ili waweze kujikomboa kiuchumi;

(ix) Serikali iendelee kuwaelimisha wanawake juu ya Sheria mbalimbali zinazowapa haki ya kumiliki ardhi na mali pamoja na sheria zinazowalinda dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia; na

(x) Kuendelea kuwajengea wanawake uwezo utakaowawezesha kujiamini na kuthubutu kujitokeza kushiriki katika ngazi mbalimbali za uongozi katika jamii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni haya, ni vyema Bunge lako Tukufu likazingatia kwamba, Wizara hii inasimamia baadhi ya masuala mtambuka ambayo pia yanagusa Wizara nyingine. Hata hiyo, kwa kuwa, masuala hayo yanahusiana na jinsia, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iyapokee na kuyafanyia kazi maoni haya ya jumla ambayo yametolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kukupongeza kwa umahiri na busara zako katika uendeshaji wa Vikao vya Bunge. Nawapongeza pia Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi wanavyokusaidia katika kutekeleza majukumu yako. Kwa niaba ya Kamati, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii ya Wizara kwa kuwasilisha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto - Mheshimiwa Sophia M. Simba; Naibu Waziri - Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu; Katibu Mkuu wa Wizara - Ndugu Kijakazi T. Mtengwa; Naibu Katibu Mkuu - Ndugu Anna T. Maembe na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa ushirikiano wao mkubwa wakati tunatekeleza majukumu ya Kamati. Ninawataktak mafanikio zaidi katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao mkubwa walionipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Jenista J. Mhagama – Mwenyekiti, Mheshimiwa Juma S. Nkamia – Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Capt. John D. Komba, Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude P. Rwakatare, Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi, Mheshimiwa Agnes E. Hokororo, Mheshimiwa Mary P. Chatanda, Mheshimiwa Moza A. Saidy, Mheshimiwa Donald K. Max, Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Salum K. Barwany, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Rebecca M. Mgodo, Mheshimiwa Saidi M. Mtanda, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshiumiwa Livingstone J. Lusinde, Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo na Mheshimiwa Joshua Samweli Nassari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashillilah akisaidiwa na Makatibu wa Kamati, Ndugu Hosiana John na Ndugu Chacha Nyakega, kwa ushauri wa kitaalam kwa Kamati na pia kuratibu shughuli za Kamati hadi kukamilisha taarifa hii. Pia namshukuru Msaidizi wa Kamati, Ndugu Tumaini Kilapilo kwa kuhudumia vyema Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na ninaomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa salaam za pole na rambi rambi kwa familia za ndugu jamaa na marafiki wote wa Marehemu waliofariki kutokana na kuzama kwa meli ya *MV. Skagit* karibu na Kisiba cha Chumbe huko Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema, aidha, awape wafiwa wote roho ya subira na ustahilimivu katika kipindi hiki kigumu. Amen.

Mheshimiwa Spika, rambirambi peke yake hazitoshi wakati Bunge linakatazwa kujadili sababu zinazosababisha ajali ambazo waathirika wakubwa ni wanawake na watoto wanaoachwa wajane na yatima. Pamoja na rambirambi hizo, tunataka Bunge hili Tukufu lijadili sababu za maafa haya makubwa ili litimizie wajibu wake wa Kikatiba wa kusimamia Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuendelea kunipigania siku zote na sasa nimesimama hapa ili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7) toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa kutupa dhamana ya kusimamia Wizara hii yenye changamoto nyingi mimi pamoja na Waziri Kivuli -Mheshimiwa Dkt. Anthony Gervase Mbassa Mbunge. Tunapenda kumhakikishia kuwa tutatekeleza wajibu wetu kwa uwezo na nguvu zetu zote kama yalivyo matarajio ya Watanzania kwa Chama chetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kadhalika, kipekee, nitoe shukrani kwa familia yangu kwa kuniwezesha kutimiza majukumu yangu ya kibunge na kichama. Aidha, pongezi ziende kwa viongozi wenzangu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo – CHADEMA Mkoa wa Kagera na Taifa kwa kazi kubwa wanayoifanya bila kuchoka katika kukidhi matarajio ya Watanzania kuwa CHADEMA ndiyo Chama mbadala kuongoza nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, malengo na majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto yanatokana na miongozo mbalimbali ya Kifaifa na Kimataifa kwa mfano, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Malengo ya Milenia na mikataba ya kikanda na Kimataifa inayohusu haki na ustawi wa mwanamke na mtoto ambayo nchi yetu imeridhia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa miongozo hiyo ya Kitaifa na Kimataifa katika maendeleo ya jamii na uchumi kwa jumla, ni wazi kwamba Wizara hii ina jukumu kubwa sana la kutafsiri miongozo hiyo katika uhalsia na kuitekeleza katika mazingira ya Kitanzania ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na miongozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, jukumu kubwa la Sekta ya Maendeleo ya Jamii ni kuwaandaa watu kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Sera, Programu na Mipango ya sekta zote zinazohusika na maendeleo ya jamii kwa jumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua mchango wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto katika kushughulikia masuala ya wanawake na watoto, Kambi ya Upinzani

inasikitishwa kuona kwamba Wizara hii imekuwa haijishughulishi nya kutosha na maendeleo ya kiuchumi ya jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote hapa nchini zimeajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii. Kimsingi Maafisa hawa kazi yao ni kuratibu na kutekeleza mipango yote ya maendeleo ya jamii katika Halmashauri husika. Hata hivyo, bado kuna upungufu mkubwa wa Maafisa Maendeleo ya jamii nchini hasa katika ngazi ya Kata jambo ambalo linasababisha miradi mingi ya maendeleo katika Kata kutokuwa na usimamizi madhubuti na hivyo kusababisha hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kujua ni Kata ngapi nchini ambazo hazina Maafisa Maendeleo ya Jamii, na Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na upungufu huo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Tume ya Mipango katika taarifa yake ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2011 ni kwamba Vyuo 54 vya Maendeleo ya Jamii viliendesha mafunzo na stadi mbalimbali za maendeleo ya jamii kwa wananchi 31,877 ikilinganishwa na idadi ya wananchi 31,493 kwa mwaka 2010. Kwa takwimu hizi, ni kwamba kuna wastani wa wataalam 30,000 kila mwaka wanaofuzu katika fani mbalimbali za maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, licha ya wataalamu hawa kuwa ni wengi, bado kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo wa Jamii hasa katika ngazi za Kata ambako ndiko msingi wa shughuli za maendeleo ulipo. Jambo hili linasababisha watu wasione kwa urahisi mchango wa Vyuo hivi nya Maendeleo ya jamii katika maendeleo halisi ya jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili kwamba ni kwanini wahitimu katika fani za maendeleo ya jamii ni wengi, lakini bado kuna upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kata hapa nchini? Pili, kwa nini Serikali isiwaajiri maafisa hawa moja kwa moja pindi wanapohitimu ili kukabiliana na tatizo la kuzorota kwa maendeleo ya jamii katika ngazi za vijiji na Kata kutokana kukosa uratibu na usimamizi madhubuti?

Mheshimiwa Spika, majibu yaliyotolewa na Wizara katika kutekeleza maagizo ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya jamii licha ya kutoridhisha, lakini pia yanalenga kukwepa majukumu. Kwa mfano, Kamati iliagiza Serikali kuititia Wizara hii kuweka utaratibu wa uimarishaji wa mifumo ya kijamii ya kutunza watoto yatima na wanaoishi katika mazingira hatarishi. Majibu ya Wizara katika hili ni kwamba bado inaendelea kuandaa mkakati wa kijamii kudhibiti tatizo la watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa jibu hili ni sawa na kukwepa jukumu. Hii ni kwa sababu mwaka mmoja umepita tangu agizo hili litolewe na halijakamilika. Aidha, idadi ya watoto wa Mitaani inaongezeka na hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri, katika suala la watoto wa Mitaani, Serikali kuititia Wizara hii, ifanye sensa ya watoto wote wa Mitaani, na baada ya kufanya hivyo ianze mchakato wa kubaini ndugu au jamaa wa watoto hao, ili wachukue jukumu la kuwalea. Kwa wale ambaeo ndugu zao hawatapatikana, basi Serikali iandae utaratibu wa kuwalea watoto hao ili kulinda utu wa watoto hawa ambaeo kwa sasa umedhalilishwa sana. Ikumbukwe kuwa siyo tu watoto waliofiwa na wazazi wao ndio wanaotoroka majumbani kwao, bali pia wengine hutoroka kutokana na ukatili wa wazazi wao na ushahidi wa hilo ni mwinci sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la mimba shulenii, Kambi ya Upinzani haioni kama kutoa chakula shulenii ili wanafunzi wa kike wasilaghaiwe kwa chipsi au soda ni dawa pekee ya kuzuia mimba kwa wanafunzi wa kike.

Mheshimiwa Spika, jambo lenye tija katika kupunguza mimba mashulenii ni kuanzisha somo maalumu la elimu-rika ya afya inayoendana na makuzi kwa wasichana na wavulana, ili wawe tayari kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya miili yao. Pia wapewe taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi na athari za mahusiano ya kingono katika umri mdogo. Aidha, msisitizo maalumu

uwekwe kwenye magonjwa yanayotokana na zinaa kama *UKIMWI* kuliko mimba peke yake. Wanafunzi waelezwe waziwazi hasara watakazozipata maishani iwapo watakosa elimu kutokana na mimba au magonjwa ya zinaa watakayoyapata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kuwa licha ya somo la elimu rika kwa wasichana na wavulana kuhusu afya ya makuzi na uzazi, kuwe na utaratibu mashulenii wa kufanya semina ya afya ya uzazi na makuzi kwa vijana angalau mara mbili kwa mwaka na taarifa za semina hizo ziandikwe na kutumwa Wizarani ili kuweza kufanya tathmini katika ngazi ya Wizara. Waelimishaji wawe ni Maafisa wa Afya wakishirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi za Kata.

Aidha, Kambi ya Upinzani inashauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ishirikiane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kuratibu jambo hili. Sambamba na hilo, Shule za Sekondari za Kata zijengewe mabweni, kwani umbali kutoka majumbani kwa watoto wa kike ni mkubwa mno na hivyo husababisha watoto wa kike kuingia kwenye mitego ya kupanga vyumba Mitaani bila ya kuwepo na uangalizi wowote ule.

Mheshimiwa Spika, wazazi nao wana jukumu kubwa zaidi katika malezi ya watoto wao. Hivyo wahamasishwe na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kuwafundisha watoto wao maadili ili kuepuka mimba za utotonii.

Mheshimiwa Spika, hali ya kiuchumi ya wanawake hapa Tanzania bado ni duni. Kwa mujibu wa tovuti ya Taifa kuhusu jinsia kama iliyosomwa tarehe 12 Julai, 2012 ni kwamba takriban asilimia 60 ya wanawake hapa Tanzania wanaishi katika umasikini wa kutupwa (*absolute poverty*). Wengi wa wanawake hawa ni wale waishio vijiji. Ni dhahiri kwamba kama kuna azma yoyote ya maendeleo, ni matumaini ya Watanzania kwamba yangeanza na wanawake hawa wanaoishi katika umasikini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashangaa kuona kwamba ari na kasi ya Serikali kuwasaidia wanawake masikini hapa Tanzania ni ndogo sana na inakwenda kinyume kabisa na kaulimbiu ya Serikali ya "Maisha Bora kwa kila Mtanzania" na vilevile inapingana na Kaulimbiu ya Chama cha Mapinduzi ya "Ari Zaidi, Nguvu Zaidi na Kasi Zaidi" katika kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi (2011) ni kwamba Serikali ilitoa mikopo ya jumla ya Shilingi milioni 88 kwa wanawake wajasiriamali kupitia Halmashauri zao. Taarifa hii hakika inatia simanzi kubwa, kwani inaonyesha dhahiri kuwa Serikali haitilii mkazo katika kuwainua wanawake kiuchumi kama ambavyo siku zote imekuwa ikijipambanua.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa huku ni kuwatania wanawake na hivyo inataka kupata majibu kuhusu wanawake waliopata mikopo hii ni wa Halimashauri zipo na walikuwa wangapi? Hivi huku ndiyo kuwezesha wanawake?

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo pia inaonesha kuwa Benki ya Wanawake ilitoa mikopo ya jumla ya Shilingi bilioni 2.1 kwa vikundi 195 vya wajasiriamali. Hata hivyo, taarifa hii haijaonesha ni wanawake wangapi katika vikundi hivi walionufaika na mikopo hiyo, ili kuweza kujua uwiano wa walionufaika dhidi ya jumla ya wanawake masikini hapa nchini. Aidha, imetaja kwamba Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilitoa mafunzo ya biashara kwa wanawake wajasiriamali 350 na iliwawezesha kushiriki maonesho ya biashara ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hakika kwa viwango hivi kusaidia wanawake 350 dhidi ya wanawake takriban milioni 20 wenye shida, ni kuwakejeli wanawake wa nchi hii na ni ushahidi kwamba sasa Serikali imeamua kuwatupa wanawake ambaa ndio msingi wa kizazi cha Taifa hili kwa sasa na baadaye.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, kama Serikali ina nia ya dhati ya kuwasaidia wanawake, iandae mfuko maalumu wa kuwasadia wanawake katika Halmashauri zote nchini. Utaratibu wa kuwatambua wanawake wenye shida ufanywe na Halmashauri za Vijiji na kukabidhi orodha hiyo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii

waliopo katika ngazi za Kata ambao ndio watakaosimamia ugawaji wa mikopo au misaada kama ambavyo itakuwa imepangwa na Wizara. Maafisa Maendeleo ya Jamii wakishirikiana na viongozi wa vijiji wahusike katika kuwaelimisha wanawake waliopewa mikopo au misaada namna bora ya kutumia mikopo au misaada hiyo katika kujiendeleza kiuchumi kwa shughuli za kilimo au biashara.

Mheshimiwa Spika, kazi nydinge muhimu ambayo Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inafanya ni kupambana na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, licha ya wanawake kuwa na jukumu kubwa kuendeleza kizazi cha Taifa hili na majukumu mengine ya malezi ya watoto na kazi mbalimbali zinazochangia sana ukuaji wa uchumi wa Taifa, bado wengi wao wameendelea kufanyiwa ukatili na unyanyasaji kutoka kwa wenzi wao na watu wengine kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, ukatili huu dhidi ya wanawake na watoto umezidi kuongezeka licha ya kwamba tuna Wizara nzima ambayo inashughulikia mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye Katiba yetu, bado kuna ibara ambazo zinamkandamiza mwanamke, na mfano wa ibara hizo ni ibara ya 24 (1),(2) ambayo inazungumzia haki ya kumiliki mali, ibara ya 22 (1),(2) ambayo inazungumzia haki ya kufanya kazi, pamoja na vifungu vingine mbalimbali nya Katiba. Ibara hizi hazimtaji moja kwa moja mwanamke kuwa ana haki ya kumiliki mali, jambo ambalo linasababisha kunyanyasika na hasa anapojikuta ni mjane.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa rai kwa wanawake wote nchini kujitokeza kwa wingi kwa ajili ya kwenda kutoa maoni yao kwa Tume ya Katiba hasa kuhusiana na haki za wanawake ili kuondoa kabisa manyanyaso na wajue wazi kabisa kuwa tunawaunga mkono kwa dhati. Aidha, waseme waziwazi kuwa vipengele vyote kandamizi dhidi ya mwanamke na hasa wajane visiwepo kwenye Katiba na Sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya wanawake unasababishwa pia na sheria mbalimbali ambazo zimetungwa na Bunge hili na mfano wa sheria hizo ni Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Kimila ya mwaka 1963 ambazo kutokana na sheria hizi, zimetoa mwanya kwa wanawake kuendelea kunyanyaswa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha Muswada wa Sheria ili Bunge liweze kuzibadilisha sheria hizi kandamizi dhidi ya wanawake ili waweze kuondokana na udhalilishaji huu unaotiliwa nguvu na sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, matukio ya wanawake kupigwa na waume zao, kutelekezwa na kuachwa na mzigo wa kulea watoto, kubakwa, kukeketwa, kunyimwa haki ya kumiliki mali licha ya kushiriki katika uzalishaji mali, yameongezeka licha ya sera, sheria na mikakati ya kitaifa na kimataifa ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake kuwepo.

Mheshimiwa Spika, hatari kubwa iliyopo ni kwamba, jamii inaona kuwa mambo haya ni ya kawaida na hivyo hakuna juhudzi zozote zinazofanywa na jamii kuyatokomeza. Kwa mujibu wa ripoti ya "Health Policy Initiative" (2008), juu ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia Tanzania ni kwamba, ubaguzi, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake hapa Tanzania ni desturi na watu hawaoni kama ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inasikitishwa kuona kwamba Serikali haiko mstari wa mbele katika kupigania haki kwa wanawake wanaonyanyaswa. Kwa mujibu wa gazeti la Uhuru linalomilikiwa na CCM la tarehe 13 Julai, 2012, ni kwamba mnamo tarehe 19 Februari, 2012 katika Wilaya ya Bunda Mkoani Mara, mwana mama Nasra Mohamed alifanyiwa unyama na mumewe Elisha Mkumbati ambaye alimgonga kwa makusudi na gari na baadaye kumburuza na gari hilo jambo liliomsababishia maumivu makali sana na hatimaye umauti.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mauti kumfika, mama huyu alilazwa katika Hospitali ya Bugando na baadaye Muhimbili kwa matibabu zaidi. Mama huyo alipokuwa amelazwa katika Hospitali ya Bugando, alitembelewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto -

Mheshimiwa Sophia Simba, ambaye aliahidi kumsaidia. Kinachosikitisha ni kwamba, makala hiyo imesema wazi kuwa Mheshimiwa Waziri alimkimbia na kumtelekeza mama huyu, hakufuatilia hata kuhusiana na watoto wanne wa mama huyu wanavyoishi.

Mheshimiwa Spika, kinachoumiza zaidi ni kwamba mpaka sasa hivi mtu aliyefanya ukatili wa kumjeruhi mama huyu na kumsababishia kifo hajakamatwa, na watoto wa Marehemu hajulikani wanaishije. Jambo hili linawafanya wanawake wajione kuwa hawana usalama ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inamtaka Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa CCM Taifa, kulieleza Bunge hili, ni kwanini alimhadaa, kumdanganya na kumtelekeza Nasra Mohamed bila msaada wowote wakati aliahidi kwa kinywa chake mwenyewe kuwa angemsaidia? Pili, Kambi ya Upinzani inataka kujua Waziri anawasaidiaje watoto walioachwa na Marehemu na pia hatua gani zitachukuliwa dhidi ya aliyetenda ukatili huu?

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza na kutokomeza manyanyaso dhidi ya wanawake, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba kuwe na mkakati madhubuti wa kiserikali wa kuanzisha kitengo maalumu katika Halmashauri zote nchini kitakachokuwa na jukumu la kushughulikia unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Kata.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri hivi, kwa sababu bado mfumo dume ngazi ya familia na vijiji bado una nguvu sana na bado jamii inaamini kwamba mwanamke kunyanyaswa ni sehemu ya utamaduni; kwa namna hii, mwanamke aliyefanyiwa ukatili anaweza asipate haki yake hasa pale ambapo wanaongoza vyombo vya haki katika ngazi nilizozitaja ni wanaume wasiojali haki za wanawake. Aidha, tunashauri kuwepo na dawati maalum la kusikiliza malalamiko na maonevu kwa wanawake na watoto na Mahakama ziweke kitengo maalum kusikiliza kesi zinazohusu kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya *UNICEF* juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania ya mwaka 2011 ni kwamba ukatili wa kijinsia mionganoni mwa wasichana na wavulana chini ya miaka 18 ni mkubwa na unazidi kuongezeka. Ripoti hii inaonesha kwamba wasichana watatu kati ya 10 na mvulana mmoja kati ya saba wameripoti kufanyiwa vitendo vya ukatili kabla ya kutimiza umri wa miaka 18. Aidha, karibu asilimia sita ya wasichana wamelazimishwa kujamiiiana kabla hawajatimiza miaka 18.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ukatili wa kijinsia, watoto vilevile wamekuwa wakifanyiwa ukatili wa kimwili na kiakili jambo ambalo limekuwa linawaathiri sana kisaikolojia na hivyo kuathiri maendeleo yao ya kitaaluma.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto umefikia hatua mbaya zaidi baada ya taarifa za vyombo mbalimbali vya habari vya tarehe 21 Julai, 2012 kutoa taarifa kuwa, kuna mwanaume mmoja kwa jina Joseph Ngisha, amediriki kumchumbia mtoto wa miaka minne na kumwoa akiwa na miaka nane Mkoani Arusha. Mwanaume huyo alishikiliwa na Jeshi la Polisi, na mtoto huyo akakutwa ana mimba ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani haikubaliani na ukatili huu na inaitaka Serikali kutoa tamko itachukua hatua gani ili kukomesha vitendo kama hivi kuendelea kujitekeza na kuwadhalilisha watoto wetu, kuwanyima haki ya elimu na kuwaharibia maisha yao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mauaji ya vikongwe na walemauvu wa ngozi (*Albino*) kutokana na mila potofu za kishirkina, ni matukio ya kutisha yaliyoikumba nchi yetu kwa miaka ya hivi karibuni. Licha ya matukio hayo kufedhehesha utu wa mwanadamu, pia yamejenga hofu kubwa mionganoni mwa rai na kujisikia kuwa sio salama ndani ya nchi yao. Aidha, vitendo hivyo vimeshusha sifa na haiba ya Tanzania mbele ya Mataifa mengine duniani.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba matukio kama haya siyo dalili nzuri hata kidogo kwa jamii inayopiga hatua katika maendeleo, bali ni dalli za jamii inayorudi nyuma kimaendeleo. Katika karne hii ambapo kuna mageuzi makubwa ya kisayansi na teknolojia za ajabu kabisa

ambazo ndiyo nyenzo za mafanikio ya haraka, eti bado nchi yetu ina baadhi ya watu wanaoamini katika ushirikina, tena wa kuutoa uhai wa wengine ili wapate mafanikio.

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu kubwa kwa Taifa, na Serikali haina budi kubeba aibu hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa na inakerwa sana na matukio haya ya kishetani ya kuwaua ndugu zetu wenye ulemavu wa ngozi na wazee. Kambi ya Upinzani vilevile hairidhishwi na kasi ndogo ya kushughulikia masuala ya uhalifu dhidi ya vikongwe na walemovu wa ngozi nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua barabara hatua na michakato ya kisheria inayopaswa kuchukuliwa tangu mshukiwa wa uhalifu akamatwe, ashitakiwe na hadi hukumu kutolewa. Ila kwa kesi kama hizi za mauaji ya vikongwe na *albino*, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba Serikali ishirikiane na Mahakama na kutazama upya taratibu hizi za kisheria ili kesi za mauaji ya *albino* na vikongwe zishughulikiwe haraka zaidi na hukumu za kesi hizi zitangazwe hadharani ili kukomesha kabisa matukio haya yanayolidhalilisha Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua ukubwa wa tatizo la vitendo vya kishirikina kama vitendo ambavyo vinachangia katika kukwamisha maendeleo ya wananchi na kinyume chake mkakati wa kupunguza umasikini kushindwa kufanikiwa. Kwa maana hiyo, kutokana na utafiti uliofanywa na kuchapishwa katika majarida ya kitaaluma, ni dhahiri kuwa vitendo vya ushirikina vina uhusiano wa moja kwa moja na umasikini. Hivyo basi, tukiondokana na umasikini, ni dhahiri kuwa ushirikina nao utapungua.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria ya uchawi ya mwaka 1928, na marejeo yake miaka ya 1935, 1956 na 1998 na mwisho ilifanyiwa marejeo mwaka 2002. Ni dhahiri kuwa Serikali inaamini kuwa ushirikina upo, na kwa kuwa imani za kishirikina zipo na matokeo yake ndiyo kama haya ya mauaji ya vikongwe na walemovu wa ngozi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge kanuni za sheria hiyo ya uchawi ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa mwaka 2011/2012 ilikuwa ni Sh. 16,256,015,000/=. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012, Wizara ilikuwa imepokea Sh. 9,711,796,323/= sawa na asilimia 59.7 ya fedha iliyoidhinishwa. Aidha, fedha za maendeleo zilizokuwa zimepokelewa kutoka hazina hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2012 zilikuwa Sh. 676,246,600/= sawa na asilimia 4.16 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi ni kwamba licha ya bajeti ya Wizara hii kuwa ndogo, bado bajeti hiyo haikutekelezwa kwa asilimia 40.3 Hii ina maana kwamba Wizara hii inafanya shughuli zake chini ya wastani kwa kuwa hakuna fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake. Kutoa asilimia 4.16 tu ya bajeti kama fedha za maendeleo kunadhihirisha kwamba, Serikali haikuwa na nia ya dhati ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika Wizara hii, na pia ni kwenda kinyume hata na lengo kuu la Wizara hii ambalo ni kuboresha maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataku kupata maelezo ya kina ni kwanini fedha za maendeleo hazikutolewa kwenye Wizara hii, ilhali Vyuo vya Ustawi wa Jamii ambavyo viro chini ya Wizara hii viko kwenye hali mbaya kutokana na kukosekana kwa fedha za uendeshaji na kwa ajili ya matengenezo na ukarabati?

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha, katika fungu 53, Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto inaomba kuidhinishiwa Sh. 15,616,991,000/= ikiwa ni pungufu ya Sh. 639,024,000/= dhidi ya fedha zilizopitishwa mwaka wa fedha uliopita?

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa bajeti ya Wizara hii kunaibua maswali mengi sana. Mojawapo ya maswali ni kwamba: Hivi Wizara hii inatambua kuwa ina jukumu kubwa la kuratibu na kusukuma gurudumu la maendeleo ya Taifa hili na hasa kwenye kundi maalum la wanawake na watoto?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Wizara hii ina shughuli kubwa ya kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo katika sekta zote (*Oversight Ministry*). Kwa maana

hiyo ina wajibu mkubwa sana wa kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za maendeleo zinazofanywa na Wizara nyingine na kupima mwelekeo wa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hili halifanyiki kwa sasa, na kwa kuwa bajeti ya Wizara hii inazidi kupungua na hivyo kukwamisha ufanisi wa Wizara hii, Kambi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

(i) Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vihamishiwe Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Wizara ibaki tu na jukumu la kuajiri; na

(ii) Idara ya Ustawi wa Jamii iliyo chini ya Wizara ya Afya, ihamishiwe kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto ili kuepuka mwingiliano wa majukumu. Mafunzo ya maendeleo ya jamii yaliyokuwa yanatolewa ikiwemo kisomo cha watu wazima ni vitu vinavyopaswa kurudishwa katika mfumo wa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za jamii, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

(i) Vituo vya ushauri nasaha vinapaswa kuanzishwa kusaidia wananchi kuondokana na misongo ya mawazo kama vile namna ya kuondokana na umasikini, ulemavu, mimba za utotoni, ukosefu wa mitaji na njia njema na za uhakika za kuinua kipato;

(ii) Vituo vya uokozi kwa wanawake au wanaume na watoto wanaofanyiwa ukatili wa kingono, kimwili na kisaikolojia vianzishwe na visimamiwe na Serikali ili viwe kimbilio kwa wahanga wa manyanyaso katika jamii. (Kwa mfano, wanawake wanaotuhumiwa uchawi, walemvu wa ngozi Albino, waliofanyiwa ukatili wa kigono wanajikuta hawana mahali pa kukimbilia kupata msaada (*safe house*);

(iii) Kuhusu kuwasaidia wazee, Serikali kuititia mifuko ya kijamii ianzishe utaratibu wa kuwapatia wazee mafao ya uezemi kama ilivyo kwa wafanyakazi wastaaifu.

Aidha, Vituo vya Malezi ya Wazee na watu wasiojiweza ambavyo kwa sasa ni kama vimetelekezwa na Serikali viboreshwe ili viweze kuwasaidia wazee na wasiojiweza kama walemvu na hivyo kuwanusuru na misongo ya kisaikolojia ambayo husabisha vifo vya mapema;

(iv) Mabaraza ya watoto yaliyoanzishwa kwenye baadhi ya Wilaya yapewe uzito na kuendelezwa na kusambazwa nchi nzima ili kuwajengea watoto uwezo wa kutambua haki na majukumu yao na majukumu ya viongozi kuendeleza malezi na makuzi yao; na

(v) Kwa kuwa ripoti ya Wizara ya Elimu ya 2009 inaonesha kuwa karibu wasichana 8000 waliacha masomo kwa ajili ya mimba. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kujenga Vituo vya Kuwalea Watoto na wanafunzi hawa ambaa wanakosa walezi na hivyo kusababisha watoto kutupwa majalalani, na wengine kukosa malezi na hivyo kuwa watoto wa Mitaani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia jina la Wizara hii, yaani "Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto" ni kwamba Wizara inatakiwa kuwa ndiyo kioo cha maendeleo, ustaarabu, na ustawi wa jamii ya Tanzania. Hata hivyo, Wizara hii haijafikia viwango vya juu kiufanisi vinavyoshabihiana na jina inalolibeba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuipa nguvu Wizara hii ili iweze kusimamia maendeleo ya jamii yetu ipasavyo. Kambi ya Upinzani inaishauri Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kutanua wigo wa shughuli zake ili zishabihiane na jina la Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatakiwa Serikali itambue kwamba ni aibu kwa Taifa kuendelea kutafunwa na umasikini wakati kuna Wizara nzima inayoshughulikia maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana na ume-time kwelikweli na umenipa na muda ambao nakushukuru sana. Sasa basi nitamwita Mheshimiwa Daktari Rwakatare ili awe mchangiaji wetu wa kwanza.

**MBUNGE FULANI:** *Time!*

**SPIKA:** Mbona mlitengua Kanuni? Hamkuwepo? Tumetengua kanuni kutokana na mwezi wa Ramadhani, tunamaliza saa 7.15 kisha tatarudi tena saa 10.00. Hii ni dalili kwamba hamkuwepo wiki iliyopita. Mheshimiwa Daktari Rwakatare!

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Lakini naomba nichukue nafasi ya kwanza ili niweze kumshukuru Mungu kwa wema, fadhila na kwa ulinzi na wote tupo salama, tunashukuru kwa hilo! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pia, naomba nichukue nafasi hii kulishukuru Kanisa langu la Mlima wa Moto, Mikocheni B kwa maombi yao, najua hakika ndio yananilinda kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma na kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam, nashukuru kwa maombi! Mchungaji wangu Noah Lukumay, Mzee Kiongozi Daktari Joe Mzwanda na wazee wote, naomba mwendelee kuniombea. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitoe pole kwa maafa yaliyotokea Zanzibar, wale ni ndugu zetu, naomba tuwaombee ndugu zetu na ndugu zao ili wapate faraja na Mungu awatieve nguvu, wakubali ya kwamba Mungu ndiye anatoa na ndiye anachukua. Kwa hiyo, jina la Bwana tulitukuzwe siku zote. Mungu ndiyo anajua. (*Makofî*)

**WAJUMBE FULANI:** *Amen!*

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Naomba nichue nafasi ya kwanza kuipongeza Wizara. Kwa kweli Wizara hii imefanya kazi nzuri sana, Wizara hii nimekuwa nayo tangu nilipoingia Bungeni mpaka hii awamu ya pili na kwa kweli tunashirikiana kwa karibu wakienda huku na kule kujaribu kusaidia wananchi wetu na hata wanawake na watoto. Nawapa hongera sana kwa kazi nzuri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wafanyakazi wote. Tunashukuru pia kwa Benki ya akinamama ambayo inaendelea kusonga mbele, tunawatia moyo wafanyakazi wa Benki ya Wanawake kwamba jamani hakika kazi yenu ni njema tuendelee mbele. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia na mimi nijikite kwenye kuchangia hoja ya Wizara, lakini ya kwanza kabisa naomba niseme kwa habari ya ufinyu wa bajeti. Tangu nimeingia Bungeni kila wakati tunasema bajeti ni finyu na Wizara ni kubwa mno, wana vyuo vingi, wana majukumu mengi, lakini badala ya kuongezwa bajeti imepunguzwa kwa 3.9%. Sasa sijui ni kwa sababu hawaoni umuhimu au pesa hazipo? Lakini kweli tusiilaumu Wizara ya Maendeleo ya Jamii kwa sababu bajeti wanayotengewa ni ndogo sana ili kuweza kufanikisha mambo yote.

Naomba tuiangalie na tuipe jicho Wizara hii maana yake mpaka tunajisikia kwamba hivi ni kwa sababu ni ya wanawake na watoto au nini? Kwa nini haitiliwi mkazo wala maanani? Tunaomba mwaka kesho bajeti iongezwe, hii kazi ya kutoa na kupunguzam, mkisema mnapuuuzwa inaonekana kama tunafanya kazi bure hapa Bungeni na kile tunachoshauri hakitiliwi maanani.

Mheshimiwa Spika, naomba niangalie kwenye ukatili wa wanawake. Kweli siku hizi nasikia kuna wanaume pia wanapigwa na wake zao, lakini naflkiri ni 2% lakini 98% ni wanawake wanaodundwa na waume zao. Sasa tunauliza hao wanaume wanavyowapiga wenzao, mwanamke amekuwa ngoma? Kwani kupiga ndiyo kunambadilisha mtu tabia? Kwa nini msikae mkaongea? Kwa nini msikae mkaonyana?

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko kila mtaa na kila Kata, unasikia mwanamke kapigwa, huyo analia ,ukienda kumuamulia anasema niachieni mke wangu, kwani mke wako ulimzaa

wewe mpaka umpige mtoto wa wenyewe? Si umempenda mwenyewe? Sasa kwa nini unampiga? Jamani kupigana ni ushamba, tuachane na tabia za kupiga wanawake. Wanawake wanakupikia chakula, wanakufulia nguo na wanakuzalia watoto, basi tuwaenzi na tuwapige na khanga, tuwapige na *wax*, tuwapige na *perfume* na mambo mazuri na siyo kuwapiga viboko. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba niangalie pia suala la ukatili kwa wazee. Wazee wetu ndiyo walijotuzaa, ndiyo walitulea na wametusomea, lakini sasa katika mikoa mingine Mzee akishakuwa mtu mzima macho yamekuwa mekundu kwa kupikia kuni, nyumba isiyokuwa na madirisha wanasema huyu ni mchawi, wanamuua! Jamani hiyo laana tutaipeleka wapi Tanzania ya kumwua mama yako wakati neno linasema waheshimu baba yako na mama yako, upate miaka mingi na kheri duniani. Sasa unamwua mama yako, kweli jamani? Au unamuua bibi yako, hivi kweli Mungu atakuacha hivi tu na wewe maisha yako ni lazima yatajumbe na wewe pia hakika utakipata cha mtema kuni maana Mungu ana macho mawili anaangalia huku na huku kwa wale wanaoneea.

Mheshimiwa Spika, jamani naomba tuwaangalie pia Wajane. Wajane wananyanyisika sana, wameolewa na unakuta kwamba ameweza kuchuma mali na mume wake, lakini mila potofu za baadhi ya makabila nchini, unakuta mume wake amekufa ndugu wanakuja wanamtoa nje, wanamnyang'anya mali, wanamuacha na watoto anahangaika, mjane anateseka kama vile na ye ye hakuchuma mali ile na mume wake.

Mheshimiwa Spika, jamani tukemee hilil, sheria za muhimu na kali zitungwe ili kukomesha unyanyasaji kwa wajane kwa sababu na wao pia hawakupenda kufiwa. Naomba basi hili tulitilie maanani na kwa kweli hakika itakuwa ni faraja tutakapoona wajane wana watetezi madhubuti, tunawatetea hata kisheria na wao pia waweze kupata mali ambazo wamezitumikia ujana wao wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naangalia tena suala la ndoa. Siku hizi ndoa ni kama mchezo, watu wanaoana, lakini baada ya mwezi mmoja wanaachana, au wiki mbili wanaachana, yaani hakuna heshima. Lakini neno la Mungu linasema kwamba ndoa na iheshimiwe na watu wote na malazi yaye safi, waasherati na wazinzi Mungu atawapa adhabu kali, ndiyo kuna UKIMWI, kuna watoto wa mitaani na kadhalika. Kwa hiyo, tuzingatie ahadi zetu na viapo vyetu vya ndoa, tuliapa wenyewe, tulipendana wenyewe sasa jamani siku hizi talaka inatolewa kama karatasi ya Daktari? Mtu anarudi nyumbani anaambiwa umeshaachwa, kweli jamani? Mwenzio unaniacha hivi hivi tu? Kwa kweli tuheshimu ndoa na tuwe waaminifu katika ndoa.

Mheshimiwa Spika, kwa njia hiyo hakika hata Mungu atabariki watoto wetu. Imekuwa ni aibu sasa hivi ukiuliza, kwa mfano, nimekuwa nikitembelea sana watoto wa mitaani, ukiuliza nini? Wanasema kha! Mimi sirudi nyumbani, mama na baba waliniacha. Watoto wamekuwa wa babu? Siku hizi mababu ndiyo wanalea watoto kama wenyewe tumekufa kwa sababu tu ya tamaa za mwili, unataka mwingine? Tuangalie sana. (*Kicheko/Makof!*)

Mheshimiwa Spika, halafu pia haki za watoto ambao wamezaliwa nje kama ni kwa nyumba ndogo au kama kazaliwa kwa mwanamke tu wa nje, jamani huyu baba akifa watoto wanakuwa hawana haki, tuangalie jamani tuwasaidie watoto wa nje pia wawe na haki, maana na wao wamezaliwa na baba huyo huyo. Inakuwaje huyu mama wa nje anatoa huduma kama mke wa ndoa, lakini wakati wa kufa watoto wake wanaachwa, jamani angalieni kwa sababu kweli hawa ni watoto vile kama watoto wengine, basi wasomeshwe pia na wapate elimu.

Mheshimiwa Spika, nasema pia jicho la huruma kama muda unaniruhusu tuangalie akinamama wa mitaani yaani omboomba, wanaozaa mitaani...

**SPIKA:** Mheshimiwa Shibuda, haiwezekani namna hiyo!

**MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, naomba pia tuangalie suala la akinamama omboomba wanaozalishwa mitaani au wanawake vichaa wanabakwa na

kuzalishwa hovyo. Wale watoto nawahurumia kwani wanakulia mitaani, lakini wanahitaji msaada. Kwa hiyo, tuwaangalie wale watoto kwani hawana makosa na unakuta kwamba hata wale...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana, tunaahirisha shughuli hizi mpaka saa kumi lakini tutakaporudi leo hii Wizara ina siku moja tu na bahati mbaya haina hata muda wa Spika kwani dakika 30 tulizipitisha siku ile haupo. Kwa hiyo, tutakaporudi nitamwita Mheshimiwa Thuwayba Muhammed atafuatiwa na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli na Mheshimiwa Josephine Genzabuke wajiandae.

Lakini pia Waheshimiwa Wabunge naomba, sisi tutaanza tena kutoa *registration* ya Wabunge mchana, tutaanza na ku-*register* na jioni na sababu mnazifahamu wenyewe.

Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Inaonekana bado kuna watu wanaendelea na utaratibu wa saa kumi na moja. Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Thuwayba Idris Muhammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza nitoe shukrani zangu kwa kunipa nafasi hii angalau kujadili juu ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo unaosema *where there is a successful man, there is a woman behind*. Huu ni ukweli usiofichika kwa sababu kuna wanaume wengi ambao wanajitahidi ili kufaulu na hufaulishwa na wanawake.

Mheshimiwa Spika, lakini ukiangalia wanawake ndiyo waathirika wakubwa. Kwa nini wanakuwa waathirika wakubwa? Hii ni kutokana na umbile lao, mila na tamaduni zetu na imani yao. Sasa kutokana na hali hii ndiyo maana wanawake wanakuwa katika hali ya kuathirika.

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba wanawake wengi wanatelekezwa, wanapigwa na wengi wao huweza kuchomwa na vifaa vyenye ncha, aidha na waume au wapenzi wao. Hili ni jambo la kusikitisha sana na yote haya yanakuja kutokana na kutojua haki zao na sheria zilizotungwa na nchi yao.

Mheshimiwa Spika, huu unyanyasaji sijui utaondoka lini kwani kuna sheria hizi hazifanyi kazi vizuri. Wizara wanasema wanatoa elimu, kwa njia ya magazeti, redio, na njia ya TV. Lakini hebu tuijulize hivi kweli kule vijijini kuna umeme? Kama umeme hakuna watu hawa watajuaje mambo yanayotokea katika ulimwengu? Hata kama mnatilia mkazo kwamba mnatoa elimu kwa njia ya redio, TV na magazeti, lakini ni watu wangapi wanaojua kusoma na kuandika katika maeneo ya vijijini? Hiyo elimu ya watu wazima siku hizi haipo imekuwa, sasa ni wangapi wanajua kusoma na kuandika hata mseme kwamba mnatoa elimu kwa njia ya magazeti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ikiwa hilo pia halitoshi, ni watu wangapi walio na redio huko hata wakawa na nafasi ya kukaa angalau wakasikiliza kwa sababu kutwa nzima mwanamke yuko katika mateso, yuko katika kushughulika? Akienda Serikalini anateswa, akienda katika jamii anateseka, akienda kuhusu watoto anateseka. Yeye yupo katika ulimwengu ambao hajui ni wa aina gani.

Mheshimiwa Spika, waathirika wa pili ni watoto. Watoto wanateswa bila ya kiasi, tena na wazazi wao, wanawake kwa wanaume. Watoto wanateswa na Serikali. Leo utamuona mtoto kaiba shilingi 100/= anachukuliwa mikono yake inachomwa moto, miguu yake inachomwa moto na hapewi chakula kwa muda wa siku saba (7) na anafungiwa ndani kwa sababu ya shilingi mia moja. Hii yote ni umaskini. Wazazi wanazidi kuwatesa watoto na Serikali inazidi kuwatesa watoto.

Mheshimiwa Spika, leo twendeni pale Dar es Salaam uone gari ikisimama tu watoto wanakuja na vindoo vyao wanaosha vioo vyia magari. Wengine wanafuta magari, wengine utaona wameng'ang'ania kwenye madirisha ya gari wanataka wapate fedha ili waweze kujilisha wao wenyewe pamoja na wazazi wao. Sasa mambo kama haya yatakuwa vipi katika miji hii, ukienda Dar es Salaam, Arusha na Mwanza hali ndijo hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli huu ni uchafu tena wa hali ya juu unaotendeka katika nchi yetu hii ya Tanzania. Serikali itashindwa vipi na mambo kama haya? Hebu Serikali tukae tujipange, kila siku Serikali inasema ina mikakati, leo asubuhi hapa Waziri amesema ana mikakati, ana mipango, mipango hii toka bajeti ya mwaka jana 2011/2012 mpaka leo hii hali bado ni ile ile tuna mipango na mikakati, lakini nini kinatendeka ambacho hakionekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hebu jamani Serikali tukae tuseme kwamba, kila mkoa tujenge angalau nyumba moja ya kuwaweka hawa watoto, tuwape elimu na tuangalie afya na hali zao na hapo ndijo maana UKIMWI unazidi kutokana na hali hii ya watoto kuzurura kila sehemu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuna kitu hiki kimoja, siku hizi tunasema kuna maadhisho ambayo ni ya ulimwengu. Maadhisho haya sisi Watanzania huwa ni wepesi wa kuyafanya, tunasherehekea kila yakija. Utakuta leo kuna siku ya watoto duniani, siku ya familia, na siku ya ajira mbaya kwa watoto, lakini hebu nimuulize Waziri haya maadhisho yana faida gani hapa kwetu? Kwa sababu wenzetu kule wakiwa wanafanya maadhisho wanakuwa wameshaweka mipango yao, mikakati yao na kila kitu, wanajua tunaleta maadhisho haya, kwa hivyo tunafanya hili na hili na hili kuondoa matatizo ya watoto, wanawake na jamii.

Mheshimiwa Spika, lakini leo sisi tunasherehekea, siku ya familia, ukiuliza ile familia kwa siku ile wamepata nini, hawajui isipokuwa wakubwa wanavaa sare, vilemba, utaona wako mbele pale na sherehe hizi huwa zinafanya mijini tu, vijijini hakuna. Kwa nini hatuendi kuzifanya vijijini angalau na wao wakaona kwamba hiki kitu kipo? Kubwa tunasema kwamba, tunaachia Halmashauri, watafanya nini wakati fedha mnazowatengea ni ndogo? Wataweza kweli kufanya mambo kama haya?

Mheshimiwa Spika, lakini tujiulize ni fedha ngapi zinazotumika katika sherehe kama hizi kwa ile siku moja tu? Hebu Waziri akija hapa atwambie kwa ile siku moja ya sherehe ni fedha ngapi wanayotumia ili na sisi tuweze kuelewa? Tunaweza kuwafanya hesabu na kuwaambia kwamba fedha hii angalau iwekeni kwa miaka miwili au mitatu mjenge nyumba ya watoto wapate kuishi vizuri kama mnavyoishi nyie na watoto wenu. Hii ni hali mbaya kabisa.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna sheria ambazo tunazipitisha hapa hapa kwenye Bunge kwamba, mtoto asipewe tabu, likimfika mtoto basi ashughulikiwe. Kwa nini sheria hizi hazifanyi kazi? Kama zinafanya kazi ni kiwango au *percent* gani iliyofikiwa katika kutatua matatizo haya? Kwa sababu ingekuwa sheria zinafanya kazi na Wizara ikaamua hasa kulifanya kazi hili wimbi la watoto wa mitaani, watoto wazururaji wanaoishi katika maisha magumu lingepungua. Lakini halipungui, liko hapo hapo na pengine kuongezeka. Sasa tunataka tuelewe huyu mwenye dhamana ya sheria hizi ni nani? Aje hapa Waziri atwambie kwamba, ni Serikali, Wizara, Bunge, Polisi au nani ili tupate kufahamu na tuelewe.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine la utafiti. Kuna tafiti nydingi sana zimefanya hapa Tanzania, moja imefanya hivi karibuni ya mwaka 2011/2012. Tafiti hizi zinafanya na NGOs mbalimbali kwa lengo la kujua hali ya ubakaji ilivyo, vipigo kwa wanawake, watoto wa kike kusitishwa masomo na kuolewa. Sababu kubwa ya tafiti hizi ni kutaka kuelewa hasa chimbuko, matatizo na athari. Je, kama Wizara mmezishughulikia vipi tafiti hizi, kwa sababu kuna kesi nyindi

ambazo bado hazijatatuliwa na ziko katika mikoa mbalimbali. Wao wametembelea mikoa 20 tu kati ya 180.

**SPIKA:** Iko Mikoa mingapi?

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Wamefanya tafiti katika mikoa 20 tu.

**SPIKA:** Ila iko mikoa 180?

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Naam!

**SPIKA:** Mikoa haiko 180?

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mia na thelathini?

**SPIKA:** Ishirini na tisa tu!

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Aah, *Inshallah* hiyo hiyo iliyokuwepo. Lakini wamefanya tafiti katika mikoa 20 tu basi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, zile dakika zangu ulizoniuliza.

**SPIKA:** Aaah, si wewe mwenyewe ulikosea. (*Makofii*)

**MHE. THUWAYBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia machache katika bajeti hii ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyeziwesha kusimama hapa nikiwa salama. Lakini pia nachukua nafasi hii kuwatachia Waislam wote heri katika mfungo Mtukufu wa Ramadhan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, bado najiliza hivi kweli Serikali yetu hii ya Tanzania ina nia au dhamira ya dhati kabisa ya kutaka kumkomboa mwanamke wa Kitanzania? Serikali hii imesahau kwamba, ukimwezesha mwanamke basi ndiyo umewezesha familia na watu wanaamini hivyo kwa sababu wanasesma baba ni kichwa cha familia, lakini mama ndiyo kila kitu katika familia. Naamini ukimwezesha mwanamke katika familia basi hata watoto wote watakuwa katika mazingira mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali hii imesahau kabisa habari ya mwanamke na ndiyo maana unaona hata *trend* ya bajeti ya Wizara hii kila mwaka imekuwa inapungua kwa takribani asilimia tatu (3%). Hii ni aibu na inaonesha wazi kabisa kwamba, Serikali hii haina dhamira ya dhati ya kutaka kumkomboa mwanamke wa Kitanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Serikali hii imesahau kwamba wanawake ndiyo watu pekee wanaowategemea na ndiyo wanaowapigia kura nydingi sana ukifika wakati wa uchaguzi. Wanasesha kabisa kwamba wanawake takribani asilimia 51 na zaidi wamekuwa wakiwapigia kura kwa kuwapa wao dhamana ya kukaa madarakani ili sasa waweze kuwatatulia matatizo yao, lakini Serikali hii imewasahau kabisa wanawake wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika ukurasa wa 18 wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri ameelleza kwa mfano, ule mpango wa wanawake kuwezesha, lakini pia hata ukiangalia lile azimio la Beijing katika vile vipengele vyake kimojawapo ni kile cha kumwezesha mwanamke

kiuchumi. Hivi kweli katika Wilaya zote ambazo ziko Tanzania hii Wizara imeweza kufikia Halmashauri 15 tu katika Tanzania nzima ambapo imetoa shilingi milioni 120 kwa Halmashauri zote?

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Halmashauri zote za Tanzania hii ambazo zina wanawake wengi wanyonge huko vijiji ni wamekosa fedha hizo kwa kiasi gani kwa kupitia Mfuko huu wa Maendeleo ya Wanawake?

Mheshimiwa Spika, ukitaka kumwezesha mwanamke basi muangalie yule ambaye yuko vijiji na ambaye ana hali dhilili kabisa na ni kweli kabisa anastahili kuwezesha. Lakini Serikali hii imekuwa ikitakaa maneno mazuri ambayo hayatekelezeki.

Mheshimiwa Spika, nataka niende kidogo katika huu Mfuko wa *WDF* ambao wanasesma ni Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Hivi kweli unaipangia au kuiptia Halmashauri shilingi milioni nane (8), hivi ni wanawake wangapi ambao watafikiwa kwa milioni nane hiyo katika Halmashauri hiyo? Huu ni usanii, uongo, Serikali hii haina dhamira ya dhati ya...

**SPIKA:** Hebu futa maneno yako ya uongo!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, nafuta.

**SPIKA:** Haya!

**MHE. KURUTHUMU J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, hayo ni maneno ya kuwardhisha tu wanawake lakini yamekuwa hayatekelezeki. Mfuko huu wa *WDF* ukiangalia kuna maneno kila siku yanatamkwa hapa na hasa ukiangalia Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Aggrey Mwanri kwamba kila Halmashauri inapaswa kuchangia asilimia tano (5%) ya mapato yake ya ndani katika Mfuko wa Wanawake. Lakini hii haitekelezeki na ni ahadi ambazo ni za kuwaongopea wanawake kila siku wawe na matumaini kwamba, kuna Mifuko ambayo itachangia maendeleo katika Halmashauri lakini ni uongo mtupu. (*Makof*)

**SPIKA:** Mbona una matatizo wewe? Hebu futa ... (Kicheko)

**MHE. KURUTHUMU J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, haya nafuta.

**SPIKA:** Haya. (Kicheko)

**MHE. KURUTHUMU J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mfano katika Halmashauri yangu ya Wilaya ninayotoka ya Rufiji, sasa hivi ni takribani miaka mitatu, Halmashauri hajatenga hata senti moja katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake hiyo ambayo inasemwa ni asilimia tano (5%) ya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake aje na takwimu sahihi kabisa hapa za kuniridhisha kwamba, ni Halmashauri ngapi katika mwaka wa fedha 2010/2011 au 2011/2012 zilitenga ile asilimia tano (5%) kwenye Mfuko wa Maendeleo ya wanawake kwenye Halmashauri zetu na siyo tu kubaki na maneno mazuri ambayo hayatekelezeki. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia Idara ya Maendeleo ya Jamii ambayo tunasema ni idara mtambuka, imesahaulika kabisa katika Wilaya zetu. Hivi unapoitengea Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri ya Wilaya shilingi 800,000/=, unategemea Maafisa Maendeleo ya Jamii hao watafanya kazi gani katika Wilaya ambayo, kwa mfano Wilaya yangu ya Rufiji ina Majimbo mawili, ina akinamama wengi tu unaitengea Idara ya Maendeleo ya Jamii shilingi 800,000/=, itafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, hivi kweli shilingi 800,000/= itawasaidia vipi Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenda kutoa elimu au huo uweschaji kwa hao wanawake ambao wako kwenye Wilaya husika? Hii bado nakataa kwamba, Wizara au idara za maendeleo ya jamii haziwatendei haki wanawake hasa wale ambao wako vijiji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiangalia suala la watoto, Serikali yetu iko mstari wa mbele sana katika kuingia katika mikataba mbalimbali, maazimio, itifaki mbalimbali ambazo zinalenga au zipo kwa ajili ya kuangalia haki za watoto na akinamama, lakini utekelezaji wake umekuwa ni hadithi. Pia bado narudi palepale katika suala la bajeti kwamba, inaelekea kabisa wanashindwa kutekeleza malengo yao mengi ya Wizara kwa kila mwaka kwa sababu ya ufinyu wa bajeti zao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, suala la ukatili dhidi ya watoto, kuna ripoti zinaonesha wazi kabisa watoto watatu (3) kati ya kumi (10) wamefanyiwa ukatili katika masuala ya kingono na masuala mengine tofauti. Lakini sasa ni kwa jinsi gani watoto hawa wanakombolewa, imekuwa ni hadithi. Tunasaini mikataba mingi, itifaki mbalimbali kama hizi za Maputo *Protocol*, maazimio ya Beijing na mengineyo, lakini utekelezaji wake umekuwa ni hadithi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia bado niko katika suala la ukatili kwa watoto wa mitaani. Tumekuwa tukisikia kila siku Wizara inakuja hapa inatwambia kuna mpango mkakati, mikakati imewekwa, sasa watoto basi tena kukaa mitaani, lakini mpaka leo sijaona Wizara imekuwa na kitu kipyka katika hii hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho anielezee hasa hivi ni kwa kiasi gani mikakati hii ambayo imepangwa na Wizara kwa ajili ya kusaidia watoto wanaoishi mitaani imefanikiwa? Siyo kila siku tunabaki na hadithi, mikakati yenye michakato ambayo haikamiliki na wala haimnufaishi huyo mtoto mnyonge wa Kitanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hii inasikitisha sana na ni jambo la aibu sana kwa sababu watoto bado wanaendelea kukaa mitaani. Leo katika Majiji yetu, ukifika Dar es Salaam watoto kwa kweli wanadhalilika. Mwaka jana kuna mtoto alifikia hatua ya kugongwa na kufa kwa ajali ya barabarani. Wakati akienda kuomba, bahati mbaya daladala ikamsaga na akafariki.

Mheshimiwa Spika, sasa je, hii mikakati ambayo inapangwa na Wizara na wataalam wetu kwa ajili ya kuwakomboa hao wanyonge inaishia kwenye masanduku tu? Naona tumekuwa na *documents* nydingi, lakini ambazo hazina utekelezaji. Kwa hiyo, naomba Wizara iniambie mpaka sasa hivi imefikia wapi katika mikakati hiyo iliyopo kwa ajili ya ukombozi wa watoto?

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka niulize swalı moja, kuna kitu kidogo kinanipa kigugumizi. Hii ni rai, naomba UWT basi ingebadilishwa jina na lingekuwa UW-CCM kwa sababu unaposema Umoja wa Wanawake Tanzania mbona katika mikutano wanabagua wanakwenda kichama? Naomba nipate ufanuzi, basi hii UWT iwe UW-CCM na siyo UWT kwa sababu wanawahadaa wanawake.

Mheshimiwa Spika, wanawaambia akinamama kuwa huu ni umoja wetu, uko kwa ajili ya maslahi yetu, lakini ikifika kwenye kukutana, kupeana mikopo, kupeana changamoto utakuta wanakwenda akinamama ambao wana kadi za CCM. Sasa je, huu ni umoja wa wanawake Tanzania au ni umoja wa wanawake wa Chama cha Mapinduzi? Naomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu na isiwe ni kuwahadaa akinamama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia bado kuna suala la ukatili kwa akinamama. Tumesikia kwenye vyombo yya habari akinamama bado wanapigwa na wananyanyasika. Kuna mfano wa yule mama ambaye amefariki kwa ajili ya kupigwa na mume wake. Lakini hivi kweli hii mikakati ambayo ipo kwa ajili ya kumkomboa mwanamke kijinsia inatekelezwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu ni hayo. Nashukuru sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Haya, ahsante Mheshimiwa Kuruthum. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa rehema zake nyingi kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto mama Sophia Simba kwa hotuba yake nzuri, lakini pia nampongeza Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ummey Mwalimu, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, leo nitajielekeza katika mambo mawili. Moja, nitachangia katika Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu, lakini pili nitajielekeza katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Spika, Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ndiyo yenyewe watendaji wanao-deal na wananchi vijiji. Lakini kwa masikitiko makubwa Idara hii katika Halmashauri zetu imetelekezwa ikiwa ni pamoja na Halmashauri za Mkoa wa Kigoma pamoja na Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Spika, watendaji katika Halmashauri zetu wamebaki kama yatima wametengwa na mara nyingi watendaji hawa hutumika kama *spare tyre*. Wakati mwagine Idara ya Mipango wakiwa hawana watu wa kufanya kazi kule huenda kuchukuliwa watendaji wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, yaani wanazunguka katika Halmashauri hawana nafasi ambayo wanaweza kusema kwamba wamesimama. Kwa hiyo, wao ndiyo maana nasema wapo kama *spare tyre*. Ukienda katika ofisi zao utasikitika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu iweze kutengewa kifungu ili iweze kujiendesha yenyewe. Enzi za uhuru Maafisa Maendeleo ya Jamii walitoa mchango mkubwa sana katika kuhamasisha shughuli za maendeleo hili halipingiki na kila mtu anafahamu. Lakini watu hao sasa hivi wamesahaulika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri najua ni mama mfuatiliaji, anaweza naomba ajitahidi mara anapopata fedha akumbuke Idara ile ili kusudi waweze kuhamasisha shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme vilevile wapewe vitendea kazi, wapewe magari, wapewe pikipiki ili waweze kuzunguka katika vijiji kuweza kuhamasisha shughuli za maendeleo ikiwa ni pamoja na kushughulikia mambo ya watoto na wanawake. Kwa sababu bila usafiri itabaki ni hadithi hawataweza kuwafikia wanawake na watoto katika vijiji.

Mheshimiwa Spika, sera ya CCM ni kuhakikisha kila Kata inakuwa na Afisa Maendeleo ya Jamii. Je, katika utekelezaji wa sera hii ni Halmashauri ngapi ambazo zina Maafisa Maendeleo katika kila Kata? Naomba njue, mfano, katika Wilaya ya Kasulu wakati ule kabla ya kutengwa na Wilaya ya Buhingwe kulikuwa na Kata takribani 40. Lakini Kata hizo ambazo zilitakiwa kila Kata iwe na Afisa Maendeleo ya Jamii kat iya Kata 41 tuseme ni Kata saba tu ndizo zenye hawa Maafisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sera tulioitunga wenyewe ukiangalia hapa tunakwenda kushindwa kwa sababu hatujaweza kuitekeleza vizuri. Kwa hiyo, naomba kila Kata ipelekwe Maafisa Maendeleo ya Jamii ili kuweza kuhamasisha shughuli mbalimbali katika vijiji yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Idara ya Maendeleo wapo mafundi ambao mafundi hao mara nyingi zamani walikuwa wakifanya shughuli za ujenzi katika vijiji yetu, lakini wale mafundi sasa hivi unakuta wamekaa ofisini hawana kazi wamekaa tu yaani wamedumaa tu mpaka sasa hivi akili zao wakati mwagine unakuta kama vile wamechanganyikiwa. Kwa sababu mtu anakwenda ofisini, anakuta hana kazi ya kufanya kwa kweli hatuwatendei haki. Sasa naomba karibu katika kila Wilaya viro Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na vile Vyuo vya Maendeleo ya Jamii kuna vijana ambao wamejifunza shughuli mbalimbali, ufundi uwashi, shughuli za ujenzi na shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nafikiri wale watu ambao wapo katika Idara ya Jamii ambao ni mafundi kwa kushirikiana na wale vijana wa Vyuo vyta Maendeleo Jamii vilivyo katika Wilaya zetu wanaweza kuwa wanafanya kazi zile ambazo zinatolewa na Halmashauri wakaenda kufanya shughuli za ujenzi kwenye Halmashauri kuliko kutoa *tender* kwa watu wengine wakati wapo watu ambao wamekaa hawana kazi yoyote na ni wafanyakazi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, watu hawa wakifanya kazi ile wale watu ambao wapo Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na hao wanafunzi ambao wanakuwa wamejifunza kwenye Vyuo vyetu vyta Maendeleo ya Jamii, Serikali haitapoteza fedha nydingi kwa kutoa *tender* kwa watu wengine ambao siyo waaminifu, wanaiibia Serikali kwa kusema uongo wakati wa ujenzi wa shule, zahanati na kadhalika. Kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kuliangalia hili.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii. Katika Halmashauri zetu Mfuko wa Wanawake umekuwa ukitengewa asilimia tano na Mfuko wa Vijana umekuwa ukitengewa asilimia tano jumla Halmashauri zimekuwa zikitenga asilimia 10. Lakini sasa hivi fedha hizo hazi pelekwi katika Halmashauri zetu. Sasa nataka tu njue ni lini Halmashauri hizo zitatoa fedha asilimia hizo kwa wanawake na kwa vijana ili kuweza kukopeshana wanapokuwa wamepata hiyo fedha asilimia tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumekwishakuwa waongo, siku zote tunazunguka vijijini tunakwenda...

**SPIKA:** Maneno hayo ya uongo humu ndani hayakubaliki.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naomba niyafute hayo maneno. Sisi Wabunge wakati mwingine tunapokwenda kuzunguka kwenye vijiji tunawahamasisha akinamama wajunge kwenye vikundi kwamba Halmashauri zitawapeleke mikopo matokeo yake vikundi vinaundwa, lakini ile asilimia tano ambayo inatolewa na Halmashauri inakuwa hakuna.

Mheshimiwa Spika, naomba fedha hizo ambazo zimekuwa zikipelekwa kule zinaweza kupelekwa. Lakini pia nataka kujua Wizara inalifuatiliaje jambo hili kujua hizo fedha zinapelekwa kule. Lakini pia nataka njue je, ni Halmashauri ngapi zimetenga asilimia tano kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake kwa mwaka wa fedha uliopita 2011/2012? Nataka njue hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika fedha hizo haziendi na hata zilipokuwa zikienda fedha hizo kulikuwa kunajitokeza matatizo makubwa. Kwanza, fedha hakuna, watalam wanaokwenda kutoa elimu kule vijijini walikuwa hawana taaluma ya mikopo. Kwa hiyo, hata wakienda kufundisha kwa sababu wao wenyewe hawaelewi hawawezi kufundisha kitu ambacho kinaeleweka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wale wanawake ambao wanapelekwa mikopo hiyo hawana elimu ya ujasiriamali. Kwa hiyo, vitu hivyo vitatu, fedha hakuna, watalam hawana elimu ya mikopo, lakini pia wanawake hawana elimu ya ujasiriamali. Naomba hivyo vitu vizingatiwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, najua kengele karibu itagonga. Nataka nieleze ubaguzi uliopo wa Madiwani wa Viti Maalum na Wabunge wa Viti Maalum. Hata katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 39(1)(c) hakuna sehemu inayosema kwamba wanawake wasigombee nafasi kubwa katika vyama vyetu pengine Urais au Uenyekiti wa Halmashauri. Naomba wanawake waruhusiwe kugombea Uenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Lolensia Bukwimba simwoni, Mheshimiwa Riziki Omar Juma hayupo, Mheshimiwa Moza Abeid hayupo, Mheshimiwa Christina Mughwai.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, mimi nipo.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Christina!

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kutoa maoni katika bajeti ya Wizara hii muhimu katika ustawu wa nchi yetu na ustawu wa jamii yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia mambo mawili tu kwa ajili ya muda nafikiri yanatosha.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kwanza suala Mahakama ya Familia. Nazungumzia suala la Mahakama ya Familia kwa sababu ya ucheleweshwaji wa kesi Mahakamani. Kutokana na taarifa tulizonazo kesi za familia ndiyo zinashika nafasi ya tatu kwa wingi katika Mahakama zetu zikitanguliwa na kesi za ardhi na kesi za pili ni kesi za ajira na kazi na kesi za tatu kwa wingi katika Mahakama zetu ni kesi zinazohusu mambo ya familia.

Mheshimiwa Spika, kuna Mahakama ya Ardhi kwa kuzingatia umuhimu na wingi wa kesi zinazohusu mambo ya ardhi. Vile vile kuna Mahakama ya Kazi na Mambo ya Ajira kwa kuzingatia umuhimu wa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini naiomba Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa kesi za familia ambazo tunaambiwa zinashika nafasi ya tatu kwa wingi katika Mahakama zetu Serikali ianzishe Mahakama za familia kurahisisha mashauri na kesi zinazofunguliwa Mahakamani zinazohusu mambo ya familia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mtu anapokwenda kufungua kesi Mahakamani akidai matunzo ya watoto au mirathi na kesi hiyo ikachukua miaka miwili, mitatu au zaidi hivi hao watoto wanakula nini wakati hiyo kesi inaendelea Mahakamani? Mtu anapofungua kesi ya mirathi na kesi hiyo ikachukua miaka hata zaidi ya mitano, hivi mjane huyo au wanufaika hao wa mirathi wanaishi vipi wakati kesi hiyo inaendelea Mahakamani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hii ndiyo maana naishauri Serikali kuwa, ni vizuri kwa umuhimu wa pekee kuwe na Mahakama za Familia kama ambavyo tuna Mahakama ya Ardhi na kama ambavyo tuna Mahakama ya Kazi na Ajira ili kuharakisha masuala ya familia na hivyo kuinua ustawu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, la pili niseme na mimi juu ya sheria kandamizi dhidi ya wanawake na watoto. Kuna Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi ambaao ulisainiwa mwaka 1979, lakini nchi yetu iliusaini mwaka 1980 na ikauridhia mwaka 1985.

Mheshimiwa Spika, toka mwaka 1985 nchi yetu ilipouridhia na kusaini Mkataba huo wa Umoja wa Mataifa wa kuondoa Sheria zote kandamizi, cha kushangaza hadi leo bado nchi yetu ina Sheria kandamizi dhidi ya wanawake na watoto. Ni kwa nini imechukua muda mrefu kiasi hiki kuondoa sheria hizi kandamizi?

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli toka tumesaini Mkataba huo mwaka 1985 hadi leo hii Sheria hizo bado zipo katika mfumo wetu wa utaratibu wa Sheria, je, ni kweli tuna nia ya dhati ya kuondoa sheria kandamizi? Tuna nia ya dhati ya kuwaondolea wanawake ukatili au ni kusaini tu mafaili na sheria halafu zinabaki kwenye makabrasha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa kuona hata baadhi ya adhabu zilizoainishwa katika baadhi ya hizo sheria kandamizi. Kwa mfano, Sheria zinazohusiana na mambo ya watu, tunaambiwa kwamba mtu au mwanamke akipigwa akivunjika kidole, akivunjika jino, akasababishiwa majeraha yanayopona adhabu yake siyo chini ya sh. 10 na isizidi sh. 100. Hivi karne hii, leo hii tuna sheria inayosema inamkomboa mwanamke kwa kutoa faini sh.10 au faini hiyo isizidi Sh. 100.

Mheshimiwa Spika, Sh. 100 hata peremende hainunui. Lakini pia tunaambiwa kwamba madhara kama ya kuharibiwa jicho, kuharibu kiungo daima yaani mtu ameharibiwa kiungo daima au amepoteza sehemu ya nje ya sikio lake au ameharibika kabisa sura yake mwanamke huyu

akiumizwa kiasi cha kuharibiwa kabisa sehemu za viungo vyake basi fidia yake isiwe chini ya sh. 200 na isizidi sh. 500. Huku ni kuwadharau wanawake na huku ni kutokuwatendea haki wanawake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza wakati haya yanaendelea Wizara hii muhimu na kwa kuona umuhimu wake inaongozwa na Mawaziri wanawake, inaongozwa na Makatibu Wakuu wanawake ambao ndiyo tungefikiri wangezivalia kibwebwe sheria hizi ili zibadilishwe ili kuwakomboa wanawake.

Mheshimiwa Spika, lakini hatujaona jitihada ya dhati ya Mawaziri wetu wanawake, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Katibu Mkuu na Mheshimiwa Naibu Katibu Mkuu ambao wote ni wanawake. Hatujaona jitihada ya dhati ya kuleta mabadiliko ya sheria hizi ili ziende na wakati. Huwezi kusema mtu anayeumizwa akapoteza viungo vyake alipwe fidia sh. 200 au isizidi sh. 500 hii ni fidia ya wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka Serikali, nimekuwa Mbunge sasa kwa miaka miwili siaona Wizara hii ikileta Muswada wa kuleta mabadiliko ya sheria hizi katika Bunge hili ili hizi sheria kandamizi ziweze kufutwa. Ni lini sasa Serikali italeta Miswada ya kubadilisha hizi sheria; kuzifuta na siyo kuzibadilisha kwa sababu sheria kandamizi hazitakiwi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la watoto wa kike wanaopata mimba wakiwa shulen. Ni kweli kumekuwa na mjadala kwamba ni muhimu hawa watoto wa kike wakaendelea na masomo, lakini mbona hatuoni utaratibu unaowekwa, mbona hatuoni hii sera imefikia wapi, ipo kati ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto au kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji anayeishughulikia ni nani na imefikia wapi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wanaopata ujauzito wakiwa shulen lisipochukuliwa kwa umuhimu wake linaweka matabaka. Kwa sababu wazazi wenye uwezo hata watoto wao wanapopata matatizo ya ujauzito wana uwezo wa kulea huyo mtoto na yule mtoto wao akaendelea na masomo. Lakini mtoto wa maskini anapopata mimba akiwa shulen ye ye basi shule yake inakuwa imeishia hapo hapo na yule mtoto wa kiume anayemsababishia kama naye alikuwa ni mwanafunzi ye ye anaendelea na masomo kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watoto ambao wazazi wao wana uwezo wataendelea na shule hata kama wamezaa wakiwa shulen kwa sababu wazazi wao wanaweza kuwasomesha. Lakini watoto ambao wazazi wao hawana uwezo wanapopata matatizo ya ujauzito wakiwa shulen wenyewe shule yao itaishia hapo hapo na wanashindwa kulea watoto wanaowazaa. Hivyo, tunaleta Taifa la omboomba, watoto wa mitaani na jamii ambayo haiko bora kutokana na matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri atakapokuwa anajumuisha hotuba yake atueleze Sera ya Watoto wanaotakiwa kuendelea na masomo baada ya kujifungua imefikia wapi, iko mikononi mwa Wizara ipi na itaanza utekelezaji wake lini? Tunataka kuambiwa suala la Mahakama ya Familia, itaanzishwa lini?

**SPIKA:** Ahsante nashukuru sana Mheshimiwa.

#### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kuanza na suala la Sheria ya Ndoa nikilinganisha na mimba za utotonu (wanafunzi) kwa nini Serikali isiruhusu wanafunzi kuolewa na kuendelea na shule baada ya kufunga ndoa. Wakati mwanafunzi anapopata ujauzito akishajifungua anaruhusiwa kurudi na kuendelea na masomo. hatuoni kuwa ni bora kuruhusu ndoa kwa masharti maalum katika kuruhusu watoto wa nje ya ndoa jambo ambalo linachangia ongezeko la watoto wa mitaani. Pia kutoa nafasi kwa ongezeko la gonjwa la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, tatizo la ukeketaji bado linaendelea katika baadhi ya makabila. Katika hili Serikali bado hajatoa kipaumbele kupambana na hali hii na ndio maana shughuli hii bado inaendelea kwani hakuna sheria inayotoa adhabu kwa yule atakayebainika kufanya vitendo hivi vya ukeketaji. Hili ni jambo ambalo ni kinyume cha sheria na haki za binadamu kwa kusababisha wanawake wengine kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Watoto; Mabaraza haya yanasaidia sana watoto kufuatilia haki zao katika maeneo ambayo tayari yameundwa pia kuna ugumu mkubwa wa kuundwa mabaraza haya kutokana na ukata wa fedha katika maeneo ambayo kuna Mabaraza wameweza kufuatilia hata utoro wa shule, ukatili wa watoto na haki nyingi ambazo zinavunjwa. Naiomba Serikali itenye fedha kwa ajili ya kuunda na kuyahudumia haya Mabaraza ya Watoto.

Mheshimiwa Spika, mimba za utotoni zinachangiwa zaidi na masafa baina ya shule na wanakoishi watoto. Hivyo basi, haja ya kujenga mabweni katika shule zetu ni muhimu sana ili mwanafunzi asipate muda wa kuwa mbali na shule ama nyumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, suala la wanawake wanaoachika au kufiwa na waume katika baadhi ya makabila, kuambiwa kwamba wanatolewa mkosi kwa kulazimishwa kufanya tendo la ndoa na mtu anayepangwa na familia. Je, mwanamke hana haki ya kujichagulia mtu ampendae. Je, huku si kuongeza tatizo la UKIMWI. Je, huu sio ukatili na unyanyasaji wa wanawake kwa kuamini mila potofu, kwa nini Serikali isipige vita tabia hizi na kupiga marufuku mila hizi potofu na ukandamizaji.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Spika, kuyaendekeza makundi mbalimbali, Wizara imeeleza kuwa kuwapatia wanawake mikopo yenye masharti nafuu kuititia Benki ya Wanawake. Kwa kuwa Benki hizo tayari zimeshafunguliwa Tanzania Bara lakini Tanzania Visiwani bado Benki hizo hazijafunguliwa namwomba Waziri hizo Benki zifunguliwe na huko Visiwani Zanzibar wanawake wa Zanzibar waende sambamba kimaendeleo na wanawake wa Bara. Je, Mheshimiwa ni lini hizi Benki ya Maendeleo zitafunguliwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mahabusu kwa watoto, kuna malalamiko makubwa kwa wafungwa watoto huwa wanawekwa pamoja na watu wazima, hili jambo hatari sana, kwa hiyo, namwuliza Waziri ni lini watajenga mahabusu kwa watoto?

Mheshimiwa Spika, wanawake kwenye siasa, wanawake kila siku wanakaa wakitumikia kama ngazi tu kwani wanawake hawa hutumika kufunga kampeni ili wanaume washinde kwenye uchaguzi na bila kufanyiwa kampeni na mwanamke hawawezi kushinda, lakini mwanamke huyu akita kugombea na hasa kwenye Majimbo kwenye kura za maoni huwa anapigwa kampeni chafu na wanaume na wanawake na matokeo yake hushindwa kwenye kura za maoni.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa wanawake wote, tuwe kitu kimoja kwenye vyama (kura za maoni) kwa kumpigia kampeni mwanamke mwenzetu ili ashinde. La si hivyo, wanaume mpaka kiama wao ndiyo watakuwa na nafasi za kugombea kwenye Majimbo. Pia kwa njia ya ushirikiano ndiyo tutafika asilimia hamsini kwa hamsini.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto umezidi siku hizi kila siku tunashuhudia watoto wanavyochomwa moto na wengine kupigwa na kujeruhwa vibaya sana na wengine kutupwa majaani kwa sababu eti wametelekezwa na wanaume, hoja hii sikubaliani nayo hata kidogo, huyu mtoto umembebea mimba miezi tisa na iweje umuue au umtese. Hawa wanawake ni makatili na naomba adhabu yao ni kifungo cha maisha. Pia naiomba Wizara itoe elimu ya kutosha kwa wanawake ili jambo hili lisiendelee.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna sheria nyingi ambazo zinamkandamiza mwanamke naiomba Wizara izipatie upya sheria hizo kuwa zimepitwa na wakati.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Mheshimiwa Ummy

Mwalimu, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya kusimamia utekelezaji wa sera na sheria zinazoongoza Wizara hii mtambuka. Napenda pia kumpongeza Bibi Kijakazi Mtengwa, Katibu Mkuu na Bibi Anna Maembe, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wa Wizara na Wakuu wa Vyuo na Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, hali duni ya idara Wilayani, ya katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha ambayo ndiyo Jimbo langu Idara ya Maendeleo ya Jamii ni moja ya idara zisizopata fedha toka Serikali kuu. Aidha, idara hii pamoja na majukumu makubwa iliyokabidhiwa ya kuhamasisha maendeleo ya wananchi wa jinsia na rika zote sio kipaumbele kwa Halmashauri ya Wilaya. Idara haina hata pikipiki licha ya gari.

Mheshimiwa Spika, ushauri na ombi Serikali iitengee idara hii fedha kupitia Wizara badala ya kuiachia Halmashauri na Wilaya kwa mwaka 2012/2013 naomba Wizara itupatие walau pikipiki tano au gari lilitumika lisaidie utekelezaji wa shughuli za idara hii kwa jamii Wilayani kwangu. Pia naomba Wizara isaidie kupatikana angalau Afisa Maendeleo ya Jamii mmoja kwa kila Kata kwenye Wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Wizara hii ni mtambuka na majukumu yake, naishauri kuwa iongezewe bajeti yake kwa asilimia mia moja au zaidi ili iweze kutekeleza majukumu yake aidha kwa kuzingatia kuwa Wizara hii ndiyo inayohusika na malezi ya watoto wakiwemo wale waathirika wa *HIV* na *AIDS*, ni vizuri Serikali iagize *TACAIDS* kupeleka sehemu ya fedha inazotengewa kwa Idara ya Watoto kwenye Wizara hii ili kuwezesha Wizara kuhudumia watoto hao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wanawake kujitegemea, katika Jimbo langu mwaka jana nilihamasisha wanawake kwenye Kata zote waanzishe *VICOBA* ili wapate mtaji utakaowawezesha kuanzishwa na kuendeleza miradi ya kiuchumi. Niliedhesa semina kwa wawakilishi wa makundi ya wanawake toka Kata zote za Wilaya hiyo. Kufuatia semina hiyo wanawake hao walanzisha *VICOBA* ambapo niliwasaidia masanduku na vitabu vya wanahisa.

Mheshimiwa Spika, tatizo linalowakabili wanachama wa *VICOBA* ni mtaji mdogo. Naomba Wizara iwasaidie wanawake hao kwa kuwapatia msaada wa fedha ili kuwaongezaa mtaji. Vile vile naishauri kuwa Wizara ihmize Benki ya Wanawake ianzishe dirisha la benki hiyo kwenye benki za kibiashara hususan *NMB* na *CRDB* kwenye Wilaya zote nchini ili wanawake walio mbali na Dar es Salaam wapate mikopo yenyenye masharti nafuu toka benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, hujuma *SACCOS* ya wanawake Wilaya ya Arumeru. Mwaka 2008/2009, wanawake wa Wilaya ya Arumeru chini ya usimamizi wa UWT, Wilaya walanzisha *SACCOS* ambayo ilizinduliwa na Mheshimiwa Daktari Ali Mohamed Shein aliyekuwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa mchango kwa *SACCOS* hiyo pamoja na mkopo toka *CRDB* na hisa za wanachama. Kwa bahati mbaya wanahisa hawakupata fursa ya kukopa kutokana na waliokuwa viongozi kushirikiana na watumishi kuhujumu *SACCOS* hiyo kwa kujikopesha wao pamoja na wizi.

Mheshimiwa Spika, jitihada za wanawake hao kudai fedha zao pamoja na msaada niliota kufuatilia bado haujafanikiwa. Naomba Wizara iingilie kati na kuwasaidia wanachama hao kurudishiwa fedha hizo. Wamekata tamaa na hawaamini tena kuwa kuanzisha *SACCOS* ni ukombozi kwao. Wengi wamepigwa na hata kutishiwa kitalikiwa kwa sababu ya kupotea kwa fedha walizotoa kama kiingilio na hisa.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kuchangia mwezi huu, Mtukufu wa Mfungo wa Ramadhani na majonzi yaliyoikuta Taifa letu kwa ujumla, natoa pole kwa wote walioguswa na msiba huu na kwa namna moja na nyngine natoa pole kwa Watanzania wenzangu kwa majonzi yaliyotukuta. Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu wote.

Mheshimiwa Spika, Tanzania iliridhia 1995 kwa maana ya kutekeleza vipengele hivyo vya mkataba wa aina zote dhidi ya mwanamke, lugha nyepesi mkataba mama wa kuondoa ubaguzi dhidi ya mwanamke uliopitishwa 10 December 1979 na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na nchi wanachama na ulianzia kutumika tarehe 3 Septemba, 1981 kama Mkataba wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Tanzania iliridhia 1985 kwa maana ya kutekeleza vipengele 14, hivyo pamoja na kutetewa 1990, hayo yote na kuwakilishwa 2010 na mkataba huo kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake umeandaliwa lugha ya Kiingereza, Kichina, Kifaransa, Kiarabu, Kirusi na Kihispania 1979, Tanzania ilitafsiri kwa Kiswahili kwani ni lugha ya Taifa kwa kila mwananchi asome.

Mheshimiwa Spika, maana ya ufanuzi bayana na maana ya usawa wa haki za usawa wa jinsia, haki za kisheria na haki ya wanawake kisheria, vile vile masuala ya uzazi na malezi na athari za baadhi ya mambo ya utamaduni na mila na desturi katika mahusiano ya kijinsia.

Mheshimiwa Spika, Serikali tokea imepokea na imechambua hayo yote na kwa makusudi ya dhati kabisa sheria hii ya haki hakuna huko vijiji na hata baadhi ya mijini bado mfumo dume upo dhidi ya ukandamizaji wanawake, ni dhahiri ubaguzi upo tu wazi wazi kuanzia utoaji haki za kushiriki nyadhifa za uongozi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikupe pongezi kuwa Spika mwanamke, sasa ni lini Serikali itaona wajibu wa mwanamke kiongozi kuwa Waziri Mkuu? Au Mawaziri dhidi ya hao wawili tulionao na wote wanaeleka Kamati hii? Je, viyi pia kuhusu Wizara nyiningine, wakati tunaweza! Maendeleo ya Jamii, Habari na Michezo.

Mheshimiwa Spika, haki hajji bila kudai, wanawake pamoja na utetezi wote huo bado elimu haijaonwa nchini hasa vijiji. Serikali kweli inajitahidi kuwasaidia wanawake kiasi hasa kutuendeleza kisiasa, kiuchumi kiutamaduni na kielimu wanawake tunaweza kufikia ngazi mbalimbali za maamuzi na maendeleo na kadhalika. Tunashuhudia Bunge hili tumefikia asilimia 36% wakati tulianza 1995 asilimia 15% na 2000 asilimia 20% na mwaka 2005 asilimia 30% mpaka leo hii 2010 tumefikia asilimia 36%.

Mheshimiwa Spika, ifike wakati tufikie angalau asilimia 50%. Tumeshuhudia nchi nyiningine wamefikia asilimia 50 kwa 50 kupitia Rwanda, wana 56%; Afrika Kusini wana 45%, sisi Tanzania tuna 36%, ni lini basi tutafikia kama wenzetu na sheria hii ifikie kuingizwa kwenye Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, haki ya jinsia hizi mbili, mwanamke na mwanaume; jinsia ambayo inadhirika sana kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni, kijamii, katika ya mwanamke na mwanaume mwathirika. Utakuta ni mwanamke anateseka, ananyanyasika na kutengwa katika maendeleo. Wanawake wanaonekana kama watu tu wa kupendeza, hawana maana na wapole na wapatanishi walezi wa kijamii na kuzaa na kuendeleza desturi, mila na utamaduni zinazorithiwa kutoka kwa mama, bibi kwenda kwa watoto, ulikuwa mtazamo wa baadhi ya jamii. Mtazamo huo sasa umepitwa na wakati wa kuangalia jinsia mbili.

Mheshimiwa Spika, Tanzania wanawake tunadhalilika, kitendo cha watoto wadogo wa kike chini ya miaka mitano na kuendelea kubakwa, kuozwa waume chini ya miaka hata kumi tu. Tumeshuhudia mwaka jana mtoto kupata mtoto mwenzake huko Arusha, mtoto miaka 11 kuolewa na kuzaa. Juzi tumeona mtoto anabakwa na baba yake mzazi hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pia juzi tu tumeona jinsi malezi yaliyomkuta mtoto Grammetid Arusha anavyochezewa ovyo kwa kubwakwa, mwingine ametoka kwenye vyombo vya habari, baba kamuoza mtoto mdogo wa kike miaka nane na sasa ana mimba ya miezi mitatu, eti kwa sababu tu asomeshe wenzake. Hata huko Kondoia pia iliokea mtoto kubakwa.

Mheshimiwa Spika, hii sheria imekuwa inaangalia haki za mtoto mfano, kukosa elimu, kufikia maamuzi ya haki zake huu ni ukatili mkubwa mno, Serikali ichukue mkondo wake kukomesha vitendo vya kuwadhulumu wanawake haki zao. Mwanamke mwenzetu tumeshuhudia

amegongwa na gari na kupoteza maisha kwani mama huyo marehemu alikuwa akipata mateso kwa mwanaume huyo na bado hajakamatwa. Ukatili huu ni mkubwa mno kwenye nchi ya uhuru na amani.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inafikia hatua mbaya na inaongezeka kwa kasi vitendo vya ukatili kuliko huko nyuma tulikotoka. Hivi haki za binadamu ina kazi gani? Vitendo vya ukatili kuongezeka hata huko kwenye magereza watoto kubakwa, kufungwa miaka ishirini kwa kosa la kubaka wakati kuna watu wakubwa wanafanya vitendo vya ukatili na kufungwa miaka michache hii imetokea Tabora, Kondoaa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimalize mtazamo mwingine wa jinsia wanaume, eti wana nguvu, hodari, jasiri, mlinzi, mvumbuzi, huo ni mfumo dume umepitwa na wakati na twende na wakati tusingoje wakati utuhabarish. Lazima Serikali iweke mkakati wa kutunasua sisi wanawake, tunayo sababu wanawake ni wengi 51%, wanawake wanalima asilimia 68%, mwanamke anapambana na kila jambo na mlezi wa familia. Wanawake ndiyo nguvu kazi na ina dhana nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, lakini Serikali iangalie haki inatendeka sawa. Ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia na kushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wa mitaaani, Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inaeleza juu ya haki za binadamu kwa watoto ikiwemo kupata elimu na kadhalika. Napenda kushauri Serikali iwe na mfumo unaoleweka na kuwabaini watoto wote wa mitaaani kwa kujua nani anasababisha ongezeko lao na pia Wizara iwe na mfumo unaoleweka wa kuwasaidia watoto wa mitaaani.

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kule Kibondo. Napenda kuiomba Wizara kama ilivyozikopesha Halmashauri kumi na tano kwa mwaka 2011/2012, sh. 120,000,000, napenda kuiomba Wizara iwakumbuke wanawake wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kwani wanawake ni maskini na Wilaya hii iko pembezoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya ujasiriamali; katika hotuba ya bajeti ya Wizara, ukurasa 19 inaonekana kwa mwaka wa fedha uliopita wanawake 350 walipatiwa mafunzo ya biashara na ujasiriamali. Napenda kuiomba Wizara mafunzo haya yafanyike pia kwa Wilaya za pembezoni kama Kibondo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwa Serikali kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii wasikae maofisini tu, wazunguke vijiji kuhamasisha vikundi na wananchi kwa ujumla. Huwezi kusema unaleta maendeleo ya jamii kwa kukaa ofisini tu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuendelea kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hususan Kibondo, ikiwa ni pamoja na kuongeza kozi za ujasiriamali kwa kushirikiana na VETA pamoja na SIDO.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya maafisa maendeleo ya jamii, napenda kuishauri Serikali iajiri maafisa maendeleo ya jamii mpaka ngazi za kata na vijiji ili wahamasishenye na kusimamia maendeleo.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuchangia kwa maandishi, pia sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara hi ina jukumu kubwa na zito kwa Taifa, ni Wizara ambayo inajenga hatima ya Taifa letu katika rasilimali watu. Kwa kuzingatia umuhimu huo, napenda kuishauri Wizara katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumtunza mtoto, mtoto huanza kutunzwa akiwa tumboni mwa mwanamke, hotuba hii ni muhimu sana hasa kwa wale wanawake wasio na uwezo. Kwa hivyo, naishauri Wizara kuweka usajili kwa wale wote wenye mimba ili kuweza kupatiwa maelekezo na misaada. Hali hii inaonekana hajafikiwa kwa kiwango kilicho bora, naendelea kuishauri Wizara kuwa na utaratibu wa usajili nchi nzima ili kunusuru madhara kwa wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Spika, ukatili kwa wanawake (ukeketaji) pamoja na juhudi za Wizara kuhusu suala la ukeketaji bado ukeketaji unaendelea nchini. Pamoja na elimu inayotolewa, kuna haja ya makusudi Wizara kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaohusika na vitendo hivi vya ukatili dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, watoto wa mitaani ni jambo lisilopingika kwamba wako watoto wanaoitwa watoto wa mitaani. Idadi ya watoto hawa inaendelea kuongezeka siku hadi siku na sababu kubwa inayoifanya hivyo ni kwa wanawake kukosa kuolewa na vile vile ukosefu wa kazi. Naiomba Wizara ifikirie upya kwa kutumia watalaam kuona ni kwa jinsi gani watoto wa mitaani watapungua na hatimaye kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya wanawake, naeleta Wizara inafanya kazi kubwa kuona kuwa wanawaendeleza wanawake kwa kuptitia *NGOs* mbalimbali. Naishauri Wizara kufuatilia kwa makini juu ya mipango ya maendeleo iwfikie walengwa.

Mheshimiwa Spika, pia kusimamia kwa makini fedha zinazotolewa na wafadhili ili kutoa changamoto wa wafadhili wetu kuendelea kuisaidia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNA M.J. MALLACK:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mungu aliye asili ya mema yote. Pia nikushukuru wewe kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara hii. Moja kwa moja nitoe salamu zangu za pole kwa wahanga wote wa ajali ya meli iliyotokea hivi karibuni. Naona sasa nijikite katika suala la watoto.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote napenda kusema kwamba, Wizara hii ina masuala mtambuka. Ni Wizara ambayo ingepewa (kutengewa) fedha za kutosha. Wizara hii ndiyo ikifurika watoto wa mitaani amba ni wengi sana na watakapokuwa vijana wasio na shughuli ya kufanya watalisumbua Taifa letu sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali isifanye mzaha na suala hili lichukue hatua kali kwa wazazi wanaotelekeza wake na watoto bila matunzo huku wana uwezo wa kuwatunza. Serikali kuptitia Wizara hii iwapatie magari (usafiri) Mafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii wapatiwe usafiri kila Wlaya ili waweze kuzunguka vijijini kutoa elimu kwa wananchi kuliko kukaa ofisini tu. Wananchi wanatakiwa kupewa elimu ya sheria kandamizi kwa watoto na jinsia zote wakiwemo wanawake.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi kuna uonevu sana kwa wanaume kuwapiga wake zao na kuwasababishia ulemavu na wengine kupoteza maisha kabisa kwa kipigo na vifo vingi vya aina hii. Vingi haviripotiwi bali hufanywa siri na kulipana fidia ndogo ya pande mbili kwa kukubaliana.

Mheshimiwa Spika, vile vile bado kuna mila nyngi potofu na hasa vijijini kama vile mwanamke, mama na watoto kula mboga ya maharage na baba (mwanaume) kubanikiwa kuku na kula peke yake, kisa tu ni mwanaume kichwa cha familia. Baba tena kuchukua sehemu ya mazao waliyolima na mkewe kuuza bila kumshirikisha mke wake ili apate fedha ya kuongeza mke mdogo. Hizi ni mila potofu na ni sheria zilizopitwa na wakati, lakini mpaka sasa zinatumika kwa ubabe sababu elimu haitolewi vijijini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuiomba Serikali kwa dhati ihakikishe Maafisa Maendeleo ya Jamii wapewe usafiri kila Wilaya wazunguke vijiji kuelimisha wananchi ili wajitambue, tutaepusha ukatili, uonevu na vifo vinavyozuilkia. Naiomba Serikali iruhusu wasichana wanaoacha shule kwa sababu za ujauzito waruhusiwe kuendelea na shule pale walipoachia baada ya kujifungua.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe dawa zinapatikana katika zahanati zote vijiji. Napenda kuuliza swali kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto, je! Serikali ina mpango gani na watoto wa mitaani tunaowaona wanazagaa hovyo usiku wakiwemo watoto wa kike?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa harakati kubwa za kutetea usawa wa kijinsia hapa nchini. Naomba kutoa maoni yangu katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara iweke mkakati wa kufanikisha wasichana wote waliofaulu masomo yao na kufuata nafasi ya kuchaguliwa vyuoni wanafuata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo kwani wasichana wengi wanadondokea katika mikono isyo salama pale wanapochaguliwa kuijunga na vyuo, lakini wanakosa mkopo. Baadhi ya wafadhili wasio na nia njema hutumia nafasi hiyo kuwaingiza wanafunzi waliofadhilli katika mambo ambayo ni kinyume na matakwa yao.

Mheshimiwa Spika, naomba Chuo cha Wananchi Kisarawe (*Folk Development Centre*) kiboreshwe ili fani mbalimbali zitolewe katika chuo hicho, kiweze kuleta manufaa makubwa kwa wananchi. Naomba chuo hiki kiboreshwe kwa ngazi ya VETA.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, wanawake wanaendelea kulalamikia haki yao nchini kwa sababu mfumo uliopo sasa hausaidii kumpa mwanamke haki yake ya kupata nafasi ya kazi anayostahili. Vile vile mfumo wetu hautoi haki ya kumwendeleza mwanamke kielimu, kisasa na hata kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipaswa kuhakikisha kuwa kila Wizara inapewa fungu kwa ajili ya kumwendeleza mwanamke katika nyanja zote kama ilivyo kwenye nchi nyingi ikiwemo Marekani.

Mheshimiwa Spika, ili tumkomboe mwanamke wa Tanzania ni lazima kila Wizara, Taasisi na hata Kampuni binafsi kuwe na kitengo kinachoshughulika na masuala yote yanayowahusu wanawake kama idadi ya wafanyakazi wanawake, idadi ya wakuu wa vitengo, idadi ya scholarship kwa wanawake na kadhalika. Endapo tutafuata mfumo wa wenzetu wa kuwa na kitengo cha wanawake kila sehemu, hakika uwiano sahihi utapatikana na matatizo ya ubaguzi kwa wanawake yatakwisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyowasilisha katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu ajira na uwezeshaji wa wananchi. Suala hili la kupanua ajira na kuwawezesha wananchi kiuchumi haliwezi kufikia kikamilifu kwa sababu fungu linalotengwa kwa ajili ya kusaidia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii havikidhi haja na hivyo naishauri Serikali yetu kufikiria mgawanyo wa fedha. Fedha za matumizi mengineyo ni zaidi ya bilioni nane wakati za maendeleo ni bilioni tatu tu. Naomba tutafakari kwa makini kama kweli tumedhamiria kuwajengea uwezo wananchi wapate mikopo nafuu, ujuzi na zana za kuanzishia vituo vya amali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ipitie upya na ilete hapa Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria inayolinda haki za watoto kwani bado kuna ukiukwaji mkubwa wa haki ya watoto hapa nchini. Hivi karibuni kule Sikunge mtoto aliuawa na baadhi ya viungo vyake kunyofolewa na sehemu iliyobaki ya mwili wake kubanikwa kama kitoweo. Wahalifu kama hawa lazima wawekewe sheria kali ili kukomesha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Serikali yetu kuitia Wizara hii kama ina mpango gani kuhusu kuandaa *sense itakayosaidia* kuwatambua watu wote wenyewe mahitaji maalum ili kuandaa mkakati wa kuwahudumia na hivyo kuwaondolea kero zinazoathiri ustawi wa maisha yao. Nafahamu kuna wajane, wazee, vikongwe, watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Walemaru na kadhalika. Wote hawa wanahitaji huruma ya Serikali na jamii yote ili kuwapatia matumaini ya kuishi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali inazochukua kwa kuwalinda watoto na kuhakikisha wanapatiwa haki zao zote za msingi, lakini bado changamoto zifuatazo zinawakabili watoto na kukosa haki zao.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaoishi katika mazingira magumu wanakosa haki ya kupata elimu, kulindwa, kuendelezwa, kushirikishwa na kadhalika. Hali hii inatokana na familia za watoto hao kushindwa kutoa huduma muhimu, hivyo watoto hao hutumiwa kama kitega uchumi kwenda kutufuta mahitaji mbalimbali na kuleta kwenye familia kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

Mheshimiwa Spika, hivyo watoto wa aina hii wanakutana na mazingira hatarishi kufanyishwa kazi na kulipwa ujira mdogo au hata kunyimwa kabisa. Je, hakuna mpango wa kuzisaidia familia anazowatumia watoto kujipatia kipato kwa ajili ya kujikimu, kuanzishwa miradi ili waweze kutoa mafunzo. Wapo watoto wengi hasa wa kike wanatumika majumbani. Je, Wizara haioni sasa wakati umefika kutoa tamko maalum la kuwatambua watoto hao popote walipo na kujua ujira wanaolipwa kama unalingana na kazi wanazofanya bila kuathiri haki zao kama elimu, kucheza, kulindwa, kuendeleza na kushirikishwa.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake, wapo Waheshimiwa Wabunge walitoa fedha kwa ajili ya hisa ya uanzishwaji wa benki hiyo. Je, michango hiyo inatambuliwa wapi maana katika akaunti zetu hazionekani? Utambulisho gani watapatiwa kwa wale walinunua hisa zao?

Mheshimiwa Spika, Sheria kandamizi, ziko baadhi ya sheria hazina tija kwa wanawake na watoto, naiomba Serikali kuziangalia sheria hizo kandamizi dhidi yetu ili kila mtu apate haki yake inayostahiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waziri Sophia Simba na Naibu Waziri Ummey Mwalimu kwa kazi nzuri wanayofanya kuongoza vema Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa na Katibu Mkuu wa Wizara anayefanya kazi yake kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi naomba kuishukuru Wizara kwa kukubali ombi langu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kuyapokea majengo ya iliyokuwa Kambi ya Wakimbizi Kijiji cha Mputa, barabara ya kwanza yawe Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Namtumbo. Pamoja na hali mbaya ya fedha katika bajeti yao wametafuta fedha ili ziweze kukarabati na chuo kiweze kuanza *by January*.

Mheshimiwa Spika, hii inadhihirisha jinsi walivyo *committed* kuwasaidia wananchi sio tu wa Namtumbo bali wa nchi nzima ili waweze kupata elimu na ujuzi wa taaluma za kuwawezesha kumudu maisha yao ya kila siku na kujiletea maendeleo katika maeneo ya wananchi wanaopata fursa ya kupata elimu na wasio pata elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri pamoja na kukikubali na kukianzisha chuo naomba ijitahidi kikitengea fedha za kukiendeleza chuo hicho kwa sababu ni kichanga ili kiweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MESHACK J. OPULKWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujuu orodha ya Taasisi zilizopata ruzuku kutoka Taasisi ya *Foundation for Civil Society* katika Mkoa wa Simiyu hususan Wilaya ya Meatu. Jedwali na sita la bajeti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, majukumu na malengo ya Wizara hii ni makubwa, hivyo bajeti ya shilingi bilioni 15 ni kiduchu mno. Naishauri Serikali itenye bajeti ya kutosha kwa Wizara hii 2013/2014 ili iweze kutekeleza malengo yake yote ili kufanikisha dhima yake ya kuhamasisha maendeleo ya jamii, usawa wa jinsia, haki za mtoto na ustawi wa familia.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, naishauri Serikali ilete Miswada Bungeni ili kurekebisha na kuhusisha sheria zilizopitwa na wakati na kupalilia ukandamizaji wa mwanamke na mtoto.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ibaini maeneo na makabila yanayoendeleza mila na desturi zinazowakandamiza wanawake na watoto na kuandaa mafunzo maalum ya kuyaelimisha makabila haya yanayoendelea kudumisha mila na desturi potofu katika dunia hii ya sasa. Inasikitisha kuwa Serikali inachangia katika kufumbia macho mateso wanayopata wanawake chini ya kivuli cha mila na desturi ikiwa ni pamoja na suala la mirathi na urithi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawatakia kazi njema.

Mheshimiwa Spika, naomba nawasilisha.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Sophia M. Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba nzuri na ya kusisimua ambayo imetolewa asubuhi hii. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu, Naibu Waziri wa Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kazi nzuri anayofanya na hivyo kuleta ufanisi mkubwa katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni kiungo muhimu katika jamii na tunaipongeza sana kwa jitihada wanazofanya kuleta maendeleo ya jamii. Naandika maoni haya kuikumbusha Wizara kuhusu kutuletea wananchi wa Wilaya ya Siha fedha hususan wanawake ili waweze kujikwamua kiuchumi. Tayari wanawake katika Wilaya yangu wamejunga katika vikundi mbalimbali. Hivyo, tunaomba wasaidiwe mikopo ambayo itarejeshwa kwa utaratibu wa *revolving fund*.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kutamka kuwa naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa kusoma vizuri bajeti yako. Tumepewa pesa kidogo sana za bajeti kwa nini?

Mheshimiwa Spika, maelezo yangu, Mheshimiwa tunataka haki ya kuwa hamsini kwa hamsini, Ubunge kisiasa kwa maana ya wanawake katika ngazi za maamuzi katika Halmashauri na Ubunge. Tupate maelezo.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza jahazi la Wizara

hii nyeti ambayo unyeti wake haujapewa heshima inayostahili hapa kwetu kama ilivyo nchi za Magharibi.

Mheshimiwa Spika, ili kunusuru utendaji wa Wizara, ni lazima tuwekeze kwenye kuwapata *qualified officers* lakini sijui ni kwa jinsi gani tutafikia lengo wakati Vyuo vya Mendeleo ya Jamii nchini vina hali mbaya. Naomba Waziri atuambie ana mpango gani na Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Mlale Songea ambacho kimefungwa toka tarehe 4/7/2012 chini ya *RPC* na *DC*. Kwa sababu zinazoweza kutafutiwa ufumbuzi za uchache wa wakufunzi (wakufunzi watatu kwa wanafunzi 417), kukosa maji safi na salama, kukosekana huduma za afya, kutokuwepo kwa umeme wala *generator* na kutokuwepo kwa darasa la *computer* (*computer* mbili kwa wanafunzi 417) na kukosekana kwa malazi ya kutosha kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, nini hatma ya taasisi hii na *implication* yake kwenye bajeti hii?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Wizara, Waziri, Naibu na Watendaji wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kuona umuhimu wa Wizara hii iliyobeba masuala yote ya wanawake na watoto. Kitendo cha kuendelea kupunguza bajeti ya Wizara kila mwaka na hata kile kidogo kinachotengwa hakitolewi hata robo ni kutotaji kundi hili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mkakati gani wa kutoa elimu na mafunzo ya kubadilisha taratibu za makabila baadhi zinazonyanyasa na kukandamiza wanawake. Makabila ambayo wanawake wanadolewa kwa mahari kubwa sana (ng'ombe 25- 30) wanaonekana kama wamenunuliwa. Wanaume zao wanaona ni haki yao kuwafanya chochote kwa sababu wamewatolea mahari kubwa, hivyo ni mali yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya jamii kupiga kelele kuhusu mateso yanayowapata watoto wa kike kwa vitendo vya kukeketwa. Kwa sasa hivi makabila yenye tamaduni hizo wameanza utaratibu wa kuwakeketa watoto wa kike wakiwa bado wadogo (wachanga). Huu ni uonevu, ni unyanyasaji wa hali ya juu, kuna mikakati gani ya kuondoa mateso haya kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, sheria zote zinazoangalia masuala ya wanawake zikiwepo zile za *JALA, marriage Act Penal Code* na kadhalika. Zina mapungufu makubwa sana. Nyingi zina vipengele ambavyo ni kandamizi. Tunaomba mpango mkakati wa Wizara kuhakikisha sheria hizo zinaletwa hapa Bungeni mapema zifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wa mitaani ni aibu kwa Taifa hili kila leo wanaongezeka miji yote. Serikali isikimbie majukumu, nchi zote wana mipango ya ndani ya kuweza kutatua tatizo la watoto wa mitaani. Mpango wa Serikali ya Tanzania kuondoa na kupunguza tatizo la watoto wa mitaani ni upi? Umefanikiwa kwa kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, kesi za watoto wanaobakwa, kukeketwa, kupigwa na wazazi na walezi wao nyingi zimekaa sana Mahakamani bila kutolewa hukumu, huku watahukumiwa wakiendelea kutesa mitaani na watoto waliathirika wakiendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianzishe dawati la watoto na wanawake kwenye Mahakama za mikoa ili kesi hizi ziondoshwe haraka na haki itendeke kama ilivyo kuwa kwa mauaji ya watu wenyewe ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, adhabu za makosa haya ya watoto na wanawake ziongezwe ili iweze kutoa fundisho kwa wengine.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa kuanzia na Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa hawa wawepo Kilakala, Maafisa hawa ngazi ya Halmashauri wapewe *OC*, Maafisa hawa wapewe vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaozagaa mitaani, Serikali ifanye uchambuzi kwanza kujua chanzo ni nini, chanzo cha ongezeko kubwa la watoto wa mitaani, iwapo sheria ya kuzuia mtoto kuzaa kama hana uwezo wa kutunza mtoto.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaozagaa waunganishwe na kuwekwa sehemu moja baada ya hapo. Serikali itoe mafunzo kwao na kuwapa mahitaji muhimu kama, chakula, malazi, matibabu na elimu. Wakishakuwa watu wazima wapatiwe kazi ya kufanya ni katika malipo yao wakati gharama zote ambazo Serikali ilitoa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2012/2013 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la mmomonyoko wa maadili linazidi kukua na kuumiza vichwa vya wadau wengi ndani na nje ya nchi yetu. Katika mchango wangu wa mwaka jana wa Wizara hii, nilijaribu kubainisha baadhi ya mambo yanayoweza kuchangia maadili kumomonyoka ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sayansi na teknolojia, umaskini, tamaa na ulafi wa mali na kadhalika. Bahati nzuri mambo haya yote yako katika jamii zetu na mengine yako katika nafsi za watu wengine nje na nafsi zao.

Mheshimiwa Spika, suala la mavazi kwa wanawake limekuwa ni kero kubwa kwa wadau wengi nikiwa mionganoni kumekuwepo na tabia isiyordhisha kwa dada na mama zetu kuvaan nguо ambazo si sawasawa na maadili yetu ya kiafrika. Lakini mbaya zaidi ni mavazi ya kudhalilisha utu wao wenyewe sababu kubwa inayotolewa na wenzetu hawa ni haki za binadamu. Nafikiria kisingizio hiki si sawa wala hana mashiko. Baadhi ya mavazi yasiyofurahisha na kupendeza ni kama vile sketi fupi, kuvaan nguо za kulalia mchana barabarani na kadhalika. Wizara hii inayohusika na jinsia hii ya kike ina mkakati gani wa kupunguza au kuondoa hali hii ambayo iko ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema kuwa na Benki ya Wanawake nchini kwa kuwa imeanzishwa kuwakomboa wanawake kiuchumi. Jambo la kusisitiza hapa ni hii benki iweze kusambaa maeneo mengi hasa vijijini ili akinamama wengi zaidi wanufaiki. Nasikitika kwamba pamoja na kuchangia katika bajeti ya Wizara hii mwaka jana bado Jimbo langu la Kibaha Vijijini halijaweza kufaidika na neema hii. Mheshimiwa Waziri naomba atambue hili na afanye kila namna ili benki hii isiwe ya kibaguzi kwa kujikita mijini tu bila ya kuhudumia wanawake vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wenyewe ulemavu wa ngozi (*albino*) ni lazima watafutiwe utaratibu mzuri ambao watakuwa salama. Wizara iweke mkakati wa kuaminika ili wauaji wa watoto hawa wakose mwanya wa kudhulumu ndugu zetu hawa. Penye nia pana njia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupokelewa maoni yangu. Naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo:-

Naomba utembelee Halmashauri ya Moshi Vijijini kukagua shughuli zinazofanywa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri za Wilaya zinatakiwa kutoa asilimia kumi ya makusanyo yao kwa ajili ya kuendeleza miradi ya akinamama na watoto. Halmashauri nyingi hazifanyi hivyo, kama Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Hesabu za Mitaa nitafuatilia fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotolewa kwa Wizara hii ndogo ukilinganisha na majukumu yake ya kuangalia watoto yatima walemau na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iendeleze jitihada zake za kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iendelee na jitihada za kukemea mauaji ya vikongwe na walemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, Masista wa *Holy Spirit Sisters* wa Rauya Marangu Moshi Mkoani Kilimanjaro wako tayari kuanzisha nyumba ya kulea wazee. Naomba kama itawezekana Mheshimiwa Waziri awaone, awatie moyo ili waanzishe kituo hicho. Kituo hicho kitakuwa cha pekee katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PEREIRA A. SILIMA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nawapongeza Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayofanya. Hongera pamoja na pongezi naomba kuchangia katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, unyanyasaji wa jinsia ni tatizo kubwa sana kwenye baadhi ya Mikoa na makabila ya Tanzania, hivi karibuni kumetokea mauaji ya kutisha kwa visingizio mbalimbali. Jambo hili lazima likemewe liwekewe adhabu kali, lakini pia msingi wa elimu kuhusu suala hili itolewe.

Mheshimiwa Spika, chokoraa watoto wa mitaani nchi yetu inaendelea kupokea idadi kubwa ya watoto kutoka kwenye familia ambazo hazithamini kuwatunza watoto. Naelewa kwamba sera ya sasa ni kutoa elimu ili familia zione umuhimu wa kuwatunza watoto. Bado hakuna dalili za mafanikio ya sera hii kwani wimbi la watoto wa mitaani bado linaongezeka. Aidha, zipo ishara kutokana na baadhi ya akinamama kutoa mamba, kutupa watoto wanaowazaa mara tu baada ya kujifungua na hata wengine kuwaua kwa sumu na au kuwanyongea.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iitazame sera yake na kama itakubaliana nami haitoshi basi mabadilko yafanywe.

Mheshimiwa Spika, ukeketaji Serikali imepiga marufuku suala la ukeketaji baada ya uchambuzi wa kina wa athari za ukeketaji kwa wahanga wa jambo hili. Nasikia kwamba hivi sasa sherehe za ukeketaji zimeshitishwa ili Serikali isigundue harakati za ukeketaji na baya zaidi watoto wanakeketwa mara tu baada ya kuzaliwa hili ni tatizo kubwa zaidi. Naomba Wizara ilifanyie kazi ili tatizo hili likomeshwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA SAADALA:** Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Wizara katika kuleta ustawi wa jamii yetu. Wizara hii ni muhimu sana katika kuleta maadili mema kwa watoto na vijana.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri watuelezee mkakati gani wanachukua hasa kwa wale watoto ambao wamezaliwa jela (gerezani). Haki zao za msingi za kitoto kucheza, kujifunza kiasilia kutokana na maumbile ya binadamu (*milestone development*) na hata kujifunza kuanzia *nursery school* mpaka *primary school* na *secondary school*. Mheshimiwa Waziri atueleze mkakati wa Wizara juu ya wafungwa hawa wa kinadharia.

Mheshimiwa Spika, ubakaji matukio ya ubakaji kwa watoto ni mengi sana. Nashauri *sensitization* ya hali ya juu ifanywe ili wananchi wasiwe na woga wa kujitokeza yanapotokea matatizo ya ubakaji wa watoto na vielelezo, sheria ya kumlinda mtoto juu ya ubakaji ili waondoe woga, matumizi ya ARV kama ni *prophylaxis*.

Mheshimiwa Spika, ajira za watoto, ijapokuwa ajira za watoto ni nyingi, Wizara ijikite katika kupunguza hili lakini iwe imara katika kukuza vipaji ya watoto.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na wafanyakazi wa Wizara hii kwa kazi nzuri. Hata hivyo, nasikitika kwa bajeti finyu inayopewa Wizara hii. Ufinyu wa

bajeti ndiyo unajionesha hadi ngazi ya Halmashauri ambapo idara huwa haipangiwi bajeti kabisa. Hii inafanya utendaji kazi uwe dhaifu licha ya ukweli kuwa Wizara hii ndiyo kiungo cha Wizara zote. Dhana ya kumwendeleza mwanamke ni kuendeleza Taifa inashindwa kutekelezwa kutokana na bajeti ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri apange ziara Jimboni Busega ili asaidie kuzindua kituo cha watoto wenye mahitaji maalum cha Lukungu ambacho kimejengwa kwa msaada wa Shirika la Kitalii la *N and Beyond* la Serengeti National Park. Kituo hiki ni muhimu sana kwa ukanda wa Ziwa Victoria. Naomba pia wafanyakazi wa Wizara hii walipo vijijiini wapewe mazingira mazuri ya kufanya kazi zikiwemo ofisi, usafiri na nyumba za kuishi. Pia lazima kuwa na vigezo vya kuwapima utendaji kazi wao ili waweze kufikia malengo yaliyokusudiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimepata taarifa kwa masikitiko makubwa kifo cha mwanamke aliyekuwa ameolewa kule Bunda kutokana na mateso na vipigo vya mumewe. Sijasikia Serikali ikilaani matukio ya aina hii wala kuisaidia familia ya marehemu katika kumsaka kwa dhati dhalili huyo ambaye anasemekana ni mfanyakiareshara na tajiri mkubwa. Haki ya uhai ya mwanamke huyo lazima ilindwe. Nashangaa kwa nini hata zile taasisi za haki za wanawake za akina Ursi Malya na Ananilea Nkya hazijatoa kauli bali kushabikia tu migogoro ya madaktari. Inasikitisha!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILIFI:** Mheshimiwa Spika, naomba kupata majibu namna gani Wizara imejipanga kukabiliana na ongezeko la watoto mitaani. Inasikitisha sana kuona baadhi ya watoto wa Kitanzania wameshindwa kabisa kusoma na sasa wanalandanda mitaani na kufanya kazi ngumu na wengine wasio na uwezo wa kufanya kazi wamekuwa omboomba. Wanaonekana kwenye majalala wakiokota vitu viliviyotupwa. Hali ambayo ni hatari hata kwa afya zao. Je, Wizara inachukua hatua gani? Mara nyingi wamekuwa wakipewa jukumu Halmashauri, ni ukweli kuwa zimeshindwa kudhibiti ongezeko hilo. Naomba mikakati ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, aidha walio wengi hawana wazazi wote, wengine wana mzazi mmoja wengine wana wazazi wote, lakini wamewatelekeza watoto japo wapo watoto wengine wanaamua kuondoka nyumbani kwa wazazi wao na kuwa wazururai, sheria inasemaje namna ya kudhibiti hali hii mbaya inayotia aibu Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwani hakuna sheria ya kuwabana Wazazi na ndugu wa watoto hawa? Kwani wakihojiwa hawajulikani wanakotoka? Je, Wizara ipo tayari kutoa amri ya kuwakusanya na kuwatambua watoto hawa kwenye mijji yetu yote? Je, wimbi hili la omboomba kwa kuwatumia watoto tunalidhibiti vipi?

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara hii isinyamaze kwani ukombozi wa watoto hawa unategemea sana utendaji bora wa Wizara hii. Kuendelea kulifumbia macho tatizo hili ni kuitafutia laana Tanzania, nchi yenye neema ambayo kwa sasa inataka kushuhudia kizazi cha Taifa hili kikigawanyika na kuwa na watoto wenye maisha bora na watoto wenye shida ya kutisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni vyeti kwa Maendeleo ya Jamii, lakini najiuliza mbona bajeti yake ni ndogo sana? Ni kwa nini fedha za maendeleo ya jamii kwenye Manispaa zisiletwe Wizarani ili Wizara iweze ku-*coordinate* jinsi ya upatikanaji wake ili ziweze kusambazwa jinsi inavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, nyumba kwa ajili ya maendeleo zilizojengwa bado zinatumika kwa kazi nyingine kabisa na nyingine zimegeuzwa mabaa. Hii inawanyima akinamama fursa ya kupata mafunzo mbalimbali. Ni mwaka sasa niliuliza swali Bungeni na nilijibowi kuwa mikakati inafanywa

kuzirudisha. Nataka kujua ni hatua gani imechukuliwa na ni lini nyumba hizi zitarudi kutumika kwa misingi yake.

Mheshimiwa Spika, benki ya wanawake tulioisikia inaundwa tulidhani ingezingatia hali halisi ya wanawake kuhusu dhamana ni kwa jinsi gani benki hii ni tofauti na benki nyingine au ni jina tu. Benki hii vile vile ingeweza kuongezwa mtaji ili iweze kuchukua kwa haraka. Benki nyingine zinatumika kupidishia fedha mbalimbali kama *TIB, CRDB*.

Mheshimiwa Spika, aidha, zinatumika kupidishia fedha za uwekezaji na mitaji zinazotolewa na Serikali na mabilioni ya Jakaya Kikwete. Kwa njia hii Benki hizi zinakuza mtaji wake kwa tozo mbalimbali. Ni kwa nini Serikali isitoe au kupidishia fedha za uwekezaji kwa wanawake na jamii nyingine zilizo nyuma kama vijana zisipitishiwe huku ili zisaidie benki hii kukuza mtaji wake.

Mheshimiwa Spika, kunahitajika sheria kali kwa watu wanaowaacha watoto kuwa wazururaji. Hii inapelekea hawa watoto kukosa kabisa mwelekeo wa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Wizara isimamie sheria ya kuruhusu watoto wa kike wanaopata mimba kuweza kuendelea na shule. Mara nyingi sana watoto hawa ni *victims* wa mafataki na mara nyingine hata hawamjui aliempa mimba au alibakwa tu.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingi sana hasa za maslahi ya watoto na wajane zinahitaji kuangaliwa upya. Hali ilivyo sasa haziridhishi kabisa.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika mambo machache katika mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kuwawezesha wanawake kiuchumi, Serikali imejitahidi kuandaa taratibu za kuwawezesha wanawake kiuchumi. Kuna Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Benki ya Maendeleo ya Wanawake ambavyo kuhusika na kuwapa mikopo wanawake. Changamoto iliyopo hapa ni kwamba, fedha inayotolewa kila mwaka kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ni kidogo na kwa hivyo wanaonufaika ni wanawake wachache.

Mheshimiwa Spika, pia fedha inayotolewa na Serikali kwenye Benki ya Maendeleo ya Wanawake ni kidogo haitoshi kwa mikopo itakayowawezesha wanawake wengi. Kwa jumla juhudhi hizi za Serikali hazitoshi kabisa kwani wanawake wanaofikiwa na huduma husika ni wachache na hasa wanaobahatika ni wanawake wa tabaka la juu na kati. Wanawake wengi wenye hali duni waishio vijijini na hata mijini hawajaguswa na juhudhi hizi.

Mheshimiwa Spika, swali kwa Serikali, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wanawake wengi wenye hali duni ili wapate kujikomboa kutokana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hotuba za Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani zimesisitiza tatizo la ukatili dhidi ya wanawake na watoto, tatizo linalozidi kukua siku hadi siku. Ni dhahiri kuwa juhudhi za Serikali hazitoshi Serikali inapaswa kuchukua hatua za ziada mbalimbali ambazo ni pamoja na zile zilizopendekezwa na Kamati na Kambi Rasmi ya Upinzani hatua nyingine ni, kampeni za uelimishaji kuhusu haki za wanawake na watoto ziimarishwe kwenye ngazi ya Kata na Vijiji nchini kote.

Mheshimiwa Spika, haki za wanawake na watoto ziingizwe kwenye mitaala ya shule za msingi na shule za sekondari na vyuo vyote pamoja na vyuo vikuu, sheria zote zihusozo wanawake na watoto zirejewe na kanuni zake ziandaliwe kwa namna itakayoziba mianya yote ambayo hivi sasa inawafanya watu wawafanyie ukatili wanawake na watoto kwa visingizio vya mila.

Mheshimiwa Spika, mshikamano baina ya wanawake dhidi ya mfumo dume, ndiyo chanzo cha matatizo yanayowakuta wanawake wengi kuhusiana na haki zao mbalimbali. Uelewa wa wanawake wengi kuhusu suala hili bado ni mdogo. Ili kuimarisha uelewa kuhusu jambo hili, nashauri Serikali iandae utaratibu wa kuanzisha Baraza la Wanawake litakaloshirikisha wanawake wa vyama vyote bila ubaguzi wa kitikadi.

Mheshimiwa Spika, Baraza kama hilo lilikuwa limeanzishwa miaka ya nyuma (miaka ya 1990) na Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, lakini kwa sababu ya sintofahamu iliyotokea likagonga mwamba. Ni wakati muafaka sasa kwa Baraza hili kufufuliwa. Lengo lake liwe kuwaelimisha watu kuhusu masuala ya usawa, haki na hatari na hasara ya mfumo dume.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, lakini kwa bahati mbaya Serikali imetoa fedha kidogo ya bajeti. Serikali ifikirie kuongeza fedha ili baadhi ya mapendekezo ya Kamati na Kambi ya Upinzani yaanze kufanyiwa kazi mwaka huu wa fedha.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii inaonekana imejikita sana katika sura ya kisasa na kujaribu kuwalaghai wanawake wa Kitanzania na Watanzania wa ujumla wake na ni Wizara inayoonesha imetafuta njia ya kuwapa baadhi ya wanasasa ajira ikilinganishwa na mtiririko wa kushuka kwa bajeti yake kila mwaka. Tokea 2010/2011 hadi mwaka huu wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ndani ya miaka mitatu bajeti imeshuka mfano, mwaka 2011/2012, bajeti ya Wizara lilikuwa shilingi 19.9, kiwango kilichopungua kwa shilingi bilioni 1.8 ikilinganishwa na bilioni 21.7 zilizotengwa 2009/2010, upungufu wa asilimia 8.3. Mwaka 2011/2012 ilipungua kwa asilimia 18.2 kutoka bilioni 19.9 zilizotengwa mwaka 2010/2011 hadi bilioni 16.3.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka huu imetengwa bilioni 15.6 zikiwa zimepungua shilingi milioni 639 (sawa na asilimia 3.9) ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 16.3 iliyotengwa mwaka 2011/2012. Hii inaonesha ni dhahiri kuwa Wizara hii haina mtiririko mzuri wa bajeti yake na hivyo kufanya Ustawi wa Maendeleo ya Jamii kuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kulaani vitendo vya kikatili na vya mteso vinavyoendelea kuwakabili vikongwe na pia jamii ya watu wenye ulemavu wa ngozi (*albino*) ambapo kumeripotiwa tukio la kuuliwa na hatimaye kukatwa viingo vyake, mmoja wa *albino* mkoani Arusha, licha ya Serikali kueleza kuwa vitendo hivyo vimekomaa, lakini ukweli umebakii kuwa jamii hii bado inaandamwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia hii ieleteze mipango endelevu iliyoiandaa kuhakikisha vitendo hivi yakiwemo mauaji haya haviendelei; hatua zilizochukuliwa mpaka sasa za kuwafikisha wahusika kwenye vyombo vya Sheria; idadi ya kesi zilizopo zilizohukumiwa na zilizokwisha na zinazoendelea na idadi ya *albino* walolipwa fidia kutokana na kadhia hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii imejiandaa vipi kuondoa ukatili na mteso yanayofanywa katika magezeza yetu dhidi ya watoto kwa kuanzisha vituo vya kulea watukutu. Kuanzisha vituo, shule, kambi za watoto wanaoishi maisha hatarishi, machokoraa na waliokosa elimu katika umri unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii ina tawimu gani za watoto na wafungwa wanaopata maambukizo ya VVU wanapokuwa katika jela zetu na kipi kimefanyika kuweza kudhibiti yasitokee maambukizi mapya kwa wao wenyewe na kwa wengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara hii imejipanga vipi kuhakikisha hakuna urasimu katika upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa katika maeneo ya vijijini ambako wananchi wengi hawaoni umuhimu wa kuwaandikisha watoto wao. Pia Serikali inasemaje kuhusu vijana hao wa vijijini kuweza kupata nafasi za mafunzo na ajira ikizingatiwa kuwa vyeti hivyo ni ghali ukichelewa kuvipata muda muafaka na hali ngumu inayowakabili wananchi huko vijijini ukizingatia moja ya sharti ni kuwa na vyeti vya kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatoa maelezo gani kuhusiana na taarifa ya vitendo vya unyanyasaji wa wasichana kwa kulazimishwa kufanya vitendo vya ngono wanapokuwa katika mafunzo ya JKT, Magereza, JWTZ, Polisi na Kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina idadi ya waliopata maambukizi wakati wa mafunzo hayo. Mkakati upi ulichukuliwa kupunguza athari hizo?

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la watoto wanaoishi katika mazingira magumu, katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Dodoma na kadhalika. Kumekuwa na ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Watoto hawa wamekuwa wanaambatana na wazee wao na hao wazee wao wanawatumia hao watoto kama kitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuwatuma kwenda kuomba barabarani, kuwatumia kwa kufanya vibarua hatarishi na baadhi ya wengine hutumiwa kwenye kufanya vitendo viovu au kujingiza katika vitendo viovu kama wizi, vitendo vya ngono na wengine hutumiwa na majambazi kuitishwa madirishaji kufungua milango ya watu na wengine kuvutishwa madawa ya kulevyia na kupelekea watoto hawa kuathirika kisaikolojia. Je! Serikali haioni hili ni janga la Kitaifa?

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali kuitia Wizara hii itaweka utaratibu wa uimarishaji wa mfumo wa kijamii wa kutunza watoto ambaa wanaishi katika mazingira magumu? Ni lini pia Serikali itatenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kulea watoto wanaoishi katika mazingira magumu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *NGOs*, kumekuwa na utitiri wa *NGOs* zinajihuisha na watoto waoishi katika mazingira magumu na *NGOs* hizi zimekuwa zikiwatumia watoto hawa kama mtaji na wamiliki wa hizo *NGOs*. Wamekuwa wakipata misaada kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi na misaada hiyo haiwfikii walengwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakiki hizo *NGOs*?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kudhibiti watoto wanaoishi katika mazingira magumu na kukimbia katika miji mikubwa, Je, hawa Maafisa Maendeleo wa Wilaya wana *sense* ya watoto wanaoishi katika maeneo yao. Je, kuna utaratibu gani unaofanyika kutoka Wilayani wa kuadhibiti watoto wanaokwenda katika miji mikubwa? Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia wazee wanaoishi na watoto waliofiwa na wazazi wao kutokana na gonjwa la UKIMWI?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabweni ya shule ya wanafunzi wa kike, hili nalo ni tatizo, watoto wanatembea umbali mrefu. Hivyo, kukutana na vishawishi kwenda au kurudi shule ikiwemo pamoja na ubakaji na mimba zisizotarajiwa. Je, Serikali ina mikakati gani kujenga mabweni ya wasichana katika shule zilizo mbali na maeneo wanayoishi?

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ni lini Serikali kuitia Wizara hii itaweka utaratibu wa uimarishaji wa mfumo wa kijamii wa kutunza watoto ambaa wanaishi katika mazingira magumu? Ni lini Serikali itajenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kulea watoto?

Mheshimiwa Spika, Vitendo hivi bado vinashamiri vya wanawake kufanyiwa ukatili na waume zao. Kwa mfano, mwanamke aliyeburuzwa na gari na mumewe katika Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara na hatimaye kufariki, lakini mpaka sasa hakuna hatua yoyote iliyochochukuliwa dhidi ya huyo mwanaume aliyefanya ukatili huo. Wizara hii ina mikakati gani ya kutokomeza unyanyasaji wa kijinsi unaoshamiri siku hadi siku?

Mheshimiwa Spika, kuitia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ina mikakati gani ya kutoa elimu kwa akinamama waliopo pembezoni ili wawzeze kujua haki zao ili kupunguza vitendo vya ukatili dhidi yao? Hata kwenye Katiba yetu bado kuna ibara ambazo zinamkandamiza mwanamke na mfano wa ibara hizo ni ibara ya 24(1)na (2) ambayo inazungumzia haki ya kumiliki mali; ibara ya 22(1)na (2) ambayo inazungumzia haki ya kufanya kazi, pamoja na vifungu vingine mbalimbali vya Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Benki ya Wanawake, wanawake wengi ambao wapo pembezoni bado hawajapata elimu kuhusu benki hii hususan wamekuwa wakijilingiza kukopa katika *SACCOS* zenyе riba kubwa na kupata matatizo. Je, Wizara hii haioni kuwa umuhimu wa kuweka riba ndogo ili kumkomboa mwanamke? Je, Wizara hii haioni bado kuna umuhimu wa wanawake wajasiriamali kupewa elimu ya kutosha katika masuala ya mikopo?

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri, pamekuwepo na upungufu mkubwa wa Maafisa Maendeleo katika Halmashauri zetu jambo ambalo hufanya maendeleo mengi kutokukamilika kwa wakati na kutokusimamiwa ipasavyo. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha Halmashauri ambazo hazina Maafisa wa kutosha mpaka kwenye Kata wanapatikana na kutosha ina mikakati gani?

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake, pamoja na ni njema ya kuanzisha benki hii ili iweze kuwasaidia hasa akinamama. Naipongeza kwa kuweza kutoa mikopo ya bilioni 2.1 kwa vikundi 195. Hizi ni jitihada za kupongezwa. Swali, je, benki hii ni lini itafungua matawi katika sehemu nyingine za Tanzania mfano Jimbo la Moshi Vijijini ili kuweza kuwasaidia waliopo vijijini ambako wengine huduma za benki haziwafikii.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, hii sheria inamkandamiza kabisa mtoto wa kike kwa kuruhusu kuolewa akiwa na miaka 15 wakati Sheria ya Mtoto ya 2009 wanamtambua kama mtoto. Lakini watoto hawa wadogo wakiolewa wakiwa wadogo wana nafasi kubwa sana ya kupata magonjwa kama *cancer* kwa sababu tayari watakuwa wamefanya tendo hilo kabla ya umri wao kuwaruhusu.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake yanapelekea vijana (wasichana) wengi kufariki kabla ya umri wao. Hivyo basi kuna umuhimu wa elimu kutolewa kwa wazazi juu ya madhara haya na Serikali iharakishe marekebisho ya Sheria ya Ndoa 1971 ili kuwanusuru watoto hawa ambao Taifa linawategemea.

Mheshimiwa Spika, Mashirika Yasiyo ya Serikali (*NGOs*), hapa nchini pamekuwepo na Mashirika mengi sana Yasiyo ya Kiserikali yanayonisikitisha ni yale yaliyojikita zaidi na malezi ya watoto yatima. *NGOs* hizi Serikali inabidi izichunguze sana kwa sababu baadhi yao zimekuwa haziwatunzi vizuri watoto wale, hawali vizuri, hawalali vizuri wao wakishapata fedha za kuwasaidia haziwalengi walengwa. Kwa mfano kituo cha kulelea watoto wa mitaani wa mkombozi kilichopo Moshi Mjini, Majengo.

Mheshimiwa Spika, kile kituo kipo pale kwa kujipatia tu fedha. Wizara fanyeni matembezi katika kituo kile, kimegeuka kituo cha majambazi bila ya kuwa kituo cha kuwalea kimaadili ili warudi katika familia zao. Wale viongozi hawapaangalii kabisa, Sera ya Mtoto ya 2008 ni kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi kama za kuishi na kadhalika. Hali siyo nzuri kabisa katika kituo kile.

Mheshimiwa Spika, haki za wenye ulemavu, sehemu nyingi hata mashulenii bado mazingira sio rafiki kwa watu wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na shule kuwa na vifaa vya kufundishia watu wenye ulemavu vyoo vya kutumia barabara za kuititia baiskeli.

Mheshimiwa Spika, ushauri, Serikali izingatie mambo haya muhimu kwa shule hizi mpya zinazojengwa, ziwe zinazingatia mazingira rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu na zile za zamani zikarabitii ili ziweze kukidhi haja.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya wanawake na watoto umezidi kuongezeka na Serikali ipo hailishughulikii suala hili ipasavyo, tunaona katika vyombo vya habari mwanaume anampiga mke wake hata kufikia kumkata sikio, wajue wanawatelekeza na watoto na kuachia mzigo wa kuwalea watoto. Mwanamke huyu hata mume akifariki hunyimwa kurithi mali, lakini baadhi ya mila na desturi zetu ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu siyo wanawake wote hasa vijiji ni wenye kuelewa kuna wataalam wa kushughulikia matatizo yao. Serikali itoe matangazo yabandikwe Makanisani, Misikitini, ofisi za Kata ili wanawake hawa wajue mahalli pa kwenda pindi wanapopata manyanyaso.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya vikongwe na walemavu wa ngozi, kutokana na imani za kishirikina kada hii wamekuwa wakiuawa kinyama bila kosa na kuwapelekea watu kutokuishi kwa amani ndani ya nchi yao licha ya haki za binadamu kulipigia kelele tatizo hili la mauaji ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, swali, mpaka sasa hivi na watuhumiwa au wanaofanya dhambi hizi ni wangapi wameshakamatwa na kufunguliwa kesi na kufungwa?

Mheshimiwa Spika, ushauri, ili kukomesha dhambi hii ni vizuri wale wote wanaohusika na mauaji haya haramu, wakatajwa hadharani katika Kata husika na picha zao zibandikwe kila mahali. Hii kwa kiasi fulani itapunguza mauaji haya.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi hotuba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja pamoja na kuwa nitakuwa na mambo machache ambayo naomba Wizara iyaangalie kwa macho mawili. Suala la kwanza, naomba sana Wizara hii iangalie ile mikopo ya akina mama inayopelekwa katika Halmashauri zetu, fedha hizi zinarejeshwa vizuri sana na akina mama na vijana lakini fungu hili ni dogo sana ni vyema likaongezwa zaidi kwani zinawafikia akina mama wengi vijiji na zinarejeshwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iangalie uwezekano wa kufungua matawi ya Benki ya Wanawake katika kila Mkoa ili kusudio lake liwafikie akina mama wengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Wizara iwaangalie watoto wanaoishi katika mazingira magumu (yatima). Wizara itenye fedha angalau kwa watoto ili kila Halmashauri waweze kuwasomesha kuanzia Kidato cha Kwanza mpaka cha Nne.

Mheshimiwa Spika, namaliza kusema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. LOESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nampongeza Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Sophia Simba, kwa hotuba nzuri kabisa. Pia nimpongeze Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri, bila kuwasahau Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Moja ya malengo walijonayo ni pamoja na kuwashamasisha wananchi kutumia rasilimali walizonazo katika kujiletea maendeleo. Hata hivyo, malengo hayo hayawesi kutimia kwa sababu katika ngazi ya vijiji, Kata hatuna wataalamu wa maendeleo ya jamii hivyo kushindwa kufikia malengo. Katika Wilaya ya Geita, tuna Afisa Maendeleo wa Wilaya ambao ni wachache sana kulingana na ukubwa wa Wilaya, hata hivyo hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba kama kweli tuna nia ya dhati ya kupunguza umaskini wa wananchi wetu, ni vema Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii, pia iajiri wataalamu mpaka ngazi ya Kata ili waweze kuwasaidia wananchi katika kujiletea maendeleo. Kina mama na vijana wanaanzisha vikundi nya maendeleo lakini kwa kukosa maelekezo na ushauri wa kitaalamu, vikundi hivi vinashindwa kuendelea, mfano mzuri ni katika Jimbo la Busanda, kuna vikundi vingi tumeanzisha vinashindwa kuendelea kwa kukosa maarifa. Naomba Serikali iliangularie hili la kuongeza bajeti ya Wizara pia kuajiri wataalamu ngazi ya Kata kwa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itujengee Chuo cha Ufundu/Chuo cha Maendeleo ya Jamii, Wilaya ya Geita na Mkoa Mpya wa Geita hauna Chuo cha Ufundu. Kupitia Chuo cha Ufundu watoto na wananchi watapata ujuzi wa namna ya kufanya shughuli zao na hii itaongeza ajira kwa wananchi wetu hawa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara inasimamia masuala ya wanawake na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ambayo ina upungufu mkubwa sana unaokandamiza mwanamke hasa sheria za urithi zenyen kufuata upande wa ukoo wa kiume. Sheria hizi zimesababisha matatizo makubwa sana kwa wanawake walio wengi. Wanawake wananyanyasika sana hasa wakati wa kufuatilia mirathi pale wanaume wanapofariki, ni wakati sasa wa kuleta mabadiliko ya sheria hizi kandamizi Bungeni ili zifanyiwe mabadiliko. Naomba Serikali kuitia Wizara hii iandae Muswada wa mabadiliko ya sheria hizi kandamizi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha mambo mawili niliyoyazungumzia hapo juu nikiamini kuwa Serikali inakwenda kuyafanya kazi kwa ajili ya ustawi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2012/2013 kama ilivowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi wa hali ya juu kabisa. Pia nampongeza Naibu Waziri kwa imani, uvumilivu na moyo wa kujitolea sana kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kama sote tunavyofahama, Wizara hii ni roho ya ustawi wa jamii yetu, hivyo majukumu yake ni mazito na yanahitaji umakini mkubwa sana katika utekelezaji. Ni kheri tuwaunge mkono na kusaidiana nao katika kuboresha na kuondoa upungufu unaojitokeza kila siku, maana sidhani kuwa ni busara kukosoa tu bila kutoa suluhisho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hotuba hii kujumuisha mengi ambapo naomba nichangie machache kufuatana na hali halisi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sana katika ajira za watoto ambao wamekuwa wakitumikishwa katika shughuli mbalimbali ambazo hazilingani na umri wao ama utu wa mwanadamu. Imekuwa ni jambo la kawaida sana kwa watoto kudhallishwa na kushirikishwa na vitendo visivyoendana na maadili ya nchi na utamaduni wetu kama ngono na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, haki za watoto zinazokiukwa ni pamoja na kutopata nafasi ya kucheza, kusoma na kushiriki masuala yanayowahu haswa kwa Serikali kutotilia mkazo Mabaraza ya Watoto. Naishauri Serikali ifanye jitihada za makusudi ili kuweka Mabaraza ya Watoto nchini.

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine linahusu lishe, ukiangalia utapiamlo umeongezeka kwa kasi sana na ajabu ambapo wataalamu wametoa angalizo kuwa ufaulu wa watoto uko chini kutokana na lishe pia. Naishauri Serikali sasa iajiri Maafisa Lishe wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuhimiza elimu ya lishe kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la vifo vya akina mama wajawazito litiliwe mkazo kwa kutoa elimu na kuboresha mazingira mazuri kwa kuweka vifaa na mahitaji kwa akina mama. Pia haki za wanawake zisimamiwe ipasavyo kwa maana wanateswa sana bila hatua kali za kisheria hazichukuliwi haraka na ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba Mheshimiwa Waziri asirudi nyuma katika jitihada zake za kuhakikisha tatizo la watoto wa mitaani ambao wamezidi kuzagaa kwa maana litagharimu sana nchi siku za usoni lakini pia linaharibu taswira nzuri ya utendaji wa Serikali yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwa nafasi hii kumpongeza Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanyika Wizarani kwa usimamizi wao.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kukumbusha kwamba, uchumi kwa maana ya maendeleo ya kilimo na sasa sekta isiyo rasmi inahudumiwa na akina mama. Ni kwa sababu hii, naomba Serikali kuondoa kero zifuatazo dhidi ya akina mama ili kuwapa nafuu katika kazi zao na hivyo kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, suala la mikopo Halmashauri zote zinatakiwa kutenga asilimia ishirini ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya mikopo kwa akina mama na vijana. Halmashauri nyingi hazitekelezi agizo hili, hata zile ambazo zinatekeleza mikopo hiyo inatolewa kwa upendeleo na marejesho yote kusuasua. Hali hii inawafanya akina mama wengi kushindwa kupata mikopo hii na ni athari kubwa kwa maendeleo yao. Naiomba Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI kuangalia uwezekano wa kupata ufumbuzi wa kero hii.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake ni muhimu sana kwa maendeleo ya akina mama. Fedha zinazotengwa kila mara kwa ajili ya kusogea Mikoani ni ndogo sana. Utaratibu ufanyakie wa makusudi kutafuta majengo Mikoani au kwa kuanzia katika Kanda ili manufaa ya benki hii yaonekane.

Mheshimiwa Spika, suala la mimba mashulen. Tatizo hili karibu litaonekana kuwa jambo la kawaida licha ya kwamba ipo tabia ya baadhi ya wanaume kuona fahari kutembea na watoto. Sheria ziangaliwe ili kutoa adhabu za kufaa kwa wale wote wanaowapa mimba watoto.

Mheshimiwa Spika, vilevile wimbi la picha, michezo na matumizi yasiyofaa ya mtandao yanawafanya vijana na watoto kuhamasika kufanya ngono toto. Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama Wizara ya Habari iangalie namna ya *ku-regulate* matumizi ya mitandao, picha na magazeti yanayohamasisha ngono kwa watoto na vijana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahabusu watoto, katika baadhi ya magereza zetu, watoto wanaotuhumiwa kwa makosa mbalimbali huchanganya na mahabusu au wafungwa watu wazima. Tatizo hili limepigwa kelele sana katika Wizara ya Sheria hata hivyo ni vema Wizara ikaangalia utaratibu wa kunusuru watoto hawa kwa kuwa ndani ya mahabusu hizo hawajengwi na hutoka huko wakiwa wamedhalilishwa na kuiga matendo maovu na hivyo kurudi wameharibika zaidi.

Mheshimiwa Spika, watoto wa mitaani, ongezeko la akina ombaomba, mateso katika familia na maafa yameongeza watoto wengi sana wa mitaani. Nashauri uangaliwe utaratibu wa kuwarudisha hawa watoto katika familia zao na au kuwawekea utaratibu wa malezi na hata elimu ili kupunguza uwezekano wa kuandaa wahalifu wajao.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha na nawatakia kazi njema.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Spika, napongeza juhud zote za Wizara hii za kuandaa, kueneza na kutayarisha mikakati na mifumo ya kutekelezwa katika kuchochea maendeleo ya jamii. Kwa kutambua bajeti ni mbegu ya kuotesha ufahamu, hamasa na kuwezesha jamii kumiliki haki sawa, hususan kwa jamii kumiliki haki sawa husasan kwa jamii ya mwanamke; na kwa kuzingatia kwamba Tanzania pana *NGO* nyingi za kuwatibu na kushughulikia haki za wanawake na watoto; na kwa kutambua pana Itifaki ambazo Serikali imeridhia kuhusu haki na utawala kwa mazingira ya mwanamke. Kwa hiyo sasa, naomba kufahamu ni juhudu zipi zitatekelezwa na Serikali, Wizara leo itamke kwamba Wanasheria wa Halmashauri wa kila Wilaya wanaagizwa kushirikiana na Wilaya zote kutoa misaada ya kisheria kwa wajane, kesi za mirathi na kwa mahitaji ya ushauri wa kulinda haki zao wanawake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa pana *NGO* za kisheria katika miji, je, sasa Wizara inaweza kutoa agizo la sifa ya *NGO* kutumikia vijiji itathaminisha *NGO* kuwa ni kwa maslahi mapana ya jamii. Kwa kuwa vijijini ndipo penye giza la haki sawa, je, atateua *NGO* za wanasheria zije Maswa

kutathmini maovu ya uonevu na atafika lini Maswa kuwasha Mwenge wa hamasa ya ukombozi wa mwanamke?

Mheshimiwa Spika, naomba tamko na majibu ya maandishi, ahsante.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Sophia Simba (Mb), Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa pamoja na changamoto zinazoikumba Wizara hii lakini bado inaendelea kutengewa pesa kidogo sana, hii inathibitisha kuwa unyanyapaa wa wanawake bado upo.

Mheshimiwa Spika, sheria zilizopitwa na wakati, wanawake wananyanyasika sana na sheria zilizopitwa na wakati, kuna sheria za mirathi, kumiliki ardhi, sheria za ndoa na kadhalika. Toka tumefika hapa Bungeni, malalamiko mengi sana ya Wabunge hasa sisi wanawake tumekuwa tukilalamikia hizi sheria ambazo bado zinawatesa wanawake. Je, mpaka sasa hivi nilitaka kujua Wizara hii imechukua hatua gani au ina mikakati gani kuhakikisha sheria hizi zinarekebishwa ili kuweza kumsaidia huyu mwanamke anayelia siku zote?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inawasaidiaje wale wanawake amba omba hivi karibuni tumeona wamepigwa, wameteswa mpaka wamepoteza maisha na kuna mwanamke mwingine amepokonywa mtoto wake na raia wa Kiasia na kadhalika kwa kuwa vitendo hivi vinatudhalilisha wakati sheria zipo.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wana ombaomba mitaani, mpaka leo sijajua dhamana ya hawa watoto pia wako mikononi mwa Wizara gani? inaumiza sana kuona hawa watoto wanaanza tabia mbaya ya ombaomba kuanzia umri mdogo sana na kuna baadhi ya wazazi/walezi wanawatumia watoto hawa kama chombo cha kutafuta pesa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inaweka mkakati gani kuhakikisha kuwa tabia hii inakomeshwa ili kumpatia mtoto huyu haki yake ya msingi hata ya kusoma shule. Ni kweli hakuna sheria inayombana huyu mzazi/mlezi anayemtumia mtoto huyu? Mkoo wa Dar es Salaam unaongoza ukipita barabara zote za Mjini wazazi wamekaa kando ya barabara wakiwasubiri watoto waombe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jela/Mahakama za watoto, napenda kujua Wizara hii inawatetea vipi hawa watoto wanaofungwa katika jela za watu wazima na wale akina mama waliofungwa na watoto wadogo au wanajifungulia jela kuhakikisha haki ya mtoto inalindwa? Je, hakuna sheria yoyote inayomlinda?

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujua hawa Maafisa Ustawi wa Jamii hivi shughuli zao ni nini na wanafuatiliwa na nani kuratibu kazi zao? Ni wa nini mambo mengi sana wanayotakiwa kuyafuatilia hawaafuatili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya Ustawi wa Jamii, kwa kweli vyuo hivi vingi vinasikitisha kwa uchakavu wa majengo na miundombinu pia kutotengewa pesa za kutosha kwa ajili ya kujiedhesha, ni kwa nini visitafutiwe ubia ili vifanye kazi zao kwa ufanisi? Chuo cha Lungembe hakuna umeme na kuna mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, suala la Benki ya Wanawake wa Tanzania, benki hii inatutia uchungu sisi wanawake tulio nje ya Mkoo wa Dar es Salaam. Benki hii ni ya wanawake wa Mkoo wa Dar es salaam, tumekuwa tukiulizwa bila majibu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni mwaka gani benki hii itakuwa inaanza kutoa huduma kwa wanawake wa Mkoo wa Iringa na atueleze mkakati gani upo kabla ya kuanza kutoa huduma hata wangeanzisha *mobile bank* tu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja. Pili nashauri kutekeleza mipango ya Wizara kwa kushirikiana kwa karibu na Wizara zingine hasa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, masuala ya *awareness raising* ambapo Wizara inatakiwa kuyafanya kwa makini, nashauri yafanyike kwa mpango wa kuwa na mkakati mahsus wa kuhakikisha kuwa '*communication strategy*' hasa kuhusu usawa wa kijinsia ili ueleweke vizuri kwa ujumla wake. Lakini pia kuhakikisha suala la usawa wa jinsia linabebwa sawasawa kwa kuwa *mainstreamed* ndani ya Wizara zote na Halmashauri zote nchini.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia vyama visivyo vya Kiserikali kwa maana ya *NGO's* zeny kusajili chini ya Wizara ni muhimu kukawa na *database* itakayowezesha kutambua kwa harakaharaka *status* ya kila moja inafanya nini, iko wapi na *objectives* zinazofanyika kama ni zile zilizombwa wakati wa usajili.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa na mpango wa Wizara kupata ripoti ya utendaji wa asasi zisizo za kiserikali katika kutekeleza waliyoyapanga. Taarifa hizi zikiwepo zitasaidia kupata picha kamili wapi kuna "*gap*" pia uandikishwaji wa asasi zingine ziwe zinalenga kujazia mapengo yaliyopo na kuleta tija katika jamii.

Mheshimiwa Spika, napongeza hatua mbalimbali hasa ya kuendeleza Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na hata huo mkakati wa kuwapa nafasi vijana kujidendeza. Nashauri pia katika hili Afisa Habari na Mawasiliano wa Wizara afanye kazi kwa karibu na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia kuwa na msukumo wa makusudi kuhimiza umuhimu wa michezo kwa vijana, wasichana na watoto kwa ujumla. Nashauri pia nafasi ya Afisa Habari, Elimu na Mawasiliano ndani ya Wizara awe katika nafasi ya *Management* awe na sauti ya kuisemea Wizara wakati wowote ikishirikiana na Wizara ya Habari.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazofanya na kwa hotuba nzuri ya bajeti ya mwaka 2012/2013. Napenda pia kutoa ushauri, mapendekezo na maombi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuendelea kuboresha Chuo cha Maendeleo Kiwanda (Muheza). Bado nashauri Wizara iendeleze ukarabati wa chuo na madarasa, mabweni na nyumba chache za Walimu zilizopo. Kutokana na kuwepo kwa Chuo hiki Wilaya ya Muheza itachelewa sana kuingizwa katika mpango wa Taifa wa ujenzi wa vyuo vya VETA katika Wilaya zote nchini. Hivyo tunashauri kuwepo na ongezeko la madarasa, mabweni na fani mbalimbali zaidi ili kuboresha chuo, pia kuongeza mfumo wa teknolojia ikiwemo ya ukaushaji wa matunda na mfumo wa viwanda vidogo vya kukamua miwa.

Mheshimiwa Spika, pili, msaada kwa Kituo cha Wagonjwa wa Ukoma -Ngomeni (Muheza). Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inalo jukumu la malezi ya kituo hicho kwa maendeleo ya ustawi wa jamii. Naomba kushauri Wizara isaidie katika maeneo yafuatayo kuboresha kituo hicho:-

(i) Kusaidia kusomesha watoto wa familia za wagonjwa hao kutoka elimu ya msingi hadi sekondari.

(ii) Kuboresha makazi ya kituo hicho.

(iii) Kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Muheza katika azma ya kufikisha maji safi na salama katika kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, tatu, kujenga mfumo na uwezo wa kusaidia watoto walemvu wa ngozi. Kwa kuwa walemvu wa ngozi ni sehemu ya jamii na inahitaji kuendelezwa, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto lazima ibebe jukumu la maendeleo ya walemvu kwa kuanza utekelezaji wa jukumu hilo Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, walemvu wa ngozi wanapata shida sana kusoma katika shule za jumla na katika mazingira ya jua kali na unyanyapaa. Hali hii inachangia kudhoofisha maendeleo yao na hivyo kuhitaji msaada na mpango maalumu wa kuwawezesha. Wizara iandae mpango maalumu kwao na uwepo katika bajeti zizazo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa utendaji wao kwenye Wizara hii nyeti. Pamoja na pongezi hizi, naomba Serikali injibju hoja zifuatazo:-

(i) Serikali imejipanga vipi kushughulikia matatizo ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu?

(ii) Je, Serikali imejipanga vipi katika kutoa elimu yenyenye manufaa kwa umma kwa lengo la kujua watoto wanaoishi katika mazingira magumu ni sehemu ya Watananzania wote?

(iii) Wilaya ya Mufindi ina watoto wanaoishi katika mazingira magumu 48,000 (elfu arobaini na nane) ambayo ndiyo idadi kubwa katika nchi yetu na sababu kubwa ni maambukizo ya UKIMWI yanayotokana na maisha magumu wanayoishi akina mama na kulazimika kuingia katika matendo ambayo ni kinyume na utu wa Mtanzania. Napenda kujua Serikali imepanga vipi kuwasaidia hao akina mama na hawa watoto 48,000 (elfu arobaini na nane) wanaoishi katika mazingira magumu?

(iv) Mwaka jana katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii, nilichangia kwa kuishauri Serikali kukiendezea Chuo cha Rungembba kwa lengo la kuwa Chuo Kikuu na sisi wananchi wa Mufindi na Kijiji cha Rungembba kwa kujua umuhimu wa elimu tumeamua kukipatia eneo walilokuwa wanahitaji kwa upanuzi wa chuo hiki. Napenda kusikia kutoka Serikalini, ni lini watabadilisha/watapandisha hadhi chuo kile kianze kutoa shahada badala ya stashahada na kiwe chuo cha kwanza kutoa elimu ya ustawi wa jamii hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja, nategemea Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri watanipatia majibu yanayostahiki.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watoto wa mitaani kila siku wanazidi kuongezeka na sio kupungua. Hii inatokana na kufariki kwa wazee na kuacha watoto yatima. Naiomba Wizara inapofanya zoezi la kukamata watoto hawa na kuwapeleka katika vituo vya kulelea watoto hao, wawahoji kwa wale waliofiliwa na mzee au wazee wao wafuatiliwe wale wazee wallobakia kama baba mdogo au familia iliyopo ya ukoo husika. Pindi ikipatikana, familia ile wapewe dhamana ya kuwalea watoto wale, hasa ukizingatia wale watoto wameachwa na jamaa zao wa damu. Kule Zanzibar hakuna watoto wa mitaani kwa sababu bado watu wana mapenzi na watoto walioachwa na wazee wao (waliofariki). Hii itapunguzia mzigo mkubwa Serikali ya kujenga nyumba nydingi za ulezi wa yatima.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri na *team* yake nzima iandae mkakati wa kuwakamata watoto wanaozurura na baadaye wahojiwe ni sababu gani inayofanya wazurure na baadaye atafutiwe familia yake ikabidhiwe kwa masharti maalum ili mzigo mkubwa Serikalini upungue. Kama itatokea familia husika itawalea basi bora wasaidiwe elimu tu sio ulezi wa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, napenda nami kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ajira kwa watoto, watoto wamekosa haki yao ya kwenda shule na kupata elimu ambayo kimsingi ni haki ya kila binadamu na inaanza katika umri mdogo kulingana na uelewa wa mtoto. Katika miji mikubwa hapa nchini mfano Arusha na kadhalika kumekuwa na watoto wengi wanaozagaa mitaani badala ya kwenda shule na wamekuwa wakifanya kazi za hatari sana kama za kuosha magari au kusafisha vioo vya magari katika barabara kuu za miji mikubwa.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zimekuwa zikipita magari mengi sana yanayoenda kwa kasi sana, kwa kweli hii ni hatari sana kwa maisha yao. Kwa mfano mjini Arusha kuna mtoto alishagongwa wakati anajaribu kuvuka barabara kuelekea upande mwininge kufuata kusafisha kioo cha gari ingine kwa bahati nzuri tu mtoto yule alipona, je, ni wangapi ambao wanakumbana na zahama hizo za ajali? Wangapi wamepoteza haki zao za kuishi kwa sababu tu wanakosa haki ya kupelekwa shule na kwamba muda huo wanaoosha magari wangekuwa shulen i wakipata elimu.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika maeneo ya vijijini, watoto wamekuwa wakikosa elimu pia kwa ajili ya kufanyishwa kazi za mikono kama kubeba matofali, kubeba mawe, kuchonga/kubonda mawe hadi kupata kokoto kwa ajili ya ujenzi. Kwa kweli hili ni tatizo kubwa sana na mfano katika eneo la Oldonyo Sambu ambako kumekuwa kukifanyika shughuli za uchomaji matofali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Wizara, naomba kuwepo na ufuatiliaji wa kina ambao utakuwa unaanza katika ngazi ya chini kabisa ya uongozi ili Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Elimu waweze kushirikiana kutambua watoto walifokisha umri wa kwenda shule lakini *either* wazazi au kama kuna tatizo lolote linalosababisha watoto hao kutokwenda shule kwa wakati. Kwa sababu nchi yetu inafuata sheria na sheria inasema ni haki ya mtoto kupata elimu bora basi na ye yote atakayebainika kukwamisha haki hiyo, achukuliwe hatua za kisheria na hapo haki itakuwa imetendeka.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, hakuna Taifa ambalo linarejea nyuma kiiadi ya watu endapo Taifa hilo halijakumbwa na majanga ya mauaji ya kimbari ambayo yatakuwa yanapoteza idadi kubwa ya wananchi wake ikiwemo jamii ya watu wazima na watoto. Mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza kwa Wizara hii mwaka hadi mwaka ni upungufu ambao haulengi kuikwamua Wizara hii kuifikisha katika malengo ya kukwamua mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, kigezo cha kauli yangu hii ni kwamba, kwa kuwa idadi ya watoto imeongezeka siku hadi siku, huwezi kupunguza (bajeti) ya Wizara hii kwa kiwango ambacho kinapunguzwa kila mwaka. Lakini vile vile huwezi kuondoa umaskini usiendelee kuongezeka kutokana na upungufu wa upunguzaji wa bajeti jambo ambalo limekuwa endelevu kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa mtoto unategemea mapenzi na malezi yatokanayo na mama mzazi na mapenzi na malezi yatokanayo na mama mzazi hayawesi kupatikana kama kiwiliwili cha mama hakujengeka kwa kupatikana virutubisho ambavyo vitawenza kujenga mwili wa mama na hatimaye mtoto apate virutubisho hivyo kutoka kwa mama hatimaye aweze kupata afya nzuri na ili mtoto awe na uwezo wa kushiriki vizuri katika masomo yake ya nasari.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni vyema ikajenga mazingira mazuri ili kuwawezesha watoto wa mitaani kuweza kuwapatia maeneo maalumu ya kuishi yenye majengo na pia kugharamiwa na Serikali kwa kuwawezesha kuimarisha, lakini pia kuwapatia fursa ya kupata elimu. Mheshimiwa Waziri ana haki na wajibu kama mama mzazi ya kuwahurumia akina mama wenzake ambao wanaishi hovyo, wanazaa hovyo na kwa sababu hawana namna ya kuwalea na kuwasomesha watoto hao hatimaye kuishia kubakia kuwa watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, ikiwa watoto wanaishi mitaani bila ya kuwa na maisha ambayo yataweza kuwalinda, kuwakuza na kuwasomesha watoto hao watakapoharibika katika maisha hayo alaumiwe nani? Je, Serikali haioni kwamba inachangia ongezeko la maradhi ya UKIMWI ukitilia maanani kwamba haijaweka sheria ya kuwadhibiti watoto wa mitaani lakini hata wale wanaosababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani?

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Miongoni mwa ukatili unaotendeka dhidi ya wanawake na watoto ni pamoja na kuvunjika ndoa kiholela na kumwachia mama watoto bila ya baba kutoa mchango katika kuwakuza na kuwasomesha watoto. Jambo hili pia humfanya mama asiwe na udhibiti wa malezi juu ya watoto alioachiwa na baba na hatimaye kuwachochaea watoto hao katika kurubunika na hatimaye kuingia katika janga la maambukizi la maradhi ya zinaa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii haikuundwa sasa hivi ni Wizara ya zamani hivyo itueleze kuna kiasi gani cha elimu kilichotolewa katika maendeleo ya jamii ili kujenga jamii ya Watanzania wasilingie katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, ni maendeleo gani ambayo yatapatikana ikiwa Wizara hii imenyamaza kimya juu ya upungufu mkubwa unaoendelea kupunguzwa mwaka hadi mwaka? Ni kwa kiasi gani Wizara hii imechukua hatua ya kuokoa mauaji ya vikongwe pamoja na walemavu wa ngozi ambao hawana hatia? Ni elimu gani imetolewa kuondoa fikra na mawazo potofu ambayo yanajengwa na baadhi ya watu wanaojifanya kuwa ni waganga wa kienyeji huwasingizia baadhi ya Watanzania wenzao kuwa ni wachawi kwa sababu ya macho yao na wengine kufikiria kwamba eti watakapopata viungo vya walemavu wa ngozi watapata utajiri? Kwa nini Serikali haiwachukilii hatua waovu wanaojiita waganga ambao husababisha mauaji ya Watanzania wengine?

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu katika siku tukufu ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Namwomba Mwenyezi Mungu akubali funga ya wale wote watakaofunga kwa ajili yake, namwomba aniwezeshe kuchangia hoja hii kwa utulivu na amani, amina.

Mheshimiwa Spika, naanza mchango wangu kuhusu watoto. Pamoja na juhudu kubwa za Serikali kushughulikia watoto lakini bado watoto wengi wanakosa haki zao za msingi, kama malezi bora, elimu na huduma nyingine muhimu kama afya. Haya yote yanalisababishia Taifa kukosa msingi madhubuti wa maadili. Mfano kina mama wengi hubeba mimba nje ya ndoa na kukusanya watoto wengi kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, watoto hukosa matunzo kwa sababu baba hayupo, ulezi unabaki kwa mama peke yake, hivyo watoto husambaa mitaani na kuwa chokoraa. Kwa kuwa watoto wana haki zao za msingi, mimi nashauri iwepo sheria itakayowalinda wanawake kubebeshwa mimba ovyo na ikitokea kabebeshwa basi mbebeshaji awajibike juu ya malezi ya mtoto kwa lazima.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ukatili juu ya watoto, wapo baadhi ya wazazi ikiwa baba au mama wanafanya ukatili mkubwa juu ya watoto wao wenyewe. Tumeshuhudia baadhi ya wazazi mtoto kaiba au kachukua shilingi 1000 (elfu moja) tu basi anafungwa mikono anachomwa moto, anashindwa hata kula na wengine wanabaki kuwa kilema wa maisha. Ushauri wangu, Serikali ilione hili kwa makini sana kwa kuwalinda watoto.

Mheshimiwa Spika, wizi na biashara haramu ya watoto. Lipo wimbi la wizi na biashara haramu ya watoto ambao huibiwa popote ambapo hupatikana fursa ya kufanya hivyo. Watoto wengine huibiwa hospitali, wengine mitaani, kwenye sherehe na kadhalika. Mmimi nataka kujua je, Serikali imefanya utafiti na kugundua watoto hawa wanapelekwa wapi na hufanywa nini? Naomba nijibiwe na kama imegundua, hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wanaochukuwa mimba shulen, kwa sasa watoto wa kike hubeba mimba shulen. Sasa imekuwa kama jambo la kawaida. Watoto wa kike wanabeba mimba wakiwa shulen. Wanaathirika katika masomo yao na wengine hukatisha moja kwa moja.

Athari hii inampata mtoto wa kike peke yake na mhusika anabaki huru. Mhusika anakimbia sehemu ya tukio na kukimbilia sehemu nyininge basi. Serikali haifanyi juhudhi ya makusudi kumkamata mhusika na kumfikisha Mahakamani. Hivyo yote haya yamekuwa kama jambo la kawaida, kwa hiyo, yanaota mizizi na kuzidi kushamiri.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu sheria kandamizi kwa wanawake. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 13 inatamka bayana kuwa watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria, lakini cha kushangaza sheria hii imekuwa haitekelezwi kwa vitendo na matokeo yake wanawake wamekuwa ni wahanga wakubwa wa ukatili unaofanywa kwao na wanaume hasa kwa kuendelea kutumia sheria mbovu zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria ambazo zimerithiwa toka nchi mbalimbali mfano India na zingine ambazo ziliikuwa zinatumika tangu enzi za mkoloni, mfano wa sheria hizi ni kama *The Judicature and Application of Laws Act, Cap.358 of RE 2002*, Ibara ya 106 inayosema kwamba ugoni wa mke ni sababu kwa talaka na ile ya 157(A) inayosema kwamba kwa kawaida za mila ugoni wa mume haufikiriwi sababu ya kuachana. Kwa nini sheria hii isiwe kwa wote kwamba ugoni kwa mume pia iwe ni sababu tosha ya talaka? Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa sana maambukizi ya Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, pili, katika sheria hizohizo, Ibara ya 167(A), (B) (C) inaeleza fidia au kipimo cha fidia kwa madhara yanayotokana na kipigo kwa mwanamke ambayo hupelekea hata ulemavu wa muda mrefu. Fidia hii inaanzia Tshs.10/= hadi Tshs. 500/=. Jamani hebu fikiria mwanamke kupoteza kiungo chake milele kama jicho au sura maisha, fidia yake ni Tshs. 200/= hadi Tshs. 500/=? Hii ni aibu na huu ni unyanyasaji mkubwa wa kijinsia. Ni lini Serikali italeta Muswada wa kuondoa sheria hizi za kimila ambazo ni mbovu kupindukia na zimepitwa na wakati?

Mheshimiwa Spika, tatu, Sheria za Urithi. Sheria hizo zimekuwa zikimkandamiza mwanamke kwa kiwango kikubwa kwani yeze amekuwa akipewa mgao mdogo kuanzia kwenye familia mpaka hata anapoolewa. Kama kwa bahati mbaya mwanamke atafiwa na mumewe hataruhusiwa kurithi mali yoyote na badala yake urithi utakuwa kwa ndugu wa kiume. Hii sheria haifai kwani mwanamke amekuwa na mchango mkubwa sana katika uzalishaji mali na utunzaji wa familia, hivyo anastahili kurithi mali pindi mumewe anapofariki.

Mheshimiwa Spika, nne, matokeo ya mikutano na mikataba mbalimbali ya Kimataifa kuhusu wanawake. Kumekuwa na mkataba na mikutano mbalimbali ya kuzungumzia masuala yanayohusu haki za wanawake na watoto, unyanyasaji wa kijinsia na namna ya kumkomboa mwanamke kiuchumi, kisiasa na kijamii. Cha kushangaza, wajumbe wa mikutano hii ambaao ni wanawake wa Tanzania kwa mfano, wanaporudi hakuna wanachofanya kuelezea umuhimu wa mikataba na mikutano hii kwa wananchi wote na hususan wanawake wanaowakilisha. Kwa masikitiko makubwa, wananchi wa vijiji ndio kabisa hakuna wanachoelewa na hivyo kuwa waathirika wakubwa wa uhalifu huu, ni kwa nini wanawake viongozi wa Kitanzania wanaokwenda kuhudhuria mikutano hii hawaleti mrejesho (*feedback*) na yale waliyoamua na kujifunza hivyo kuwaunganisha wanawake wote kudai haki zao kwa pamoja?

Mheshimiwa Spika, tano, bajeti finyu ya Wizara. Wizara hii kusema ukweli imetelekezwa na Serikali kwani imekuwa ikitengewa fedha kidogo na hata hizo kidogo hazitolewi zote kwa wakati au hazitolewi kabisa. Sasa kwa bajeti isiyokidhi tutegemee nini katika kumkomboa mwanamke? Maana yake mfumo dume utaendelea kutawala milele. Wizara ipewe fedha za kutosha ili ifanye kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Spika, sita, Mkataba wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake wa mwaka 1979. Tanzania iliridhia mkataba huu mwaka 1985 kwa maana ya kukubali kutekeleza vipengele vya mkataba huo na hivyo kila nchi mwanachama ina jukumu la kutoa taarifa ya utekelezaji kwa Kamati Maalum kuonyesha namna ilivoytekeleza mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, moja ya kipaumbele kwenye mkataba huu ni kile kinachosema kwamba, wanawake wanayo haki sawa na wanaume kutika nyanja za elimu, ajira, huduma ya afya pamoja na kuwezeshwa kiuchumi kwa kuwepo kwa mipango thabiti inayosaidia wasichana kuendelea na shule ikiwa ni pamoja na wale wanaokatiza masomo katikati kutokana na sababu mbalimbali, sababu hizo zinaweza kuwa ni ujauzito au uyatima na kadhalika. Sasa ni kwa nini mpaka sasa hivi mkataba huu hautekelezwi na matokeo yake watoto wengi wa kike hasa wanaopata ujauzito hawaruhusiwi kurudi shule ili kuendelea na masomo?

Mheshimiwa Spika, tatizo liko wapi endapo Serikali itakuwa na mkakati wa makusudi wa kuwaanzishia vituo maalum na walimu ili kuwafundisha watoto hao? Je, kwa kukosa elimu si kweli kwamba mwanamke hatakuwa na nafasi milele ya kushiriki katika '*senior decision making positions*' hapo baadaye? Hii haipielekei mfumo dume kutawala milele? Bila elimu ni kwa vipi tutegemee mwanamke atajikomboa? Ni kwa namna gani Wizara imeipigia kelele Wizara ya Elimu ili kulazimisha kutii mkataba huu amba Tanzania imesaini? Naomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni mtambuka kwa kuwa inasimamia maendeleo ya jamii kwa ujumla. Wanawake na watoto ndio wanaokandamizwa kwa kiwango cha juu kutokana na mila, desturi na kubwa zaidi mfumo dume. Pamoja na umuhimu wa Wizara hii lakini siku zote imeonekana kama Idara na hivyo kuendelea kupata mgao mdogo sana wa bajeti ya Taifa. Unajua kwamba Wizara hii inabidi kuwa kiongozi wa Wizara nyingine katika masuala ya jinsia lakini cha kujuiliza watafanya vipi kwa bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na Maafisa Maendeleo katika Halmashauri zetu lakini hawapati ushirikiano wa kutosha kutoka Idara nyingine mfano katika suala la usafiri hali inayopelekea kuonekana hawapo hivyo lawama kila kona. Ni vyema basi Wabunge kama Madiwani tutizame ni kiasi gani Mabwana/Bibi Maendeleo wanapata nafuu ya kutosha ili kutekeleza kazi zao kwa umahiri/umakini.

Mheshimiwa Spika, vyuo vyetu vya maendeleo viko katika hali mbaya sana. Vyuo hivi kama vitaboreshwa vitasaidia sana vijana wanaomaliza elimu ya sekondari kujunga navyo. Ni vyema Waziri akaeleza ni kwa kiasi gani Wizara imejipanga kuboresha vyuo vyetu ili wanaohitimu waweze kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, wanawake tumeendelea kukandamizwa kutokana na mfumo uliopo na unaoendelea kushamiri hapa nchini na mfumo huu unaendelea kukolezwa na sheria kandamizi zilizopo kama zile za mirathi, mahari na ndoa. Ni lazima sheria hizi zifanyiwe marekebisho ya haraka ili wanawake na watoto wa kike wapate haki zao.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa, tangu ulipoanza mfumo wa vyama vingi wanawake hususan wa upinzani tumekuwa tukiwasihii wanawake wa CCM kubadili jina la umoja wao UWT na kuwa na jina jingine kwani kuendelea kutumia jina hili ni kuwarubuni wanawake hususan wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuendelea na jina hilo kwa kisingizio cha historia kimepitwa na wakati kwani hata TANU pamoja na historia yake haitumiki tena. UWT-Umoja wa Wanawake Tanzania maana yake ni wanawake wote *including* sisi wa upinzani jambo ambalo si kweli, tunataka kujua ni lini UWT watabadil jina hili?

Mheshimiwa Spika, miaka miwili imepita toka BAWATA ashinde shauri lake cha ajabu hatuambiwi muundo wake ukoje na uongozi wake ni kina nani. Tulitegemea BAWATA sasa ingeunganisha wanawake wote nchini ili tuwe na sauti moja ya kutetea agenda za wanawake wote nchini, lakini kwa ubinafsi BAWATA haitanyanyuka. Tunaomba Serikali na wanawake wote tuipiganie ili itukomboe.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi iliyobahatika kuingiza wanawake wengi katika vyombo vya maamuzi huku ikishika nafasi ya tano kwa Afrika na Dunia, lakini pamoja na hilo bado Wabunge/Madiwani wa Viti Maalum tumekuwa na changamoto nyingi zikiwemo uhalali wao na

wanamwakilisha nani? Jambo hili limezua tafrani kubwa huku wengine wakihoji manufaa yao na kwamba ni gharama tu kwa walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, wanashindwa kuelewa kwamba bila mfumo huu wa *quorta* wanawake wangekosa kabisa nafasi za maamuzi hapa nchini. Ni vema basi wakati tunaelekea katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba, suala hili lipewe kipaumbele. Ni mategemeo yangu Wizara hii itaratibu utaratibu huu kupitia ulingo na *TWPG* ili tuweze kupata nafasi ambazo zinaeleweka.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, niruhusu nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri ndani ya ukumbi wetu. Pia nawapongeza kwa kazi zao katika kulihudumia Taifa letu. Hata hivyo ninayo machache ya kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la uhaba wa Maafisa Maendeleo ya Jamii. Illi maendeleo halisi yawafikie walengwa, ni muhimu Maafisa Maendeleo ya Jamii waende na waajiriwe katika ngazi ya vijiji na Kata kwani ndiko wananchi wetu wahitaji waliko. Nchi yetu imefanikiwa kuelimisha Maafisa Maendeleo ya Jamii wa kutosha na wengi wao hawana ajira, naomba waajiriwe ili wakatoe michango yao katika vijiji vyetu kama walivyofanya kwa Maafisa Kilimo na Mifugo walioajiriwa katika Vijiji.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la Benki ya Wanawake, naipongeza sana Serikali kwa kuanzisha Benki ya Wanawake na katika hili naomba nitoe pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri Sophia Simba kwa juhudhi zake binafsi kuhakikisha Benki ya Wanawake inakuwepo. Pamoja na pongezi hizi bado sijaridhika kuona Benki hii iko Dar es Salaam peke yake. Nashauri matawi ya Benki hii yafunguliwe ngazi za Wilaya na baadaye iende kwa kila Kata kwani wanawake walengwa wako Wilayani na vijijini. Ni kwa kufanya hivyo tu Benki hii itakuwa imewahudumia wanawake.

Mheshimiwa Spika, hali ya mikopo kwa wanawake. Mfuko wa kukopesha wanawake ngazi ya Halmashauri haujafanikiwa hata kidogo kumkomboa mwanamke kwani fedha zinazotengwa ni kidogo sana hivyo kutoleta '*impact*' kwa yule anayekopa. Pia wanawake wengi fedha hizi hawazijui na hivyo haziwafikii walio wengi, ni vizuri Serikali itafute njia mpya ya kuboresha mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wa mitaani, janga la watoto wa mitaani linazidi kulisumbua Taifa letu. Miji ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Arusha na kadhalika inaendelea kushuhudia wimbi la watoto wa mitaani. Wengine wanatumiwa na wazazi wao kwa ajili ya kuomba fedha na kisha kuwapelekea wazazi fedha hizo. Ni mkakati gani wa makusudi ambao Serikali imejipanga kukomesha hali hii moja kwa moja?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ndoa za jinsia moja, Taifa letu limekuwa likihuishwa na vitendo vya ngono za jinsia moja kwa maana ya mwanaume kuoa mwanaume mwenzake au mwanamke kumuo a mwanamke mwanzake au mwanamke kumuo a mwanamke mwenzake. Hali hii ni kinyume na mila na desturi za Mtanzania. Pamoja na kwamba nchi haina dini lakini wakiwemo Waislamu na Wakristo, Misahafu yote miwili kwa maana ya Biblia na Qoran Tukufu zinapinga vitendo vya ndoa za jinsia moja. Ni ombi langu kuwa Serikali isiruhusu vitu kama hivi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukatili dhidi ya wanawake, vitendo vya ukatili kwa wanawake bado vinaendelea, wanawake wanapigwa ovyoovyo na kuwadhalilisha mama zao. Wanawake wengi kwa sasa hawawezi kucheka mbele ya watu kwa sababu hawana meno kinywani ni mapengo tu. Kuna baadhi ya makabila bado yanaendeleza ukatili wa kuwapiga wake zao kwa imani kuwa usipompiga mkewe sio upendo. Hii siyo sawa, watani zangu Wakurya wa Mkoa wa Mara ni mfano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja, mchango wangu utakuwa katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mauaji ya Albino. Binafsi bado sijaridhika namna matatizo haya yanavyokabiliwa na Serikali kwa kuwa ni vitendo vibaya na vya kikatili. Hatujawahi shuhudia nchi itunge sheria maalum kulikabili suala hili ili adhabu iwe kali na itolewe mapema kwa wahusika. Suala la walemavu wote nchini hata kama si wamesaidiwa na Serikali yao hata kama si kwa asilimia mia lakini watambuliwe na wasaidiwe ili kupunguza unyanyapaa unaowapata jamaa zetu hawa, uchumi wetu unaweza kubeba tu, hili si jambo kubwa sana, kwa ajili ya Albino na walemavu wengine.

Mheshimiwa Spika, suala la makambi ya wazee, tulitembelea kambi ya wazee ya Sukamahela, wanaishi kwa shida, hawajasaidiwa inavyotakiwa. Naomba mkazo na msaada zaidi ufanyike kuwafikisha katika hali iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa utoaji elimu nchini, sasa inaonekana wazi jamii ya Kitanzania si muda mrefu itagawanyika kwa sababu maeneo ya kutolea elimu *primary* na hasa sekondari wenye uwezo wanapata ilio bora.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Mchango wangu kipekee nauelekeza katika maendeleo ya chuo chetu cha Mabughai kilichoko Lushoto (Chuo cha Maendeleo ya Wananchi).

Mheshimiwa Spika, chuo hiki ni muhimu sana kwa Wilaya ya Lushoto. Naomba Wizara iendelee na juhudhi za kuendeleza chuo hiki, pia napongeza juhudhi za Wizara kufufua chuo hiki. Naomba mafunzo ya ufundi katika vyuo hivi vijielekeze kwenye mahitaji ya kila eneo (*local need*)

Mheshimiwa Spika, kwa hilo moja, naomba kuwasilisha na litendewe kazi. Naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenyewe mikakati mizuri ya kuendeleza jamii ya Watanzania ingawa fedha zilizotengwa ni ndogo sana ukillinganisha na majukumu mengi mazito ya Wizara. Vilevile naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii, inaonyesha Kamati hii chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati hii ipo makini sana na inayo nia thabiti ya kuisaidia Wizara hii ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Ninawapongeza sana, nami naanza kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza na athari ya bajeti ndogo. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa zamani Idara iliyokuwa inafanya kazi karibu sana na wananchi ni Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Idara ilikuwa inasaidia sana kuwaelimisha wananchi namna bora ya kujiletea maendeleo yao wenyewe, hivyo kupunguza bajeti hii kwa kiwango kikubwa ni kutokuwa na mpango thabiti wa kuikomboa jamii yaani wanawake, watoto na jamii kwa ujumla. Hivyo ninaiomba Serikali itafakari upya namna ya kuongeza bajeti, nasubiri majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pili ni suala la ajira kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Kata. Kuna umbali mkubwa sana kati ya jamii na Maafisa Maendeleo ya Jamii, Wilaya ingawa Serikali sasa hivi inaaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata, bado kuna upungufu mkubwa wa Maafisa hawa wa Maendeleo ya Jamii wa Kata. Napenda kujua kuitilia bajeti hii, Serikali imejipanga vipi kuajiri Maafisa wa Kata kwa nchi nzima ili kuwa na daraja la jamii na Wilaya ili kutoa elimu mbalimbali za kuwaletea maendeleo. Nasubiri maelezo ya Serikali wakati wa kujibu hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya kupewa Idara mbili kwenye Halmashauri ili kuzisimamia. Kwenye Halmashauri nyangi Maafisa wa Maendeleo ya Jamii ni waratibu pia wa masuala ya Ukimwi wa Halmashauri, utaratibu huu sio mzuri kabisa ukiwabebesha watendaji majukumu mazito ya Idara mbili hali inayowafanya washindwe kufanya kazi yao ipasavyo. Namwomba Waziri aishauri Serikali kuajiri waratibu wa masuala ya Ukimwi wa Wilaya ili kuwapunguzia majukumu Maafisa Maendeleo ya Jamii waweze kutekeleza majukumu vema. Nitashukuru kusikia kauli ya Serikali itakayosaidia hata masuala ya Ukimwi kusimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mfuko wa Wanawake wa Halmashauri, ninaendelea kuipongeza Serikali kwa jinsi ilivyoona umuhimu wa mfuko wa wanawake kwenye Halmashauri, mfuko ambao unasaidia sana kuwakopesha wanawake ambao wameunganisha nguvu zao kuendesha miradi ya kuondokana na umaskini. Mfuko huu unaochangiwa na Halmashauri asilimia 10 na Wizara ya Maendeleo ya Jamii huchangia kiwango kidogo cha fedha.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa kuna tatizo kubwa sana, Halmashauri nyangi hazitengi hizi fedha asilimia kumi, naomba sana Serikali itoe kauli ya Serikali ili Wakurugenzi waweze kutekeleza wajibu wao. Vilevile ninaishauri Serikali kuongeza kiasi cha kuchangia kwenye mfuko huu wa wanawake ili mfuko uweze kusaidia wanawake wengi zaidi. Napenda njue Serikali inachangia kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii (*FDC*). Napenda nitumie nafasi hii kukipongeza Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Singida kwa juhudi zake kubwa za kujitafutia fedha za kuendesha chuo kwani Serikali inatoa fedha ndogo sana. Chuo kina mazingira mazuri na miradi mingi ya kuingiza pato la chuo. Naomba Serikali iwapongeze pamoja na kuwatia moyo kwa kuwaongeza fedha za kuendesha chuo. Vilevile naomba mpango madhubuti wa kuitengetea vyuo hivi fedha za kujidesha kikiwamo Chuo cha Maendeleo ya Wananchi cha Msingi. Naomba maelezo ya kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto wa mazingira magumu. Napenda kuiomba Serikali kulitazama suala la watoto wa mazingira magumu kwa kufanya sensa upya na kuangalia namna ya kuwashudumia ikiwemo kuweka utaratibu wa kuwashirikisha wazazi wanaokwepa wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Familia, napenda kuunga mkono mpango wa Serikali kuanzisha Mahakama ya Familia ili kupunguza unyanyasaji wa akina mama kwenye ndoa zao. Vilevile bado sheria za kuwagandamiza wanawake na watoto nazo zifanyiwe haraka kuletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, mwisho, namalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja nikitegemea zitafanyiwa kazi.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayofanya pamoja na kupangiwa bajeti ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara isaidie kutatua kero za miundombinu ya majengo ya Vyuo vya Maendeleo ya jamii vilivypo Jimboni Sengerema ambavyo ni *Sengerema FDC, Karumo FDC* na Chuo cha *VETA* cha Nyatukara Mjini Sengerema. Aidha Vyuo hivi (Sengerema na Karumo) vina majengo mengi yaliyochakaa hivyo kuhitaji maboresho. Aidha, ninaomba Wizara itoe vifaa ikiwemo samani ili kuviwezesha vyuo hivi kutoa huduma kwa kiwango kinachotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami nitoe mchango wangu katika bajeti ya Wizara hii muhimu kwa Ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nzungumzie suala la ucheleweshwaji wa kesi Mahakamani. Kesi za familia zinashika nafasi ya tatu kwa wingi wa kesi katika Mahakama zetu, kesi za Ardhi ndio

zinazoongoza zikifluatiwa na kesi za ajira. Kesi za ardhi kwa kupewa umuhimu wake, Serikali imeanzisha Mahakama za Ardhi na vivyohivyo kwa kesi za ajira kwa kupewa Mahakama ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kuwa kesi za familia ambazo ndizo za tatu kwa uwingi Mahakamani, Serikali hadi leo haijaanzisha Mahakama ya Familia ili kuharakisha kesi za familia zisichukue muda mrefu Mahakamani. Mathalani mtu anapofungua kesi ya madai ya matunzo ya watoto au mirathi na kesi hiyo ikachukua miaka miwili au mitatu, hivi hao watoto wamekuwa wanaishi vipi wakati kesi hiyo inasubiri maamuzi ya Mahakama kwa muda mrefu hivyo? Ni wakati muafaka sasa Serikali ikaanzisha Mahakama za Familia ili kuharakisha kesi za kifamilia na hivyo kutoa haki kwa wakati kwa watoto, wanawake na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie pia sheria kandamizi dhidi ya wanawake. Tanzania iliridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake mwaka 1979 na Itifaki ya Nyongeza ya Kuzuia na Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto mwaka 1998. Nchi yetu ilikubali mkataba huu na kuusaini mwezi Julai 1980 na kuridhia mwaka 1985. Cha kushangaza Mheshimiwa Spika ni kwamba mpaka leo hii sheria kandamizi dhidi ya wanawake bado zipo na zinatumika. Nitaje kwa mfano Sheria za JALA, Jedwali la Kwanza, sheria zinahusu hali ya watu.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kuwa sheria zetu na adhabu zake ni kandamizi sana na zimepitwa na wakati. Kifungu cha sheria hii cha 167 kinaleza fidia kwa kufuata ubaya wa madhara, mapigano, michapo, kuvunjika kidole, jino, jeraha dogo ambalo limepona. Fidia yake isizidi Tsh. 100/= na isipungue Tshs. 10/=, hivi Mheshimiwa Spika Tshs. 10/= na Tshs. 100/= ni nini katika uchumi wetu na kumfidia mwanamke aliyeumizwa? Serikali iharakishe kuleta Bungeni Muswada wa kuzifuta sheria hizi kandamizi dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja ilioletwa mbele yetu. Baada ya kuunga mkono hoja, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna usemi usiopingika kwamba ukimuelimisha mwanamke ni kulelimisha Taifa kwa maana nydingine ukimwezesha mwanamke analiwezesha Taifa kwa maana kwamba wanawake wamekuwa wakijihuisha kwa kiasi kikubwa na uangalizi wa familia. Jambo la kushangaza ni namna gani Wizara hii jinsi ambavyo hajatiliwa maanani kwa kupewa uzito unaostahili ili kuiendeleza jamii kwa ujumla wake. Katika Jimbo langu na Wilaya mpya ya Kalambo zile Ofisi nilizozoea za Bibi Maendeleo nikiwa mdogo zimebomoka na kubaki baadhi kama magofu. Naiomba Wizara ihakikishe kwamba Ofisi hizi zinafunguliwa na kujengwa nydingine Wilaya zote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ifuatilie na kuona kama bado sheria zilizopo kweli zinalenga kumkomboa mtoto wa kike. Ninao mfano wa dhahiri ambaeo mtoto wa shule ya sekondari aliyeptiwa ujauzito akidai kwamba aliyesababisha ni Mwalimu lakini cha kushangaza Mwalimu bado anaendelea na kazi kama kawaida huku binti akiwa kaachishwa shule. Tunaambiwa mpaka kipimo cha DNA ifanyike ndio kesi ifikishwe Mahakamani, jambo hili halikubaliki.

**MHE. WILLIAM V. LUKUVI:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Maendeleo ya Jamii cha Pawaga kiliungua mwaka 2007. Kituo hiki kilijengwa na Wizara hii na UNICEF. Mheshimiwa Waziri anajua na aliahidi kufuatilia ili kijengwe tena, naomba Wizara ikijenge tena.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aombe msaada TANAPA na Idara ya Wanyamaporii ili wasaidie kujenga kituo hiki kwani Pawaga ni eneo linalozunguka Ruaha National Park na Pori la Lunda Mkwambi Park. Kituo hiki kilikuwa kimesaidia kuhamasisha jamii kuacha ujangili. Wizara itumie ubunifu ili kituo kijengwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Sophia Simba na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa jinsi wanavyofanya kazi kubwa katika kuleta maendeleo ya Wizara hii, napenda kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuanzisha Benki hii ya Wanawake, inasaidia sana katika maendeleo ya wananchi na hasa wanawake katika kuwapatia mikopo ya uhakika na yenye tija. Napenda kuishauri Serikali kuanzisha huduma ya Benki ya Wanawake katika upande wa pili wa Muungano Zanzibar. Serikali ilijibu katika Bunge lako Tukufu kwamba ipo katika *process* ya kuanzisha Benki hiyo Zanzibar. Naomba kujua lini au mwaka gani huduma hiyo itaanza rasmi katika Kisiwa cha Zanzibar. Naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchangia kuhusu swala la maendeleo ya jamii. Ili nchi iendelee, ni lazima pawepo na ustawii wa watu wake na ustawii huu wa watu ni kuhakiki huduma za kijamii zinaboreka mfano elimu, afya, maji na kadhalika. Serikali inahitaji kuweka mikakati zaidi katika huduma hizi ikiwa ni pamoja na kupunguza zaidi vifo vya akina mama na watoto wakati wa kujifungua. Ili haya yafanikiwe, elimu zaidi inahitajika kwa kina mama walio vijijini kuenda kujifungulia hospitalini na sio nyumbani.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili, hatuna budi kuhakikisha hospitali zetu zinakuwa na vifaa vya kutosha vya tiba, wahudumu wa kutosha wenye nidhamu na maadili ya kazi kwa wahudumu hao. Serikali isaidiane na sekta binafsi katika kuendelea kuboresha na kusimamia suala la huduma za afya kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, suala la jinsia, Serikali haina budi kuweka mikakati ya dhati ili kupambana na manyanyaso wanayopata/wanayokumbana nayo wanawake, kupitia vyombo vya habari bado kuna matukio mengi ya unyanyasaji kwa wanawake jambo ambalo linahitaji elimu itolewe zaidi kwa jamii na Serikali pia iweke mkakati kuanzia ngazi za Wilaya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na Mahakama ili angalau kupunguza manyanyaso wanayoyapata wanawake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ushirikishwaji wa wanawake katika jamii na katika sekta mbalimbali bado inahitajika kutiliwa mkazo zaidi na kuweka sera ambazo zitaweka mazingira mazuri ya kumwinua mwanamke.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja. Vilevile naomba kuchangia katika mambo mawaili yafuatayo; kwanza tatizo la mimba mashulenii na pili watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mimba mashulenii ni kubwa katika nchi yetu. Sasa umefika wakati wa kuwafikiria wanafunzi wa kike ambaa huwa wanapata mimba wakati wa masomo, kuwafikiria kurudi shulenii baada ya kujifungua. Maana unakuwa uonevu mkubwa kwa kutowapatia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwa vile wenzetu wa Zanzibar wameweza kuikabili hali hii kwa uzuri sana, wao wamebadilisha sheria ili watoto wa kike wapate kuendelea na masomo yao, naomba Wizara ikachukue ushauri kwenye Wizara ya Elimu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mimba linatokana na mambo mengi kama vile:-

- (i) Kutokekewepo kwa mabweni ya watoto wa kike ili kuwakinga na vishawishi.
- (ii) Kutokekewepo chakula cha mchana katika shule za kutwa kunachangia wanafunzi kudanganywa na kupewa pesa za kununua chakula.

(iii) Kutokuwepo kwa masomo maalum ya afya yanayoendana na ukuaji wa wanafunzi ili waweze kujija na kuwa na tahadhari inapofika wakati wa kujamiiiana.

Mheshimiwa Spika, watoto wanaishi katika mazingira hatarishi. Watoto wengi wa mitaani ndio mionganoni mwa wanaishi katika mazingira hatarishi. Bado watoto wanaishi mijini kila siku wanaongezeka, iko haja Wizara iwe na utaratibu wa kuimarisha mifumo ya kijamii na kuwatunza watoto hao amba wanaishi katika mazingira hatarishi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mashirika mengi ambayo yanajidai yanafanya kazi ya kusaidia watoto wanaishi katika mazingira magumu lakini hawafanyi hivyo, wapo katika kutafuta pesa zinazotokana na wafadhilli. Naiomba Wizara ichukue hatua ya kuyachunguza mashirika hayo yaani (*NGO'S*) zenyenye malengo mabaya kwa Tanzania yetu hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara iwe na mikakati maalum ya kupunguza watoto wa mitaani iwe kila mwaka wanapungua badala ya kuzidi.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya binadamu yana dhana pana sana, kwa kuzingatia utambuzi wa utu wa mwanadamu, kwa kufuata mila, desturi, utamaduni, elimu rasmi na isyo rasmi na kadhalika. Mahitaji muhimu ya binadamu ya chakula, malazi na mavazi yote ni sawa kwa kila binadamu. Jamii ya Kitanzania tutafanya makosa makubwa kama tutajilinganisha na jamii zenyenye mazingira tofauti na ya kwetu hasa kwenye mahitaji muhimu ya kukuza na kulinda utu wa mwanadamu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka 2015 nchi yetu ni mionganoni mwa nchi tutakazopimwa kwa ufanisi wa malengo ya milenia (*MDGs*), nashauri ni vema Wizara ikawa na utaratibu maalumu wa kujipima kwa vigezo vilivyofikiwa na hasa lengo la tatu la milenia la usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kufanya kazi pamoja kuhusu filamu zinazodhalilisha utu wa mwanamke hasa zile zinazooneshwa kwenye luninga kuhusu unyanyasaji na uteswaji wa jinsia ya kike kama ni jambo chanya katika jamii yetu ya Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jamii yetu ni ya kimfumo wa upendeleo kwa jinsia ya kiume zaidi (mfumo dume), elimu itolewe zaidi kwa wanaume kuhusu kutambua haki za binadamu wote bila kujali jinsia na bila ya kuathiri mila zilizo nzuri katika jamii yetu.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Uongozi wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na mipango mizuri iliyowasilishwa kwa kuendeleza Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Wananchi viro katika hali mbaya sana kimajengo na wanapewa fedha kidogo sana kuvendeleza, je, Wizara haioni Vyuo hivi vitakufa kabisa na hivyo kupoteza lengo zima la uanzishwaji wake? Mfano ni Chuo cha Ulembwe kilichopo Jimbo la Njombe Magharibi. Vyuo hivi ni msaada sana kwa wananchi na vijana wanaokosa nafasi za kuendelea na masomo wakiwemo watoto yatima amba vituo hivi vinaweza kuwasaidia kupata "skills" na mafunzo mengine yanayotolewa *VETA* ili waweze kujajiri.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na tatizo la watoto kutelekezwa na kuishi mitaani, je, Wizara inao mkakati gani wa kumaliza tatizo hili katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza jinsia ya kike, Wizara hii ina mkakati gani wa kuwasaidia kupata mikopo ya elimu ya juu kama ilivyo kwa Madaktari?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii ya mapato na matumizi kwa Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, kwani jamii isipoendelea maana yake nchi haitakuwa na mustakabali ulio chanya, tutakuwa na Taifa lisilo na dira. Wizara hii imekuwa ikipewa kipaumbele cha mwisho na kutengewa fedha kama vile ni Idara tu.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukishuhudia unyanyasaji wa kijinsia ambao kina mama na watoto wanafanyiwa lakini bado Serikali haichukui hatua na hii inachangiwa sana na kuwepo na sheria zilizopitwa na wakati ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili ziendane na hali halisi ya sasa na kasi ya matendo ya unyanyasaji yaliyokithiri kwenye jamii yetu. Ni wakati muafaka sasa sheria kandamizi zote kuondolewa.

Mheshimiwa Spika, pia nimekuwa nikishangazwa na kasi ambayo Wizara hii inayo katika kukwamua wananchi kiuchumi, fedha ambazo zinategemewa kwenda kwenye Halmashauri haziwfikii welengwa na ni kidogo sana. Huwa najiuliza kwa nini mipango ya kuwainua au kuwaendeleza wananchi huwa haifanikiwi kwa maana ya kuwafikia walengwa, badala yake kuishia kwenye mifuko midogo ya wajanja. Tumeshuhudia uwepo wa mifuko mingi kama TASAF, Mabilioni ya Kikwete, Mfuko wa Wananchi na mingine mingi ambayo haina tija yoyote.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia miradi ya kuwainua wananchi kiuchumi tena wale wa kipato cha chini inafanikiwa kuliko hii ya Serikali ambayo haionyesi mafanikio kwa walengwa. Mfano ni mradi wa 'MWEL' ambao unaendeshwa na Kampuni ya Vodacom, mradi huu unafuatiliwa sana, sasa kwa nini Serikali tunashindwa wakati tunatumia mabilioni ya fedha?

Mheshimiwa Spika, ni muda muafaka sasa tuwe na *database* ambayo yataainishwa majina ya wafaidika wa miradi husika na sehemu walipo na si kuambiwa tu kwa nadharia kuwa wanufaikaji ni wengi, kuwa fedha billioni kadhaa zimetolewa lakini bila kubainisha ni kina nani wanufaika na ni wa kada gani, vinginevyo tutaendelea kuimba wimbo wa kumnyanya mwananchi kimaendeleo lakini bila kuwa na mipango ambayo ni timilizi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuzungumzia suala zima la Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (*FDC*) kilichopo Wilayani Tarime. Juzi wakati Naibu Waziri wa Elimu akijibu swalii la Mheshimiwa Nyangwine, Mbunge wa Tarime ambaye alitaka kujua ni kwa nini Wilaya ya Tarime haina chuo cha *VETA* na ni lini kitajengwa Wilayani pale ili wananchi wanufaikie na mafunzo ya chuo kile. Naibu Waziri huyo wa Elimu alisema kuwa hamna haja ya kuwa na chuo cha *VETA* Tarime na mbadala wake ni chuo cha *FDC* ambacho kipo.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, kama dhamira ya Serikali kweli ni kuweza kutoa mafunzo ya dhati kwa wananchi wake hususan wa Mkoa wa Mara na Tarime kwa ujumla. Maana hichi chuo cha *FDC* Tarime kimetelekezwa na Serikali na ni aibu kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa tano nilifanya ziara yangu katika chuo hiki ambacho kina wanafunzi 120, lakini nasikitishwa sana jinsi kile chuo ambacho kilijengwa tangu mwaka 1985 kikiwa kama *TARDEP* kiliviyotelekezwa na sasa kipo katika hali mbaya sana, hata taswira ya shule ya msingi iliyopo vijijini ina nafuu mara dufu ya chuo hiki. Kama Serikali ingekuwa na nia ya dhati na dhamira ya kweli ya kutenda inayoyasema mbele ya Watanzania kweli nchi yetu ingekuwa mbali sana.

Mheshimiwa Spika, nilifarrijika kusikia Mama Sophia Simba (Waziri) alitembelea chuo hiki tarehe 2/3/2012, nilipata faraja sana kwamba sasa chuo hicho ambacho kinasaidia sana kitakuwa kimepata mwarobaini wake. Chuo hiki kina changamoto nydingi sana, hivyo naomba Serikali inipatie majibu ya hizi changamoto kwamba zimeshatatuliwa au zitatataliwa lini? Sababu ni aibu kwa Taifa letu kama hatutatoa kipaumbele kwenye kuelimisha wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya kwanza ni kutopelekwa fedha kwenye chuo hiki tangu Julai 2011, hii inapelekea ugumu wa kuendesha shughuli zote za chuo kile. Ni dhahiri hamna dhamira ya kweli kwani Serikali kupitia Wizara haijapeleka fedha tangu mwaka 2011 na hii imapelekea kuwepo na malimbikizi ya madeni ya wazabuni kufikia Tshs. 8,300,000/= na yale ya bili za umeme na maji kufikia Tshs. 1,300,000/=.

Mheshimiwa Spika, jumla ya deni hili hadi natembelea ilikuwa ni Tshs. 9,600,000/= na wazabuni pamoja na *TANESCO* walikuwa wametishia kusitisha huduma. Sasa bila nishati ya umeme na maji hawa wanafunzi na wakufunzi wataishije? Napenda kujua kama Serikali imeshapeleka fedha hizi na kama bado ni kwa nini?

Mheshimiwa Spika, vilevile watumishi walilalamika juu ya madai/madeni yao ya posho za likizo, posho ya uhamisho na posho za mizigo pamoja na usafiri ambapo imekuwa ni tatizo sugu. Vilevile wakufunzi na watumishi walilalamikia kuhusu kutopandishwa madaraja ya kazi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya pili ni kuhusu uchakavu wa madarasa ambayo hata idadi yake haikidhi haja. Madarasa ni machache na chakavu. Mahitaji halisi ya chuo ni kuwa na karakana saba (7) lakini hadi leo hamna karakana hata moja bali ipo ambayo haijakamilika tangu mzabuni apewe mwaka 2002, je, hawa wanafunzi watajifunzaje kwa vitendo bila karakana hizi, ndio maana wanaishia kujifunza kwa nadharia.

Mheshimiwa Spika, Chuo hiki hakina vitabu wala maktaba, wana vitabu vichache sana na vya zamani ambavyo vimepitwa na wakati, kuna uhitaji wa maktaba ambayo haipo kabisa vilevile hamna maabara yoyote kwa ajili ya kujifunzia kivitendo. Chuo hakina bwalo, kumbi, jiko, bweni zilizopo ni za zamani na hazikidhi mahitaji ya sasa, ni majengo ya zamani sana, hata jengo la utawala ni dogo sana hata la shule za msingi lina unaafuu.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya tatu ni juu ya vifaa vya kufundishia ambavyo chuo hakina kabisa na ambavyo viro kama vyerehani vyote ni vibovu na havifanyi kazi. Chuo hiki hutoa kozi nydingi kama fani ya ufundi magari, umeme, sayansikimu, *welding*, *computer*, uashi, useremala, ushonaji, uelewa na kadhalika. Hizi fani zote hazina vifaa vya kufundishia kama vyerehani viro vitatu (3) tu lakini vyote vilikuwa vibovu hadi nikawajibika kupeleka fundi ili atengeneze lakini mahitaji ni zaidi ya vyerehani tisa (9), hawana *computer* kabisa, ipo moja tu ya Mkuu wa Chuo, hawana randa na vifaa vingine ambavyo ni vya kisasa kwa ajili ya uashi, kama nyundo na msumeno.

Mheshimiwa Spika, vile vile hakuna *garage* kwa ajili ya kujifunzia ufundi gari, wanawajibika kwenda Mjini Tarime kwenye *garage* binafsi ambayo mtu kajitolea, *garage* ya Babu 'G', hawana vifaa kwa ajili ya kufundishia somo la umeme, pia chuo hakina madawati/viti vya kutosha pamoja na meza za kutumika madarasani.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya nne, ni kuhusu uchache wa wakufunzi na wataalamu wengine. Mahitaji ya chuo kwa sasa ni walau wakufunzi 16 lakini pale wapo wakufunzi sita (6) tu, hii ni hatari sana. Kupelekea upungufu huu, wapo wakufunzi watano ambao wamejitolea na hulipwa ujira kidogo tu na chuo, wakufunzi hawa wanafundisha fani muhimu sana kama za umeme, ufundi magari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua kwa nini Serikali isiwajali hawa wakufunzi wanaojitolea sanjali na kuongeza uajiri wa wakufunzi wengine pamoja na wataalamu kama Afisa Ugavi na Mhasibu, Mhudumu wa Ofisi, Wapishi na Karani. Afisa Ugavi na Mhasibu ni watu muhimu sana kwa mustakabali wa chuo kile. Hivyo napenda kupata majibu juu ya utatuzi wa ubaha huu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni juu ya Bodi ya Chuo kutokaa tangu mwaka 2010. Hii haikubaliki kwani chuo bila bodi inakuwa vigumu kwani kero na matatizo hujilimbikiza kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kuomba sana Wizara kushughulikia kero za *FDC* ili Watanzania wanaopata huduma ya elimu katika chuo kile wafaidike/wanufaikie kama vyuo vingine.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara hii kwa juhudi za kuhudumia watoto, wanawake na hata wazee katika nchi hii.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine kwa kuisimamia vizuri Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia bajeti hii, binafsi nitajikita katika maswali ambayo yatahitaji majibu. Hivyo namtaka Mheshimiwa Waziri ajibu hoja hizi kwa makini.

Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu, kuna *NGO*'s nyingi zilizosajiliwa kwa lengo la kusaidia watoto yatima na hata wazee. *NGO*'s hizi hukusanya fedha nyingi toka kwa wafadhili na hata Wahisani. Je, Serikali inadhiliti vipi *NGO*'s hizi ambazo zinatumia mwavuli wa watoto yatima kujitajirisha?

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinakabiliwa na matatizo chungu nzima. Je, Serikali kupitia Wizara hii, imejipanga vipi kutatua matatizo ya:-

- Ukoefu wa vitendea kazi;
- Upungufu wa wafanyakazi hasa wakufunzi;
- Uhaba wa wanavyuo hasa baadhi ya maeneo ya wafugaji;
- Tatizo la mitaala inayoendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia; na
- Uhaba wa majengo?

Mheshimiwa Spika suala la Maendeleo ya Jamii katika jamii yetu ni nyeti sana, hivyo kukosekana kwa wataalamu wa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Kijiji, Kata hata Tarafa ni pengo kubwa Watanzania wengi kukosa wataalam hao. Je, Serikali kupitia Wizara hii imejipanga vipi kuhakikisha kuwa inazalisha wataalam wengi ambao watahudumia angalau kila Kijiji au Kata au Tarafa?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ina mpango gani wa kukibadilisha Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Tarime na kukifanya kuwa Chuo cha *VETA*? Mpango huo utaanza lini na utakamilika lini? Je, mpango huo utawashirikisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Maendeleo wakiwemo wawekezai wa mgodi wa Barrick *North Mara* ambao wako tayari kuisaidia Serikali kutekeleza mpango huu?

Mheshimiwa Spika, Dirisha la Habari kwa wanawake kupitia Wizara hii, tangu ianzishwe limewasaidiajje wanawake hasa wa vijijini kuwa na uelewa juu ya Wizara hii; kufahamu shughuli za maendeleo zinazowahu; na kuelewa haki zao za msingi?

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake wa Tanzania (*TWB*) tangu ianzishwe imewanufaishaje wanawake wa vijijini wakiwemo wale wa Wilaya ya Tarime? Ni sababu zipi zinazoleteleza kutokupanua Matawi ya Benki hii kwa kila Mkoa katika nchi yetu?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imewalipa mishahara watumishi wote wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii? Je, malimbikizo yao ya mishahara yameshughulikiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara imefanya utafiti wa kutosha juu ya unyanyasaji na ukatili kwa wanawake na watoto? Je, tafiti hizi zimesaidiaje kubadilisha tabia hiyo? Kama tafiti hazijafanyika, ni kwa nini? Je, tafiti hizo zitafanyika lini Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa inayoruhusu Ndoa za Kimila katika nchi yetu ya Tanzania imepitwa na wakati, kwani ndoa hizi hizi za kimila kwa kiasi kikubwa ndizo zinazoruhusu unyanyasaji, ukatili, ubaguzi, unyonyaji na mateso kemkem kwa wanawake. Je, Wizara imejaaandaa vipi kuifanya marekebisho Sheria ya Ndoa inayoruhusu kuwepo ndoa za kimila hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, je, Wizara imefanya tafiti gani/ngapi ili kubaini tatizo gani la msingi linalowakabili wanawake wanaokeketwa? Je, Wizara inatoa elimu gani kwa jamii zinazokeketa wanawake ili kuachana na mila hizi kandamizi?

Mheshimiwa Spika, tatizo la kuongezeka kwa watoto wa Mitaani limekuwa ni kero kwa wananchi wengi wa Tanzania hasa wanaoishi Mjini. Kuna sababu mbalimbali zinazopelekea kuwepo kwa tatizo hilo hapa nchini. Napenda kuuliza maswali yafuatayo:-

- Je, Wizara imefanya tafiti ngapi za kina ili kubaini chanzo cha kuongozeka kwa tatizo hilo?
- Je, Wizara imejiandaa vipi kukomesha tabia hii?
- Kwa nini Serikali hailishuhulikii tatizo hili kwa jicho pevu?
- Ni *NGO*'s ngapi hapa nchini zinazoshughulikia tatizo la watoto wa Mitaani? Zimefanikiwa vipi au zimeshindwaje?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watoto huajiriwa katika kazi hatarishi kama vile kwenye migodi, kwenye ujenzi wa barabara na hata kutumikishwa kwenye mashamba na kwenye majumba. Hali hii inapelekea watoto hao kunyanyasika, kuonewa, kudhalilishwa, kunyonywa, kukandamizwa. Je, Wizara hii inaishaurije Serikali ili iweze kukomesha hali hii? Je, Wizara hii ina mkakati gani endelevu wa kutokomeza kabisa vitendo hivi?

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kipatacho mwaka mmoja hadi sasa kuna taarifa kuwa wanawake nchini Kenya wamekuwa wakitoa kipigo kitakatifu kwa wanaume wanaoishi katika nchi hiyo. Je, Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii analifahamu hili? Je, amejiendaaje kupitia Wizara yake kutoa elimu kwa wanawake/wanaume kuhusu tabia hiyo ambayo itahatarisha amani katika familia zetu?

Mheshimiwa Spika, nyumba Ntobbu ni nini? Kuna madai kuwa, kuwepo kwa nyumba Ntobbu hapa nchini kunasababisha suala la maambukizi ya virusi vya Ukimwi hapa nchini. Je, Wizara inakubaliana na suala hili? Je, Wizara imetoe elimu gani kuhusu utokomezaji wa nyumba Ntobbu kwa baadhi ya koo Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Spika, je, ndoa za mitala kwa baadhi ya jamii hapa nchini kwetu Tanzania zinasaidiae kuimarisha au kudhoofisha suala la upendo katika familia? Je, Serikali haioni kuwa kutokana na suala la maambukizi ya ugonjwa hatari wa Ukimwi ni bora ipige vita (marufuku) ndoa hizi za mitala hapa nchini Tanzania?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishauri Serikali iongeze fedha za bajeti kwa Wizara hii ili iweze kufanya tafiti na hivyo kutoa mapendekezo kwa namna gani tunaweza kuondokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake, watoto na wazee hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nawapongeza kwa kufanya kazi kwa kujibana kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Sumve, tunacho Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Malya ambacho kimekuwa kama hakina mwenyewe. Imefikia wakati Chuo kuomba msaada wa chakula kwa wananchi nikiwemo mimi mwenyewe ambapo nilitoa magunia matano ya mahindi ili wanachuo waendelee na masomo. Je, tatizo ni nini? Kama ni ufinyu wa bajeti, kwa nini Wizara isikae na Wizara ya Elimu ili Vyuo hivyo vya *FDC* viwe Vyuo vya *Ufundi (VETA)*? Haingii akilini kuendelea kung'ang'ania kitu ambacho huwezi kukihudumia. Hapa naomba majibu kwa hili, kwani tangu mwaka 1995 Chuo hicho kimekuwa kikiendeshwa kwa kujikimu.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiwasiliana mara kwa mara na Naibu Waziri na jana tarehe 23 Julai, 2012 nikiongea na Katibu Mkuu kuhusu malimbikizo ya madeni ya Wazabuni.

Mheshimiwa Spika, katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Malya kilifanyiwa ukarabati zaidi ya miaka minne sasa, lakini cha kushangaza ni kwamba hadi leo hajalipwa madai yake. Mara kwa mara mzabuni huyo amekuwa akija kwangu kama Mbunge wa eneo lakini pia kama Mjumbe wa Bodi kunilalamikia kuhusu kutolipwa haki yake ya zaidi ya Shilingi milioni 50. Je, ni lini mzabuni huyu aliyetumia pesa yake kukarabati majengo ya *FDC* Malya atalipwa?

Mheshimiwa Spika, nikijibowi hayo mawili ya mzabuni kulipwa na *FDC* ya Malya na nyingine kuzikabidhi Wizara ya Elimu ili ziwe *VETA*, ili Wizara ibaki na vichache ambavyo inaviweza kuvihudumia.

Mhesimiwa Spika, nitaunga mkono kwa asilimia mia moja bila kusimama katika vifungu.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ya wataalamu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda ushauri wangu niuelekeze katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wazo la kunzisha Benki ya Wanawake, lilikuwa ni wazo zuri sana. Akina mama wanahangaika kutafuta mitaji kwa ajili ya biashara zao ndogo ndogo. Benki hii bado ni ndogo sana, inahitaji kuimarishwa kwa kupewa mtaji mkubwa ili ifungue matawi Mikoani karibu na akina mama wengi zaidi. Pia ni muhimu kwa benki hii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa akina mama ili waunde vikundi vyao vya *VICOBA* kisha wawapatie mikopo yenyenye riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatakiwa kuwa “*more serious*” katika kulishughulikia tatizo la watoto wa Mitaani. Ni vyema kwa Serikali kuwa na mkakati wa kuwasaidia hawa watoto au kuratibu vizuri jithada ninazofanywa na *NGO*’s mbalimbali zinazosaidia watoto hawa. Watoto hawa wanahitaji kupata elimu na mahali pa kukaa ili baadaye waweze kushiriki katika kujenga nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ijitätidi kukabiliana na tatizo la ajira ya watoto wadogo kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo cha Lemela kilichoko Wilaya ya Ngara, kiko katika hali mbaya sana. Siyo vibaya kwa Wizara ikaiga mfano wa Vyuo vya *VETA* ambavyo vinafanya kazi nzuri. Chuo cha Lemela ni vizuri kikawa Chuo cha Ufundı ili vijana wanaomaliza *Form IV* na Darasa la Saba wajifunze ufundi stadi ambazo zitawasaidia waweze kujajiri.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara hii isaidie kuwajengea wanawake hali ya kujiamini (*Self confidence*). Hatuwezi kuendelea bila ukomo na sera ya kuwapendelea akina mama na hasa katika uwakilishi. Akina mama wanatakiwa waingie katika ushindani na wanaume wakati wa kusaka vyeo vya uwakilishi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika uteuzi wa Rais, ni vyema Mheshimiwa Rais akashauriwa kuzingatia sifa zinazotakiwa kwa ajili ya uteuzi.

Mheshimiwa Spika, kazi za Maafisa Maendeleo hazionekani. Afisa Maendeleo wanakaa zaidi ofisini. Nadhani hawajui wanatakiwa kufanya nini.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imeainishwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba katika Ibara ya 204 na 205 ya Ilani ya CCM ya mwaka 2010 imetekelezwa kwamba mikataba ya haki za wanawake na watoto iliyordhiwa itekelezwe kikamilifu, hali ambayo pia ilipelekea kutungwa kwa sheria ya mtoto Na. 21 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tumekuwa tukishuhudia matukio kadhaa ya unyanyasaji wa mama na mtoto/watoto yanayofanyika na kutangazwa hata kwenye vyombo vya habari, pasipo kusikia kauli yoyote ama hatua zozote kutoka kwenye Wizara ambayo ndiyo ina dhamana ya kukusimamia suala hili.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni vyombo vya habari ikiwemo *ITV* na *EATV* wamekuwa wakitoa taarifa ya Sakata la mama aliyenyang'anywa mtoto wa miezi minne na familia ya mume wake amba ni Wahindi, huku Mahakama ikitumika kuhalalisha ukatili huu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aliambie Bunge hili Tukufu na kwa kuzingatia ukatili na unyanyasaji uliomkuta mama huyu, wameshachukua hatua gani kama Wizara kuweza kumsaidia huyu mama na mtoto kupata haki yake?

Mheshimiwa Spika, moja kati ya changamoto wanazokumbana nazo watoto wa kike ni mimba za mashulenii. Mfano, kupata ujauzito, pamoja na maambukizi ya virusi vya Ukimwi. Kuna taarifa zinazoonyesha kwamba mimba na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa wanafunzi inachangiwa na Walimu kushiriki ngono na wanafunzi. Wizara imejipanga vipi kulifanya kazi tatizo hili sugu ili kuokoa kizazi ambacho ni tegemeo kubwa kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua, Wizara imejipangaje kwa kushirikiana na washirika wake (kama alivyowabainisha kwenye hotuba yake) kuondokana na tatizo la watoto "Mtaani" amba wamekuwa ni kero kubwa sana katika Jiji la Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, je, kuna hatua zozote zimechukuliwa ili kuweza kufanya utambuzi kuweza kubaini wapi ni watoto wasio na wazazi au wanaotoka katika mazingira magumu ili Wizara kuititia wadau wake waweze kuwapatia msaada stahiki?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto. Ni kwanini watu wengi wanachukulia kama ni Wizara mahsus kwa wanawake na watoto pekee? Wizara haioni hili kama tatizo?

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ningependa kujua Wizara ina nafasi gani katika kuhakikisha kwamba sheria kandamizi (hususan kwa wanawake) zinaletwa Bungeni kufanyiwa marekebisho? Mifano michache, *JALA – Judicature and apparition of laws Act. Cap. 358*, Sheria ya Ndoo 1971, Sheria ya Mirathi na kadhalika.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuungana na wenzangu katika kutoa salaam za rambirambi kwa ndugu na wafiwa wa wahanga wa meli ya *MV. Skagit* iliyotokea jirani na Kisihi cha Chumbe kuelekea Unguja na Pemba. Jambo muhimu ilikuwa Bunge lijadili ajali zinazomaliza maisha ya wananchi. Bunge lingejadili, ingetoa maamuzi ambayo yangeweza kukaribisha kupatikana kwa ufumbuzi wa kukinga ajali nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, Adhabu ya Fimbo inayotolewa kwa watoto wa Shule, ni ukatili, ni kinyume cha Sheria na taratibu za Kimataifa. Nashauri ifutwe.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iache kuonyesha vipindi vya *TV* vinavyochangia katika mmomonyoko wa maadili. Ama sheria ya kudhibiti vipindi vya TV itumike kwa kuhakikisha vipindi kama hivyo havionyeshwi kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya wanawake, elimu iendelee kuhakikisha haki ya wanawake kuhusu miliki ya ardhi, mirathi na ndoa; wajibu wa wanandoa wakati ndoa ikiwa hai au baada ya talaka, itolewe kwa wanandoa katika ngazi zote. Desturi ya wanawake kupingwa ikome. Wapatiwe elimu ya kwamba, ni Sheria ya Ardhi kwa watoto wa kike na wakiume watamiliki ardhi sawa kwa sawa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ihakikishe wanawake na watoto wa kike wanavaa nguo za sitara, hasa viongozi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wanawake.

Mheshimiwa Spika, kama wanawake watakuwa na tabia njema, jamii nzima itakuwa na ustaaribu mzuri.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri inayoeleweka chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri Sophia Simba; Naibu wake, Mhesimiwa Ummy Mwalimu; Katibu Mkuu na Naibu wake, Wakurugenzi na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kama ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Sheria kandamizi zilizopitwa na wakati, nashangaa bado kuna kigugumizi kikubwa kwa Serikali kudhamiria kuzirekebisha. Kwa mfano, Sheria ya Ndoa, mirathi, ambayo wanawake wengi hapa nchini wanakosa haki zao wakati wanapookewa na wanapobaki wajane. Nashauri kwamba, wakati umefika sasa wa sheria hizi kurekeblishwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hali za Maafisa Maendeleo katika Halmashauri ni ngumu katika utendaji wao kazi, kwani hawathamini kama ni kada ya maana, hata Wakuu wa kazi, Wakurugenzi, ingawa wajibu wa Maafisa Maendeleo ndio wahamasishaji wakubwa wa shughuli za maendeleo/jamii katika maeneo yao. Wakitumiwa vizuri, wao ndio wachochearaji wa mafanikio wa programu/kampeni mbalimbali kwa jamii. Lakini kwa kiasi kikubwa wanakabiliwa na ukosefu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, sielewi ni sababu zipo zinafanya kada hii kudharaulika, hupewa kazi wakati wageni wa kitaifa labda wanapotembelea maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kuhakikisha madai ya Maafisa Maendeleo inarudi kwa kila hali kama iliyokuwa enzi za miaka baada ya Uhuru, wapewe fedha za kutosha, usafiri na kuhusishwa kikamilifu katika program za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi, ni kwa kiasi gani mikakati ya Wizara imezingatia uwepo wa wanawake wenye ulemavu na watoto wenye ulemavu pia? Ingawa masuala ya wenye ulemavu yako chini ya Idara ya Ustawi wa Jamii, lakini naamini Wizara ya Maendeleo ya Jamii ina wajibu wa kutoa miongozo na maelekezo kuhusu wenye ulemavu kwa Wizara nyingine hasa inapohusu watoto na wanawake.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana Wizara hii mwaka hadi mwaka kuendelea kutengewa bajeti ndogo ambayo naamini haiwezeshi kutimiza wajibu wake kwa jamii. Kwa mfano Wizara inawajibika katika uendeshaji wa Vyuo vyta Maendeleo ya wananchi, lakini vingi ya Vyuo hivyo viko hoi bin taaban. Majengo yake ni chakavu, vitendea kazi vichache, au hakuna kabisa, fedha za uendeshaji ni kidogo na hazipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ijithabidi kujitetea ipewe fedha za kutosha hata kabla mgawanyo wa fedha za bajeti haujaanza, kwa sababu Wizara hii ni kinara wa kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali hata kabla ya programu za utekelezaji hazijaanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu mdogo, naunga mkono hoja.

**MHE. SAADA M. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, uongozi na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya kuhakikisha kuwa maendeleo yanafikiwa kuititia MKUKUTA II. Hata hivyo, naomba kutoa mchango kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanawake na watoto, wameendelea kupata athari kubwa kutokana na unyanyasaji unaoendelea kila leo. Hata hivyo, sisi wananchi hatusikii hatua ambazo Wizara inachukua katika kutatua tatizo hili, au angalau kushiriki katika harakati za wanaotatua tatizo hili. Mifano ya hivi karibuni ya kunyang'anywa kwa motto, msichana aliyezaa na mume ambaye hajakubalika, msichana amenyang'anywa mtoto kutokana na amri ya Mahakama na Wizara imekaa kimya. Mfano kama hii ipo mingi sana kiasi cha wananchi kutokuwa na imani na Serikali yetu. Naomba Wizara iwe inafuatalia mienendo ya kesi kama hizi na iwe inatoa taarifa zake.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha leo na kuchangia kwa maandishi hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Mkwerekwe, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kuhusu wanawake wanavyodhalilika, baada waume wao kufariki. Wanawake au wanandoa hawa wakiwa na watoto wao kukosa haki ya kurithi mali ilioachwa na waume wao.

Mheshimiwa Spika, mali hizo huhodhiwa na ndugu au baba wa Marehemu, jambo ambalo siyo haki kabisa.

Mheshimiwa Spika, wanawake wakidai mali hukataliwa kabisa na wazee wa Marehemu, matokeo yake, mjane huyo huwa na maisha magumu sana huku akihanganya na watoto.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali isimamie vizuri mambo haya ili wanawake wapate haki yao.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mmomonyoko mkubwa sana wa maadili hapa Tanzania na hasa kwa upande wa wanawake. Hivi sasa wanawake wa Tanzania havaa nguo zinazoashiria kuwa nusu uchi. Wengine hvuva magauni yao au sketi fupi sana, wengine hvuva suruali ambazo sehemu ya siri zinaonesha, aidha akienda au akikaa, jambo ambalo siyo zuri kwa maadili ya Mtanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu, Wizara yake imejipanga vipi ili kuzuia mmomonyoko wa maadili usiwepo hapa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, watoto wanakosa haki yao ya msingi pale tu baadhi ya wanawake wanapotupwa watoto baada ya kujifungua au wazazi wanapotwalekeza za watoto. Kwa hiyo, wazazi kama hawa wadhibitiwe na Serikali na wakijulikana, sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, nazidi kukushukuru wewe binafsi na nazidi kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu katika kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la sheria zilizopitwa na wakati. Jana tulibahatika kuwa na semina. Tulipata mada mbili ambazo zilituonyesha jinsi akina mama wanavyoathirika na sheria hizi ambazo zimepitwa na wakati. Mfano, Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi. Tunalombwa Wizara hii iweze kuleta mabadiliko ya sheria hizi. Naamini tukishirikiana kwa pamoja, haya yote yatawezekana.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiona kwenye vyombo vya habari jinsi akina mama na watoto wanavyonyanyasika pale ndoa zinapovunjika, haki hazitendeki kwa akina mama na watoto hao na ndiyo maana tunaona watoto wa Mtaani wanaongezeka siku hadi siku. Tatizo hili linazidi kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kuna kila sababu sheria nilizotaja hapo, pamoja na nyingine zenye upungufu zifanyiwe marekebisho haraka ili tuondoe matatizo yaliyopo na lawama ambazo tunatupiana za Wabunge, Serikali na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie suala la mama aliyenyang'anywa mtoto anayenyonya kwa kisingizio kwamba mama huyo ni kichaa. Najua suala hili liko Mahakamani, lakini ningombwa mama huyu apewe mtoto wake hata kama ni chini ya uangalizi wa ndugu ili aweze kunyonyesha mwanaye. Uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi, hasa mama anayebeba

mimba na kuzaa kwa uchungu. Pia ni vizuri mambo haya yakachunguzwa kwa undani na siyo kutoa majibu ya haraka kwamba mtoto alichukuliwa na ndugu wa mume kwa sababu mama yule ana matatizo ya akili.

Mheshimiwa Spika, masuala ya unyanyasaji wanawake yanazidi kushamiri katika nchi yetu. Hivi karibuni iliokea tendo la kinyama ambalo limesababisha kifo kwa mama aliyepigwa na mumewe, kisha akamfunga kamba na kumburua mama yule barabarani na kusababishia mama huyo majeraha makubwa na hata kusababishia kifo kwa mama huyo. Ningependa kujua ni hatua gani zimechukuliwa juu ya mume huyo aliyefanya kitendo hicho cha kinyama kiasi hicho? Taarifa zilizopo, mtu huyu bado yuko Mtaani. Kwanini hakamatwi ili aweze kufikishwa kwenye vyombo vya sheria? Hamwoni kuchelewa kukamatwa kwa mtu huyu ndiko kunakofanya wananchi kujichukulia sheria mkononi?

Mheshimiwa Spika, hivi majuzi kuliokea mauaji ya ndugu zetu katika moja ya mbuga za wanyama (*hotel*) lakini wahusika wa tukio hilo wameshakamatwa. Ni kwa nini hili la huyu mama limetokea kabla ya hili, bado mtuhumiwa hajakamatwa mpaka sasa?

Mheshimiwa Spika, ningependa haya yote niliyoyaandika yafanyiwe kazi kama kweli tunataka kumkomboa mwanamke wa Kitanzania kwenye huu mfumo dume.

**MHE. PHILIPA MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nazipongeza hotuba zote mbili zilizotolewa, kwa maana ya Wizara, na ile ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kuzungumzia juu ya utumikishwaji kazi wa watoto wadogo.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili limekuwa sugu hasa Mjini ambapo watoto wengi wenye umri wa kwenda Shule wamekuwa wakionekana kufanyabiashara maeneo ya stendi za mabasi, mfano, *Ubungo Terminal Bus* na Stendi ya Kahama Mkoani Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, mbali na kufanya biashara, watoto wamekuwa wakitumikishwa kufanya kazi mashambani, kugonga mawe kwa maana ya kutafuta kokoto. Hii ni hatari sana, tunaitaka Wizara itafute ufumbuzi wa haraka wa tatizo hili ili kuwaokoa watoto hawa.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni mtambuka, inaingia katika Wizara zote kuangalia ni kwa namna gani mgawanyo wa keki ya Taifa inazingatia jinsia. Hivyo, fedha iliyotengewa ni kidogo sana. Wizara hii haiwezi kufikia malengo yake kiukamilifu kama haithaminiwi.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii ni watu muhimu sana katika Wizara hii. Lakini katika hali isyo ya kawaida, wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu, hawana usafiri wa uhakika na hata fedha katika kitengo hiki hazitolewi ipasavyo au kupewa kipaumbele. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge tabia hii ya kitengo hiki kutothaminika, itakomeshwa lini, na Wizara itawachukulia hatua gani Wakurugenzi ambao watawanyima fedha Maafisa hawa katika Halmashauri zao?

Mheshimiwa Spika, mila na destrui zimekuwa zikimduimisha mwanamke. Aidha, sheria zilizopitwa na wakati nazo pia zimekuwa chanzo cha kumdhaliilisha mwanamke.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali kupitia Wizara hii kupitia upya sheria kandamizi dhidi ya wanawake na kutengeneza sheria rafiki na zenye lengo la kumkomboa mwanamke. Aidha, mila potofu zote zipigwe vita na tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe tamko dhidi ya mila hizi potofu zinazomduimisha mwanamke.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii iongezewe fedha za kutosha ili elimu itolewe, iwafikie walengwa wowote, popote pale walipo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kueleza ya kuwa naunga mkono bajeti ya Wizara hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ingawa Wizara hii imechukua hatua nyingi za kudhibiti ukatili dhidi ya akina mama, lakini bado ukatili huu unaendelea kwa kasi kubwa. Mfano wa ukatili wa kuhuzunisha sana, ni ule aliofanyiwa Ndugu Nasra Mohamed na mumewe Elisha Mkumbati. Elisha alimgonga kwa makusudi kwa gari na baadaye akamburura kwa gari hiyo hiyo barabarani. Kama vilivyoeleza vyombo vya habari, mama huyu aliumia vibaya na baadaye kufa. Licha ya juhudhi zilizofanywa na hospitali ya Bugando na Muhimbili, mama huyu alifariki dunia. Mungu amlaze mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni hatua gani Serikali imechukua dhidi ya Ndugu Elisha mpaka hivi sasa? Je, watoto wa Marehemu wanalelewa na nani?

Mheshimiwa Spika, hoja yangu mimi ni moja tu. Napenda Mheshimiwa Waziri atapojuisha, alitolee ufanuzi suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti hii.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa hotuba yake inayolenga Maendeleo ya Jamii ya Watanzania na changamoto zake.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba kumekuwa na uzoefu sasa uliodumu kwa muda mrefu kwa Wizara hii kuendelea kutengewa bajeti finyu siku hadi siku, mbali ya michango ya Waheshimiwa Wabunge wanavyoendelea kuiomba Serikali kutokana na changamoto nyingi za Wizara hii muhimu na mtambuka.

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue kwamba, kuimarika wa Wizara hii ni kuimarika kwa jamii iliyotuzunguka, kwani fedha zake zingeelekezwa katika changamoto zinazoikabili Wizara nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vinaendeleza wananchi walioamua kujunga na vyuo hivi kiufundi, kimaarifa na kuwawezesha kujajiri na kuajiri wengine na kuondokana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi kwa muda mrefu sasa vimeduwa vikitengewa ruzuku ndogo kutoka Serikalini. Hata hivyo, naipongeza Serikali kwa uamuji utakaowezesha Vyuo vipatavyo 25 nchini kutoa mafunzo ya ufundi stadi (*VETA*) kuanzia Januari, 2013 kwa kuanzia na udahili wa vijana 1,250.

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Serikali kuendelea kutenga fedha angalau ya kutosha Vyuo hivi viendelee kukarabatiwa hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Bunge hili lilipitisha Sheria ya Mtoto ya mwaka 2008 kwa mantiki ya kuondoa unyanyasaji wa watoto, kupatiwa elimu watoto, kulindwa na kutunza kwa watoto.

Mheshimiwa Spika, la kusikitisha hadi leo hii, tunajadili suala la kushamiri watoto wa Mitaani katika maeneo ya Miji. Sheria ile imefanyiwa kazi kwa kiasi kuhusiana na na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, bado watoto wanaendeleo kuyanyaswa, wanakosa elimu na pia wanaendelea kuchanganywa na watu wazima mahabusu na kwingineko. Tabia hiyo inaendelea kuwadhalilisha watoto, na kuwafundisha tabia mbaya walizonazo baadhi ya watu tofauti Gerezani na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika iendelee kuisimamia sheria hiyo katika maeneo yote nchini ili watoto waendelee kupewa haki zao kisheria na kuondokana na unyanyasaji na udhalilishaji Mijini na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wanaume wanaendeleoa na tabia ya kuwadharau na kuwadhalilisha wanawake nchini kwa kuwanyima haki zao za kimsingi, awe ndani ya ndoa au nje ya ndoa, iwe ofisini au nje ya ofisi kwa kushurutishwa rushwa za ngono na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kufuatilia malalamiko yanayoendelea kutokana na wanawake kwa mujibu wa Mikataba ya Umoja wa Mataifa wa mwaka 1981 ili wanawake wajione wanazo haki kama watu wengine nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo machache, kwa kuwa bajeti hii bado ni ndogo kutokana na majukumu ya Wizara hii, naomba kutokana na kazi ngumu za Wizara hii, Serikali iangalie namna ya kuandaa mikakati ya kuiongezea fedha katika bajeti ijayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kutekeleza na kuyafanya kazi maoni na maagizo ambayo yalitolewa na Waheshimiwa Wabunge, Kamati pamoja na Kambi Rasmi ya Upinzani mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutekeleza na kuyafanya kazi baadhi tu ya mambo, bado kuna mambo mengine ambayo yanahitaji yafanyiwe kazi kulingana na mahitaji. Kimsingi, nimesikitishwa na bajeti kiduchu iliyopewa Wizara hii mwaka huu 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni nyeti sana na inashughulikia mambo mengi na kundi kubwa la watu ambaa ndio nguvu kazi ya familia ya kila Mtanzania. Upungufu huu au ufinyu huu wa bajeti utaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumelbe vichache ilivyojiwekea katika mwaka huu wa fedha, vikiwemo kuimarisha utoaji wa mafunzo ya taaluma ya maendeleo katika Vyuo vya Maendeleo ya (*FDC*), kuwajengea uwezo wanawake ili waweze kushiriki katika ngazi zote za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuna mikataba na sheria pamoja na sera zinazotakiwa kusimamiwa ili itekelezewa na hasa mikataba ya kimataifa inayohusu haki, ustawi na maendeleo ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, ufinyu huu wa bajeti utakwamisha yote haya ambayo Wizara imojiwekea ili iliyotekeleza. Kumekuwa na matatizo mengi sana ikiwemo unyanyasaji wa wanawake na watoto pamoja na ukatili. Haya yote yasipofuatiiliwa kwa kutekeleza sera, bado tutakuwa hatujayamaliza. Matatizo haya yapo mengi na kila kona ya nchi kwa mgawanyo huo wa bajeti watatekeleza sera vipi ili kuwanusuru wanawake hawa ambaa wamekuwa wakionewa kila mwaka, kila siku na hata kila saa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na sera na shera zilizowekwa kupinga ukatili huo kwa wanawake, lakini bado wanawake wengi hawajajua haki zao. Pamoja na fedha hizo kiduchu, Wizara iandae utaratibu utakaowawezesha wanawake na hawa walloko pembezoni wazifahamu sera na sheria hizi, kwani zitawasaidia, ukizingatia ni wanawake hao kwa kiasi kikubwa ndio wahanga.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ije na mpango mkakati ambaa utawawezesha wanawake na watoto kujua haki zao.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni sheria kandamizi, kwani imebagua umri wa jinsia kwa kijana wa kike tofauti na kijana wa kiume pamoja na kubagua umri wa kijana wa kike. Sheria hii inakinzana pia na sheria ya mtoto ya mwaka 2009 ambayo inatambua mtu aliyechini ya umri wa miaka 18 kama ni mtoto. Kwa hali hiyo, sheria hii inafanya watoto wa kike kuruhusiwa kuingia kwenye ndoa.

Mheshimiwa Spika, sheria hii imepitwa na wakati, kwani inarudisha nyuma maendeleo na afya pamoja na ustawi wa mtoto wa kike. Kuna haja ya Serikali na Wizara kupitia upya sheria hii ili iweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, sheria hii inamnyima haki kijana na mtoto wa kike huku ikimpendelea kijana wa kiume ambaye kwa upande wake yeye anatambuliwa kama tayari ni mtu mzima.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali kuwasilisha Muswada wa Sheria ili Bunge liweze kuzibadilisha sheria hizi kandamizi dhidi ya wanawake na watoto wa kike ili waweze kuondoka na udhalilishaji huu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na matukio mengi yakiwemo kupigwa kwa wanawake na wanaume zao, kutelekezwa sambamba na kuachiwa mzigo wa wa kulea watoto, kubakwa, kukeketwa pamoja na kunyimwa haki ya kumiliki mali ingawaje wanawake wamekuwa ni wachangiaji katika kuleta mali hizo kwa njia moja ama nyingine. Matukio haya yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku licha ya sera na mikataba ya kimataifa na kitaifa ya kutokomeza ukatili huu dhidi ya wanawake kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vilivyopo nchini, kwa miaka ya nyuma vilikuwa chachu katika kuleta tija kwa wasichana na wavulana na wengi waliohitimu walifaidika sana. Sasa hivi Vyuo hivi hata kusikika tena havisikiki, kwani Serikali imeviacha na pengine kuvisahau kabisa wakati vilikuwa vinasaidia kutoa elimu kwa vijana wa kitanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie tena kwa jicho la tatu Vyuo hivi pamoja na kujenga Vyuo vingine katika maeneo ambapo hakuna ili vijana wetu waendelee kunufaika na elimu inayotolewa katika Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali/Wizara iongeze uwezo wa Vyuo hivyo ili viweze kutoa wataalamu ambao wataweza kusambazwa mpaka kwenye ngazi ya Kata ili kuleta ustawi mzuri wa Maendeleo ya Jamii wanayoifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, Lengo la kuanzishwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi mwaka 1975 ilikuwa kutoa elimu ya maarifa na stadi za maisha kwa wananchi wallomaliza Elimu ya Msingi na wallomaliza Elimu ya Watu Wazima ili waweze kujajiri au kuijendeleza zaidi kielimu.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vingi vimetekelizwa, havifanyi kazi, na sababu eti *SIDA* walisitisha toka mwaka 1990, na Serikali imekuwa haitoi ruzuku, hali inayopelekea kutoonekana kwa umuhimu wa uanzishwaji wa Vyuo hivyo. Serikali ituambie, kwanini inatelekeza Vyuo hivi muhimu ambavyo vingesaidia maendeleo ya wananchi wa Tanzania ambao hawakupata bahati ya kusoma elimu ya juu kwa kukosa stadi za maisha?

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba kujengwa kwa Vyuo vya *VETA* kuende sambamba na kuijendeleza Vyuo vilivyopo, kwani vingesaidia wananchi wengi, lakini vile vile wahitimwa wa Vyuo hivyo vya Maendeleo ya Wananchi, wangeweza kuendelea kwenye *VETA* kwa mafunzo zaidi. Nini hatua ya Vyuo hivyo na hasa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Kihinga Kigoma?

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, inabainisha umri wa binti kuolewa ni miaka 15 na kwa watoto wa kiume awe na umri wa miaka 18. Lakini sheria hiyo ya mwaka 1971 inakinzana na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inatafsiri kwamba mtoto ni yule mwenye umri wa miaka chini ya 18. Ili Sheria ya Mtoto 2009 iende sambamba na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ni dhahiri sasa Serikali kupitia Wizara hii, mabadiliko ya sheria yaletwe Bungeni ili tumtendee haki mtoto wa kike anayezeshwa wakati bado mdogo.

Mheshimiwa Spika, vifo vya wanawake wajawazito vinachangiwa pia na ndoa za utotoni zinazoruhusiwa na sheria hiyo kandamizi ya mwaka 1971, kwani wengi hujifungua katika umri mdodo na wengine hupoteza maisha hasa waishio vijijini ambapo huduma za afya ni duni mno.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile watoto wadogo hukosa fursa ya kujipatia elimu, kwani anaingizwa katika ndoa wakati anatakiwa awepo shulenii katika umri alionao.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ilete Muswada wa Sheria utakaosaidia watoto kuruhusiwa kusoma hata kama wameshajifungua, kwani watoto wengi wa kike hukutana na changamoto nyingi ikiwemo kubakwa hadi kupata ujauzito na maradhi mbalimbali. Hivyo kutomruhusu mtoto huyo kupata elimu, ni kuwabagua na kumkosesha haki ya kupata elimu, kwani ni haki ya msingi.

Mheshimiwa Spika, ninashangazwa na jinsi bajeti ya Wizara hii inavyopungua kila mwaka. Ni vigumu Wizara hii kutekeleza majukumu yake kwa mtindo huu wa kuipa bajeti kidogo. Ukiangalia *trend* ya upangaji wa Wizara hii, mfano mwaka 2011/2012 ilividhinishiwa Shilingi bilioni 16.2; mwaka 2010/2011 ilipangiwa Shilingi bilioni 19.9 na mwaka 2012/2013 Wizara iumeomba Shilingi bilioni 15.6. Kwa nini fedha zinapungua kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, kwa nini kuna Wizara hii kama umuhimu wake hauonekani hali inayopelekea kupewa fedha kidogo? Serikali haioni kuwa Wizara hii ni muhimu, kwani inashughulikia masuala muhimu na yote mtambuka yanayoishus jamii nzima ya Watanzania wote wa jinsia zote kwa watu wazima na watoto wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe majibu, kwa nini hali hii inaendelea? Kuthibitisha hilo, angalia bajeti ya Wizara hii toka miaka mitano mfululizo iliopita na mfano ni huo wa miaka mitatu, imeonyesha dhahiri jinsi bejeti hii inavyoshuka.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, sina budi kutoa pongozi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakichukua kila tahadhari kuhakikisha haki za watoto na akina mama zinalindwa na kuheshimiwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Wizara kuendelea kukaa na kufanya mawasiliano ya karibu na viongozi mbalimbali wa kimila katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia Wizara kueleza na kufikisha ujumbe wao kwa wananchi walio wengi ambaao upataji wao wa habari ni mdogo, ili na wao waweze kuelewa na kujua haki zao za msingi. Pia kutatoa nafasi kwa Wizara kueleza ni kwa namna gani haki za watoto zinalindwa na suala zima la unyanyasaji au kuwa na mfumo dume.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara ina changamoto kubwa ya suala zima la watoto wa Mitaani. Hatujaona juhudhi za dhati za Wizara kupambana na wimbi hili kubwa la watoto wa Mitaani katika Miji yetu Mikuu ambapo baadaye hupelekea watoto hawa kuwa ni ombo ombo, wengine kufanyiwa vitendo vibaya vya utumiwaji mbaya wa maumbile.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuititia Wizara hii iachane na kutoa maelezo mengi na ukweli unaowekwa dhahiri katika barabara kuu na Mitaa mbalimbali ambapo watoto hao hupendelea kuwepo ama kwa ajili ya kuomba au kuiba.

Mheshimiwa Spika, makampuni mengi ya kigeni ambayo yameingia hapa nchini kwa ajili ya utendaji kazi zao, yamebainika kufanya mambo mengi maovu kwa kuwatumikisha watoto wadogo (ambao huwalipa pesa kidogo), vile vile unyanyasaji wa hali ya juu ama kwa wanawake ambaao huomba kazi kwao na hata akina baba pale wanapodai hai zao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Seriali kuititia Wizara hii iangalie sana maeneo ya wawekezaji na Makampuni ya kigeni yanayofanya kazi hapa nchini, pia ichukue hatua za haraka za kisheria kwa wawekezaji hao ambaao huwanyanya sana watoto wadogo na hata akina mama.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iunde kikundi au Chama cha Wanahabari ambaao wataandika taarifa kamili kuhusu ajira za watoto wadogo, lakini pia unyanyasaji wa wazawa kutika makampuni ya kigeni na wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, hali siyo ya kuridhisha hata kidogo katika maeneo hayo, kwani Watanzania wanateseka bure ndani ya nchi yao.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia kwa maandalizi mazuri ya hotuba yao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni kati ya nchi zinazoheshimu na kutekeleza haki za binadamu kwa nadharia na vitendo. Aidha, Tanzania inaheshimu usawa wa jinsia kama sera zake zinavyoonyesha ikiwamo Sera ya Wanawake na Maendeleo ya Jinsia ya mwaka 2000. Hata hivyo, Tanzania kama iliyotamka hivi karibuni, haiungi mkono matendo yanayokinzana na mila na desturi zetu kwa kisingizio cha kutekeleza haki za binadamu. Mojawapo ni ndoa za jinsia moja. Mahusiano haya kati ya jinsia moja ambayo yanakumbatiwa na Mataifa hasa ya nje, hayakubaliki kabisa, na ni kinyume cha mila na desturi zetu Watanzania kama Serikali ilivyokwishatamka.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sera iliyopo haitoshi kuwabana Watanzania wachache wanaoiga vitendo hivyo vya kinyama. Hivyo naomba nifahamu ni lini Mheshimiwa Waziri ataleta sheria hapa Bungeni ambayo itatoa adhabu stahiki kwa watu wenye kutenda vitendo hivi visivyokubalika ambavyo kiutamaduni wa Mtanzania, ni uchafu, ili kuzuira usienee kwa watoto wetu na vizazi vijavyo kwa kisingizio cha haki za binadamu. Tunasikia tetesi kuwa kuna baadhi ya Viongozi, Waheshimiwa Wabunge wanajihuksika na vitendo hivi vya mahusiano ya kindoa ya jinsia moja kwa kisingizio kwamba hakuna sheria inayokataza hivyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapojoju hoja yake, anipatie majibu ni lini ataleta sheria hiyo hapa Bungeni na maelezo ya ziada kuhusu suala hili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za watoto, naomba Mheshimiwa Waziri atupe maelezo ni hatua gani zinazochukuliwa kwa watu wazima hasa wanawake wanaowatumia watoto kuomba omba Mitaani na kuwakosesha haki yao ya kusoma?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. KASSIM M. MAJALIWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mpango mzuri wa Serikali wa kuwezesha wanawake kwa njia ya mikopo, ni vyema utaratibu wa uwezekano wa kufikia wanawake hadi ngazi ya viji, ukawekwa wazi ili kila anayehitaji kupata uwezeshaji huo aweze kufikiwa. Hii inaikabili Wilaya ya pembezoni ya Ruangwa ambayo iko mbali na Makao Makuu ya Mkoa ambako hata hiyo Benki ya Wanawake haipo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Ruangwa ni Wilaya mpya na Wilaya jirani ya Nachingwea haina Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, naomba Wizara iweke mpango wa ujenzi wa Chuo hicho ili kutoa Elimu ya Ujasiriamali kwa Wilaya zote mbili za Ruangwa na Nachingwea.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, vijana wetu wataweza kupata elimu ya ujasiriamali utakaowawezesha kujitegemea badala ya kutegemea ajira kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ya mwaka 2012 – 2013, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, watoto wengi mashulenii na hata majumbani wanatendewa vitendo vya ukatili kinyume na mkataba wa Afrika wa haki na ustawi wa mtoto. Hata hivyo, wakati mwingine watoto hupewa adhabu kwa makosa yasiyokuwa yao. Mfano, mtoto kutokuwa na sare za shule au baadhi ya vifaa vya Shule kama vile madaftari, peni na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, makosa haya yanakuwa ni ya wazazi ambao wameshindwa kuwapatia watoto mahitaji ya Shule, lakini anayeadhibiwa ni mtoto ambaye hana uwezo wa kutafuta vitu hivyo. Wakati mwingine mtoto hupewa adhabu bila hata ya kupewa nafasi ya kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ingalie kwamba, haki na heshima ya mtoto inalindwa na watoto wasipewe adhabu kwa mambo ambayo yanawahusu wazazi au walezi wao. Kwa mfano, mtoto kutokuwa na ada ya shule, sare ya shule na michango mingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ni kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika ngazi zote za utekelezaji wa miradi na mipango mbalimbali ya maendeleo na kufaidika sawa katika maendeleo hayo.

Mheshimiwa Spika, je, ni katika miradi gani wanaume wamejengewa uwezo?

Mheshimiwa Spika, tatozo la mimba shuleni limeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Ukosefu wa chakula mashulen'i imeonekana kuwa mojawapo ya sababu zinazowaponza watoto wa kike kuanguka mtegoni kwa sababu ya mlo mmoja.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara kuitia Halmashauri za Wilaya zitenge fedha kwa ajili ya kugharimia utoaji wa chakula shuleni. Aidha, ujenzi wa mabweni katika Shule za Kata upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, napendekeza elimu ya afya inayohusu mabadiliko ya mwili ifundishwe mashulen'i ili wasichana waihofu wanapokabiliwa na changamoto ya mabadiliko ya mili yao. Wasichana wapate taarifa sahihi kuhusu afya zao, afya ya uzazi na pia wafundishwe nini matokeo ya kujamiihana katika umri mdogo.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya watoto nchini yanafanya kazi kubwa yakisaidiwa na Shirika lisilo la Kiserikali, *Save the Children*. Mafanikio haya ni pamoja na adhabu za viboko kufutwa mashulen'i, watoto wengi waliokuwa watoro kurudishwa shuleni, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kuna changamoto nyingi ambazo Mabaraza ya Watoto wanakutana nazo kama vile:-

(a) Shule nyingi za Sekondari hazina mabweni, jambo ambalo linasababisha wasichana kuingia katika tatozo la mimba za utotonii.

(b) Watoto wa jamii ya wakulima hutoroka shule na kwenda kufanya kilimo pamoja na wazazi wao. Baadhi ya watoto hutoroka shule kutokana na adhabu kali za viboko.

(c) Mabaraza ya watoto hukosa ushirikiano na Halmashauri zetu za Wilaya, pia watoto wa Mabaraza kutokuwa na vitambulisho ambavyo vitawapa urahisi wa kufanya kazi yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo mengine mengi, napendekeza kwamba Wizara itilie mkazo wa Mabaraza ya watoto kuanzishwa nchi nzima, na Mabaraza hayo yatengewe fedha za kutosha kujimarisha na kutekeleza shughuli za Mabaraza katika maeneo yao. Lakini pia hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale wote wanaokatisha masomo ya watoto wa kike kwa kuwapa mimba.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshuruku Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa kuchangia siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kwamba; kwanza, Wizara hii ingepatiwa bajeti kubwa zaidi ili kuweza kufanya kazi yao vizuri zaidi. Kutokana na upungufu wa bajeti, wanashindwa kutekeleza na kutoa elimu juu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Kwa sehemu kubwa, hata huko Wilayani, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, hawana vitendea kazi (usafiri wa vifaa muhimu kutolea mafunzo) na kubaki kuwa Ma-MC wakati wa sherehe. Tunashauri Wizara itoe maagizo na kufuatilia kwa kufanya ziara katika Halmashauri zetu na kubaini upungufu.

Mheshimiwa Spika, bado haki ya wanawake na watoto katika jamii yetu, sehemu nyingi ni tazito. Elimu zaidi ingetolewa juu ya suala zima ya maendeleo kwa kuweka haki sawa ya akina mama na watoto. Mahali ambapo wanawake wamepewa fursa ya kushiriki katika nafasi ya kupanga maendeleo na kupata fursa ya kupata uongozi, wanaonesha uwezo mkubwa na kuleta mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, leo hii hata katika nchi zinazoendelea na wa uchumi wa kati, wanawake viongozi wameweza kuleta mabadiliko makubwa. Nchi ambayo ina mfumo dume na mila zinazokandamiza wanawake, na watoto wa kike, pia wameweza kupata Viongozi Wakuu wa nchi mfano Indira Ghandi wa India, Benazir-Blutto wa Pakistan, Sheikh Hasina wa Bangladesh, pia mfano mzuri hapa kwetu nchini ni Mheshimiwa Asha-Rose Migiro – Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, tuna Mheshimiwa Anne Makinda – Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano Tanzania. Tunaomba elimu zaidi kwa jamii iendelee kutolewa juu ya uwezo na haki sawa.

Mheshimiwa Spika, kuna ukatili mbaya unaofanya dhidi ya wanawake na watoto, hasa watoto wenye ulemavu. Kuna mila potofu nyingi husababsiha ukatili huu kuendelea. Tunashauri elimu zaidi itolewe na pia katika Vituo vya Polisi pawe na Askari maalum kuwashughulikia wanawake na watoto wanaonyanyaswa, hatua kali zichukuliwe dhidi ya wanaofanya hivyo. Mfano, Wilaya ya Babati akina mama Kata ya Bashnet waliandamana na kujitolea kupambana na pombe haramu ya gongo. Wanaume kwa asilimia kubwa hawakuunga mkono pale mwanamke mmoja alipopigwa risasi ya mguuni. Kesi ilimalizwa kimila bila hatua za kisheria kufika mwisho.

Mheshimiwa Spika, tunashauri *NGOs* nyingi ambayo zinahudumia watoto zichunguzwe ili kubaini fedha wanayopokea na huduma wanayotoa, pia zile zinazota elimu kwa wananchi, wengi wao wanatumia vibaya fedha hizo na kuwa njia ya kujipatia fedha bila kufikisha kwa walengwa. Pia Serikali iangalie namna ya kuboresha vituo vya kulea watu wenye ulemavu na watoto.

Mheshimiwa Spika, Ustawi wa jamii, zina hali mbaya sana. Mfano ni kile Kituo cha Magogo – Kijiji cha Sarame, majengo yana hali mbaya, hakuna watumishi wa kutosha, vifaa na vitendea kazi hakuna, maji ni tatizo kubwa hapo. Tunashauri Vituo kama hivyo vyote vipewe vipaumbele, vikarabatiwe na viwe vya mfano. Ni sehemu ya sisi kujifunza ili badala ya kuwa na vituo vya kulelea watoto vinavyoota kama uyoga, basi vituo hivi viweze kulea watoto na vitakuwa na usimamizi wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, muhimu hapa ni elimu kwa jamii juu ya haki ya watoto na akina mama walemaru. Vile vile Maafisa Jamii wapatiwe vitendea kazi na uwezo wa kusafiri.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaomba bajeti longezwe.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, jamii yetu inategemea sana wanawake katika malezi ya familia. Mwanamke anapewa nafasi kubwa sana katika jamii hasa ya kiafrika. Mwanamke akielimishwa ni sawa na kuelimisha jamii nzima. Kwa hiyo, mwanamke ni lazima aheshimiwe katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto ambazo mwanamke wa Kitanzania hatendewi haki, kwa mfano, mwanamke kutopewa haki ya urithi hasa wa kurithi ardhi anapokuwa kaachika na

mume au akifiwa na mumewe; mwanamke kutopewa nafasi katika maamuzi ya kijamii katika familia; mwanamke kupigwa na mume; mwanamke kuachiwa familia akiachana na mume wake; na fidia ya kulipwa mwanamke akiwa amepigwa na mume.

Mheshimiwa Spika, hizi ndizo changamoto ambazo zinamkabili mwanamke wa kiafrika hata Tanzania. Naomba sheria iletwe hapa Bungeni ili tuweze kurekebisha baadhi ya sheria, ingawa wapo wanawake wengine wanawanyanya waume zao katika familia, kwa mfano, mwanamke kukataa kuchangia katika kujenga familia kifedha, wanasema ni jukumu la mwanaume kulea familia; na kuna wanawake wakipata madaraka wanawaacha waume zao kwa sababu ya kipato kikubwa anachopata.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kwamba mafunzo yatolewe kwa jamii nzima mume na mke kwa kujua sheria ya mama na mtoto; wanawake kuheshimiwa katika jamii zetu na watoto waheshimiwe ili waweze kusoma bila kunyanyaswa na jamii hasa kubakwa na wanaume.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda uchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wanawake wengi wanadhlumiwa haki ya kurithi, kwa sababu tu ya jinsia zao. Je, Wizara ina haja sasa ya kubadilisha au kutunga sera zitakazomwezesha mwanamke?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi kubwa la watoto wa Mitaani, na hakuna majengo ya kuwa-*accommodate* watoto hao. Je, kama Serikali imeshindwa, kwanini Wizara sasa isihamasishe moyo wa kujitolea kwa Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Wakuu, tugawane hawa watoto kwa kuwalea na kuwasomesha ili kupunguza tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo dhidi ya ukatili kwa wanawake. Kwanini hatua za makusudi hazichukuliwi ili kukomesha hali hiyo? Ukatili huo unajumuisha vipigo, kukataa ujauzito hali inayopelekea utoaji mimba holela, kutelekezwa pamoja na watoto na wa baba kwenda kuanza maisha mapya na kuanzisha familia mpya, kuchomwa moto na mengineyo. Nataka kujua ni lini Serikali itamaliza matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tatizo kwa watoto wanaishi na wanaume ambaio sio baba zao au wanawake ambaio sio mama zao, hivyo kupata mateso na wakati mwingu kushindwa hata kusoma.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na sheria kandamizi dhidi ya wanawake, kwa mfano, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1977, Sheria ya Mirathi, Sheria ya Fidia na Sheria ya Mahari. Nataka majibu, ni lini Serikali italeta Muswada huo Bungeni ili kurekebisha sheria hiyo?

Mheshimiwa Spika, shukurani.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kwa kumpongeza mama yangu mpenzi Mheshimiwa Waziri Sophia Simba na dada yangu mpenzi Naibu Waziri, Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu kwa kazi nzuri wanayoifnaya katika Wizara hii, kwa kukamilisha kwa mpango utakaowezesha Vuyo vya Maendeleo ya Wananchi vipatavyo 25 kutoa mafunzo ya ufundi stadi (*VETA*) kuanzia Januari, 2013. Pia kwa kutoa mafunzo kuhusu masuala ya jinsia kwa Watendaji katika ngazi mbalimbali za utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia kwa kuanzisha klubu za watoto mashulenii ambazo zitawapa fursa ya kuelimishwa na wataalam wa afya juu ya afya ya uzazi, mabadiliko ya kimwili na athari katika mahusiano ya kimpenzi katika umri mdogo. Mengi tu Wizara imefanya, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi, naomba sasa Wizara ijikite katika kuboresha mambo yafuatayo:-

Kwanza, sheria zilizopitwa na wakati kama Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi ambayo inawakandamiza wanawake na watoto wa kike. Pia watoto omba omba wamezidi Mitaani, naiomba Wizara iangalie suala hili kwa macho mawili. Jela na Mahakama za watoto, Wizara ishirikiane na Wizara nyiningine katika kuboresha Mahakama na jela za watoto.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Benki ya wanawake ifike Iringa na Njombe pia wanawake wapo.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Spika, watoto yatima Jimbo la Igalula wanahitaji misaada ya kujikimu na ada za Shule. Mbunge ninajitahidi kuwalipia, lakini uwezo ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa vikundi vyta akina mama bado ni kidogo sana ukilinganisha na mahitaji. Pia Elimu ya Ujasiriamali itolewe kwa vikundi hivi na mikopo ipatikane. Halmashauri hazipati asilimia tano kwa wanawake na asilimia tano kwa vijana. Naomba zinapatikane.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Igalula Wilaya ya Uyui halina Chuo cha Maendeleo ya Jamii. Tunaomba tujenge Chuo hicho kuharakisha maendeleo Jimboni na Wilayani kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za kupunguza na kuondoa unyanyasaji wa kijinsia, kuwe na nyumba za kuwasitiri wake kwa muda, wakati wa usuluhishi wa mgogoro baina ya mke na mume.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itafute vyanzo mbalimbali ili kujenga mabweni hasa ya wasichana katika Shule za Sekondri ili kuepusha mimba za utotoni. Wanafunzi wa kike wapewe utaratibu wa kumaliza masomo wapatapo ujauzito shulenii ili hasara isiwe mara mbili, elimu duni kwa mama na itaririka mpaka kwa mtoto.

**MHE. DKT. PUDENCIA KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania, wanawake wafahamishwe ni vigezo vipi viliviyotumiwa kuchagua Halmashauri 15 tu kupewa pesa za Maendeleo ya Akina mama? Kwa nini hazikupelekwa Halmashauri zote? Je, akina mama wa Tanzania wote wanafahamu jambo hili? Kama sivyo, akina mama watanufaika vipi na pesa hizi hasa wa vijijini ili waweze kunufaika na kujikwamua kiuchumi?

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuipongeza Wizara ya Maendeleo na Jinsia kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuandaa bajeti. Pongezi za kipekee kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya ukosefu wa fedha na bajeti ndogo wanayopewa.

Mheshimiwa Spika, katika hoja hii, nitachangia juu ya mali za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ambazo ni majengo yake ya *Community Center* yaliyokuwa yanatumia kwa kiliniki za wanawake na watoto na mambo mbalimbali ya kijamii. Nitafurahi nikisikia majengo yote yamerejeshwa mikononi mwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Vyuo vya *UMATI* naomba viangaliwe, vinatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ione umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria kandamizi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Vyama vya Siasa visaidie kukubali kuweka suala la usawa wa jinsia kama kigezo muhimu cha uendeshaji wa shughuli zote za Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale kina mgogoro, naomba Wizara imalize mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba maazimio ya kimataifa na Mikataba ya Kimataifa ambayo hatujairidhia, iletwe ili iridhiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana, naiomba Serikali kupitia Wizara hii iongeze bajeti ili iweze kukabiliana na changamoto ambazo zinaikabili Wizara hii, kwani pindi kikiboreshw, itawasaidia sana akina mama walio wengi ambaa ndio wengi katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwanza hawatoshi na walipo wahawajibiki ipasavyo, kwani wengi wao wako maeneo ya Mijini tu. Kwa hiyo, naomba Serikali ilekeze nguvu maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto yatima, lazima Serikali iandae mpango mkakati wa mazingira mazuri ya kutenga fedha kwa ajili ya kuanzisha Vituo vya Watoto yatima. Eneo hili ni muhimu sana, kwani bila kuwa na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi watoto hawa tutakuwa na watoto wengi wa Mitaani.

Mheshimiwa Spika, wale la akina mama wanaonyanyaswa kwa tuhuma za uchawi ni vyema ikatoa elimu kwa jamii ili iwe na ufahamu wa kuwaenzi hawa akina mama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kwa kuwa inahusu watu wote, yaani wanawake, watoto na wanaume.

Mheshimiwa Spika, naona Wizara hii inanyanyapaliwa, hata ukiangalia bajeti inayotengewa, inapungua mwaka hadi mwaka. Pia hata ukiangalia wanaochangia kwa mdomo hapa Bungeni, wengi ni Wabunge wanawake. Labda wengi hawajui uhusiano wa Wizara hii na jinsia. Hivyo nashauri elimu itolewe kwa mkazo zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la watoto mitaani linaongezeka na linaongezeka kwa sababu mojawapo, sheria haizijaboreshw na kusimamiwa, kwa kuwa baadhi ya wazazi hasa wanaume wengi wametelekeza familia zao na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo cha Ifakara ni cha muda mrefu na hakijaboreshw na wananchi wameongezeka ingawa miundombinu ya Chuo haijaongezeka. Hivyo nashauri kipewe fedha za kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu kuhusu UWT, uhusiano wake na wanawake wa Tanzania ukichukulia sasa kuna mfumo wa Vyama Vingi. Naomba jina libadilishwe.

**MHE. FAITH M. MTAMBO:** Mheshimiwa Spika, nianze kuunga mkono hoja katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wanawake na Watoto. Napenda kutoa mchango kama vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado kasi ni ndogo katika kuwawezesha akina mama. Naomba Wizara iwawezeshe akina mama kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwawezesha mikopo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake bado haisaidii sana akina mama wenyewe vipato vidogo, kwa kuwa kuna urasimu mkubwa kupata mikopo kwa ajili ya vikundi nya akina mama au mama mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, hebu Benki ilegeze masharti ya kuwawezesha akina mama kupata mikopo kwa ajili ya kufanya miradi yao na tutakuwa tumewasaidia kujikwamua kimaisha.

Mheshimiwa Spika, wanawake wajane, watoto yatima na kadhalika, bado Wizara ina kazi kubwa kwa ajili ya kuweka vyema mazingira ya watu hawa katika jamii, hasa kuwawezesha kufanya miradi, kusomesha watoto ambao hawana uwezo au yatima, na inapotokea masuala ya mirathi, wapewe haki zao na stahili zao wanazostahili. Kuna uonevu mwangi katika hilo, Wizara iendelee kuangalia hili.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Maendeleo ya Jamii katika vijiji na ngazi za Kata na Tarafa ni muhimu kuwepo. Wizara iliangular hilo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya kufanya hesabu kabisa kabisa za namna gani inakuwa, sasa lazima nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika 20.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama katika Bunge lako Tukufu katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Niwatakie Waislamu wote wanaoshiriki ibada hii muhimu *Ramadhani Mubarak Inshallah Mwenyezi* Mungu atutakabalie swaumu zetu na azikubali toba zetu. Amina.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pole kwa ndugu, jamaa na marafiki waliopoteza wapendwa wao katika ajali ya meli iliyotokea Zanzibar wiki iliyopita.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kuniamini kuitumikia Wizara hii kama Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Sophia Simba kwa kuniongoza vyema, Katibu Mkuu Bi Kijakazi Mtengwa, Naibu Katibu Mkuu Bi Anna Maembe, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa kusimamia na kuliongoza vyema Bunge letu, kwangu naamini kwa wanawake na wasichana wengi hapa nchini utaendelea kuwa mfano mwema kwetu na alama ya kudumu ya ushindi wa haki na maendeleo ya wanawake hapa Tanzania na Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, umekuwa ukinishauri, ukinlongoza, ukinipa moyo, nakushukuru sana wewe ni mama na ni zaidi ya mama kwangu. Lakini pia niwashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao mzuri kwangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wanawake wanachama wa UWT, Mkoo wa Tanga ndio walioniwezesha kuwemo katika Bunge lako Tukufu. Hivyo, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru kwa ushirikiano mkubwa wanaendelea kunipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Naahidi kuendelea kushirikiana nao katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wanawake, watoto na wananchi wa Mkoo wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, familia yangu imeendelea kuwa mhimili mkubwa wa utendaji mzuri wa kazi zangu. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru mume wangu mpenzi Paskal Kasi kwa kunitia moyo mara kwa mara ili kufanya vizuri katika kazi zangu, lakini pia kwa imani na uvumilivu wake mkubwa kwangu hasa wakati wote ninapokosekana nyumbani kutokana na shughuli za ujenzi wa Taifa. Namshukuru sana pia kwa kutoa mchango mkubwa sana katika malezi ya watoto wetu Faith na Ayana.

Mheshimiwa Spika, wazazi wangu Mzee Makwaya Ally Mwalimu na Bi Mzuri Adhio, nawashukuru sana kwa kunitia moyo, kunishauri na kwa kuzielekeza dua zao za kila siku kwa Mwenyezi Mungu kwangu, lakini pia kwa kunijengea msingi mzuri wa maisha yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto aliyoiwasilisha leo hii hapa Bungeni kwa kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Majibu yangu yatalenga hoja zilizoelekezwa katika eneo la Maendeleo ya Jamii. Wabunge wengi wamezungumzia sana eneo ambalo kwanza nitapenda kuliongea, kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Wabunge waliochangia hoja hii ni wengi akiwemo Mheshimiwa Antony Mbassa, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Lwenge na Mheshimiwa Felix Mkosamali.

Mheshimiwa Spika, hapa kuna hoja mbili ambazo zinakinzana zimetolewa katika michango ya Wabunge. Wabunge wengine wanasema kwamba hivi vyuo viko katika hali mbaya, kwa hiyo havifanyi kazi vizuri, inabidi tubadilishe matumizi yake. Lakini kuna Wabunge wengine wamesema vyuo hivi vinahitajika sana kuwapatia vijana wetu stadi za kuwawezesha kujiajiri kwa hiyo tuviongeze katika Wilaya nyingine zaidi. Kwa hiyo nataka kutoa msimamo wetu kama Wizara na kama Serikali.

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba ni kweli Vyuo vyetu vya Maendeleo ya Wananchi viko katika hali mbaya, baadhi sio vyote na historia ni kwamba, hivi vyuo vilianzishwa mwaka 1975 ikiwa ni sehemu ya Elimu ya Watu Wazima na lengo lake kubwa limekuwa ni kutoa maarifa na stadi za maisha kwa wananchi mbalimbali kwa ajili ya kuweza kujitatulia changamoto mbalimbali zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, nikuthibitishie tu, lakini katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita Wizara imefanya kazi kubwa sana ya kuhakikisha hivi vyuo tunaviboresha, viko vyuo 55. Ili kuonesha kwamba tumefanya kazi kubwa sana ingawa bado hatujaweza kupata fedha nyingi za kutosha, ukisoma Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vimewekwa pale kama sehemu ya vipaumbele vya Serikali katika eneo linaloitwa *Human Capital Development*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunakubali kwamba ndio, baadhi ya Vyuo viko kwenye hali mbaya, lakini tutaendelea kuviboresha na ili kuonesha kwamba vina umuhimu mkubwa hasa katika karne hii ambapo vijana wengi wanamaliza elimu ya darasa la saba na wanakosa nafasi ya kuendelea sekondari tumeweza kupata fedha kutoka CIDA, Canada ya kuboresha vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi na Waheshimiwa Wabunge ambao watapenda kujua ni vyuo gani ambavyo tutaanza navyo kwa mwaka huu tutawapatia hiyo taarifa.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nijibu ambalo watu wanasema havitumiki tubadilishe matumizi. Ni kwamba mwaka 2010 aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi aliunda Kikosi Kazi cha Wataalam mbalimbali pale Serikalini kwa ajili ya kutazama kama je, vyuo hivi bado vinahitajika au havihitajiki. Kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wanataka viwe Vyuo vya Elimu, wengine wanataka vifanywe Vyuo vya Kilimo, lakini ile stadi ambayo ilifanyika mwaka 2010 imethibitisha kwamba vyuo hivi bado ni muhimu sana na inabidi tuendelee kuviboresha ili kuweza kutoa au kufanya kazi ile ambayo imekusudiwa kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano niipongeze Halmashauri ya Monduli wao wameona kuna umuhimu wa kuwa na hivi Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi baada ya kwamba kile Chuo cha Monduli tulikipandisha hadhi na kuwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii wakaamua Halmashauri

yenye we kutafuta Chuo pale Mto wa Mbu, kinatoa mafunzo ya Maendeleo ya Wananchi. Lakini pia na Halmashauri ya Nandembo pia wameweza kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ambalo limelalamikiwa ni uhaba wa wataalam na vitendea kazi vya kujifunzia na kufundishia na uchakavu wa majengo. Lakini kama nilivyosema tutaanza na vyuo 25 kwa kutumia hiyo fedha ya *CIDA* Canada, lakini pia katika bajeti yetu kuna baadhi ya vyuo ambavyo pia tutavirekebisha. Mtanisamehe Wabunge ni wengi sana walioongelea kuhusu Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Lakini kwa ufupi tayari vyuo 38 sasa hivi ukitembelea hali kidogo inaridhisha si kama ile hali ya zamani.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ambayo napenda kuizungumzia iliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni suala la Maafisa wa Maendeleo ya Jamii katika Kata na wanaauliza wengine ni Kata ngapi nchini ambazo hazina Maafisa Maendeleo ya Jamii. Hili limeulizwa na watu wengi Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mheshimiwa Phillipa Mturano, Mheshimiwa AnnMaryStella Mallac, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Goodluck Ole Medeye, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Gosbert Blandes.

Mheshimiwa Spika, kama hotuba ya Mheshimiwa Waziri asubuhi iliyooonesha mpaka sasa hivi ni asilimia 58 ya Kata ambazo hazina Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Kata, lakini Sera yetu ya Maendeleo ya Jamii inaelekeza angalau awepo mtaalam mmoja, Afisa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata. Kwa hiyo changamoto iliyokuwepo sio ukosefu wa wataalam, vyuo vyetu kwa mfano katika mwaka 2011 vimetoa jumla ya wataalam 1,820, kwa hiyo tatizo lillokuwepo ni uchache wa nafasi za ajira kwa wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu na nyie ni Madiwani, mnashiriki katika vikao vya Halmashauri, tunawaomba mtusaidie sana katika kuhakikisha kwamba Halmashauri wanaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata, lakini niupongeze Mkoa wa Dar es Salaam kwa sababu wao Halmashauri zao zote ndizo zenye Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Kata zote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Josephine Genzabuka aliuliza ni Wilaya ngapi zina Maafisa Maendeleo ya Jamii? Wilaya zote zina Maafisa Maendeleo ya Jamii, changamoto yetu hii kubwa ni kuhakikisha kwamba tunawapeleka katika ngazi ya Kata. Sitaki kueleza umuhimu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, lakini wote tunaelewa kwamba wao ndio wapiga debe wakubwa, wahamasishaji wakubwa na wao ndio kila kitu.

Mheshimiwa Spika, unaweza kuwa na mipango mizuri sana ya kilimo, maji, afya, lakini kama hutokuwa na mtu ambaye atakwenda kule kuongea na wanakijji, kuwapa hamasa, kuwapa moyo na kuwaelimisha umuhimu wa mipango mbalimbali, basi ina maana hatutawenza kufanikiwa malengo ya mipango yetu mingine. Kwa hiyo, suala hili ni muhimu na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Pinda alishatoa agizo mwaka 2008 kwamba Halmashauri zihakikisha kwamba zinaajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kila Kata.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo katika Idara hii ya Maendeleo ya Jamii ni suala la kuimarisha Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri zetu. Hili limeongelewa na Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na baadhi ya Wabunge. Ni kweli wanasema kazi yetu ya Wizara ni nini? Kazi yetu ya Wizara ni nini mbona tumeacha ile Idara ya Maendeleo ya Jamii kama watoto yatima hawana baba, mama na wala fedha na hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kazi yetu ni kuandaa miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa sera katika Halmashauri. Pia kazi yetu kubwa ni kuhakikisha kwamba wataalam hawa wa Maendeleo ya Jamii wanapatikana katika Halmashauri mbalimbali, lakini pia kuwajengea uwezo na kuweka mazingira wezeshi ili waweze kufanya kazi mbalimbali. Sasa anayeajiri Maafisa Maendeleo ya Jamii na kuwapangia fungu ni wenzetu wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, lakini tunawashukuru sana ingawa watu wanalamika kwamba hii Idara haina fedha kuanzia mwaka 2008, Serikali kwa kupitia TAMISEMI imeweza sasa kuweka fungu maalum la bajeti kwa ajili ya Idara ya Maendeleo ya Jamii. Kwa mfano, mwaka 2008/2009, Serikali iliipangia Idara hii ya Maendeleo ya Jamii shilingi milioni 3.6, ukitoka sifuri, si haba *Mashallah*, lakini mwaka 2009/2010 imeongezeka ile bajeti imekuwa milioni 7.2, mwaka 2010/2011, bajeti imepanda mpaka shilingi milioni 10.8.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni kweli kwamba bado Idara hizi za Maendeleo ya Jamii hazina fedha, lakini mnaona *trend* ya Serikali katika kuhakikisha kwamba inazifanyia kazi. Kwa hiyo, tutawaomba Waheshimiwa Wabunge, narudia tena kwa sababu nyie ni Madiwani pia katika Halmashauri, mtusaidie basi mnapokaa katika vikao vya Baraza la Madiwani kuhakikisha kwamba, Maafisa hao wa Maendeleo ya Jamii wanapangiwa kazi, wanapewa vitendea kazi vikiwemo baiskeli, pikipiki na gari kwa ajili ya kuwafikia wananchi na pia kwa ajili ya kuwaendeleza kielimu. Yaani wamekuwa ni kama vile *spea tyre* watu wanasma, leo mtu wa UKIMWI ana mradi anamchukua Afisa Maendeleo ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, kesho mtu wa kilimo ana mradi anamchukua, matokeo yake sasa mwisho wa siku anaonekana mtu wa Kitengo cha Maendeleo ya Jamii hana kazi anayofanya, kwa sababu ye ye kazi yake anakimbia kimbia tu kila sehemu yupo. Kwa hiyo, tutaomba mtusaidie wakati mnaptisha zile bajeti za Halmashauri mhakikishe hasa Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa Viti Maalum, Idara hii ambayo ndio inahusika na Wanawake na Watoto fedha kiasi gani imepangiwa, ni vipaumbele gani vitatekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Tutawashukuru sana kama mtusaidia kwa hilo. Hayo ni makubwa matatu ya ujumla ambayo nilitaka kuyaongelea kwa kuyapa msisitizo.

Mheshimiwa Spika, sasa niende katika hoja binafsi zilizoongelewa na Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa anasema Chuo cha Rungemba tangu kimepandishwa hadhi, kwa nini kimepandishwa hadhi badala ya kutoa yale mafunzo ambayo yalikuwa yametolewa. Ni kweli tumepandisha hadhi chuo hiki, sasa hivi kinatoa taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Stashahada na baadaye Stashahada kwa wanawake. Lakini tutazingatia ushauri ambao umetupa wa kuanzisha mafunzo ya taaluma hii katika ngazi ya Shahada mara tu taratibu zitakaporuhusu.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja hii ya Mheshimiwa Mgimwa sasa inakuja na hizi ambazo tunasema *contradictions*. Kuna wengine wanadhani hivi vyuo tuvibadilishe matumizi, lakini kuna wengine wanasma tuviache. Lakini sisi msimamo wetu ambao tutaendelea nao ni kwamba, bado vyuo hivi ni muhimu sana especially kwa mujibu wa takwimu za (*BEST Basic Education Statistics in Tanzania* kama unakuwa na wanafunzi laki tano kila mwaka wanaomaliza darasa la saba na hawako katika shule za sekondari za Serikali wala za binafsi wala Vyuo vya VETA ina maana hawa watoto wanakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni muhimu sana hivi vyuo vikaendelea kuwepo, lakini ambacho tumelisema na tumeliamua, viendelee kufanya mafunzo ya Maendeleo ya Wananchi, mtu yoyote ambaye kama hajasoma, unajua kusoma, hujui kusoma, utakwenda pale, wanawake watakwenda kujifundisha masuala ya kunyonyesha mtoto vizuri, masuala ya ukaushaji wa chakula, masuala ya kuhifadhi chakula cha mtoto, lakini sasa tumeamua kwamba sambamba na kutoa mafunzo ya Maendeleo ya Wananchi vitatoa pia mafunzo ya VETA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuanzia Januari mwakani, Vyuo 25 vitachukua wanafunzi 50 kwa ajili ya mafunzo ya VETA. Kwa hiyo hii ni changamoto ambayo inatukabili na kadri muda utakavyokwenda tutafanya tathmini tuamue, tena nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu aliniambia siku moja kuhusu kile chuo chake kule Katavi. Kwa hiyo, tutaamua haizuiwi kufanya mafunzo ya Maendeleo ya Wananchi, lakini pia tunaweza tukafanya na mafunzo mengine ya Nyuki, mafunzo ya asali na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa wengine wameongelea kuhusu mitaala isiyoendana na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Nyambari ameongea, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, kwamba mafunzo yetu hayazingatii mabadiliko ya

Sayansi na Teknolojia na fani zinazofundishwa zimepitwa na wakati. Nakubali kuna baadhi ya vyuo ni kweli fani zimepitwa na wakati kwa mfano unakuta watu wanasuka ukili, lakini inategemea ukili nao ni biashara nzuri sana na sasa hivi unalipa. Kwa hiyo, niseme fani zote zinavyofundishwa sasa hivi vyuoni zinatokana na mahitaji halisi ya wananchi ambao wanakaa katika eneo husika. Tumeanzisha fani nydingine 47 mpya ili kuhakikisha kwamba tunakwenda na wakati.

Mheshimiwa Lukvi aliongelea suala la Chuo cha Maendeleo ya Jamii Pawaga. *Of course* ametoa ushauri kwamba tukawaone *TANAPA* na tushirikiane kukijenga. Kwa hiyo ushauri tunauzingatia, lakini kabla ya kengele ya pili hajjanililia niseme ambalo kubwa nalo limeongelewa na Waheshimiwa Wabunge ni suala la mwanamama ambaye amenyang'anywa mtoto, limeoneshwa katika vyombo vya habari *ITV, East African Television*.

Mheshimiwa Spika, kama Mwanasheria suala hili liko Mahakamani, kwa hiyo huo ndio ukweli AG atanisaidia, liko Mahakamani, lakini niseme mimi kama mtetezi wa Haki za Wanawake na Watoto, kama Wizara tunaamini kwamba Mahakama kwa sababu leo ndiyo ilikuwa itolewe *ruling*, lakini itatolewa kesho. Kwa hiyo, nitakachosema kikubwa tunaamini Mahakama itasikiliza hili shauri na kulitolea uamuzi kwa kuzingatia kanuni za haki za mtoto. Sheria ya Mtoto inasema maamuzi yoyote Mahakama chombo au taasisi yoyote inayofanya ni lazima izingatie *principle* moja, tunasema *best interest of the child*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naamini na nawaomba Waheshimiwa Wabunge tusubiri mpaka kesho *ruling* itakapotoka kama bado litakuwa limeleta maneno sisi tunafuatilia. Pia tunadhani kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Maafisa Ustawi wa Jamii wao ndio walitakiwa wafungue kesi wapeleke maombi kwa Mahakama kwamba huyo mama hayuko sahihi kwa ajili ya kumnyonyesha mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani ni kitendo kibaya cha kumnyang'anya mama mtoto wake wa miezi minne. Lakini kwa sababu shauri liko Mahakamani, naomba tuache Mahakama ifanye kazi yake, lakini naamini kesho *ruling* itakapotoka Mheshimiwa Hakimu atafanya maamuzi kadri ya Sheria ya Mtoto inavyoolekeza.

**SPIKA:** Mbona kuna mazungumzo mengi yasiyokuwa rasmi. Naomba tumsikilize anayeongea tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, huu ndio msimamo, kanuni za Bunge zinasema.

**SPIKA:** Mheshimiwa yaliyoko kwenye Mahakama yako Mahakamani *full stop*.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nadhani ni hayo makubwa ambayo nilitaka kuyaongelea na kwa kumalizia niseme tu Mheshimiwa Waziri atajibu hoja nydingine, lakini ambalo nimalizie kwamba ujenzi wa Vyuo vya Maendeleo vya Wananchi kwenye Wilaya zisizo na vyuo tunaomba nyie wenyewe mkakae kwenye Halmashauri husika kama mnadhani hivi vyuo ni muhimu basi mtaamua viwepo au visiwepo.

Mheshimiwa Spika, sitaki kupigiwa kengele ya pili baada ya kusema hayo machache nakushukuru sana na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri, kwa maoni na kwa msaada mkubwa ambao wanani patia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita mtoa hoja aweze kujumuisha mazungumzo yetu.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema na utukufu kwa kuniyalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Naomba nichukue fursa hii kwa mara nydingine kumshukuru kwa dhati

Mheshimiwa Rais kwa imani yake aliyeonesha kwangu. Naahidi kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kuendelea kutekeleza majukumu niliyopewa kwa kushirikiana na watumishi wenzangu na wadau wengine wote ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ushauri na maelekezo ambayo wanaendelea kutupatia. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha nakushukuru kwa kuongoza majadiliano wakati Waheshimiwa Wabunge wakichangia. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Naibu Waziri wa Wizara yangu kwa ushirikiano mkubwa anaonipa wakati wote na pia kwa kujibu hoja nyngi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kuzungumza au kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Wabunge wa Kamati hiyo kwa ushauri na maelekezo ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuishukuru sana familia yangu watoto wangu na ndugu zangu bila kumsahau ndugu yangu wa hiari, Mheshimiwa aliyekuwemo humu zamani, mzee wangu Kitwana Kondo kwa mapenzi makubwa ambayo ananionesha wakati wote nikiwa kazini na kwa ushauri akiwa kama mwanasiasa mahiri, amekuwa mshauri wangu siku zote pamoja na kwamba hali yake imedhoofika kidogo. Namshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia bajeti yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimirambue Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Pia nimirambue na kumshukuru Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ambaye amewakilisha Kambi Rasmi kwa maoni na michango yao mizuri ambayo naamini kabisa itatusaidia katika kuboresha maendeleo ya jamii nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda niwatambue Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza kwanza nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Daktari Getrude Rwakatare, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhammed, Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Christina Mughwai. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda niwatambue Wabunge waliochangia masuala ya maendeleo ya jamii katika hotuba ya mjadala wa bajeti ya Waziri wa fedha na Waziri Mkuu nao walikuwa Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Suleiman Masoud Suleiman, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Daktari Antony Mbassa, Mheshimiwa Abdullah Haji Ali na Mheshimiwa Namelok Moringe Sokoine.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi ambao wanafika 89, nao ni kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Pamoja na hao uliowataja.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na hao niliowataja. Wa kwanza ni Mheshimiwa Chacha Nyangwine, Mheshimiwa Joyce Mukya,

Mheshimiwa Cecilia Pareso, Mheshimiwa Anna MarryStella Mallac, Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Hussen Mussa Mzee, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Deogratias Ntukamanzina. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Sulemani Jafo, Mheshimiwa Daktari Fenella Mukangara, Mheshimiwa Rachel Mashishanga, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Philipa Mturano, Mheshimiwa Muhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Amina Andrew Clement, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Rita Kabati, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah Mohamed na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Joseph Selasini, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mheshimiwa Goodluck Ole Medeye, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Jitu Soni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile wengine ni Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa William Lukuvi, Mheshimiwa Moza Abeid Said, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kahigi, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mheshimiwa Ignas Malocha, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Asha Nshimba Jecha, Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba, Mheshimiwa Augustine Prema, Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi na Mheshimiwa Joshua Nassari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia wengine ni Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Zarina Madabida, Mheshimiwa Daktari Titus Kamani, Mheshimiwa Abdallah Juma Sadala, Mheshimiwa Pereira Silima, Mheshimiwa Daktari Pudenciana Kikwembe, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Athuman Mfutakamba, Mheshimiwa Christina Mughwai, Mheshimiwa Hamoud Abuu Juma, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Josephat Kendege na Mheshimiwa Henry Shekifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hao ndiyo waliochangia na kama ilivyoonekana ni walikuwa wengi sana, kwa hiyo itawezekana kabisa wakati nikijibu nikayajibu kwa ujumla, lakini mengi yalizungumzia kuhusu ufinyu wa bajeti masuala ya watoto, ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Kwa ujumla tukubali kwamba, mambo mengi yanahusu mila na desturi na mazoea ambayo tuliyonayo.

Mheshimiwa Spika, masuala haya tukubaliane pia Sheria peke yake bila ya jamii kubadilika itakuwa vigumu na kwamba sisi tukiwa kama Wabunge tunapokuwa katika mikutano yetu tuwakumbushe masuala ya ubaya wa ukatili dhidi ya watoto na wanawake. Sheria zinazolinda mtoto zipo lakini bado hali sio nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba hali sio nzuri, lakini tunafarijika kuona sasa hata mtoto akipigwa nyumbani kwao mtu wa jirani anahamasika kwenda kumshtaki. Kwa hiyo, jamii kwa ujumla sasa inaona ukatili dhidi ya watoto na ukatili dhidi ya wanawake pamoja na ukatili dhidi ya wanaume hautakiwi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti, nashukuru sana Wabunge wengi wamelizungumzia hilo lakini ukweli bajeti yetu imekuwa finyu kila mwaka, lakini yote hii inatokana

na umuhimu wa mambo. Kuna mambo mengine yana umuhimu zaidi pamoja na kwamba mambo ya watoto yana umuhimu lakini sungura mdogo tuliye naye jinsi tunavyogawana inatokea kwamba Wizara yetu inakuwa haipati kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Spika, lakini kutokupata kiasi cha kutosha tunaamini kabisa kule kwenye Wilaya na Mikoa ambako wapo Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao ndiyo wanatekeleza sera za Wizara yangu kule wakipatiwa rasilimali fedha na vifaa vya kufanya kazi haya yote ambayo tunayasema yataweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kuna tuhuma moja ambayo imetolewa kwamba, Waziri wa Maendeleo ya Jamii amemtelekeza mgonjwa. Yule mama ambaye aliteswa na mumewe kwa kugongwa na gari na kuburuzwa na hivyo alikuwa mahututi Bugando Hospitali.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri tu nilipotoka Bungeni wale wenye mgonjwa wao walipiga simu na kusikitika sana kwa sababu nilikuwa nao karibu mpaka dakika ya mwisho mgonjwa yule anakufa na nilikuwa mmoja wa watu wa kwanza kupigiwa simu kutoka hospitali. Taarifa za mgonjwa huyu zilitokea mara ya kwanza kwenye TV na kwenye magazeti na bahati nzuri nilikuwa Musoma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikwenda Polisi Bunda nikaauliza na nikaambiwa utaratibu unaofanya kumtafuta yule mtuhumiwa. Ukweli mtuhumiwa amekimbia, gari lake limekamatwa na ndugu yake yupo ndani anaisaidia Polisi.

Mheshimiwa Spika, mara nydingi nimekuwa naongea nao kwa sababu niliguswa sana na udhalimu huu uliotendeka, ndiyo maana nimekuwa nikilifuatilia. Kwa hiyo, si kweli kwamba nimewacha. Nimekwenda kumwona katika hospitali ya Bugando, kitu ambacho si cha kawaida, Waziri kumwona kila mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, Kila anayepigwa na mumewe nimfuate, sina uwezo huo wa kufanya hivyo. Lakini kwa huyu *specifically* nilikwenda hospitali ya Bugando nikamwona, nikaongea na Madaktari na nikatoa na msaada wangu mdogo wa kusaidia madawa. Wenzangu waliokuja kunilaumu hapa na wao kama wameguswa wangesema wamefanya nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naona hilo halina mjadala zaidi isipokuwa wao wenye wapo na gazeti la kwanza lilitoripoti liliikuwa la Majira na litiripoti vizuri sana jinsi nilivyolishughulikia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee na nianze kwenye masuala ya jinsia. Kamati ilizungumzia kuhusu kuongeza uwakilishi wa wanawake katika nafasi za uongozi na vyombo vya maamuzi. Wizara inakubaliana nayo na tunasema tuko...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mtu akiwa anaongea huwa tunanyamaza, hapa si mahali pa kuongea.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, katika Mabadiliko ya Katiba nawashauri wanawake na wanaume wote kwa pamoja tuzungumzie hili la kufikia  *fifty, fifty* katika nafasi zote za uongozi na za uwakilishi. Sisi tuna nafasi sasa hivi ya kuzungumzia  *fifty, fifty* sio humu Bungeni, lakini pia katika ile Tume inayopita. Kwa hiyo, hili nakubaliana na Kamati kabisa.

Mheshimiwa Spika, lingine liliikuwa linasema kwamba Kamati inaombwa Serikali kufanya utafiti wa kina kwa lengo la kujua chanzo cha kupungua kwa watoto wa kike wanaojunga na elimu ya juu na namna ya kuondoa tatizo hilo ili kuleta usawa wa kupata elimu. Masuala haya yanaendelea na kwamba Wizara ya Elimu inayafanya kazi, lakini kwa kiwango kikubwa sasa hivi tuna wasichana wengi zaidi katika elimu ya juu kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Mtakumbuka kuna wakati mpaka Serikali iliweka vigezo rahisi zaidi vya wanawake kuingia kwenye vyuo vikuu. Lakini

sasa baada ya kuona wanawake wanaweza vile vigezo vimepunguzwa. Kwa hiyo, hili linafanyika na nashukuru sana kwa hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imezungumzia Sheria ambayo inamkandamiza mwanamke ambapo pia zimezungumziwa na wengi. Masuala ya Sheria Kandamizi tumeyaona umuhimu wake na juzi Wabunge jana tulikuwa na semina naamini mmeyaelewa vizuri na nilijua hapa yataulizwa. Kwa hiyo, nitayajibu kwa pamoja hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Aggrey Mwanri na Mheshimiwa Joseph Selasini walitaka kujua taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2011, Serikali ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 88 kwa wanawake kupitia Halmashauri zao. Wanauliza ni Halmashauri zipi. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba Halmashauri 16 zilipata fedha kwa mwaka 2011 Halmashauri hizo ni Njombe, Makete, Liwale, Babati Vijiji, Bunda, Mbozi, Ruangwa, Geita, Rufiji, Bagamoyo, Mpanda, Manispaa ya Songea, Pangani na Manispaa ya Tanga.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuwafahamisha kuwa utumaji wa fedha katika Halmashauri unategemea na Halmashauri zenyewe kurejesha kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kama Halmashauri haitarudisha zile ambazo zimetolewa Wizara haitopeleka. Kuna uwajibikaji kwa upande wa Halmashauri kwamba, lazima na wao watoe ile asilimia yao lakini na zile ambazo sisi tunatoa lazima zirudishwe na wakirudisha, tunawarudishia zile na tunawapa mara mbili yake. Kwa hiyo, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge inapotokea masuala ya mfuko wa WDF suala kubwa ni nidhamu ya marejesho kwa wale ambao wamepewa pesa hizo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na wengi ni kuhusu huduma ya Benki ya Wanawake. Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii imezungumzia, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Felister A. Bura amezungumzia hilo, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazina, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine na Mheshimiwa Joseph R. Selasini wote walilizungumzia hilo.

Mheshimiwa Spika, Benki imeandaa mpango mkakati wa miaka minne (*Cooperate Strategic Business Plan*), Mkakati huo unaainisha namna benki hii itakavyojipanua na kukuza mtaji wake. Naomba wote tukumbuke kwamba ilianza na mtaji mdogo na huu muda uliokuwepo ni mfupi, mpango huu umeainisha haja ya benki kujitanua na kuwafikia wananchi wote wa Tanzania kwa kufungua tawi na vituo vya mikopo nchi nzima kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza benki inatarajia kufungua matawi katika eneo la Kariakoo, Dar es Salaam na vituo vya utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo, katika Mikoa ya Mwanza, Dodoma, Mbeya na Iringa. Kuhusu kuongeza mtaji wa benki, Serikali itaendelea kutoa shilingi bilioni mbili kila mwaka kuanzia mwaka 2010 hadi 2015 kama utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete aliyoitoa siku ya maadhimisho ya wanawake duniani iliyoonyika Kitaifa katika Mkoa wa Tabora mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha benki imedhamiria kutafuta mtaji kwa kuza hisa kwa wananchi wote wa Tanzania, ili kufanikisha suala hili la uuuzaji wa hisa, benki imeshakamilisha mchakato wa kuibadilisha Katiba ya Kampuni *Memorandum and Articles of Association* ili kuifanya iwe kampuni ya umma na siyo binafsi kama ilivyo sasa. Sasa inajulikana kama Tanzania *Women's Bank Public Limited Company*.

Mheshimiwa Spika, tuna imani kwamba, sasa mchakato wa uuuzaji wa hisa za benki kupitia soko la mtaji utaendelea kwa kasi na mara uuuzaji utakapoanza wananchi wakiwemo Wabunge watahamishwa kuchangamkia fursa hii ya kumiliki hisa.

Mheshimiwa Spika, ningependa nichukue nafasi hii pia kuwahamisha Wabunge jinsi tutanunua hisa ndiyo jinsi benki hii itaweza kutanuka na kwenda maeneo mengine. Kwa wale ambao tuliweka *deposit* ya hisa zile zitatambulika, pale mwanzo Wabunge tulichanga pesa ili kuwezesha uanzishwaji, ilikuwa kama ni *deposit* tu, lakini zile hisa zao bado zitachukuliwa *into account* wakati wa uuuzaji wa hisa hizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia inataka kujua ni wanawake wangapi wamefaidika na mikopo ya vikundi ya benki ya wanawake na walipata shilingi ngapi. Benki ya Wanawake toka kuanzishwa kwake hadi Juni 2012 imeshatoa mikopo kwa vikundi 190 vya wajasiriamali yenye thamani ya shilingi bilioni kumi na milioni mia mbili na tisini.

Mheshimiwa Spika, idadi ya jumla ya wanufaika wa mikopo hii ni watu elfu sita mia nne ishirini na saba ambao kati yao wanawake ni 5,270, sawa na asilimia 82 ya wanufaika wote na wanaume ni 1,157, sawa na asilimia 18. Ningependa kuwashauri wanaume wajitokeze zaidi na wao kutumia benki hii ili iendelee kukua.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni dhahiri kuwa wanawake ndiyo wanufaika wakubwa kwa mikopo hii ya benki kwa sababu wanaume hamjitokezi, kwa hiyo tafadhalini tunaomba mfike.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ntukamazina, Mheshimiwa Ole-Medeye na Mheshimiwa Amina Abdulla Amour wote wanasema kwamba, ni muhimu Benki ya Wanawake kutoa elimu ya ujasiriamali kwa akinamama ili waweze kuunda vikundi vyao vya VICOBA ili wapate mikopo yenye riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Wanawake imekuwa ikitoa mafunzo ya wiki tatu kwa wanawake wajasiriamali kabla ya kuwapatia mikopo yenye riba nafuu. Mpaka Juni, 2012 wanawake 5,270 sawa na asilimia 82 ya wanufaika wote wa mikopo ya vikundi kutoka Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani walipatiwa mafunzo maalum ya ujasiriamali na uendeshaji biashara kabla ya kupatiwa mikopo yenye riba nafuu yenye thamani ya shilingi bilioni kumi na mia mbili sitini.

Mheshimiwa Spika, ni lini na mwaka gani Benki ya Wanawake itafungua matawi Zanzibar swali hilo limeulizwa na Mheshimiwa Amina Abdulla Omar, Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar Wabunge wa Viti Maalum, Pemba. Kama ilivyoinishwa katika mpango mkakati wa kibiaresha mwaka 2009-2013, Benki ya Wanawake imedhamiria katika mwaka huu wa bajeti kuanzisha, kituo cha mikopo na mafunzo ya ujasiriamali Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mchakato huu unaendelea kwa ushirikiano mkubwa kati ya benki na Wizara ya Ajira, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ya Zanzibar na Wizara ya Fedha ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mtaji mdogo, moja kati ya mambo yanayojadiliwa kwa sasa ni ombi la benki kupewa msamaha wa tozo ya shilingi milioni kumi kwa kampuni ya Bara inayotaka kufanyakazi Zanzibar. Ni matumaini yetu kuwa msamaha huu utatolewa mapewa ili kuiwezesha benki kukamilisha mchakato wa kufungua ofisi ya Zanzibar. Tunatumaini Wabunge wa Zanzibar kwa kiu mnayoionesha ya kutaka ianze kazi Zanzibar mtakuwa chache ya kuiomba Serikali ya Mapinduzi iondoe tozo hii ili kama ikiwezekana benki ianze kazi kabla ya mwaka huu kwisha.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya sheria zinazowakandamiza wanawake hususani Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mirathi ya Mwaka 1965 na Sheria ya Kimila ya Mwaka 1963.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imezungumzia suala hilo, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii pia imezungumzia suala hilo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Nyambari M. Nyangwine, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu na Mheshimiwa Nassib Suleiman Omary Mbunge wa Mfenesini, Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mheshimiwa John P. Lwanji na wengine wengi mmetaka kujua kuhusu sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria na wadau wengine tumeainisha na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria mbalimbali kuhusu Sheria ya Mirathi na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa sasa sheria iko katika mchakato wa kuanda waraka wa Serikali *White Paper* kwa ajili ya kukusanya maoni ya wananchi kwa nia ya kuziboresha Sheria

hizo. Waraka huu wa Baraza la Mawaziri tayari umeshaandaliwa na unashubiri kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri kwa ajili ya maoni.

Mheshimiwa Spika, masuala ya mirathi na masuala ya Sheria ya Ndoa yamekuwa na utata sana, kwa hiyo tumeona ni vema tukiwa na *white paper* ili kusiwe na matatizo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Cecilia Pareoso, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Sereweji, Mheshimiwa Riziki Omary Juma, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Yusuf Haji Khamis na Mheshimiwa Hamad Abdallah wamezungumzia ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema mwanzo suala la ukatili ni suala gumu sana na limejikita katika jamii zetu, lakini katika kushughulikia masuala ya unyanyasaji na ukatili kwa wanawake na watoto ikiwemo vipigo, ubakaji, ukeketaji, unyanyasaji, Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mpango kazi wa kuondoa na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa miaka mitano. Wizara pia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake na watoto na watu wenye ulemavu wa ngozi kupitia vyombo vya habari. Serikali pia imeweka mazingira mazuri kwa asasi za kijamii na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kushiriki kikamilifu katika kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeunda na kuzindua Kamati ya Kitaifa ya kupiga vita ukatili dhidi ya wanawake, watoto wenye ulemavu wa ngozi *Albino*. Kamati hiyo ilizinduliwa tarehe 19 Disemba 2011. Kamati hiyo inayo wajumbe 25 kutoka Wizara za Serikali, Idara zinazojitegemea, asasi za kiraia, mashirika ya Umoja wa Mataifa na Taasisi za Kidini.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendesa kampeni mbalimbali za kupiga vita dhidi ya wanawake na wasichana, kwa mfano mwezi Machi mwaka huu Serikali iliratibu kampeni ambayo ilianzishwa Ban Ki-moon ambapo nchi mbalimbali ziliuka Tanzania na kupanda Mlima Kilimanjaro na kuweka bendera kuashiria kukataa ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wanaume wachache ambao wanafanyiwa ukatili.

Mheshimiwa Spika, pia tumeanzisha Madawati ya Jinsia katika baadhi ya Vituo vya Polisi. Ilionekana kwamba masuala ya kijinsia yakienda Polisi yalikuwa hayachukuliwi kwa umuhimu wake, lakini sasa vituo vingi vya Polisi vina madawati ya wahanga wa ukatili wa kijinsia, mwanamke aliyepigwa, mtoto aliyebakwa, wote hawa kuna dawati ambalo linawashughulikia.

Mheshimiwa Spika, kupiga vita mila na desturi zinazoleta madhara, Wabunge wengi wamezungumzia suala hili, lakini suala hili linahitaji mashirikiano ya wote kwa sababu mila na desturi zitabadilika kwa elimu zaidi, tunaamini kwamba jinsi elimu inavyokwenda sehemu zote nchi nzima, zile mila na desturi ambazo siyo nzuri zitakuwa historia kwa wakati ujao.

Mheshimiwa Spika, kuna swali limeulizwa na Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye ambalo linasema ni lini Waziri wa Maendeleo ya Jamii atawasilisha sheria kudhibiti vitendo vya ushoga.

Mheshimiwa Spika, Sheria inayozuia Ushoga ipo nchini na ipo chini ya (*SOSPA*) *Sexual Offence Special Provisional Act No. 4, 1998*, kifungu cha 154(1). Sheria hii inazuia vitendo vya ushoga na kutoa adhabu ya kifungo cha maisha jela au kifungo kisichopungua miaka 15 kwa wanaume wanaojihusisha na tabia hii chafu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *NGO's* katika kitabu cha hotuba yangu kulikuwa na maswali ambayo yaliulizwa na Mheshimiwa Aden Rage anauliza ni *NGO's* zipi ambazo zimepata pesa katika Mkoa wake wa Tabora. Ni kweli *NGO's* 16 za Mkoa wa Tabora zilipata fedha za ruzuku kutoka taasisi ya *Civil Society Organization* kiasi cha shilingi milioni mia tano.

Mheshimiwa Spika, majina ya *NGO*'s hizo naomba kumuahidi Mbunge kuwa tutampatia majina ya *NGO*'s. Ni vema Wabunge pia mkizifuatilia *NGO*'s hizi kama anavyofuatilia Mheshimiwa Ismail Aden Rage kwa sababu *NGO*'s zisijinasibu kwamba wanapata pesa zao wenyewe. Fedha zinazoingia kwenye *NGO*'s zinapitia Serikalini.

Mheshimiwa Spika, zipo *NGO*'s nyingi zilizosajiliwa kusaidia watoto yatima na wale walio katika mazingira magumu, je, ni hatua zipi zimechukuliwa na Wizara kudhibiti *NGOs* hizi ili ziwanufaishe walengwa. Serikali kwa kutambua kuwa *NGOs* ni wabia muhimu katika maendeleo imekuwa ikijenga mazingira wezeshi kwa mashirika hayo kuchangia katika nyanja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua ambazo Serikali imezichukua ni kuwezesha *NGOs*, kupata rasilimali za ndani za kutosha pamoja na kuwezesha marekebisho ya Sheria ya *NGOs* ya mwaka 2005 ambayo inatoa fursa kwa mashirika hayo kuendesha miradi mbalimbali ya kuzalisha faida na kujiongeza kipato katika kutekeleza majukumu yao ya msingi na si kugawana faida. *NGOs* hazitakiwi kugawana faida.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya yanawezesha mashirika hayo kuwa na nguvu ya kuhimili na kumiliki mali kisheria. Kupitia Baraza la Taifa la *NGOs* na taasisi mbalimbali kama vile *foundation for Civil Society Organisation*, wamekuwa wakijengewa uwezo wa kuijendesha kiuongozi na pia ubunifu katika kuongeza vyanzo vya fedha. Utekelezaji wa Kanuni za maadili ya *NGOs* unaosimamiwa na kuratibiwa na Baraza la Taifa la *NGOs* unasaidia sana sekta ya *NGOs* kujitawala na kujiongeza taswira chanya kwa jamii, hivyo kuongeza uungwaji mkono na michango kutoka kwa jamii husika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lucy Owenya amezungumzia kituo cha kulelea watoto Mkombozi, Moshi Mjini. Naomba suala hili ulirudishe kwenye Wilaya yako kwa sababu vituo vyote vinaandikishwa na Afisa wa Ustawi wa Jamii wa Wilaya na Afisa huyo yupo kwenye Halmashauri, unaweza ukazungumza naye ili kusaidia.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa Wabunge wote wafahamu kwamba, wale Maafisa wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Jamii ndiyo wanaoshughulikia masuala ya watoto, masuala ya mateso na kupambana na ukatili na masuala mbalimbali ya yatima. Wapo maafisa ambao wanaingia katika mabaraza yetu ya Madiwani na sisi wote ni Madiwani. Ni rahisi zaidi masuala kama haya tukiwapa wao ili wajue wapo watu ambao wanawafuatilia katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magalle John Shibuda, Jimbo la Maswa Magharibi anashauri kuhusu suala la kutoa agizo la sifa ya *NGOs* kutumika Vijiji Kuliko Mijini na *NGOs* nyingi ziente Maswa kutathmini maovu, kuwasha hamasa kwa wanawake kudai haki zao hasa kwa sababu najua huko kuna tatizo la macho mekundu pia. *NGOs* huwa hazianzishwi na Serikali huanzishwa na wananchi wenyewe, baada ya kuona kuwepo kwa tatizo la kiuchumi, kijamii au vinginevyo. Serikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa na *NGOs* itaendelea kuhimiza *NGOs* kuelekeza program zao nyingi vijiji ikiwemo Wilaya ya Maswa.

Mheshimiwa Spika, ukatili dhidi ya watoto nimeshalizungumzia, Daktari Anthony G. Mbassa na Mheshimiwa Rebecca Mngodo wameongelea kuhusu adhabu ya viboko, kuna hoja imetolewa na Mbunge mmoja anasema kuna mtoto wa miaka minane na amezaa akiwa na miaka kumi na moja, Arusha.

Mheshimiwa Spika, suala hili tutalichukua, lakini linapotokea jambo kama hili tunaomba sana mambo haya yapelekwe Polisi kwa sababu ni kinyume na Sheria ya Mtoto ambaye haruhusiwi kuolewa akiwa chini ya miaka 18. Lakini pia hata Sheria yetu ya Ndoa inasema mtoto wa miaka 15, lakini kama ikitolewa ruhusa ya mzazi. Kwa hiyo, naomba kitendo hiki kifuatiliwe na sisi pia tutafuatilia.

Mheshimiwa Spika, lingine wanasema adhabu ya viboko kwa watoto mashulen iifutwe, hili ni suala nyeti na ni tatizo kwa sababu tunalfanyia kazi sisi tukienda kwenye mikutano ya Kimataifa, wanatushangaa wakisikia bado kuna viboko shulen. Kutokana na hilo Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Elimu, tunalfuatilia kwa karibu kuangalia tutafute adhabu ya namna gani. Lakini

hairuhusiwi mwalimu yejote kumpiga mtoto fimbo isipokuwa Mwalimu Mkoo ambaye anaruhusiwa kumpiga viboko vinne.

Mheshimiwa Spika, tunajua kuna hadithi nyingi, watoto wengi wameacha shule kwa sababu ya kupigwa viboko visivyokuwa na utaratibu na ile dhana ya kusema Mwalimu na sisi tulipigwa, lakini wao walikuwa wanatembea bila viatu walipokuwa wakienda shule mbona sasa wanatembea na viatu. Kwa hiyo, mambo ya sisi tulipigwa, mama yangu alinipiga na wewe unampiga mtoto ni ukatili dhidi ya watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba kutoa wito kwa wazazi wote kuacha vitendo vya ukatili kwa watoto kwa sababu hasa akina mama tunawachapa sana watoto. Watoto hawa baada ya kuchapwa na mama zao wanaanza kuwa wakatili na mwishowe watoto wanakuja kuwachapa wake zao. Kwa hiyo, hii ni *vision cycle* ambayo tunaianzisha kule majumbani.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja ililamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

### MATUMIZI YA KAWAIDA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuna mila na desturi zetu wakati *Sergeant At Arms* anakuja kuweka hii Siwa tunanyamaza kimya. Naomba tafadhalii tunaendelea na kazi. Kama mnavyofahamu hatuna zile dakika za Spika. Kwa hiyo, ikifika saa kumi na mbili kasoro kumi tunapitisha kwa *guillotine*. Kwa sababu tulishakubaliana na wenzetu kwamba, wanakwenda kwenye kufuturu. (*Makofî*)

### FUNGU 53 – WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

*Kif. 1001 – Admin. and Human Res. Manag.... ...Sh. 1,009,182,000/=*

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, kigezo kinachotumika kupeleka ama kuanzisha Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, (*Folk Development College*). Wilaya ya Magu ni Wilaya ambayo imeanza miaka mingi na maombi yameletwa muda mrefu. Kwa nini Wilaya ya Magu hajapangiwa kuanzishiwa Chuo cha Maendeleo ya Jamii (*Folk Development College*). Nashukuru. (*Makofî*)

**SPIKA:** Kipo hicho Chuo au hakipo?

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Hakipo, toka kianzishwe mwaka 1972 mpaka leo hakuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi. Ni kigezo gani kinatumika kupeleka vyuo katika Wilaya mbalimbali?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza vyuo hivi vilanzishwa siku nyingi na sehemu zile ambazo hazina Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Halmashauri ya Wilaya inaweza kuleta maombi ya kuanzisha Chuo kama hicho na sisi tukawapa utalaam wote ambaa tunafundisha katika vyuo kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, kama unaona uko umuhimu kiwepo, basi katika Halmashauri yenu mnaweza mkazungumza hilo na sisi tutafurahi sana kuleta Chuo cha Wananchi katika eneo lako.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati nachangia nilipenda kujuwa kwamba ni Halmashauri ngapi mpaka sasa ambazo kwa mfano, katika miaka ya karibuni zimetenga hela asilimia tano kwenye Mfuko wa Wanawake, maana yake hili kidogo ni tatizo? Naomba nipate ufanuzi.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali kwamba ni Halmashauri ngapi zimepanga asilimia tano mpaka sasa. Naomba nimjibu baadaye kwa sababu haya mambo yapo kule kwenye Halmashauri na sisi tunachokifanya tunajua wale waliolipa wakija kwetu. Sasa hivi tunao 15 ambaa wametimiza yale masharti.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hapa tunaomba tuliweke jambo hili vizuri kwa sababu tunaweza tukawa tunachanganya iko hii ambayo amezungumzia Halmashauri 16, hizi hela ni zile hela zinazokwenda kwenye vikundi vilivyoko katika Halmashauri ambazo zinatoka katika Wilaya ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo hatuna tatizo nazo, tatizo lake kubwa ni kwamba zinaingia kwenye *Revolving Fund* na tuna Halmashauri ambazo zinaonekana mpaka sasa hivi hazijarudishwa, ndio maana Waziri anasema hapa kwamba, hao hawawezi kupata mikopo tena mingine.

Mheshimiwa Spika, lakini hizi zinazosemwa sasa za 5% kwa wanawake na 5% kwa ajili ya wanaume, Halmashauri zote na bajeti zote tulizopitisha hapa ndani yake tumeingiza 5% kwa ajili ya wanawake na 5% kwa ajili ya wanaume. Hizo hela zinatoka katika *own source*, zinatoka na tumetoa maelekezo katika Halmashauri zote kwamba, kuanzia sasa na mkiangalia katika *CAG's Report* inaonesha kabisa kwamba, ni kweli kama wanavyosema Wabunge hapa zipo Halmashauri ambazo hazifanyi hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kupitia kikao hiki tumeziagiza Halmashauri kwa sababu zinatuletea hata ripoti chafu kwa sasa hivi. Kwa hiyo, hizo hela ni hela ambazo tumezipitisha katika Bajeti hii iliopita kila Halmashauri imetenga 5%. Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli alipouliza sijui ni wa Kilwa ni 40,000,000 wametenga kule, 20 milioni kwa ajili ya akinamama na milioni 20 kwa ajili ya vijana. (*Makof*)

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mchango wangu wa maandishi nilieleza kwa jinsi gani ambapo kesi zinazotokana na kunyanyaswa kwa watoto kama kubakwa, kulawitiwa matatizo ya akinamama, zinachukua muda mrefu sana kwenye Mahakama za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiomba miaka yote Serikali iweke Mahakama maalum kwa ajili ya kushughulikia kesi hizi za watoto na akinamama kama ilivyofanya kwenye kesi za mauaji ya Ma-albino ili ziweze kwenda haraka, lakini pia watoto na akinamama waweweze kupatiwa haki zao za msingi. Naomba kupata maelezo kuhusiana na hili. Ahsante. (*Makof*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa na (*Family Court*) Mahakama ya Familia ambayo itashughulikia masuala ya watoto, ya wajane huwa inaitwa Mahakama ya Familia. Sisi Wizara na wana harakati mbalimbali tumekuwa tukilipigia debe hili na bado tunaendelea kuihamasisha Serikali, lakini kwa sasa ilianza na hizo Mahakama ambazo zipo lakini tunaamini kwamba jinsi tunavyoendelea siku moja tutapata Mahakama kama hiyo. (*Makof*)

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wote tunaamini kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Ni kweli kwamba wanawake wengi tukiwa na sauti moja itasikika zaidi na kwa kuwa akinamama tumekuwa na matatizo mengi, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Baraza la Wanawake Tanzania lilianzishwa baadaye kukawa na kesi Mahakamani, lakini mwaka jana kesi hiyo, BAWATA ilishinda. Sasa naomba kujua, nini hatima ya BAWATA kwa sababu mpaka sasa hivi halifanyi kazi na muundo wake ukoje? (*Makof*)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli upo umuhimu wa kuwa na Baraza la Wanawake na ni kweli kwamba Baraza la Wanawake lilishinda ile kesi na ninavyojuu mpaka sasa hivi lipo *active isipokuwa hawajafanya uchaguzi ili waweweze kuanza kuendesha shughuli zao*.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nitaka kupata ufanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba mojawapo ya majukumu ya Wizara hii ni kuwajengea uwezo wanawake na wanaume ili waweze kushiriki katika miradi ya maendeleo na hivyo kunufaika sawa katika miradi hiyo. Napenda kujua je, ni katika miradi ipi wanaume wamejengewa uwezo?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kutumia Vyuo vyake vya Maendeleo ya Wananchi vinawajengea uwezo wanawake kwa wanaume.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilzungumzia kadha inayowapata vijana hasa wa kike wale wanaofaulu kwenda Vyuo Vikuu, bahati mbaya hawapati mikopo katika *Loan Board*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niliomba kujua jinsi gani Wizara itaweka mkakati makusudi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, kuhakikisha vijana hawa sasa wanapata fursa ya mikopo asilimia mia moja badala ya hivi sasa wengine wanakosa mikopo, wanakaa mitaani, hatimaye kuna wengine wana wafadhili ambaa mwishowe wanaishia katika hali ngumu sana. Naomba *clarification* katika eneo hilo. (*Makof*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi wa suala la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Serikali imeanza utaratibu huu wa kutoa mikopo kwa baadhi ya wanafunzi kama njia ya kianzio. Lakini inafahamu kwamba kuna uhitaji mkubwa kwa vijana ambaa kila mwaka Serikali imeazimia kuongeza namba ya wanafunzi ambaa wanapata elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza taratibu mbalimbali na hivi karibuni tumei-*commission* ambayo inaangalia namna ya kupata vyanzo zaidi ya fedha zile za Serikali kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi. Tutakopofanikiwa tutaweza kutoa ama kwa wingi zaidi ama kwa wote kama ambavyo tungependa kufanya.

**MHE. NEEMA M. HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kumuuliza Mheshimiwa kutokana na zile sheria ambazo zinaonekana kabisa zimepitwa na wakati na zinamkandamiza mwanamke je, ni lini sheria hizi zitaletwa hapa Bungeni ili tuweze kuzifanya marekebisho?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivoyeleza katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba, sasa hivi tuko katika mchakato wa kutengeneza *white paper* iko katika hatua za mwisho na itakwenda kwenye Baraza la Mawaziri halifu tutakwenda kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, sheria hizi ziko *very sensitive* kuna ubishani hasa katika wenzetu wa madhehebu ya dini, kwa hiyo, ni lazima tupate maoni ya Watanzania wote, wa dini zote wa jinsia zote na wa hali zote. (*Makof*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge inabidi tuvumiliane kwa mujibu wa kanuni ya 104(2) inanitaka nifanye *guillotine*.

*Kif. 1002 – Finance and Accounts ... ... ... ... Sh. 508,849,000/=*  
*Kif. 1003 – Policy and Planning ... ... ... ... Sh. 278,412,000/=*  
*Kif. 1004 – Internal Audit Unit ... ... ... ... Sh. 68,766,000/=*  
*Kif. 1005 – Government Communication Unit ... Sh. 58,389,000/=*  
*Kif. 1006 – Procurement Management Unit ... Sh.111,502,000/=*  
*Kif. 1007 – Information, Comm. and Technology ... Sh.19,050,000/=*

*Kif. 2001 – Training and Folk Dev. Colleges ... Sh. 5,161,586,000/=  
Kif. 2002 – Community Development ... Sh. 3,108,397,500/=  
Kif. 2003 – Community Dev. Coll. – TENERU... Sh.1,163,354,000/=  
Kif. 3001 – Gender Development ... Sh. 271,189,000/=  
Kif. 3002 – Children Development ... Sh. 201,989,000/=  
Kif. 4001 – Non – Government Organizations ... Sh. 194,984,500/=*

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **FUNGU 53 – WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO**

*Kif. 1001 – Admin. & Human Resource Manag. ... Sh.942,637,842/=  
Kif. 1003 – Policy and Planning ... Sh. 76,433,553/=  
Kif. 2001 – Training and Folk Dev. College ... Sh. 598,038,605/=  
Kif. 2002 – Community Development ... Sh. 282,890,000/=  
Kif. 2003 – Community Development College – TENERU ... Sh.0/=  
Kif. 3001 – Gender Development ... Sh. 1,400,000,000/=  
Kif. 3002 – Children Development ... Sh. 161,341,000/=*

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)  
(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka 2012/2013, imepitia mafungu kwa mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofu*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo  
ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa mwaka 2012/2013  
yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto pamoja na Watalaam wao kwa kufanya kazi nzuri na kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge kwa maandishi na kuchangia kwa kuongea endeleeni kuifanya Wizara hii iweze kuonekana mionganii mwa wananchi jinsi inavyoweza kuwahudumia na matumizi mazuri ya fedha yanayotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, naona kuna wengine walikuwa hawajui mabadiliko, leo hii tumepitisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kesho ni Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Naomba muangalie ratiba, tumefanya mabadiliko makubwa ya ratiba. Kwa hiyo, msije mkawa mnajipanga kwa ratiba ambazo hazihusiki. Siku ya Jumatano tutakuwa na Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Alhamisi itakuwa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Muangalie mabadiliko ya ratiba.

Tutaendelea na utaratibu, sasa tutamtambua Mbunge aliyehudhuria siku hiyo kwa kusaini asubuhi na jioni ndio tutamtambua amehudhuria. Kama amesaini asubuhi tu jioni hayupo sisi tutajua hakuwepo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa siku ya leo kwa mahudhurio yenu. Naomba tuendelee namna hii hii. Nawatakia jioni njema na futari njema kwa Waheshimiwa Wabunge amba wanakwenda kufuturu.

Sasa naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne,  
Tarehe 24 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*